

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 31 Mei, 2016

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

(Hapa Wabunge wa Kambi ya Upinzani Bungeni Walitoka nje)

NDG. JOHN N. JOEL - KATIBU MEZANI: Kiapo cha Uaminifu.

KIAPO CHA UAMINIFU

Mheshimiwa Mbunge afuataye aliapa kiapo cha uaminifu:

Mhe. Jaku Hashim Ayoub

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. JOHN N. JOEL - KATIBU MEZANI: Hati za kuwasilisha mezani.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. JULIANA D. SHONZA – (K. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama juu ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msigwa, huwa hakuna ndugu humu ndani. Mheshimiwa Msingwa, Kanuni tafadhali! Hamna ndugu humu ndani, hamna mtu anayekuwa *addressed* kama ndugu, endelea.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Nilitegemea wewe ni ndugu...

NAIBU SPIKA: Kanuni unazijua.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Mambo ya Nje. Naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Amina Mollel.

Na. 266

Idadi ya Shule za Awali Nchi

MHE. AMINA S. MOLLEL (K. n. y. MHE. SUSAN A. J. LYIMO) aliuliza:-

Elimu bora ni uti wa mgongo wa maendeleo ya jamii yoyote ile na ni msingi bora wa elimu kwa watoto unaoanzia toka shule za awali na za msingi:-

- (a) Je, kuna shule ngapi za awali kati ya mahitaji halisi?
- (b) Je, ni nini mipango ya haraka kuhakikisha shule za awali zinakuwepo katika shule zote za msingi za Serikali nchini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji halisi ya madarasa ya awali ni 16,014 ambayo ni sawa na idadi ya shule za msingi zilizopo nchini kwa sasa. Shule zenye madarasa ya awali ni 14,946 ambazo ni sawa na asilimia 93.33 ya mahitaji. Hivyo, shule za msingi 1,068 hazina madarasa ya awali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa vyumba vya madarasa ya awali unafanywa na Halmashauri kwa kushirikisha na nguvu za wananchi kupitia Mpango wa Fursa na Vikwazo yaani *O and OD (Opportunity and Obstacle to Development)*. Azma ya Serikali ni kuhakikisha inajenga na kukamilisha vyumba vya madarasa vya awali kwa shule zote 1,068 zenye upungufu huo. Hivyo nitoe wito kwa Halmashauri zenye mapungufu haya kuangalia upya vipaumbele vyake na kutenga bajeti ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu hiyo muhimu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kutokana na mwamko ambao umejitokeza hivi sasa kwa watoto wengi kuhudhuria shule kutokana na elimu bure, lakini vilevile kumekuwepo na changamoto mbalimbali yakiwemo pia malalamiko kutoka kwa wananchi.

Je, Serikali inajipanga vipi kuhakikisha kwamba changamoto hizi inaziondoa ili watoto wote waweze kupata elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, watoto wenye mahitaji maalum bado wao wanakabiliwa na changamoto nyingi; je, Serikali ili kuendana na kasi hii, inajipangaje kuhakikisha watoto wenye ulemavu ambao jamii imekuwa ikiwaficha na wao pia wanapata nafasi ya kupata elimu bure na kuifurahia nchi yao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya kwanza ni changamoto zinazozikabili shule zetu. Ni kweli mara baada ya mchakato wa Serikali yetu ya Awamu ya Tano, ilipojielekeza kwamba elimu kuanzia shule ya awali mpaka *form four* kuwa ya bure, tumegundua kuna mambo mengi sana yamejitokeza.

Jambo la kwanza ni kitendo cha watoto wengi waliokuwa wakibaki mitaani kwa kukosa fursa ya kujiunga na shule, hivi sasa wanaende shule. Baada ya hilo kilichotokea ni kwamba tumekuwa na tatizo kubwa la upungufu wa madawati na mambo mbalimbali. Katika hili ndiyo maana Waziri wangu wa Nchi sambamba na Waziri Mkuu walitoa maelekezo kwamba ikifika 30 Juni, madawati yote yawe yameweza kupatikana maeneo ili kuondoa changamoto ya watoto wanaokaa chini. Hata hivyo, Serikali imejielekeza kuhakikisha kwamba tunajitahidi katika ujenzi wa miundombinu ikiwemo madarasa lengo likiwa watoto wote wanaofika shuleni waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna swali la pili linalohusu watoto wenye ulemavu. Ni kweli mimi mwenyewe nikiri kwamba nimetembelea shule kadhaa za watoto wenye ulemavu, kule Mufindi hali kadhalika pale Dar es Salaam, maeneo hayo nilioyatembelea ni kweli watoto hao wana changamoto mbalimbali, lakini nimeweza kutoa maelekezo mbalimbali kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, wahakikishe kwanza watoto hao wenye ulemavu wanapewa kipaumbele. Ndiyo maana katika bajeti yetu ya TAMISEMI mwaka huu tumejielekeza wazi jinsi gani tumejipanga katika suala zima la watu wenye ulemavu ili kwamba watoto wote wanaoenda shuleni kutokana na hali zao wote waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Amina Mollel, najua kwamba wewe ni mwakilishi halisi na makini sana wa walemavu, tutahakikisha ombi lako hili linafanyiwa kazi katika Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa nguvu zote. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwalongo, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni kwa nini sasa katika yale madarasa ya awali ukiangalia fungu lile la elimu bure wanapotoa ile fedha, wale watoto wa madarasa ya awali hawapati ile fedha na inawafanya wazazi waendeleo kuchangia yale madarasa ya awali.

Je, ni lini Serikali itanza kutoa fedha kwa ajili ya madarasa ya awali?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema katika majibu yangu ya msingi, ukija kuangalia maeneo mbalimbali ambapo watoto wale wa awali waliokuwa wakienda shuleni, mara nyingi sana walimu waliokuwa wanafundisha utakukuta ni walimu waliokuwa wanachukuliwa mtaani, waliomaliza *form four*, darasa la saba ambaye anaweza akafundisha. Katika maelekezo ya utaratibu wetu wa elimu, wale watu wote wanaomaliza *grade 'A'* wanakuwa na *component* ya elimu ya awali. Kwa hiyo, utakuja kuona kwamba, wakati mwingine watoto walikuwa wakienda shule wanalazimishwa walipie fedha kwa ajili ya mwalimu wa awali, jambo lile tumesema kwamba, walimu wote sasa hivi wanaomaliza *grade 'A'* walimu wale wanaopelekwa mashuleni, kuna mwalimu anayefundisha darasa la awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yetu kama Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ni kuhakikisha Wakurugenzi, wanahakikisha katika *allocation* ya wale walimu katika shule mbalimbali, wawapeleke walimu ili kusaidia kuondoa ule utaratibu wa wazazi kuwa wanachanga kwa ajili ya kumchukua mtu mtaani kuja kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumeenda mbali zaidi, ndiyo maana watu walioshudia mwaka jana hapa katika Chuo chetu cha UDOM, tulipeleke takribani walimu wapatao 17,000 katika somo la KKK. Lengo ni kuwawezesha watoto wanapoingia shuleni kuanzia awali na watoto wa darasa la kwanza waweze kujua kusoma na kuandika.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ni kweli Serikali tunajua changamoto ni nyingi kutokana na suala la elimu bure, lakini Serikali inaangalia jinsi gani tutatatua matatizo mbalimbali. Mara baada ya kufanya jambo hili tumegundua jambo changamoto nyingi zimeweza kujitokeza, changamoto hizi ni kutokana na hii fursa sasa, Serikali ya Awamu ya Tano iliweza kufungua sasa na kupitia hizi changamoto, ndiyo tunaenda kuhakikisha kwamba tunalijenga Taifa la kupata elimu bora. Changamoto hizi, tutakuwa tunazitatua awamu kwa awamu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Issaay swali fupi la nyongeza. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, naona Mheshimiwa Issaay yuko busy!

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Samahani! Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, amesimama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri Jafo, ninataka kuongezea kwenye swali alilokuwa analijibu hivi punde kwamba, isichukuliwe kwamba watoto wanaojiunga kwa darasa la awali ni tofauti na watoto wanaoanzia darasa la kwanza mpaka la saba. Wote ni wanafunzi isipokuwa tu wale wana *special treatment*, lakini fedha inayopelekwa kwa ajili ya uendeshaji wa shule, ndiyo hiyo itumike katika kuendesha na mahitaji ya wale watoto wa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa tunafahamu Serikali kwamba mahitaji ya watoto wa awali ni maalum sana. Jitihada kubwa itakayokuwa inafanyika ni kuona namna gani tutaongeza hii bajeti, pia kutafuta *facilities* kwa ajili ya watoto hawa wa awali kwa sababu namna yao ufundishwaji ni tofauti na hawa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii tu kuwaomba Walimu Wakuu wa shule na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kuhakikisha kwamba hawatenganishi zionekane kwamba kuna shule ya awali na shule ya msingi inayoanzia darasa la kwanza. Hii shule ni moja na ndiyo maana hata walimu wake ni walewale, kwa sababu wale walimu wanaomaliza *grade 'A'* wanakuwa wana *component* ambayo wamefundhishwa namna ya kufundisha watoto hawa wa madarasa ya awali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara umekuwepo usumbufu wa walimu wa awali kupata mishahara yao kwa wakati.

Je, kuna mkakati gani wa kuwapatia mishahara yao kwa wakati?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri hapa amelizungumza punde kwamba walimu wa awali ni walewale ambao wapo katika utaratibu wa walimu walioajiriwa. Kwa hiyo, ina maana kwamba, hatutarajii mishahara wa mwalimu wa awali uchelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wote wanapata mishahara yao katika utaratibu ule wa kawaida sambamba na walimu wengine katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Isipokuwa inawezekana kama nilivyosema awali katika majibu yangu ya msingi ya mwanzo kwamba inawezekana katika maeneo mengine watu walikuwa wanawachukua walimu kutoka mtaani, kutoka katika mfumo usiokuwa rasmi, ambao wazazi walikuwa wanachangia. Kwa sababu jukumu letu kubwa sasa tumepeleka walimu wengi wa *grade 'A'*, ili sasa waweze kufundisha yale madarasa ya awali kama ilivyokusudiwa kwa sababu wamepewa ile *package* ya kufundisha watoto wa awali ili mradi matatizo hayo yote Mheshimiwa Ishengoma yatakuwa hayapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimeona, swali lako lilikuwa makini lakini huo ndiyo utaratibu, ambao tunaenda nao. Lengo letu ni kwamba, watoto wetu wapate elimu bora katika shule zetu.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi, sasa aulize swali lake.

Na. 267

Hitaji la Shule za Kidato cha Tano na Sita Jimbo la Masasi

MHE. RASHID M. CHUACHUA aliuliza:-

Jimbo la Masasi lina shule moja tu ya sekondari kwa kiwango cha kidato cha tano na sita, ambayo ni Sekondari ya Wasichana Masasi, ambayo imekuwa haitoshelezi kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaofaulu:-

(a) Je, ni lini Serikali itazipandisha hadhi shule za sekondari za Mwenge Mtapika na Sekondari ya Anna Abdallah ili ziweze kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita?

(b) Je, ni lini Serikali itaajiri walimu katika Jimbo la Masasi ikiwa lkama ya walimu wa sayansi katika shule za sekondari tisa zilizopo ni walimu 84 lakini waliopo ni 24 tu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashidi Mohamed Chuachau, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuwa na shule za sekondari ya kidato cha tano na sita kila tarafa. Halmashauri ya Mji wa Masasi imeteua shule mbili za sekondari, ambazo ni Anna Abdallah na Mwenge Mtapila ili ziweze kuboreshwa na kuwa za kidato cha tano na cha sita. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Halmashauri imetenga shilingi milioni 140 ili kuanza upanuzi wa miundombinu ya majengo ya shule hizo ikiwemo bwalo la chakula, jiko na huduma za maji na umeme. Aidha, Halmashauri imewasilisha andiko katika Mamlaka ya Elimu Tanzania yaani TEA kwa ajili ya maombi ya fedha shilingi milioni 125 za kukamilisha ukarabati wa miundombinu hiyo ya shule.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa walimu wa masomo ya Sayansi katika Halmashauri ya Mji wa Masasi ni walimu 60. Serikali imeendelea kuwapangia vituo walimu wa masomo ya sayansi kadri wanavyohitimu na kufaulu mafunzo yao katika vyuo ili kukabiliana na upungufu huo. Mkakati tulionao kama Serikali ni kuongeza udahili wa walimu wa masomo ya sayansi katika vyuo ili kukidhi mahitaji kwa nchi nzima. Halmashauri ya Mji wa Masasi itapangiwa walimu wa sayansi na kila mara tutakapo kuwa tunaajiri walimu hao ili kupunguza pengo lililopo hivi sasa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashidi Chuachau, swali la nyongeza.

MHE. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Swali la kwanza, namuomba Mheshimiwa Waziri anipe *specific time*, kwa sababu wanafunzi hawa hawafundishwi masomo ya sayansi, ni lini mpango wa Serikali wa kuwaajiri walimu hawa utatimizwa?

Swali la pili; naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze ni lini Serikali itatenga pesa kwa ajili ya kukamilisha maabara kumi ambazo zipo katika mchakato wa kujengwa na vifaa katika maabara 14 za shule za sekondari? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikiri miongoni mwa matatizo makubwa sana tunayokabiliana nayo ni ukosefu wa walimu wa sayansi katika shule zetu za sekondari. Katika hili, ndiyo maana Serikali tumesema pale wazi kwamba tunachokifanya ni nini, tunajipanga kwa kadri iwezekanavyo, walimu wanavyopatikana baada ya udahili ule, watoto wanapohitimu masomo yao tunawaelekeza katika shule zile za sekondari. Inawezekana mwaka huu tukaja na *approach* nyingine tofauti, kwa sababu imeonekana maeneo mengine walimu wakipelekwa katika Halmashauri husika, walimu wale wengi wanaishia maeneo ya mijini. Sasa mwaka huu inawezekana tukawapeleka walimu moja kwa moja katika shule husika ili kuondoa tatizo la walimu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, *time frame*, tulisema hapa kwamba katika michakato yetu ya ajira hapo itakapokamilika, ni kwamba walimu tunatarajia kuwaajiri ambao lengo ni kuweza kuwapeleka, kwa hiyo ni suala zima la utaratibu ambao unaendelea hivi sasa. Ndiyo maana mwaka huu tumejielekeza kwamba ikiwezekana kuna walimu wengine takribani 2,000 ambao tunaona kwamba walikuwa wana uwezo wa kufundisha sayansi, Serikali inaona kwamba itaweza kuwachukua walimu wale kwa mkataba maalum, ili kuwaingiza katika suala zima la ajira kupunguza tatizo kubwa la walimu wetu hawa ambao imekuwa kero sana kwa walimu wa sayansi. Sambamba na hiyo, tunafanya harakati nyingi sana, lengo letu ni kuboresha vijana wetu ili tupate walimu wengi wa sayansi katika maeneo yetu ili watoto waweze kufuzu masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ujenzi wa maabara kukamilika, ndugu zangu nimesema haya juzi tu, tena tumetoka katika mchakato wa bajeti. Nimesema haya mambo kila Halmashauri ina vipaumbele vyake na kila Halmashauri itenge vipaumbele kama tumejenga maabara kuna upungufu wa vifaa, lengo letu iwe ni kutenga vifaa. Naomba niwapongeze kwanza Wabunge wote na viongozi wote, tumesimamia vya kutosha katika ujenzi wa maabara katika Halmashauri zetu. Kwa mara ya kwanza tumefanya mapinduzi makubwa kama nchi ya Tanzania kuhakikisha tumejenga maabara katika kila shule ya Kata, hili ni jambo kubwa tena ni jambo la kujipongeza. Ujenzi huu ni lazima utakumbana na changamoto mbalimbali kama suala la upungufu wa vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuelekeze Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu najua uko makini na asubuhi tulikuwa tunaongea hapa katika suala la Halmashauri yako, kuhakikisha kwamba katika *own source* inayowezekana hivi sasa, kama kuna baadhi ya vifaa vinavyohitajika ili maabara zile ziweze kufanya kazi, muweze kuzitenga kusaida vijana wetu. Serikali pia vilevile tuko mbioni kuhakikisha kwamba tunaboresha shule zote ziweze kutoa elimu bora kwa wanafunzi wetu hasa elimu ya sayansi.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Napenda kuuliza swali moja.

Katika hii Mikoa na Wilaya mpya, nyingi zina matatizo ya kutokuwa na shule za kidato cha tano na sita. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzisaidia hizi Wilaya mpya ikiwepo Busega, ambayo mpaka leo hii hatuna shule ya A-Level? Mheshimiwa Waziri anaweza kunipa mkakati gani wa Serikali kusaidia hizi Wilaya na Mikoa mipya?

NAIBU SPIKA: Umeshauliza swali Mheshimiwa Chegeni amesikia swali. Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba yapo baadhi ya maeneo makubwa hadi Wilaya nzima ambako hakuna shule ya kidato cha tano na sita, lakini nilisema hapa kwamba sekta ya elimu imekuwa *decentralized* na kwa hiyo maana ya *decentralization* ni kwamba mipango yote inapangwa kuanzia kule chini na ikiletwa kwetu ni kwa ajili ya kuona tu kwamba tunaipokea na kukubaliana na wadau kama ambavyo tunavyosema kwamba Halmashauri ndizo zinazomiliki shule hizi na kwa kufanya hivyo tunaamini kwamba ndiyo sera ile ya *D by D* inapokuwa imetekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninamsihi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama wao wataanzisha jambo hili wakalikamilisha, wakileta kwetu hatuna pingamizi kama watakuwa wameziteua shule watakazodhani zinaweza zikawa ni rahisi kuzifanya ziwe *high school*.

Na. 268

Kuimarisha Ulinzi na Vitendea Kazi Mkoa wa Kigoma

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma umekumbwa na wimbi kubwa la wakimbizi wa kutoka Burundi na Congo (DRC), kutokana na wimbi hilo ujambazi umeongezeka sana.

Je, Serikali iko tayari kuongeza ulinzi wa kutosha na vitendea kazi vya kutosha ili mamlaka husika iweze kukabiliana na tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba suala la wakimbizi kuja nchini hutokea mara nchi jirani zinapokuwa katika hali tete ya usalama katika nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiongeza ulinzi pamoja na vitendea kazi ikiwemo magari na pikipiki kwa lengo la kudhibiti uhalifu unapojitokeza katika maeneo mbalimbali. Aidha, hivi karibuni Mkoa wa Kigoma umepokea magari 11 na Serikali itaendelea kuongeza na kuimarisha ulinzi katika Mkoa wa Kigoma na mahali pengine popote nchini ambapo kutakuwa na tatizo kama hilo.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma unapakana na nchi za Burundi na DRC, na kwa kuwa eneo kubwa la mpaka halina ulinzi, hali inayopelekea wahalifu kupita na kupitisha silaha nzito kuingia Tanzania, wahalifu hao kwa kushirikiana na raia wasiokuwa waaminifu hufanya ujambazi na unyang'anyi.

Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti wa kukagua mpaka upya na kubaini maeneo yasiyokuwa na ulinzi ili kuweza kuweka ulinzi maeneo yasiokuwa na ulinzi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa mara nyingi vituo vya polisi hukabiliwa na ukosefu wa mafuta, hivyo kuwafanya polisi kushindwa kufanya kazi yao kikamilifu. Je, Serikali iko tayari kuongeza bajeti ya vituo vya polisi, hasa Mkoa wa Kigoma ili polisi waweze kukabiliana na majambazi hao? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la Mheshimiwa Genzabuke limekuja wakati muafaka kwa sababu jana tulikuwa tuna kikao kizito ambacho kilikuwa kinahusisha Wakuu wa vyombo vyote vya usalama vilivyopo nchini, vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Moja katika ajenda ya msingi ambayo tulizungumza ilikuwa ni hiyo.

Ninachotaka kumuelezea tu kwa sasa hivi ni kwamba tumetoa jukumu hilo kwa Idara ya Uhamiaji ambayo kazi hii wameshaianza kufanya huo utafiti ambao anauzungumza wa kubaini vipenyo vyote ambavyo vinakisiwa viko vipenyo takribani 248 nchi nzima. Kuazia Mkoa wa Kagera, nchi nzima kwa maana ya mikoa yote ambayo imepakana na nchi jirani. Kwa hiyo,

tumeshaanza hiyo kazi na pale itakapokamilika wataliwasilisha hilo andiko Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia haina maana kwamba hivi tunavyozungumza kuna tatizo kiasi kikubwa hivyo, kwa sababu kuna kazi kubwa ambayo inafanywa na vyombo hivi vya usalama, ikiwemo kuendesha doria na misako katika maeneo hayo ambayo ni maeneo tete. Lakini kutoa elimu vilevile kwa wananchi pamoja na Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji wa maeneo ambayo yanapakana na mipaka hiyo pamoja na kuimarisha vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili ambalo amezungumzia changamoto ya mafuta; ninataka tu nimueleze kwamba moja katika majukumu ya msingi ya Wizara yetu hii ambayo tumefanya kwa mafanikio makubwa ni kuhakikisha kwamba kuwepo kwa wakimbizi katika maeneo hayo ambayo yapo katika Mikoa inayopakana na mikoa hii ambayo ina machafuko ikiwemo Kigoma, kusilete athari kwa wananchi na badala yake kuwe kuna manufaa. Katika kufanya hivyo tumeweza kuzungumza na mashirika haya ambayo yanahudumia wakimbizi kuweza kuchangia, siyo tu kwa maendeleo ya jamii ya wananchi ambao wanaishi pale, lakini hata kwa vyombo vya usalama wakati wa kutekeleza majukumu yao. Moja katika mafanikio hayo ni kwamba hivi tunavyozungumza UNHCR wametoa magari sita, pikipiki mbili kwa kambi tatu za Nyarugusu, Mtendeli na Nduta, na gari moja aina ya *Land Cruiser* kwa Ofisi ya RPC. Pia shirika hilo huwa linatoa mafuta kwa kuwalipa posho ya shilingi 15,500 kwa siku, kwa askari ambao wanalinda kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na jitihada za Serikali ambazo zinafanyika kuweza kuimarisha bajeti ya polisi ya mafuta kadri hali ya uchumi itakavyoimarika. Kwa hiyo, kuna kazi ambayo inafanyika tu na imekuwa na mafanikio kwa kiasi kikubwa, hata hivyo tunazitambua changamoto ambazo Mheshimiwa Genzabuke amezungumza na hii mikakati niliyoizungumza ni moja kati ya njia ambazo tunakabiliana nazo.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii uliyonipatia.

Kwa kuwa tatizo la ujambazi linaloipata Mikoa ya Kagera na Kigoma lipo pia tatizo la namna hiyo katika Jimbo letu na Wilaya yetu ya Mkuranga ambapo hapa karibuni tulipata tatizo la uvamizi wa majambazi katika Benki yetu ya NMB, Bupu na pale Mbagala Rangitatu na mengineyo.

Je, Serikali sasa iko tayari kuhakikisha kwamba Wilaya yetu ya Mkuranga inapata nyongeza ya vifaa kazi lakini pia na Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba ujibu kwa kifupi tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa kuwa hili ni ombi, basi tunalichukua, halafu mimi na yeye tutakaa, tunajuana ma-comrade, tuweze kuona uwezekano wa kulitimza hilo.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kumekuwepo na wimbi kubwa sana la ujambazi ambalo linafanywa na hawa vijana wanaojulikana kama *panya road* ambao wamekuwa wakileta utata sana katika miji mikubwa na sasa hivi mpaka Iringa wameshatokea, Serikali ina mpango gani ama mkakati gani wa kuondoa ujambazi, hawa *panya road* kwa sababu ni vijana ambao nasikia wanafahamika kwenye mitaa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la *panya road*, ni kweli kulikuwa na kundi la vijana ambalo lilikuwa linafanya uhalifu. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kabati kwamba Jeshi la Polisi limefanya kazi nzuri kudhibiti kundi la vijana hawa na nadhani Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba kwa kipindi fulani sasa matukio hayo hayajitokezi na vijana hao wamedhibitiwa.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Kwa kuzingatia kwamba Mkoa wa Songwe ni mpya na ni mkoa ambao uko mpakani, lakini kiongozi ambaye anahusika na mambo ya ulinzi na usalama wa Mkoa wetu wa Songwe ambaye ni RPC anaishi kwenye nyumba ambayo ni sawa na gofu. Nilitaka kupata kauli ya Serikali kwamba ni lini RPC wa Songwe atapatiwa nyumba nzuri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, msaidie tu Mheshimiwa Mbunge, *otherwise* swali lake liko nje kabisa ya swali la msingi, lakini msaidie kumjibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua changamoto ambayo inakabili makazi ya RPC kule Songwe hasa ukitilia maanani kwamba mkoa huu ni mpya, kwa hiyo utakumbana na changamoto mbalimbali na unahitaji muda mpaka kuweza kukaa sawa. Kwa kulitambua hilo basi, nikiamini kabisa kwamba tuna programu kabambe ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa askari ambazo tumekuwa tukizitungumza hapa kila siku, tutaangalia huo uwezekano kufikia utaratibu huo ama utaratibu

mwingine wowote ili tuweze kurekebisha hilo jambo, tunalifahamu na tutalifanyia kazi.

Na. 269

Vitendo vya Uonevu Vinavyofanywa na Wenye Mgodi wa GGM – GEITA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA aliuliza:-

Mgodi wa GGM – Geita unaongoza kwa kuwapiga vijana na kuwachapa viboko na pengine kuwasababishia vifo, lakini wahusika hawachukuliwi hatua stahiki.

Je, Serikali inachukua hatua gani sasa dhidi ya wahusika pale inapotokea wameua watu au kujeruhi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwepo na vitendo vya uonevu na matukio kadhaa baina ya wamiliki wa Mgodi wa GGM na wananchi wanaozunguka mgodi huo. Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua stahiki kwa watuhumiwa mara tu taarifa zinapotolewa polisi. Mathalani, tarehe 14/2/2016 majira ya saa 07.15 ndani ya Mgodi wa Dhahabu wa Geita, watu wawili walijeruhiwa kwa kupigwa risasi za mpira wakiwa wanaondolewa na mlinzi ambapo mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa mahakamani na kufunguliwa kesi Na. CC67/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwenye Bunge lako hili Tukufu kutoa rai kwa wananchi wanaozunguka mgodi wa Geita kuheshimu sheria na taratibu ili kuepuka vitendo vya kuvamia mgodi vinavyoweza kusababisha madhara kwao.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nilitaka kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Wananchi kwenye vijiji vya Majimbo yetu wanapojichukulia sheria mkononi, kunavyopigwa mwano, pengine kumetokea kibaka, polisi wanakuja kukamata viongozi wa vijiji na kuwa-suspect na ile kesi, lakini kwenye mgodi ni tofauti, zinapookotwa maiti zenye risasi za moto na matukio mengine mabaya, hakuna suspect yeyote anayekamatwa kutoka kwenye Mgodi wa GGM na

zinachukuliwa maiti zinakwenda kutelekezwa hospitali ndugu wanakwenda kutambua na kuchukua bila kuchukuliwa hatua yoyote.

Je, Waziri yuko tayari kufuatana na mimi baada ya Bunge hili kwenda katika Kijiji cha Nyakabale ambacho kina wahanga zaidi ya 100 waliopigwa risasi za moto na kuumishwa mbwa wa mgodi, kwenda kuwaona na kuja kutoa majibu sahihi kwenye Bunge lijalo? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tatizo ndiyo hilo, kwa nini Mgodi wa GGM usiweke uzio kama ilivyo migodi mingine hapa nchini kama Acacia, Nyamongo na Kahama Mine?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu swali langu la msingi ambapo nilitolea mfano wa hatua ambayo Serikali ilichukua kwa askari ambaye aliwapiga risasi wananchi, kwa hiyo nadhani siyo kweli kwamba hakuna hatua hazijachukuliwa, hatua zinachukuliwa na huo ni mfano mmoja tu. Inawezekana pengine kuna baadhi ya matukio hayajachukuliwa hatua labda kwa kukosekana kupatikana taarifa kwa mamlaka husika. Sasa wazo lake hili alilolitoa la kuambatana mimi na yeye nadhani ni wazo la msingi ili aweze kunionesha maeneo ambayo yalipaswa kuchukuliwa hatua lakini hatua hazikuchukuliwa tuweze kuchukua hatua. Kwa hiyo ombi lake hilo tumelipokea kwa mikono miwili ni wajibu wetu kuweza kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kuwatumikia wananchi, hasa wanyonge, ambao wamekuwa wakionewa, kwa hiyo kwa kuwa yeye ana ushahidi basi tutafuatana pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kwamba Mgodi ya GGM haujawekwa uzio, hili siwezi nikalijibu sasa hivi kwa sababu sijafika kwenye mgodi huu. Lakini kwa kuwa tuna ziara hiyo mimi na yeye nadhani wakati huo utakuwa ni muafaka wakuweza kutembelea kuangalia mazingira pale tukashauriana kwa pamoja sasa na vyombo vinavyohusika na usalama kuimarisha usalama katika mgodi huo ili wananchi wasiweze kupata athari zaidi. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashidi Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa katika Wilaya yetu ya Lushoto tuna pakana na nchi jirani ya Kenya na Kituo cha Polisi cha Mnazi kina upungufu mkubwa wa vitendea kazi zikiwemo pamoja na silaha.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu suala hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo niseme tu kwamba tutalichukua tuangalie upungufu huo ambao anauzungumzia Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na yeye tuone hatua muafaka ya kuchukua ikiwemo kuongeza vitendea kazi kadri ya mazingira na hali halisi na ushauri wa kitaalamu utakapokuwa unaruhusu. Maana yake wakati mwingine uwekaji wa vitendea kazi hivi unazingatia vigezo vingi ikiwemo silaha, kwa hiyo, kuna haja ya kukaa na wataalam kwa maana ya Jeshi la Polisi kushauriana ni sababu gani ambazo zimesababisha eneo hilo liwe na upungufu halafu tuchukue hatua stahiki kwa wakati muafaka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Venance Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la ulinzi na usalama ni tatizo na sasa hivi ukichukulia kumetokea mauaji ya mara kwa mara nchi hii, na watu wamelalamika kwamba hawasilizwi wanapokwenda kwenye vituo vya polisi na mahakama na kwa hivyo kujichukulia sheria mkononi. Serikali haioni sasa inabidi ifanyie kazi suala hili ili kupunguza haya mauaji ambayo yamekuwa ni kero na shida katika nchi hii?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza jambo ambalo ni la muhimu sana wananchi wakalifahamu mauaji ni kweli yanatokea, lakini siyo sahihi kwamba hali ya mauaji haya imekuwa kubwa na inaongezeka zaidi ya ilivyokuwa. Ninasema hivyo kwa uthibitisho wa kitakwimu ambapo takwimu za haraka ukiangalia kwa mfano katika kipindi cha Januari mpaka Aprili, 2016 jumla ya matukio yaliripotiwa yalikuwa ni 1,030 na idadi ya watu waliouawa ni 1,060 ukilinganisha na watu 1,173 katika kipindi kama hicho ambayo ilikuwa kwa matukio 1,153 kwa mwaka uliopita.

Kwa hiyo, inaonekana kuna upungufu wa matukio kama 123 ambayo ni sawa na asilimia 10.7. Hata hivyo punguzo hilo halimaanishi kwamba hatuyachukulii uzito matukio ambayo yanatokea hasa katika kipindi hiki cha karibuni tumeona kulikuwa na matukio yameshamiri kidogo ya mauaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze Bunge lako Tukufu pamoja na kujibu swali la Mheshimiwa Mwamoto kwamba nataka niwatoe wasiwasi wananchi na Wabunge, kimsingi matukio haya ya mauaji yanasababishwa na vyanzo tofauti, kwa mfano kwa haraka haraka nizungumze najua muda ni mfupi lakini asilimia 33 ya matukio ya mauaji ambayo yamejitokeza kipindi cha karibuni ni yanatokana na wizi, 11.6 yanayotokana na ugomvi wa kifamilia, imani za kishirikina asilimia 10.3, wivu wa mapenzi asilimia 7.6, risasi asilimia 6.5, ugomvi wa ardhi asilimia 6.2 na nyinginezo asilimia 24 nukta kadhaa.

Kwa hiyo, utaona kwamba matukio haya ingelikuwa yanatokana na tukio moja tu tungenesema kwamba kuna mtandao hatari labda wa jambo fulani. Hata hivyo Serikali lazima ichukulie kwa uzito kupotea kwa maisha ya raia mmoja iwe kwa chanzo chochote kile. Na ndiyo maana sasa Jeshi la Polisi likafanya kwa mafahikio makubwa kwa haraka sana kuweza kuwakamata watuhumiwa mpaka sasa hivi matukio hayo yaliyotokezea aliyoyazungumza Mheshimiwa Mwamoto kwa karibuni watuhumiwa 72, mpaka sasa hivi ambao wanatupa dalili nzuri ya kuwashughulikia na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendeleo na hiyo kazi na naamini kabisa kazi hiyo ya Jeshi la Polisi itaifanya kwa mafanikio na Waheshimiwa Wabunge na wananchi msiwe na wasiwasi watu wote ambao wamejihusisha katika matukio haya ya mauaji iwe kwa sababu yoyote. Iwe kwa wivu wa mapenzi, iwe kwa ujambazi, iwe kwa ugomvi wa ardhi, iwe kwa kifamilia watatafutwa popote walipo na watachukuliwa hatua za kisheria.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu swali fupi la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Swali langu la nyongeza ni kwamba kwa kuwa sehemu kubwa ya askari wanaolinda maeneo ya Geita hasa maeneo ya pembeni na mgodi wanalinda mawe ambayo hayana thamani na matokeo yake wanakamata watu hovyoy. Ni lini sasa askari hao watatolewa na kwenda kulinda usalama wa raia sehemu nyingine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu Mheshimiwa Naibu Waziri anaomba urudie swali ajalisikia vizuri.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwamba sehemu kubwa ya askari ambao wanalinda maeneo ya kuzunguka Mgodi wa GGM wanalinda mawe ambayo hayana thamani ambayo hata mgodi hawayahitaji, matokeo yake ndiyo wanakamata watu kila siku. Je, ni lini Serikali itaondoa askari hao kwenda kulinda usalama wa raia sehemu nyingine?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, tutalichukua swali lake tuone umuhimu huo kama bado upo, kama utakuwa haupo kama Mbunge anavyoshauri basi tutaondoa kama upo wataendelea kubakia.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 271

Kufufua Shirika la Uvuvi - TAFILO

MHE. MARIAM N. KISANGI (K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE) aliuliza:-

Hapo zamani kulikuwa na Shirika la Uvuvi la TAFILO lenye Makao Makuu yake Kigamboni ambalo lilikufa kutokana na uendeshaji mbovu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua shirika hilo?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kusimamia *deep fishing* ili iweze kunufaika na mapato yatokanayo na uvuvi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri samahani naona kuna watu wawili mmesimama sijaelewa sababu ni nini?

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba 270 umeliruka linalohusu maji.

NAIBU SPIKA: Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Almasi Athuman Maige na hili ni swali la Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 270

Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Tabora

MHE. ALMAS A. MAIGE aliuliza:-

Sehemu kubwa ya Jimbo la Tabora Kaskazini, Uyui haina maji chini ya ardhi na hivyo wananchi hawawezi kupata maji kwa kuchimba visima. Wananchi wanaipongeza Serikali kwa kubuni mradi wa kuleta maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria kupitia Shinyanga, Kahama, Nzega mpaka Isikizya na maeneo mengine ya Mkoa wa Tabora.

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi huo ili wananchi wa jimbo la Tabora Kaskazini katika vijiji vya Isikizya, Upuge, Majengo na Kanyenye wapate huduma ya maji?

(b) Kwa kuwa bomba hilo la maji litatoa maji kwa umbali wa kilometa 25 kuwafikia wananchi wachache. Je, Serikali haioni kuna sababu ya kuanzisha

mradi wa kuchimba mabwawa na kuinga maji ya mvua kama chanzo kingine cha maji kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naona baada ya kupitisha bajeti jana watu wameridhika na maji.

Kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Sikonge pamoja na vijiji 89 vilivyopo ndani ya kilometa 12 kwa kila upende kutoka bomba kuu, vikiwemo vijiji vya Isikizya, Upuge na Majengo. Kwa sasa taratibu za kupata wakandarasi wa ujenzi mradi huo zinaendelea ambapo ujenzi wa mradi unategemewa kuanza mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, kijiji cha Kanyenye utekelezaji wake utajumuishwa katika mipango ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kuboresha huduma ya maji Serikali itaendelea akutenga fedha pamoja na kutafuta vyanzo vingine vya maji ikiwemo ujenzi wa mabwawa na kuweka utaratibu kupitia Halmashauri husika kuvuna maji ya mvua kwa maeneo yote ambayo hayatapitiwa na mradi pamoja na yale yenye shida kubwa ya maji.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa vile umethibitisha kweli kwamba hakuna maji chini Uyui Kaskazini; je, Serikali iko tayari sasa kuanzisha mradi kabambe wa kuchimba mabwawa katika eneo hilo?

Swali la pili, katika kijiji cha Majengo kuna chanzo kizuri cha maji ambacho watu wanateka maji kila siku kwa kuchimba kwa mikono. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda na mimi na Wataalam wake wa maji kuangalia eneo hili kama inaweza kuchimbwa visima virefu ili yapatikane maji ambayo ni salama badala ya haya maji ambayo hayana usalama? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameuliza mabwawa, mabwawa ndiyo sera ya Wizara ya Maji. Maeneo yote ambayo yana matatizo ya ukame na yanapata mvua tumeamua kumaliza tatizo la maji, moja kwa kuvuna maji kutoka kwenye mapaa ndiyo maana tumeagiza Halmashauri ziweke utaratibu kila

wanapopitisha michoro ya nyumba wahakikishe kwamba wanaainisha uvunaji wa maji ya mvua.

Pili, ni sera yetu kwamba tuna hakikisha na tayari tumeshaagiza kila mwaka, kila Halmashauri wahakikishe wanafanya usanifu wa bwawa moja na kuleta maombi ya pesa ili tuweze kuwapa wajenge mabwawa kuhakikisha tunamaliza matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili linalohusu eneo la Majengo, Mheshimiwa amesema kwamba watu wanafukua maji na maji wanayapata. Ikolojia ya ardhi huwa ni ngumu, lakini kwa sababu umetueleza hili naomba nikuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalifanyia kazi, lakini niagize Halmashauri husika waende katika hilo eneo wakaangalie halafu watupe taarifa ili tuweze kuona tunalifanyia nini.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linaongelea suala la visima; na kwa kuwa Tabora Manispaa wananchi walichangia pesa kwa ajili ya uchimbaji wa visima kwa masharti ya mradi lazima kila Kata ichangie pesa ndiyo wachimbiwe. Visima hivyo vilichimbwa maji hayakupatikana.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia na kwa sababu Serikali ilifanya *research* Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia yule mtu aliyefanya *research* na kutupotosha wananchi pamoja na mradi, tuchimbe visima virefu wakati hakuna maji, Serikali ilimchukulia hatua gani? Ili tuweze kujua kwa sababu pesa za Watanzania zimepotea na pesa za mradi? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walichangishwa pesa, utafiti ulifanyika, lakini visima vikachimbwa na havikutoa maji! Kwa bahati nzuri Mkoa wa Tabora ni miongoni mwa mikoa ambayo imepata bahati ya kupata msaada wa Wajapani, Wajapani wana teknolojia ya hali ya juu sana ambayo wao wanaweza wakabaini kama kweli chini kuna maji. Kwa bahati mbaya pamoja na tafiti walizozifanya bado na wao kuna maeneo ambayo wamekosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli teknolojia ya maji chini, bado dunia haijawa nayo. Kwa hiyo, bado tunakwenda kwa kubahatisha. Unaweza ukapima ukakuta maji yapo lakini unakwenda kuchimba unakuta maji hakuna. Vilevile ameuliza kwamba huyu mtu anachukuliwa hatua gani? Huu ni utafiti ulifanyika na kwa bahati mbaya kwamba maji yale hayakupatikana na kimikataba kwa sababu tunafanya kazi kwa kutumia

mikataba kama hatukuweka kifungu kwenye mkataba kwamba kama utakosa maji tutakuchukulia hatua fulani basi huwezi kuchukua adhabu yoyote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, umetutisha kwamba huo utafiti unafanywa lakini ni kubahatisha kwa hiyo maeneo mengi ambayo watu wameahidiwa visima yatakuwa ni yakubahatisha. Hebu tuelezee kidogo hapo kwenye huo utafiti wa visima maana kwenye ile bajeti yenu tuliyopitisha jana habari za visima ziko nyingi sana mle. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwamba tunafanya kwa kubahatisha ila nasema kwamba tunapofanya tunakuwa tumelenga kwamba tutapata maji. Lakini *trend* au historia inaonyesha kwamba mara nyingi unaweza ukafanya utafiti wa visima kumi lakini ukachimba ukapata visima saba, vitatu vikakosa maji ndiyo maana nikatumia hilo neno kubahatisha. Lakini siyo kwamba tunapofanya utafiti tunafanya kwa kubahatisha hapana tunakuwa tumedhamiria kwamba tunafanya utafiti ili tuweze kupata maji, lakini kwa bahati mbaya kutokana na mabadiliko ya miamba kule chini inatokea wakati mwingine unataka kuchimba visima 100 unachimba visima 80 vinapata maji, visima 20 vinakosa, kwa hiyo hatufanyi kwa kubahatisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niongezee kipengele kidogo, ni kwamba tulivyoanza huu mradi wa vijiji kumi, aliyekuwa anafanya utafiti alikuwa ni Mhandisi Mshauri na aliyekuwa anachimba kisima alikuwa ni Mkandarasi. Sasa tumeunganisha kwamba Mkandarasi atapewa mkataba utakaofanya kazi zote za kufanya utafiti na kuchimba. Kwa hiyo, akikosa maji sasa itakuwa ni gharama kwake kutafuta eneo lingine ili kusudi isiwe hasara kwa Serikali. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile Mbunge wa Kigamboni swali lake litauliwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 271

Kufufua Shirika la Uvuvi - TAFICO

MHE. MARIAM N. KISANGI (k.n.y MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE)
aliuliza:-

Hapo zamani kulikuwa na Shirika la Uvuvi la TAFICO lenye Makao Makuu yake Kigamboni ambalo lilikufa kutokana na uendeshaji mbovu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua shirika hilo?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kusimamia *deep fishing* ili iweze kunufaika na mapato yatokanayo na uvuvi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) lilianzishwa mwaka 1974, lengo likiwa ni kuendesha shuguli za uvuvi kibiashara. Aidha, mwaka 1996 TAFICO iliwekwa chini ya iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) kwa ajili ya utaratibu wa ubinafsishaji. Mwaka 2005 TAFICO iliondolewa kwenye orodha ya Mashirika yaliyotakiwa kubinafsishwa na kurejeshwa Wizarani kuendeleza ubinafsishaji wake. Hata hivyo, mwaka 2007 Baraza la Mawaziri lilisitisha uuzwaji wa TAFICO na kuelekeza kuwa mali zisizohamishika ikiwemo ardhi zibaki kwa ajili ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizaru kwa kushirikiana na wadau wengine inaendela na mpango wa kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mapendekezo ya Baraza la Mawaziri kwa hatua husika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusimamia mapato yatokanayo na uvuvi katika ukanda wa uchumi wa bahari, Serikali zetu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa pamoja zilianzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority*) kupitia Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 1 ya mwaka 1998 na marekebisho ya mwaka 2007. Taasisi hii ina jukumu la kusimamia uvuvi katika eneo la Uchumi la Bahari Kuu, ikiwemo utoaji wa leseni kwa meli za kigeni na za ndani zinazovua kwenye ukanda huo. Aidha, mamlaka

inaendelea kufanya doria za anga na kuhuisha mfumo wa kufuatilia meli, kufuatilia vyombo vya uvuvi baharini (*Vessel Monitoring System*) ili taasisi iweze kudhibiti wanaovua bila kulipa leseni. Pia Serikali inaendelea na taratibu za kuwezesha ujenzi wa bandari ya uvuvi ambayo itawezesha meli za kigeni zinazovua bahari kuu kutia nanga hapa nchini na hivyo kuongeza ajira na kipato kwa Watanzania pamoja na Pato la Taifa kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Pamoja na juhudi za Serikali za kuboresha Soko la Samaki la Feri, naipongeza sana Serikali kwa kuwapa hata majiko ya gesi pale katika Soko la Samaki la Feri, mimi kama Mbunge wa Dar es Salaam napongeza.

Kwa kuwa utoaji wa leseni za uvuvi imekuwa ni kero kubwa sana kwa wavuvi kwani wanatakiwa kulipia leseni za uvuvi kila wanapotoka sehemu moja kwenda nyingine.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwaondoshea wananchi kero hiyo ya kulipia leseni za uvuvi kwa kila wanapoenda kuvua?

Swali la pili, kwa kuwa Jimbo la Kigamboni na Mkoa wa Dar es Salaam kwa ujumla umezungukwa na Babari Kuu, na kwa kuwa wavuvi wa Mkoa wa Dar es Salaam, hawana mipango yoyote ya kuboreshewa mazingira ya kazi yao ya uvuvi na Serikali.

Je, Serikali imejipanga vipi kuwasaidia wavuvi wa Kigamboni na Dar es Salaam kwa ujumla katika kuboresha kazi yao ya uvuvi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi,

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kisangi kwa maswali mazuri, kuhusu swali la leseni kutozwa kila wanapovuka mpaka mmoja kwenda mwingine, jambo hili linahusisha Wizara zaidi ya moja, Wizara ya Kilimo tumeandaa waraka ambao tunategemea tutakaa pamoja na wenzetu wa TAMISEMI na wa Wizara ya Fedha, tunategemea jambo hili lipate ratiba hapa kabla ya Wizara ya Fedha ku-*table Finance Bill*, ili kuweza kukubaliana kuhusu mambo haya ya leseni ambazo zinatozwa kwa wingi, hili jambo linaendana sambamba na makato yanayotozwa kwa wazalishaji wetu wa sekta hizi. Hili ni agizo la Mheshimiwa Rais la kuhakikisha kwamba Watanzania wanaofanya kazi zao wanapata tija kutokana na shughuli hizo wanazozifanya kwa kuwaondolea makato mengi

wanayoyapata kutokana na vyanzo mbalimbali kukata kutoka kwenye shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwaboresha mazingira, moja ya mazingira linahusiana na hili alilolisemea la makato, Wizara tumepanga baada ya Bunge hili kukutana na Wavuvi wanaovua katika Jimbo lake na Waheshimiwa Wabunge, tutawakaribisha ili tuweze kupokea mapendekezo yao kuhusu mazingira ambayo tutayaboresha. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Mheshimiwa Keissy swali la nyongeza.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji cha Kipili, Wilaya ya Nkasi, Mkoa wa Rukwa, tulikuwa na Chuo cha Uvuvi, na kulikuwa na *generator* na *cold room*, lakini bahati mbaya awamu zilizokuja ikageuzwa ikawa *secondary school* na uvuvi ukaisha, na sisi watu wa mwambao tunategemea sana uvuvi, hasa mwambao wa Ziwa Tanganyika, na hakuna Chuo:-

Je, ni lini Serikali itakirudisha Chuo cha Uvuvi cha Kipili ili kusaidia wavuvi wetu wa mwambao wa Ziwa Tanganyika?

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, suala alilolisema Mheshimiwa Keissy, Serikali ilikuwa na nia njema kufuatana na mahitaji la kupanua elimu, ikafanya mabadiliko hayo, lakini kwa kuzingatia kwamba Jimbo la Mheshimiwa Keissy wananchi wake wanategemea uchumi wa uvuvi, sisi pamoja na TAMISEMI tutashirikiana kuangalia utaratibu mpya wa kuweza kurejesha utaratibu wa kuwa na chuo ambacho kitasaidia vijana wetu kuweza kujifunza na kuweza kumudu kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili litaendana pia na mpango wa Wizara ya Elimu na Ufundi, ambao unahusisha vyuo vya VETA katika kila Wilaya ili tuweze kupata wanafunzi wengi ambao watafanya kazi kwa utalaam zaidi. Hili jambo linaenda sambamba na Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso wa Jimbo la Pangani ambaye alishaongelea kwamba wananchi wake pia wanahitaji sana kufufuliwa kwa chuo ambacho uchumi mkubwa wa Pangani wa vijana unategemea uvuvi.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 272

Ahadi ya Kuunda Mahakama ya Coroner

MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y MHE. UPENDO F. PENEZA) aliuliza:-

Kufuatia vifo vyenye utata vya kisiasa na vinavyohusisha vyombo vya dola, aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda alitoa ahadi katika Bunge la Kumi ya Serikali kuunda Mahakama ya *Coroner (Coroner's Court)* kwa ajili ya kuchunguza vifo mbalimbali vyenye utata:-

Je, Serikali iko katika hatua gani kutekeleza ahadi hiyo?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na msingi wa swali hili kuwa na utata, napenda ieleweke wazi kuwa uchunguzi wa vifo vinavyotokea katika mazingira yenye utata ambayo sababu zake hazijulikani, hufanywa kwa uchunguzi maalum (*inquest*) na mchunguzi maalum anaitwa *coroner* kwenye Mahakama Maalum ya Uchunguzi (*Coroner's Court*). Utaratibu huu tumekuwa tukiutumia hata kabla uhuru chini ya Sheria ya Uchunguzi Maalum (*Inquests Ordinance*) Sura ya 24. Sheria hii ilifutwa na kutungwa upya kuwa *Inquests Act No. 17* ya 1980 ili kuendana na mazingira mapya ya haki jinai nchini baada ya uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii mpya iliridhiwa na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Mwalimu Julius Nyerere tarehe 21 Mei, 1980, chini ya kifungu cha 5(1) Waziri wa masuala ya Sheria wa wakati huo alitangaza sifa za uteuzi za kuwa *Coroner* na chini ya kifungu cha 5(2) na (3), Jaji Kiongozi kwa kushauriana na Jaji Mkuu, aliwateua Mahakimu Wafawidhi wa Mahakama za Wilaya na za Hakimku Mkazi kuwa *Coroners* au Makorona.

Aidha, kwa tangazo la Serikali Na. 252 la tarehe 16 Julai, 2004, Mahakama za Wilaya na za Hakimku Mkazi ziliateuliwa kuwa Mahakama za *Coroner* pale zinapoketi kwa uchunguzi wa vifo vyenye utata.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo tu mawili ya nyongeza.

Kwanza nikushukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako, ningependa kujua tofauti kati ya hizi Mahakama za kawaida na Mahakama za *Coroner*?

Swali la pili, kwa kuwa hata katika Mkoa wetu wa Iringa, vipo vifo ambavyo huwa vinatokea vyenye utata; je, ni vifo vingapi ambavyo vilipelekea kuundwa hii Mahakama ya Coroner?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ipo tofauti kati ya Mahakama ya Coroner na Mahakama za kawaida za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya.

Kwanza kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Mahakama ya Coroner kazi yake kubwa ni kupata chanzo cha kifo ambacho kimetokea na kina utata, kujua chanzo chake ni nini. Kwa hiyo, hiyo ndiyo kazi kubwa Mahakama ya Uchunguzi inafanywa ikiongozwa na Coroner na ndipo hapo unakuta atatumia madaktari, *ma-pathologist, forensic experts, criminologist* waweze kumsaidia kujua chanzo cha hicho kifo ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya, wao wanakwenda mbele zaidi, wakishapata tukio kwamba limetokea wao sasa wanaangalia vilevile dhamira ya yule aliyetenda hilo kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe ni Mwanasheria na kwa Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wanasheria pia wataelewa lakini naomba nieleze tu kwamba Mahakama za Hakimu Mkazi, wao wanaongozwa na Kanuni ya Sheria inayosema tendo pekee halitoshi kuweza kumhukumu mtu, lazima liendane na dhamira ovu ya yule aliyetenda, yaani *the act alone* haitoshi *it must be accompanied by blameworthy state of mind* na kwa kilatini mnakumbuka mliosoma sheria '*actus non facit reum nisi mens sit rea*'; kitendo pekee hakitoshi. Kwa hiyo, Mahakama ya Hakimu Mkazi kazi yake ni kuangalia kitendo kiendane vievile na dhamira ovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kuhusu swali la pili la matukio yaliyotokea na kwa nini iliundwa hiyo Mahakama. Mheshimiwa naomba tu nikiri kwamba naliona tatizo la elimu kwa umma hapa, kwamba haijatosha na ndiyo maana pengine huduma hii ya Coroner naona Watanzania wengi hawajaiielewa sana. Hili naliona ni tatizo ambalo Wizara yangu sasa nafikiri tutalikazania sana katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba mashauri yanayopelekwa kwa Coroner au kwenye Mahakama hizi yapo, nakumbuka shauri moja ambalo mimi mwenyewe nilihusika ni Shauri Na. 152 la mwaka 2003, lilitokea Mbeya ambapo Mahakama ya Hakimu Mkazi ilika chini ya Coroner ya kuweza kupata ufumbuzi wa kitu kilichotokea katika Kituo cha Polisi na matokeo yake yalikuwa mazuri. Ndiyo maana nimesema kwa kweli ni wajibu wa Wizara hii sasa kuueleweshwa umma vizuri zaidi kuhusu

huduma hii ambayo ipo na hata muuliza swali wa kwanza alidhani kwamba hii mahakama haipo ni huduma ambayo tunafikiria kuianzisha. (Makofi)

Na. 273

Ujenzi wa Barabara ya Geita – Bukoli – Kahama

MHE. STANSLAUS H. NYONGO (K.n.y. MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA) aliuliza:-
Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga barabara ya Geita – Bukoli - Kahama kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) tayari imeanza maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Geita – Bukoli – Kahama yenye urefu wa kilometa 139, kwa kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo. Ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, TANROADS itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali ili barabara hii iweze kupitika majira yote ya mwaka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nyongo swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, ahadi nyingi zinazotolewa na Mheshimiwa Rais, kuanzia Awamu ya Nne na mpaka sasa awamu ya Tano, tunavyotambua ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kama amri.

Je, ni kwa nini ahadi zinazotolewa na Rais wetu hazitekelezeki mapema? (Makofi)

Swali la pili, kuna ahadi vilevile ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne katika Halmashauri ya Mji wa Maswa, ilisemekana kwamba zitajengwa kilometa tatu ilitolewa ahadi na Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete; je, ni lini ujenzi huu utaanza? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wetu wakuu wanapotoa ahadi huwa wanaonesha

dhamira na baada ya hapo utaratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza dhamira hiyo unafuata. Kuchelewa kujenga au kutekeleza ahadi ni kutokana na kukosekana kwa upatikanaji wa fedha na kwa kawaida mara fedha zinapopatikana ahadi huwa zinatekelezwa. Ninamhakikishia hata hiyo barabara analiyoongelea maadamu dhamira ilishaoneshwa ni wajibu wetu tuliopo katika sekta ya ujenzi kuhakikisha dhamira hiyo iliyooneshwa na viongozi wetu wakuu inatekelezwa. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekimbia, Wizara Maliasili na Utalii Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 274

Usalama wa Nchi yetu katika Mpaka wa Mto Kagera na Pori la Akiba Kimisi na Burigi

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU aliuliza:-

Je, Serikali ina uhakika gani na usalama wa nchi yetu katika mpaka wa Pori la Akiba la Kimisi na Burigi na Mto Kagera?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori zilizopo ndani ya Mapori ya Akiba yakiwemo ya Kimisi na Burigi katika kukidhi malengo ya uhifadhi endelevu kwa maslahi ya Taifa. Hii ni pamoja na kupambana na uvamizi wa mifugo, shughuli za kilimo, uharibifu wa mazingira na ujangili ndani ya hifadhi hizo. Aidha, pamoja na ulinzi wa ndani ya hifadhi, eneo la mpaka wa Mto Kagera na Pori la Akiba la Kimisi na Burigi limeonesha kuwa na changamoto zaidi zikiwemo za uhamiaji haramu na uingizaji wa silaha ambazo zinatumiwa kwa ujangili na ujambazi hivyo kulifanya eneo hilo la mpakani kuhitaji ulinzi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama ngazi za Wilaya na Mkoa, kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi kwa upana wake katika eneo hii mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kuimarisha doria ndani ya mapori ili kuboresha uhifadhi wa wanyamapori na kuhakikisha usalama katika maeneo hayo. Aidha, wavamizi wa hifadhi kwa shughuli za

mifugo wanaweza kutumiwa kuhatarisha usalama wa nchi. Hivyo tunatoa rai kwa wananchi na wadau wengine kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika dhana nzima ya ulinzi shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama itaendelea kuimarisha ushirikiano na nchi jirani kuhakikisha ulinzi na usalama wa mipakani unakuwa madhubuti ili kudhibiti madhara yanayotokana na uvamizi wa mifugo na wahamiaji haramu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kanyasu swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpaka wa Tanzania katika eneo la Rusumo mpaka unapoenda Kagera ni hifadhi, lakini mpaka huo kwa upande wa Rwanda ni vijiji ambavyo viko mpaka kwenye Mto Kagera, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba changamoto zilizopo katika hifadhi hiyo ni pamoja na hifadhi hiyo kutumiwa na wahamiaji haramu, watu wanaopitisha silaha na ujambazi.

Je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atahakikisha kwamba eneo hilo linalindwa kwa usalama wa nchi? Hilo swali la kwanza.

Swali langu la pili, katika hifadhi hizo za Burigi na Kimisi kuna Maziwa Ngoma na Maziwa Burigi, ambayo miaka yote yamekuwa yakitumiwa na watu kutoka nchi za jirani kwa uvuvi katika maziwa hayo na kwa ulinzi mkubwa wa askari wa wanyamapori. Ni lini Serikali itaanzisha *seasonal fishing* kwa Watanzania ili waende kuvuna maliasili hiyo?

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza lini Serikali itaimarisha ulinzi kwenye maeneo hayo, nimejibu kwenye swali la msingi, kwamba mpaka sasa hvi tunavyozungumza, changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza katika eneo tunalolizungumzia zimekuwa zikishughulikiwa kwa pamoja kwa ushirikiano baina ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamati ya Ulinzi ya Wilaya, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ameeleza kwamba yapo mashaka ambayo yanaendelea kuongezeka kila siku, basi Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mkoa kuweza kuona namna gani tunaweza kuboresha vizuri zaidi au kufuatilia zaidi ambazo zinaonekana kujitokeza upya kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ni lini, napenda pia nimkumbushe Mheshimiwa Kanyasu kwamba tumesema mara tu baada ya Bunge hili tunapita maeneo yote ambayo yana changamoto za kiulinzi na usalama

kuhusiana na masuala ya mipaka ili tuweze kuboresha vizuri zaidi changamoto za ulinzi na usalama na changamoto za migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mabwawa yaliyopo ambayo yana samaki na kwamba kwa sababu yapo ndani ya hifadhi basi kwa mujibu wa sheria wananchi hawaruhusiwi kufanya uvuvi. Napenda kujibu kwamba sababu za kuzuia kufanya uvuvi zitakuwa ni sababu za kiuhiifadhi, lakini kwa kuwa kuhifadhi maana yake siyo kuacha kutumia maana yake ni kutumia kwa busara na hekima, kuhifadhi maana yake ni kutumia ukijua kwamba ipo kesho na kwamba unaweza ukatumia leo ukijua kabisa kwamba kesho utahitaji kutumia kitu kile unachokitumia leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwa maana ile ya kufanya uhifadhi endelevu tutaliangalia suala hili kuona ni namna gani tunaweza tuka-engage wananchi waliopo katika maeneo haya waweze kufanya uvuvi kama taratibu za kisayansi za uhifadhi zitaruhusu. Lakini tunakwenda kufanya jambo hili kwa pamoja liwe shirikishi ili wote tuone ukweli sasa kwamba kitakachofanyika kiwe kwa maslahi ya Taifa. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali, nitaleta kwenu matangazo machache baada ya matangazo haya Mwenyekiti wa Bunge atakuja kuchukua hii nafasi kwa sababu nina wageni ofisini.

Wageni waliotufikia leo, wapo wageni ambao wamekaa katika Jukwaa la Spika na kundi la kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine P. Mahiga, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa ambao ni Bibi Elizabeth Mahiga - mke wake, karibu sana wifw yetu.

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni Balozi Dkt. Aziz P. Mlima - Katibu Mkuu wa Wizara na pia Balozi Ramadhani Mwinyi - Naibu Katibu Mkuu, karibuni sana. (Makofi)

Wapo pia Mabalozzi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini ambao ni Mheshimiwa Mehdi Aghajafari - Balozi wa Irani, yupo pia Mheshimiwa Zakaria Anshar - Balozi wa Indonesia, yupo pia Mheshimiwa Monica Patricio Clemente - Balozi wa Msumbiji, yupo pia Mheshimiwa Muhia Mudhia - Balozi wa Kenya, tunaye pia Mheshimiwa Jean Pierre Tshampanga Mutamba - Balozi wa Congo, yupo pia Mheshimiwa Saleh Kusa Arze Ceda - Balozi wa Jamhuri ya watu wa Libya, yupo Mheshimiwa Zhang Biao - Naibu Balozi wa China na pia Mheshimiwa Mohammad Dehghani - Naibu Balozi wa Iran. (Makofi)

Wageni wengine ni Mheshimiwa Philip Marmo - Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, yupo pia Ndugu Amir Khan - Mwakilishi wa Balozi wa Pakistani,

Ndugu Preferee Ndayishimiye - Mwakilishi wa Balozi wa Burundi, Ndugu Issa Mugabutsinze - Mwakilishi wa Balozi wa Rwanda, Ndugu Mu Lin - Afisa kutoka Ubalozi wa China na Ndugu Regan Francis Mkalimani wa Balozi wa Congo, karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunalo kundi la tatu la wageni ambao ni Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki ambao ni pamoja na Mheshimiwa Makongoro Nyerere, Mwenyekiti wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki pia ameambatana na Mheshimiwa Bernard Murunya, Mheshimiwa Dkt. Twaha Taslima, Mheshimiwa Angela Kizigha na Mheshimiwa Shyrose Bhanji. Pia wapo wawakilishi kutoka *Trademark East Africa* na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ni Dkt. Josephat Kweka Mkurugenzi Mkazi wa *Trademark East Africa*. Yupo pia Ndugu Wilberforce Mariki - Mkurugenzi wa Mipango Jumuiya ya Afrika Mashariki, karibuni sana. (Makofi)

Wageni wengine ni Mabalozi ambao ni Wakuu wa Idara katika Wizara, Wakurugenzi na Watendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa hao wasimame kwa pamoja, karibuni sana viongozi wetu. (Makofi)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Waziri Kivuli wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa ambao ni Madiwani kutoka Iringa wakiongozwa na Mheshimiwa Alex Kimbe, Meya wa Iringa Mjini, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni kumi wa Mheshimiwa Dkt. Merdad Matogolo Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati na Madini wanaotokea Chama cha Wafanyakazi wa Migodi na Nishati (NUMET) wakiongozwa na Ndugu Albert Machumu ambaye ni Mwenyekiti na Ndugu Nicodemus Kajungu ambaye ni Katibu, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa William Olenasha - Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambao ni wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Huruma iliyopo Mjini Dodoma, karibuni sana.

Vilevile tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Daimu Mpakate wanaotokewa Tunduru Mkoani Ruvuma ambao ni Ndugu Nasra Mpakate - mke wa Mheshimiwa Mbunge na Ndugu Faraja Ngailo ambaye ni shemeji yake, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea ambao ni viongozi wa Serikali ya mtaa wa Makangarawe, Temeke - Mkoani Dar es Salaam, Ndugu Omary Njani - Mwenyekiti wa uwazi na ndugu Juma Kabelwa

Mjumbe. Pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ambao ni wadogo zake wanaotokea Tunduru, Mkoani Ruvuma wakiongozwa na Ndugu Muksini Ubwa ambaye ni mtoto wake, karibuni sana. (Makofi)

Tunao pia wageni watano kutoka Jumuiya ya Wazazi CCM wanaotokewa Mkoa wa Magharibi Unguja wakiongozwa na Ndugu Subira Uruwa ambaye ni Mwenyekiti, karibuni sana.

Tunao pia wageni 54 wa Mheshimiwa Daniel Mtuka ambao ni wanafunzi wanaotokea Shule ya Sekondari Manyoni wakiongozwa na Ndugu Mfaume Kitunga ambaye ni Kaimu Mkuu wa Shule, Ndugu Wilhard Silayo, Mwalimu wa Vifaa vya Miradi na Ndugu Renata Rweyongeza ambaye ni *matron*, karibuni sana. (Makofi)

Pia tunao wageni 61 wa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare wanaotokea Kanisa la KKKT *Cathedral* - Dodoma naona hawapo.

Tuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Juliana Shonza ambaye ni Baba yake mzazi anayetokea Kinondoni, Jijini Dar es Salaam Ndugu Julius Andiel Shonza, karibu sana. (Makofi)

Pia tunaye mgeni mmoja wa Mheshimiwa Hussein M. Bashe ambaye ni Mwanadiplomasia mwakilishi wa Tanzania katika *African Youth Leadership Association* ambaye ni Ndugu Basilla Mwanukuzi, karibu sana. (Makofi)

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya kujifunza na hawa ni wanafunzi 55 kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (St. John's) kilichopo Mjini Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni waliotufikia leo, lakini ninayo matangazo kadhaa mengine. Mkurugenzi wa Idara ya Shughuli za Bunge anawatangazia wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwamba leo Jumanne tarehe 31 Mei, kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi kitakachofanyika katika ukumbi wa Spika, kuanzia saa saba kamili mchana.

Nimeambiwa kuna mgeni hapa alisahaulika kwenye *list* na huyu ni *His Excellence* Roeland Van der Geer, Balozi wa Umoja wa Ulaya, karibu sana. (Makofi)

Tangazo lingine linatoka Idara hiyo hiyo ya Shughuli za Bunge na hili ni kwa Waheshimiwa Wabunge wa Makanisa ya Kiprotestanti yaani CCT mnaombwa wote mnaosali makanisa ya *protestant* yaani CCT kuhudhuria ibada katika jengo la Pius Msekwa leo siku ya Jumanne tarehe 31 Mei, saa saba

kamili mchana baada ya kusitishwa shughuli za Bunge na wengine wote pia mnakaribishwa.

Kuna tangazo lingine linasema napenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Kampuni ya *Treans Water System* ya Uswis ambayo inashughulika na utengenezaji wa mitambo ya kutoa chumvi kwenye maji wapo hapa Dodoma. Kampuni hiyo inatarajiwa kufanya maonyesho kuhusu huduma zao kuanzia tarehe Mosi Juni, 2016 hadi tarehe 4 Juni 2016, kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni katika viwanja vya *Nyerere square*, hivyo Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kwenda kuona teknolojia hiyo ya kutoa chumvi kwenye maji ya visima vyenye chumvi sugu, kuanzia muda wa saa saba mchana katika muda wa mapumziko kabla ya Bunge kurejea saa kumi jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo ninalo jambo moja tu kwa ajili ya wenzetu wa vyombo vya habari kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa adhabu zilizotolewa jana na Bunge zinahusu kosa lililofanywa tarehe 27 Januari, 2016 na Kamati ya Haki, Maadili na Maradaka ya Bunge ilileta maazimio jana.

Kwa hiyo matukio ya kuhusu wananfunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma halijatoa adhabu kwa mtu yeyote. Kwa hiyo kwa ajili tu ya kuwaka kumbukumbu sawa sawa maana wakati mwingine taarifa hazitoki inavyopaswa. Kamati ilikaa, imeleta mapendekezo na Bunge limetoa azimio kwa ajili ya adhabu za jambo lililofanyika mwezi wa kwanza na siyo jana, pamoja na kwamba Kanuni zinaruhusu kiti ama Spika kutoa adhabu jana, Spika hakutoa adhabu yoyote hilo likae vizuri na watu wa vyombo vya habari walipate kwa namna hiyo.

Kwa hiyo, baada ya kuyasema hayo Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Mwenyekiti atakuja kwa ajili ya kuendelea na hoja zinazoendelea. (Makofi)

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika..

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mwongozo wa Spika...

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Mwambalaswa, Mheshimiwa Kasheku. Nani mwingine Mwongozo? Tuanze na Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Nakushukuru, kwa kunipa nafasi niweze kuuliza Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) kwa ruhusa yako naomba nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jambo lililotokea asubuhi hapa Bungeni, nilitaka kupata Mwongozo wako kwamba maana ya posho tunayolipwa ni kusaini na kuondoka ama ni kusaini na kujadili matatizo ya wananchi yaliyotuleta Bungeni? Nilitaka kupata Mwongozo wako Mwenyekiti na kama ni kusaini na kuondoka hata sisi tuna kazi nyingine za kufanya, maana wenzetu wanasaini wanaenda kufanya kazi wana saluni na maduka huko mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka kupata Mwongozo wako. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwambalaswa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwenye *Order Paper* ya leo kuna *item* ya kwanza ni kiapo cha uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiapo ni mkataba mzito sana ambao anayeuingia mkataba huo akiukiuka anachukuliwa hatua au anaadhibiwa. Kwa hiyo, inatakiwa hicho kiapo kiandikwe vizuri kisheria ili kisimletee matatizo anayekiingia kiapo hicho.

Sasa mambo makubwa mawili ambayo yapo kwenye kiapo hicho ni kuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia na kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aliyeapa asuhahi leo ndivyo Wabunge wote tulivyoapa, niseme tu amemaliza hivi kwenye Katiba hiyo kuilinda, kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anamaliza anasema kwa mujibu wa sheria iliyowekwa; kuilinda, kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa. Lakini kiapo hicho hicho wakiapa Serikali hicho hicho mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano na kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano Serikalini wanamaliza hivi iliyowekwa kwa mujibu wa sheria. Wabunge tumeapa hivi kwa mujibu wa sheria iliyowekwa, Serikalini wanaapa iliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahisi kwamba kundi mojawapo limekikosea hiki kiapo na kama limekikosea inabidili liape upya kwa sababu ni mkataba wa misingi mno, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwashukuruni sana kwa miongozo yenu. Suala la Mheshimiwa Mwambalaswa ningeweza kulijibu hapa lakini ngoja nichukue muda kidogo nikalitafakari kwa sababu ile *angle* yako uliyoileta ile ya mwisho, kwa hiyo, acha nichukue nitatoa mwongozo wangu baadae.

Swali la Mheshimiwa Musukuma hili siyo geni, limeshatolewa Mwongozo na Spika, ninachotaka tu ni kusisitiza kwamba Wabunge tupo hapa kufanya kazi iliyotuleta kwa niaba ya Watanzania na siyo kuja tu na kuweka sahihi yako na kuondoka au kuweka dole. Sasa sijaelewa matukio au kilichomsukuma Mheshimiwa Musukuma kusema hivyo, labda yawezekana kwa sababu ninaona ukanda huu upande wangu wa kushoto, ndiyo maana niliuliza leo huku hakuna Mwongozo naona karibu wote hawapo, sasa ningependa nijue kama ndiyo hilo alikuwa anasema, ili tulichukue ili upande wa utawala wakalionene. Lakini sote tunapaswa kutekeleza wajibu wetu, posho yako *you have to earn it* kwa kuifanyia kazi, huwezi tu ukaja hapa nakusema nilikuwa kazini lakini kumbe haupo kwenye shughuli za Bunge kwa maana ya Kamati au nini, kwa hiyo hilo acha tulipate kwa uhakika kama kweli leo ndiyo yanayoendelea hayo. Kwa hiyo, huo ndiyo Mwongozo wangu kwa hilo la pili lakini la kwanza nalichukua tutakuja kulitolea Mwongozo baadaye. Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali, kwamba Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wiraza ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali
kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya
Mambo ya Nje na Ushirikiano wa
Afrika Mashariki**

MWENYEKITI: Ahsante, mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Dkt. Augustine Mahiga.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2016/2017. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa fursa hii adimu ya kuwakilisha mbele ya Bunge lako kwa mara ya kwanza bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kama unavyofahamu, Wizara hii ni mpya baada ya kuunganishwa kwa zilizokuwa Wizara za Mambo ya Mje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa Kwanza wa Wizara hii. Napenda kumwahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa nitatumia ujuzi na uzoefu mkubwa niliouvuna katika nyanja za diplomasia ya kikanda na Kimataifa kuongeza na kuongoza Wizara hii mpya kwa uaminifu na weledi mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia Uchaguzi Mkuu uliyofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake madhubuti na makini unaoakisi kauli mbiu yake ya “Hapa Kazi Tu.” Sisi sote ni mashahidi wa namna uongozi wake ulivyogusa siyo tu wananchi wa Tanzania bali pia ulivyopokelewa na kuwa mfano wa kuigwa katika nchi za Barani Afrika na duniani kwa ujumla. Sifa zake zinasikika kila pembe ya dunia na kutufanya kutembea kifua mbele. Nampongeza sana kwa kumteua Mheshimiwa Samia Suluhu kuwa mgombea mwenza na baadaye kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais, hivyo basi, kuwa mwanamke wa kwanza kuweza kushiriki na kushika wadhifa huo katika historia ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar kwa kipindi cha pili katika uchaguzi ulioendeshwa kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara yangu imefaidika sana na uongozi wao na miongozo mbalimbali wanayoitoa na kuendelea kuitoa katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili Tukufu la Kumi na Moja. Uongozi wa Spika na Naibu wake wa hekima na busara, ni nuru ya pekee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu walionitangulia kuwashukuru na kuwapongeza watoa hoja waliozungumza kabla yangu wakiongozwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge; Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Mbunge; Waziri wa Fedha na Mipango ambao hotuba zao zimeweka msingi

mzuri kwa kuainisha bila ya masuala muhimu ya Kitaifa na Kimataifa ambayo baadhi yake yanaangukia katika majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais kujenga Tanzania ya viwanda na kama ilivyotafsiriwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Wizara yangu nayo imejielekeza katika kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, natangaza diplomasia ya viwanda sambamba na diplomasia ya kilimo na miundombinu. Sera yetu ya Mambo ya Nje lazima iwe kioo kinachoeleza na kufanikisha sera ya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu imefanywa kuwa nyepesi zaidi kutokana na ushirikiano mzuri na ushauri tunaoupata mara kwa mara kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge na Makamu wake Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis, Mbunge, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo. Kwa pamoja wamekuwa ni msaada mkubwa sana kwa Wizara yangu katika utekelezaji wa sera ya mambo ya nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu imejumlisha shughuli zilizokuwa zikifanywa na zilizokuwa Wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. Hivyo nitatolea taarifa ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuwasilisha malengo na mipango ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu ina sehemu kuu saba kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba. Hivyo basi, nitasoma muhtasari wake na ninaomba hotuba hiyo iingizwe kwenye kumbukumbu za Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki hali ya dunia imekuwa ya mchanganyiko wa matumaini na mashaka. Kwa upande wa matumaini, tumeshuhudia kusainiwa kwa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi ya Paris pamoja na kuridhiwa kwa Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 yanayochukua nafasi ya Malengo ya Millennia ambayo utekelezaji wake ulifikia tamati mwaka 2015. *(Makofi)*

Aidha, kwa upande wa mashaka, hali ya usalama duniani imeendelea kutoridhisha kutokana na wasiwasi wa kiusalama kati ya Ulaya Magharibi na Urusi hali tete katika Rasi ya Korea Kusini na kutokana na Korea kaskazini

kuendelea kutengeneza silaha za *nuclear* na kuhatarisha usalama wa Korea Kusini na nchi nyingine jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, vita vinavyoendelea huko nchin Syria na nchi za Mashariki ya Kati na kupanuka kwa shughuli za dhana ya himaya ya *Islamic State* katika eneo lote hilo la ukanda huo na katika nchi mbalimbali kumeongeza hali ya wasiwasi kiusalama duniani pamoja na Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mgogoro wa umiliki wa eneo la Bahari ya Kusini mwa China umeendelea kuhatarisha usalama Barani Asia. Tanzania inaunga mkono msimamo wa China kuhusu kumaliza mgogoro huo kwa njia ya mazungumzo na ushirikiano baada ya nchi na nchi kati ya Kanda hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Jumuiya ya Kimataifa na vyombo vyake kuzingatia azimio Namba 298 la mwaka 1982 la Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari; taarifa ya kina kuhusu hali halisi ya tathmini ya dunia inapatikana katika aya ya 12 hadi 18 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 19 ya hotuba yangu imebainisha malengo makuu yaliyopangwa kutekelezwa kwa upande wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2015/2016. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu hayo, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 170,367,129,238; kati ya fedha hizo shilingi 162,367,129,234 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida; shilingi bilioni nane ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo katika fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 153,698,142,238 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 8,668,987,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara na Balozi zake ilitarajiwa kukusanya maduhuli ya Serikali kiasi cha shilingi 20,036,019,000 hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016 Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 16,296,307,020 ikiwa ni sawa na asilimia 81.3 ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 126,407,697,228 sawa na asilimia 77.8 ya bajeti iliyopitishwa na Bunge; kati ya fedha hizo shilingi 117,783,609,618 ni kwa ajili ya bajeti ya matumizi mengineyo na shilingi 8,628,087,610 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Aidha, Wizara ilitumia kiasi cha fedha kilichopatikana kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Balozi zake, taasisi nyingine na Serikali na sekta binafsi imeendelea kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje yenye lengo la kukuza uchumi kupitia diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilifanikisha kufanya makongamano na maonyesho ya biashara na uwekezaji yaliyolenga kutangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo hapa nchini. Makongamano hayo yalijumuisha wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania na nchi za Oman, Urusi, Rwanda, Ujerumani, China, India, Czech Republic, Comoro na Singapore. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imefanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Sekta za Ujenzi, Uchukuzi, Nishati, Biashara, Viwanda Uwekezaji, Utalii, Kilimo na Mifugo kama inavyoonekana katika aya ya 28 hadi 35 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara iliratibu na kusimamia uwekezaji saini wa mikataba minne kama inavyoonekana katika aya ya 36 na katika hotuba yangu. Aidha, Wizara iliendelea kufuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo ili kusimamia masilahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa katika kipindi hiki, Wizara yangu imeratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 70 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Serikali wa Jumuiya ya Madola na Mkutano wa Kumi wa Nchi Wanachama wa Shirika la Biashara Duniani. Vilevile Wizara yangu iliratibu uridhiwaji wa Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa kina kuhusu masuala ya uridhiwaji wa amani na utiwaji saini wa Mkataba wa Mabadiliko Tabianchi ya Paris, unapatikana katika aya ya 38 hadi 50 na aya ya 76 hadi 79 ya hotuba yangu.

Aidha, katika nyanja za Kimataifa Watanzania wameendelea kupewa nafasi muhimu kwenye Mashirika na Taasisi za Kimataifa ambazo mwezi Februari, 2016 Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa na Bwana Ban Ki-Moon - Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuwa mmoja wa Wajumbe wa jopo la ngazi za juu la Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu masuala ya uwekezaji na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mwezi Januari, 2016 Mheshimiwa Kikwete alichaguliwa kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Jopo la Watu Mashuhuri la Umoja wa Mataifa lenye jukumu la kutoa mwongozo wa ajenda ya akinamama na watoto wakati huu wa mpito kutoka Malengo Milenia kwenda Malengo Endelevu ya 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi wetu na polisi zaidi ya 2,328 wanashiriki katika vikosi vya Umoja wa Mataifa vya kulinda amani katika nchi mbalimbali zenye migogoro. Tanzania itaendelea kuhakikisha kuwa uadilifu na nidhamu vinadumishwa ndani ya vikosi vyetu ili kulinda heshima ya nchi yetu; na kwa hilo angalia lbara ya 42 mpaka 45 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushirikiano Barani Afrika katika kipindi hiki Wizara imeratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 26 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, Mkutano wa Tatu kati ya Afrika na India na Mkutano wa Sita wa Wakuu wa nchi na Serikali za Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika. Maelezo ya kina kuhusu malengo pamoja na maazimio ya mikutano hiyo, yamebainishwa katika aya 54 mpaka 61.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushirikiano na kanda nyingine, Wizara yangu imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri wa Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi kuhusu *Blue Economy* na Mkutano wa Jumuiya za Ukanda wa Maziwa Makuu; maelezo ya kina kuhusu malengo, masuala yaliyojadiliwa pamoja na maazimio yaliyofikiwa yanapatikana katika aya ya 72 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea na juhudi za kuwahamasisha na kuwashirikisha wana-*diaspora* wa Tanzania waishio maeneo mbalimbali duniani katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu. Jitihada hizo zimeleta mafanikio katika nyanja za uwekezaji, biashara, kubadilishana uzoefu, elimu na ujenzi. *Diaspora* waliopo katika nchi mbalimbali kama vile Australia, Botswana, Marekani, Oman na Thailand wamekuwa mstari wa mbele katika kutafuta fursa za biashara, elimu pamoja na kutangaza utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu ushiriki wa Watanzania walioko ughaibuni katika maendeleo ya nchi yetu, yanapatikana kuanzia aya ya 80 mpaka ya 86 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Wizara iliendelea kusimamia na kuratibu masuala ya itifaki ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu kinga,

upendeleo na haki za Kibalozi kwa Wanadiplomasia waliopo nchini kulingana na mkataba wa Vienna wa mwaka 1961. Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuratibu masuala ya itifaki na uwakilishi, kuanzishwa na kusimamia huduma za Kikonseli, aya ya 87 mpaka 100 zinabainisha taarifa ya kina kuhusu utekelezaji wa masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi karibuni limeongezeka wimbi la Watanzania wanaojishughulisha na biashara ya madawa ya kulevya. Inasikitisha sana kuona zaidi ya Watanzania 408 wamekamatwa ughaibuni wakituhumiwa na kufungwa kwa makosa ya kubeba na kuingiza madawa ya kulevya katika nchi hizo. Wengi wamefungwa katika nchi za CAhina, Hongkong, Afrika Kusini, Thailand, Iran, nchi za Ulaya na Marekani kwa makosa hayo. Jina zuri la nchi yetu limetiwa doa na Watanzania hao wanaofanya biashara hiyo haramu. Serikali ya Awamu ya Tano, itaendelea na juhudi zake kupambana na janga hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge hili, natoa wito kwa Watanzania wenzangu na jamii kwa ujumla kushirikiana na Serikali katika vita hivi ili kuepusha Taifa letu na aibu kuu nje ya nchi na kunusuru maisha ya vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya itifaki kwa viongozi wetu, Wizara yangu inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kutazama upya sheria itakayoweza viongozi ambao hawajatajwa na sheria hii kupatiwa pasi za kidiplomasia. Katika zoezi hili, tutapendekeza Muswada mpya uletwe hapa kwenye Bunge hili Tukufu ili kuboresha huduma za itifaki ikiwa ni pamoja na kutoa pasi hizo kwa wenza wa viongozi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Wizara iliajiri watumishi 42, kubadilisha kada mtumishi mmoja, kupandisha vyeo watumishi 59 na kuthibitisha kazini watumishi 15. Aidha, ulifanyika uteuzi wa Mabalozi kuiwakilisha nchi yetu katika nchi za Uholanzi, Malawi, Kuwait, Japan, Uingereza na Zimbabwe. Vilevile Wizara imeendelea kutekeleza mpango wa mafunzo wa miaka mitatu ambapo watumishi 43 walihudhuria mafunzo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imewarejesha nyumbani Mabalozi watano na watumishi tisa baada ya kustaafu na wengine kumaliza muda wao wa kufanya kazi Ubalozi. Aidha, Wizara iliwapelekea vituoni Mabalozi wanne katika vituo vya Lilongwe, Harare, Kuwait na Tokyo; Naibu Mawaziri watatu katika vituo vya Kampala, Pretoria na Stockholm na watumishi 30 waliopolekwa katika vituo mbalimbali. Zoezi la kuwarudisha Mabalozi na watumishi wanaostaafu na wanaomaliza muda wao na kupeleka mbadala wao ni endelevu na Wizara itaendelea kuitekeleza kadri inavyopata fedha. Katika zoezi hili, idadi ya Maafisa na wafanyakazi kwenye Balozi zetu na hasa wale wenyeji itapungua ili kupunguza matumizi na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inasimamia Taasisi tatu ambazo ni Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini, Jijini Dar es Salaam, Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha ambacho pia kinasimamia Kituo cha Mikutano wa Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Dar es Salaam. Taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli za taasisi hizo, imebainishwa katika aya 109 hadi 116 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza utekelezaji wa majukumu kwa upande wa Mambo ya Nje, naona sasa nieleze Bunge lako Tukufu kwamba aya ya 117 inaeleza majukumu makuu manne yaliyopangwa kutekelezwa kwa upande wa Afrika Mashariki katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu hayo katika mwaka wa fedha 2015 na 2016, iliyokuwa Wizara hiyo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 26,666,486,300; kati ya fedha hizo shilingi 24,047,468,300 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 2,614,968,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi. Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kimejumuisha mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kiasi cha shilingi 18,570,055,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 19,003,440,560 sawa na asilimia 71 ya fedha zote zilizotengwa; kati ya fedha hizo, shilingi 15,506,375,000 zilitumika kulipa mchango wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Shilingi 1,689,936,100 zilitumika kulipa mishahara ya watumishi na shilingi 1,807,129,700 zilitumika kutekeleza shughuli za Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umepiga hatua kubwa ambapo nchi wanachama wa Jumuiya zimekubaliana kutekeleza masuala mbalimbali kwenye nyanja za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kwa kiasi fulani kisiasa. Lazima tuwe makini katika kila hatua zinazopigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa, Jumuiya yetu ilianzishwa rasmi Julai, 2000 baada ya nchi Wanachama kukamilisha na kuridhia Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliotiwa saini na Wakuu wa Nchi Wanachama tarehe 30 Novemba, 1999. Nchi hizo zilikuwa Tanzania, Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 Rwanda na Burundi zilijiunga na Jumuiya na mwaka huu Sudan ya Kusini nayo imejiunga kwenye Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi hizi sasa zinamaanisha kuwa eneo lote la nchi sita za Jumuiya ya Afrika Mashariki lenye zaidi ya watu milioni 160, kimsingi limeungana katika nyanja mbalimbali na hivyo kutoa motisha ya ushindani mkubwa wa ndani ya Jumuiya na kubainisha na kwa manufaa ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa Tanzania ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiye Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo na kwa kupitia Wizara yangu ameelekeza Wimbo na Bendera ya Jumuiya zitumike hapa nchini sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa kuongezwa kwa matumizi ya Bendera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye Ofisi za Umma nchini zikiwemo na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Taasisi za Umma na sisi wenyewe Wabunge na Magari yetu na ofisi zenu huko katika Majimbo yenu. Bendera za Taifa letu Tukufu pamoja na za *East Africa* zitasambazwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natoa rai kwa Taasisi za Serikali na vyombo vya habari viweze kutumia wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pale ambapo Wimbo wa Taifa letu Tukufu unapigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa hatua hii itasaidia kuwajengea Watanzania uelewa zaidi wa Jumuiya yetu na hatimaye waweze kujiandaa kushiriki na kupata manufaa yanayotokana na fursa zilizopo za kibiashara, kiuchumi, kiuzalishaji, kijamii na kitamaduni na kwa kuzingatia uwepo wa soko kubwa la Afrika Mashariki na fursa nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 7 ya mkataba wa uanzilishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inasisitiza kuwa na ninanukuu: "Jumuiya yetu hii imejengwa katika wananchi na ushirikiano wa Kimataifa" Mwisho wa nukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtangamano huu unaendelea na juhudi za Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, katika kuhakikisha kuwa Jumuiya hii inaleta manufaa kwa wananchi wetu kwa kutumia fursa za ushirikiano katika kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 17 wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Mikutano na wa 32 na 33 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Malengo na maazimio ya mikutano hiyo yameainishwa katika aya ya 125 hadi 127 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya 128 hadi 138 zinabainisha masuala mbalimbali yaliyotekelezwa katika hatua mtengamano wa Afrika Mashariki ambapo ni Umoja wa Fedha, Soko la Pamoja na Shirikisho la Kisiasa la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu na miradi ya Kitaifa yenye sura ya kulinda iliyocainishwa katika mipango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya kutoa huduma kwa pamoja mipakani; uendelezaji wa mtandao wa barabara na uainishaji wa uzito wa magari. Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji huo wa programu hiyo na miradi hiyo ni kama ilivyoainishwa katika aya 146 hadi 160 ya hotuba yangu.

Aidha, kiambatisho Na. 5 kinabainisha hatua iliyochukuliwa katika ujenzi wa vituo vya utoaji huduma kwa pamoja mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliratibu ushiriki wa Watanzania katika ushindani na uandishi wa Insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki lililoshirikisha wananfunzi wa shule za sekondari kutoka nchi tano wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kijana wetu Mtanzania, Simon Mollel Sabaya kutoka shule ya sekondari ya Mzumbe aliibuka mshindi kwa kuwa wa kwanza katika shindano hilo. Huu ni ushindi mkuu kwa vijana wetu na kuonyesha kwamba wanaweza na wana uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya Jumuiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi kwa kijana huyu na kuwatia moyo vijana wengine waendeleo kushiriki kwenye mashindano haya ili waweze kuliletea sifa Taifa letu na pamoja kuitangaza Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki imehamia rasmi katika Makao Makuu yake yaliyopo Zanzibar. Hii ni kufuatia kusainiwa kwa mkataba wa uwenyeji baina ya Jumuiya ya Muungano wa Tanzania na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 28 Disemba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imepata Katibu Mkuu mpya ambaye ni Balozi Libérat Mfumekeko kutoka Jamhuri ya Burundi, atakayeiongoza Jumuiya kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Aidha, naomba kumshukuru Balozi Dkt. Richard Sezibera kutoka Jamhuri ya Rwanda kuwa

Katibu Mkuu wa Jumuiya aliyemaliza kipindi chake cha miaka mitano ya uongozi kwa mchango wake mkubwa katika kuindeleza Jumuiya yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki ambapo Bunge hilo lilijadili na kupitisha Miswada ya Sheria ya Jumuiya, Maazimio na Taarifa mbalimbali kama yalivyoonyeshwa katika aya za 173 hadi 175 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kutekeleza mkakati wake wa Mawasiliano unaobainisha njia za kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa mbalimbali zilizopo katika Jumuiya na jinsi ya kutumia fursa hizo. Maelezo ya kina yanapatikana katika aya 184 hadi 186 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kuimarisha uwezo wa utendaji wa utekelezaji mpango mfupi na mrefu wa mafunzo kama inavyoonekana katika aya ya 184 na 187 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zilizokuwa Wizara za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ziliendelea kupata hati safi za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza watendaji wa Wizara na kuwahimiza waendeleo kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote wa maendeleo kwa moyo wao wa kujitolea katika kufanikisha majukumu mbalimbali na kwa mchango wao mkubwa na urafiki kati yao na sisi katika kufanikisha utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu imepanga kutekeleza malengo makuu kumi kama yalivyoainishwa katika aya ya 193 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu haya, Wizara imepangiwa bajeti ya kiasi cha shilingi 151,396,775,775; kati ya fedha hizo, shilingi 143,396,775,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 8,000,000,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika bajeti ya matumizi ya kawaida shilingi 133,056,021,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 10,370,754,000 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za matumizi mengineyo shilingi 720,160,000 ni kwa ajili ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala katika Bara la Afrika. Shilingi 3,154,721,000 ni kwa ajili ya fedha za mishahara na matumizi

mengineyo ya Chuo cha Diplomasia na shilingi 686,298,374 ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika fedha za Bajeti ya Maendeleo ya kiasi cha shilingi 8,000,000,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kiasi cha shilingi 2,375,250,000 zitatumika kufanikisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara ambapo ni sehemu ya Kituo cha Mikutano wa Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Dar es Salaam; shilingi 1,316,435,000 zitatatumika kukamilisha ukarabati wa jengo la ghorofa tisa ambalo yako kwenye makazi ya Balozi na Mkuu wa Utawala Ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji; shilingi 2,172,880,000 zitatumika kukarabati makazi ya Balozi, watumishi yaliyopo Stockholm, Sweden; shilingi 1,113,871,000 zitatumika kukarabati majengo mawili yanayomilikiwa na Serikali yaliyopo Khartoum, Sudan na shilingi 321,564,000 kwa ajili ya kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Wizara na Balozi za Tanzania huko nje. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara kupitia Balozi zake, unatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 24,001,150,000 kama maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyotajwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya shilingi 151,396,775,000; kati ya fedha hizo shilingi 143,396,775,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 8,000,000,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante kwa uwasilisho wako Mheshimiwa Waziri. Hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA MHESHIWIWA BALOZI DKT. AUGUSTINE PHILIP MAHIGA (MB),
WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI
AKIWASILISHA MAKADIRIO YA BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI YA
WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017-
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nakushukuru kwa fursa hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, naomba nitumie nafasi hii adhimu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015.

3. **Mheshimiwa Spika**, naungana na walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake madhubuti na makini unaoakisi kauli mbiu yake ya 'Hapa Kazi Tu'. Sisi sote ni mashahidi wa namna uongozi wake ulivyogusa si tu wananchi wa Tanzania bali pia ulivyopokelewa na kuwa mfano wa kuigwa katika nchi za bara la Afrika na duniani kwa ujumla. Sifa zake zinasikika kila pembe ya dunia na kutufanya tutembeke kifuu mbele. Nampongeza sana kwa kumteua Mheshimiwa Samia Suluhu kuwa Mgombea Mwenza na baadae kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya nchi yetu. Kuchaguliwa kwake kumeidhihirishia dunia hatua kubwa ambayo nchi yetu imepiga katika kumpa fursa sawa mwanamke.

4. **Mheshimiwa Spika**, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kipindi cha pili katika uchaguzi ulioendeshwa kwa amani na usalama. Kadhalika, nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara yangu imefaidika sana na uongozi wao na miongozo mbalimbali wanayoitoa katika utekelezaji wa majukumu yetu.

5. **Mheshimiwa Spika**, niungane na wenzangu walionitangulia kuwashukuru na kuwapongeza watoa hoja waliozungumza kabla yangu wakiongozwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango ambao hotuba zao zimeweka msingi

mzuri kwa kuainisha dira na masuala muhimu ya kitaifa na kimataifa ambayo baadhi yake yanaangukia katika majukumu ya Wizara yangu. Kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais kujenga **'Tanzania ya Viwanda'** na kama ilivyotafsiriwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021, Wizara yangu nayo imejielekeza katika kutekeleza **'Azma ya Serikali ya kujenga Uchumi wa Viwanda'**.

6. **Mheshimiwa Spika**, kama unavyofahamu, Wizara hii ni mpya baada ya kuunganishwa kwa zilizokuwa Wizara mbili za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa ajili hiyo, namshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa kwanza wa Wizara hii. Napenda kumuahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa nitatumia ujuzi na uzoefu mkubwa niliouvuna katika nyanja za diplomasia ya kikanda na kimataifa kuendelea kuipaisha diplomasia ya Tanzania.

7. **Mheshimiwa Spika**, k a z i yangu imefanywa kuwa nyepesi zaidi kutokana na ushirikiano mzuri na ushauri tunaoupata mara kwa mara kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mheshimiwa Balozi Adadi Mohammed Rajab (Mb), na Makamu wake Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis (Mb) pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo. Wamekuwa wa msaada mkubwa sana kwa Wizara yangu katika utekelezaji wa majukumu.

8. **Mheshimiwa Spika**, ukiniona nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kujiamini ni kwa sababu ninao nyuma yangu viongozi wenzangu, watendaji na wafanyakazi wanaonisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Susan Alphonse Kolimba, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Aziz Ponary Mlima, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Balozi Ramadhan Muombwa Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mabalozi, Maafisa na Wafanyakazi walioko Makao Makuu, Balozini na Ofisi ya Zanzibar kwa msaada mkubwa wanaonipatia. Uzalendo wao, ari yao na imani yao kwangu, vinanipa kila sababu ya kuamini kuwa malengo tuliyojiwekea katika Bajeti hii tutayatekeleza kwa ufanisi mkubwa.

9. **Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si mwisho kwa umuhimu, namshukuru kwa dhati mke wangu mpendwa Mama Elizabeth Mahiga, Watoto na familia yangu yote kwa ujumla kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kunipa utulivu wa kutosha kuniwezesha kuyakabili majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais kutimiza matarajio ya Watanzania.

10. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa, naungana na Wafanyakazi wa Wizara yangu kutoa salamu za pole na rambirambi kwa familia za Watumishi wenzetu watatu, Marehemu Manfred Ngatunga,

Marehemu Apolonia Mbogo Mwangosi na Marehemu Ezekiel Makonda, ambao walifikwa na mauti wakati wakiendelea kuitumikia Wizara na Taifa kwa ujumla. Tuendelee kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani. Amina.

11. **Mheshimiwa Spika**, hotuba hii imejumuisha shughuli zilizokuwa zikifanywa na iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hivyo, nitatoa taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

TATHMINI YA HALI YA DUNIA

Hali ya Uchumi, Siasa na Usalama Duniani

12. **Mheshimiwa Spika**, hali ya dunia imeendelea kuwa ya mchanganyiko wa matumaini na mashaka. Katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita dunia imepiga hatua kwenye masuala kadhaa ya msingi kwa ustawi na mustakabali wa dunia. Katika kipindi hiki tumeshuhudia kusainiwa kwa Mkataba wa Paris kuhusu Tabianchi mwezi Desemba, 2015 ambao umesubiriwa kwa muda mrefu. Kusainiwa kwa Mkataba huu kunatoa matumaini kwa nchi za Afrika na zile zinazoendelea kwa kuwepo kwa uhakika katika Kudhibiti na Kukabili athari na changamoto za tabianchi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa nchi zetu zinaathirika zaidi na athari za tabianchi wakati ni wachangiaji wadogo sana wa tatizo hilo. Kusainiwa kwa Mkataba huu kunatoa fursa kwa nchi maskini kufidiwa na kujengewa uwezo katika kukabiliana na changamoto hizo. Hili ni jambo ambalo nchi yetu imekuwa mstari wa mbele kulipigania na Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliongoza jitihada hizi akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

13. **Mheshimiwa Spika**, jambo lingine la kutia matumaini ni kusainiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo yanachukua nafasi ya Malengo ya Milenia ya mwaka 2000 - 2015 ambayo utekelezaji wake ulifikia tamati mwezi Septemba, 2015. Majadiliano kati ya nchi zetu yaliyofikia malengo haya yalizingatia uzoefu katika utekelezaji wa Malengo ya Milenia, haja ya kumaliza viporo vya Malengo ya Milenia na umuhimu wa kuhakikisha kuwa malengo mapya yanazingatia mahitaji ya leo na kesho kwa kuhakikisha kuwa ni endelevu. Malengo ya Maendeleo Endelevu ndio mwongozo wa agenda ya maendeleo duniani kote na ndiyo yatakayokuwa rejea ya majadiliano na makubaliano mengine duniani. Sisi tumejipanga vyema kutekeleza malengo hayo na bahati nzuri yanashabihiana kwa kiwango kikubwa na Dira yetu ya Taifa ya 2025 na Mpango wa Pili wa Maendeleo 2016/2017 – 2020/2021.

14. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita kumekuwa pia na matukio ambayo yana mwelekeo mzuri kwa ustawi wa amani na usalama duniani. Kwa kuwa yako mengi, niruhusu niyataje mawili makubwa. Kwanza, ni hatua ya nchi za Marekani na Cuba kuamua kurejesha urafiki wao baada ya kuwepo kwa vikwazo vya Marekani dhidi ya Cuba kwa zaidi ya miaka 50. Hatua hii ni muhimu na tunaungana na wapenda amani kote duniani kumpongeza Rais Barack Obama wa Marekani na Rais Raul Castro wa Cuba. Ikumbukwe kuwa Marekani na Cuba ni rafiki wa Tanzania, na Tanzania imekuwa mstari wa mbele kupinga vikwazo vya Marekani dhidi ya Cuba. Ni faraja kuwa uhasama huo umekwisha, kwani kuondolewa kwa vikwazo vya Marekani dhidi ya Cuba kutawezesha Cuba kushiriki kikamilifu katika uchumi wa Dunia, na hali kadhalika itaimarisha ushirikiano mzuri wa kiuchumi tulionao kati yetu na Cuba. Makubaliano hayo yamemaliza mabaki ya misugvano ya vita baridi ya miongo ya nyuma na kuendeleza amani duniani.

15. **Mheshimiwa Spika**, tukio la pili, ni kuondolewa kwa vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Iran kuhusu Mpango wa Iran wa Nyuklia tarehe 16 Januari, 2016, kufuatia Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki kuthibitisha kuwa Iran imekamilisha hatua zote ilizopewa na Wanachama wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Ujerumani. Hatua hii nayo ni muhimu sana kwa kuwa inaondoa hali ya mashaka iliyokuwa imetanda katika eneo la Mashariki ya Kati kuhusu nchi ya Iran kutengeneza silaha za nyuklia. Mashaka hayo ndiyo ambayo yamekuwa yakiyumbisha sana dunia kiuchumi kwa kuathiri bei za mafuta. Iran ni nchi rafiki ambayo tunashirikiana nayo kiuchumi. Hivyo, kuondolewa kwa vikwazo hivyo kunatoa fursa ya kukua kwa ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi hizi mbili katika mazingira ya amani.

16. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na matumaini hayo, yako matukio na mambo ambayo yanaiweka dunia katika hali ya tahadhari. Hali ya uchumi duniani haijaimarika sana na inapitia katika mashaka makubwa. Hii inatokana na sababu kadhaa zikiwemo kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi mkubwa wa China kutoka asilimia 6.9 hadi asilimia 6.3; kushuka kwa bei ya bidhaa duniani kama dhahabu, mafuta, shaba na bidhaa nyingine muhimu; na kupungua kwa mitaji na uwekezaji. Kuteremka kwa bei ya mafuta hakujaleta unafuu sana kwetu kwa sababu bei ya bidhaa zetu muhimu kwenye soko la dunia nazo zimeporomoka na thamani ya fedha imepungua. Aidha, riba ya mikopo na mitaji imepanda. Hali hii si afya kwa uchumi wa nchi masikini na zinazoendelea kwa kuwa kushuka kwa bei ya bidhaa kunaathiri sana uchumi wa nchi zetu zenye uwezo mdogo wa kuhimili misukosuko ya uchumi wa dunia.

17. **Mheshimiwa Spika**, hali ya usalama duniani nayo imeendelea kutoridhisha. Kumekuwepo na kuongezeka kwa wasiwasi wa kiusalama kati ya Ulaya Magharibi na Urusi, Korea Kaskazini na nchi za Asia hasa Korea Kusini inayosaidiwa na Marekani, Syria na nchi za Mashariki ya Kati na kupanuka kwa

shughuli na dhana ya himaya ya *Islamic State* katika eneo lote la ukanda huo. Dhana hiyo inayosimamiwa katika eneo lote na kundi la *Islamic State of Syria* (ISS) imeanza kujipenyeza Afrika Mashariki, Magharibi na Kaskazini hasa Lybia. Dhana ya himaya hiyo au *Caliphate* ni kali zaidi kuliko mlengo wa Al - Qaeda. Dunia inaelekea tena kwenye ushindani mkali wa mataifa makubwa hasa kati ya Marekani, Urusi na China. Kwa muktadha huo, Tanzania itaendelea kufuata siasa isiyofungamana na upande wowote. Yote haya kwa pamoja yanaiweka dunia katika hali ya tahadhari kubwa na hivyo kuilazimu dunia kuelekeza fedha na muda wake mwingi katika ushindani na kutafuta ufumbuzi badala ya kuelekeza muda na rasilimali hizo kujenga uchumi na kuinua hali ya maisha ya watu. Tanzania imeendelea kutoa mchango wake wa moja kwa moja na kwa kushirikiana na nchi nyingine katika kutatua migogoro ya Kanda na kudumisha amani duniani. Kwa mantiki hiyo, Mheshimiwa Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete aliteuliwa kuwa Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Afrika katika Mgogoro wa Libya na Mheshimiwa Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa aliteuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa Msuluhishi wa Mgogoro wa Burundi. Uteuzi wa Viongozi wetu Wastaafu wa Kitaifa ni ushahidi kuwa kauli ya Tanzania inasikilizwa na kuheshimika kwenye majukwaa ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika.

18. **Mheshimiwa Spika**, Macho na masikio ya dunia yameelekezwa huko Asia-Pacific kutokana na fukuto la mgogoro wa umiliki wa eneo la Bahari ya Kusini mwa China unaohusisha nchi za China, Brunei, Vietnam, Malaysia na Ufilipino. Pamoja na kuwa kijiografia eneo hili laweza kuonekana ni mbali sana na nchi yetu, athari za mgogoro huo zitagusa kila pembe ya dunia kama hautamalizika kwa njia za amani. Eneo hilo ndio penye kitovu kikubwa cha ukuaji wa uchumi, uzalishaji na biashara katika kipindi hiki ambacho uchumi wa dunia kiu jumla unasuasua. Tanzania inaamini kuwa njia ya uhakika ya kumaliza mgogoro wa Bahari ya Kusini mwa China ni kupitia mazungumzo baina ya nchi na nchi na kanda. Kwa sababu hiyo, tunaunga mkono juhudi za utatuzi wa mgogoro huo kwa njia ya mazungumzo na mashauriano. Tunaitaka Jumuiya ya Kimataifa na vyombo vyake kuzingatia Azimio Na. 298 la mwaka 1982 la Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 ILIYOKUWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

19. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kueleza utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2015/2016, naomba uniruhusu niainishe kwa ufupi majukumu ya iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kama ifuatavyo:-

- i. Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje;

- ii. Kusimamia Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa;
- iii. Kuratibu Masuala ya Uhusiano baina ya Tanzania na nchi mbalimbali, Ushirikiano wa Kimataifa, Bara la Afrika na Kikanda;
- iv. Kulinda na kuendeleza Maslahi ya Taifa ya Kiuchumi na Mengineyo nje ya nchi;
- v. Kusimamia masuala yanayohusu Kinga na Haki za Kibalozi kwa Wanadiplomasia waliopo nchini kulingana na Mkataba wa Vienna wa mwaka 1961;
- vi. Kusimamia na kuratibu masuala ya Itifaki na Uwakilishi;
- vii. Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli;
- viii. Kuratibu shughuli za Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano; na
- ix. Kusimamia utawala na Maendeleo ya Utumishi Wizarani na kwenye Balozi zetu.

20. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu hayo kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilitengewa kiasi cha Shilingi 170,367,129,238.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 162,367,129,238.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 8,000,000,000.00 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida, shilingi 153,698,142,238.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 8,668,987,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi.

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara na Balozi zake ilitarajia kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi 20,036,019,000.00. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2016, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 16,296,907,020.00 ikiwa ni sawa na asilimia 81.3 ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

22. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 126,407,697,224.00 sawa na asilimia 77.8 ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo Shilingi 117,783,609,614.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 8,624,087,610.00 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi. Hadi hivi sasa, Wizara bado haijapokea mgao wowote wa fedha za bajeti ya maendeleo.

23. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje

24. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Balozi zake, Taasisi nyingine za Serikali na sekta binafsi imeendelea kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje yenye lengo la kukuza uchumi wa nchi kupitia diplomasia ya uchumi iliyo endelevu. Aidha, jukumu hili limepewa uzito zaidi na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati alipozindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo aliziagiza Balozi zetu kushiriki Mikutano inayofanyika nje kwa niaba ya Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali. Jukumu hili kubwa limetekelezwa ipasavyo na Balozi zetu na hivyo kupunguza gharama kubwa za safari ambazo zingefanywa na Watumishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

25. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa hapa nchini kutoka nchi za Vietnam na Msumbiji. Wizara pia iliratibu ziara za viongozi mbalimbali kutoka nchi za Saudi Arabia, Oman, Qatar, Ujerumani, Norway, Umoja wa Falme za Kiarabu, Sweden, Finland, Ireland, Czech, Italia, na Urusi. Pamoja na mambo mengine ziara hizo zililenga kuimarisha, mahusiano ya biashara na uwekezaji kati ya nchi yetu na nchi hizo. Aidha, baadhi ya nchi hizo tayari zina mikataba ya Ushirikiano na Tanzania na nyingine zimeanzisha ushirikiano kwa mara ya kwanza.

26. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilifanikisha kufanyika makongamano na maonesho ya biashara na uwekezaji yaliyolenga kutangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo hapa nchini. Makongamano hayo yalijumuisha wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania na nchi za Oman, Urusi, Rwanda, Ujerumani, China, India, Czech, Comoro, Misri na Singapore.

27. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na makongamano hayo, Tanzania iliweza kutangaza fursa zake mbalimbali katika biashara na uwekezaji na kufanikisha yafuatayo:-

(a) Kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya ushirikiano baina ya Chama cha Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima Tanzania na Chama cha Wafanyabiashara wa Oman wa kuanzisha Kampuni ya Uwekezaji kati ya Tanzania na Oman. Kampuni hiyo imeanzishwa kwa lengo la kutafuta fursa za uwekezaji Tanzania na Oman na imeazimia kuanza na mtaji wa Dola za Marekani milioni 25 ambazo zitatumika kutoa mikopo kwa wawekezaji. Mkataba huo ulisainiwa mwezi Aprili 2016, Dar es Salaam wakati wa Kongamano la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Oman;

(b) Serikali ya Oman pia imeanza mazungumzo na kiwanda cha sukari Kagera kwa nia ya kuingia makubaliano yatakayowezesha Serikali ya

Oman kuwekeza katika kiwanda hicho. Hatua hii inalenga kukiwezesha kiwanda kuzalisha tani laki nne za sukari ambazo zitauzwa hapa nchini na hivyo kupunguza tatizo la upungufu wa sukari. Ongezeko hili la uzalishaji pia litawezesha kuzalisha hamira, spiriti na umeme. Hamira itauzwa Oman na sehemu nyingine wakati umeme utaingizwa katika gridi ya taifa; na

- (c) Kuanzishwa kwa Kiwanda cha utengenezaji wa pikipiki katika eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi wa Bagamoyo kupitia Kampuni ya Guangzhou Fekon Motorcycle Co. Ltd. ya China. Aidha, Kampuni hiyo imeahidi kufungua Chuo maalum kwa ajili ya mafunzo ya ufundi wa pikipiki na makenika. Vilevile, mwekezaji huyo ameahidi kutoa nafasi kwa ajili ya vijana wa Tanzania kwenda China kupata ujuzi wa masuala hayo katika kiwanda mama kilichopo China. Makubaliano hayo yalifanyika wakati wa kongamano la biashara na uwekezaji baina ya Afrika na China lililofanyika mwezi Agosti 2015 mjini Guangzhou China.

28. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje imefanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta za miundombinu, nishati, viwanda, kilimo na mifugo. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni pamoja na:-

(a) Mradi wa barabara ya Ndundu-Somanga yenye urefu wa kilomita 60 uliozinduliwa mwezi Agosti, 2015. Barabara hiyo imejengwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait kwa kushirikiana na Mfuko wa Umoja wa Nchi zinazozalisha Mafuta Duniani na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Kidahwe-Uvinza yenye urefu wa kilomita 76.6 uliozinduliwa mwezi Septemba, 2015. Barabara hiyo imejengwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 57 pamoja na mchango wa fedha za ndani;

(c) Mradi wa Daraja la Kikwete kwenye mto Malagarasi mkoani Kigoma lililozinduliwa mwezi Septemba, 2015. Daraja hilo limejengwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Uchumi wa Jamhuri ya Korea;

(d) Mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu cha Tengeru, Arusha kilichozinduliwa mwezi Agosti 2015 ambao ulitekelezwa kwa ushirikiano na Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu; na

(e) Mradi wa ujenzi wa bandari mpya ya Bagamoyo na Eneo Huru la Kiuchumi uliozinduliwa Oktoba 2015. Mradi huo utatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania, China na Oman.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine Wizara imeendelea kuzungumza na kuwashawishi wadau mbalimbali wa maendeleo ili kusaidia jitihada za Serikali katika kukabiliana na changamoto ya ujangili hapa nchini, hususan upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya kufanyia doria kwenye Mbuga na Hifadhi za Taifa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi hiki, Serikali ya Ujerumani imeipatia Tanzania ndege mbili ndogo kwa ajili ya kupambana na ujangili. Tunaamini kuwa ndege hizo zitaongeza ari na ufanisi kwa askari wetu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kuendesha doria katika Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba yaliyopo nchini. Vilevile, nchi nyingi za Ulaya, Marekani na Mashirika ya Kimataifa kama vile *World Wildlife Fund*, *Frankfurt Zoological Society* zimeonyesha utayari wa kuisaidia Tanzania kwa hali na mali katika kulinda hifadhi za wanyamapori.

30. **Mheshimiwa Spika**, Kadhalika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, imefanikisha majadiliano na Serikali ya Ufaransa kwa ajili ya kusaidia mpango wa maboresho ya jengo la abiria (*Terminal II*) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo imekubali kuipatia Serikali ya Tanzania kiasi cha Euro Milioni 65 kwa ajili ya ukarabati na uboreshaji wa uwanja huo.

31. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeendelea kutafuta fursa za masomo nje ya nchi ili kuliwezesha Taifa kuwa na hazina kubwa ya wataalam katika sekta mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa nchi rafiki za Algeria, Malaysia, Indonesia, Pakistan, Iran, Malta, Misri, Sri Lanka, Brunei Darussalam, Canada, Ujerumani, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Ubelgiji, Oman, Urusi, Australia, Japan, China, Cuba, Ufaransa, Thailand, Uswisi na Korea pia zimeendelea kushirikiana nasi katika kuwajengea uwezo Watanzania kupitia ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali.

32. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeratibu na kufanikisha upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 20 kutoka Serikali ya Italia, kupitia Shirika la Maendeleo la nchi hiyo. Mkopo huo utatumika kutekeleza mradi wa *Technical and Labour Market Support Programme* unaolenga kuimarisha na kukuza elimu ya Ufundi kwa kuvijengea uwezo vyuo vya ufundi ili kutoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko la ajira. Vyuo vitakavyonufaika na mradi huo ni pamoja na Chuo cha Ufundi Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.

33. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na juhudi za kuwatafutia fursa za ajira na kuwaandalia mazingira mazuri watanzania wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi. Kufuatia Mkataba wa ajira baina ya Tanzania na Qatar, Watanzania wapatao 250 wamekwenda Qatar kufanya kazi kuanzia mwezi Desemba, 2015. Timu za pande zote mbili zinaendelea na uratibu wa kuwapata Watanzania watakaoweza kunufaika na fursa hiyo. Aidha, Wizara pia inaendelea kuwasaidia Watanzania kupata kazi katika makampuni mbalimbali nje ya nchi mathalani katika Mashirika ya Ndege yanayofanya safari zake hapa nchini. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Watanzania 18 walipata kazi katika Shirika la Ndege la Emirates na jitihada kama hizo zinaendelea kufanyika kwa mashirika mengine. Nichukue fursa hii kutoa wito kwa vijana wa Tanzania kujitokeza na kuomba kazi katika Mashirika ya Kimataifa.

34. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kufanikisha makubaliano kati ya Tanzania na Poland yaliyofanyika mwezi Oktoba 2015, ambapo Poland ilikubali kutoa mkopo wa masharti nafuu wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 110. Makubaliano hayo yatawekwa saina baina ya Shirika la Maendeleo la Taifa kwa upande wa Tanzania na kampuni ya URSUS ya Poland. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Dola za Marekani milioni 55 zitatumika kwa ajili ya uanzishaji kiwanda cha kuunganisha matrekta hapa nchini yanayotengenezwa na kampuni hiyo. Chini ya makubaliano hayo kampuni hiyo itafundisha vijana wetu kuunganisha na kutengeneza matrekta. Aidha, kiasi cha Dola za Marekani Milioni 55 kitatumika kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya kuhifadha mazao. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa miradi hii miwili utaanza hivi karibuni.

35. **Mheshimiwa Spika**, katika suala zima la utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo katika Diplomasia ya Uchumi, Tanzania itaendelea kujenga mahusiano ya karibu na mashirika mbalimbali ya kimataifa kama vile Benki ya Dunia; mashirika yasiyo ya kiserikali yenye nguvu za kiuchumi na kisiasa; na makampuni ya kimataifa ya mafuta, nishati, mawasiliano na miundombinu ili kupata mitaji na teknolojia inayohitajika nchini kwetu.

Kusimamia Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa

36. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara iliratibu na kusimamia uwekwaji saina wa mikataba ifuatayo:-

(a) Hati za Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali za Sri – Lanka, Serbia, Ghana, Malta, Qatar, Kuwait na Morocco kuhusu masuala ya Usafiri wa Anga yaliyotiwa saina mwezi Oktoba, 2015;

(b) Hati ya Makubaliano kati ya Wizara na Taasisi ya Maendeleo ya Miundombinu kuhusu kuendeleza viwanja na nyumba zinazomilikiwa na Serikali nje ya nchi, uliwekwa saini tarehe 08 Desemba, 2015 – Dar es Salaam;

(c) Mkataba wa Uenyeji kati ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kuhusu Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yaliyoko Zanzibar. Mkataba huo uliwekwa saini tarehe 28 Desemba, 2015; na

(d) Mkataba wa Ushirikiano kati ya Tanzania na Ufalme wa Saudi Arabia katika nyanja za uchumi, biashara, uwekezaji, michezo na vijana uliosainiwa tarehe 24 Machi, 2016.

37. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo ili kusimamia maslahi ya nchi.

Kuratibu Masuala ya Uhusiano baina ya Tanzania na nchi mbalimbali, Ushirikiano wa Kimataifa, Bara la Afrika na Kikanda Ushirikiano wa Kimataifa

Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030

38. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2015 utakumbukwa sana na Jumuiya ya Kimataifa kutokana na makubaliano na maamuzi muhimu ya kimataifa yaliyofikiwa. Miongoni mwa makubaliano hayo ni kupitishwa kwa Ajenda Mpya ya Maendeleo kwenye Mkutano Maalum wa Umoja wa Mataifa wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika New York, Marekani mwezi Septemba, 2015. Katika Mkutano huo, viongozi hao walikubaliana kuwa na dira mpya ya maendeleo ya dunia ijulikanayo kama Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 yenye jumla ya Malengo 17 na shabaha 169. Ajenda hii mpya ya maendeleo endelevu inarithi Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya miaka 15 yaliyomalizika mwaka 2015.

39. **Mheshimiwa Spika**, malengo hayo yamejikita katika kutokomeza umaskini; kuhifadhi mazingira; kupambana na mabadiliko ya tabianchi; na kushirikisha makundi yote kwenye jamii katika masuala ya maendeleo. Ninajivunia kuwa Tanzania ilitoa mchango mkubwa sana katika ngazi mbalimbali kipindi chote cha majadiliano yaliyopelekea kupatikana kwa malengo hayo na hivyo kuhakikisha kuwa vipaumbele vya nchi vinakuwepo kwenye Ajenda hiyo mpya ya Maendeleo. Tanzania ilikuwa ni miongoni mwa nchi 30 zilizounda Kikundi Kazi kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu ambacho ndicho kilichopendekeza malengo hayo.

40. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Malengo hayo umeanza rasmi mwezi Januari mwaka huu na napenda kuliifu Bunge lako Tukufu kuwa malengo hayo yameshaingizwa kwenye mipango mbalimbali ya maendeleo ya nchi ili kuendana na vipaumbele vyetu hasa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021) uliowasilishwa kwenye Bunge lako Mwezi Aprili 2016 na Waziri wa Fedha na Mipango.

41. **Mheshimiwa Spika**, inazidi kubainika katika Jumuiya ya Kimataifa kuwa moja ya vikwazo vikubwa vya maendeleo ni rushwa na ufasidi. Uongozi wa Awamu ya Tano umezidi kutambulika duniani na kusifiwa kwa ujasiri wa kupambana na janga la rushwa. Tanzania ilikuwa moja ya nchi na mashirika makubwa 40 duniani yaliyokaribishwa na Mheshimiwa David Cameroon, Waziri Mkuu wa Uingereza kushiriki Mkutano uliojadili juu ya mkakati mpya wa pamoja duniani wa kupambana na rushwa. Mkutano huo ulifanyika London, Uingereza mwezi Mei, 2016 ambapo Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Majaliwa alipata nafasi ya kufafanua hatua mbalimbali za kisiasa, kisheria na utawala ambazo Serikali ya Tanzania inachukua katika kupambana na tatizo hilo sugu la rushwa na pia kuonyesha ushirikiano wa kitaifa katika kuimarisha juhudi hizo.

Usimamizi wa Amani Duniani

42. **Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa masuala yanayoiletea heshima kubwa nchi yetu ni suala la ulinzi na utetezi wa amani na usalama kwenye ukanda wetu na sehemu mbalimbali duniani. Hadi sasa Tanzania imepeleka askari, wanawake kwa wanaume zaidi ya 2,328 kwenye misheni saba tofauti za kulinda amani za Umoja wa Mataifa na bado tunaendelea kufanya hivyo. Tunayafanya yote haya kwa kuwa tunaamini amani ndiyo msingi wa maendeleo na ustawi wa binadamu. Pia, tunatimiza wajibu wetu kama sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa katika kuhakikisha kuwa dunia inakuwa sehemu nzuri na salama ya kuishi.

43. **Mheshimiwa Spika**, Taifa linajivunia sana Askari wetu wanaofanya kazi hizo za kulinda amani kwani pamoja na kushambuliwa mara kadhaa, wamekuwa wakiifanya kazi hiyo kwa umahiri, kujitoa, bidii na weledi mkubwa. Ndiyo maana haishangazi kuona Watanzania mbalimbali wakiwa wanateuliwa kushika nyadhifa za juu kwenye misheni hizo za kulinda amani. Ninatoa pongezi za pekee kwa askari wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Polisi na raia walioshiriki kwa vipindi mbalimbali katika vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika.

44. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na askari hawa wazalendo, hivi karibuni tumepokea tuhuma kwamba baadhi ya askari wetu wamehusika kudhalilisha kijinsia wanawake huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Tanzania ilizichukulia tuhuma hizi kwa uzito mkubwa sana na iliunda timu ya uchunguzi kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania ndani ya siku tano badala ya siku kumi zinazotakiwa na Umoja wa Mataifa baada ya Nchi husika kupokea taarifa za tuhuma. Tuhuma hizi zimeisikitisha sana Serikali na endapo zitathibitika hatua kali za kinidhamu dhidi ya wale wote waliohusika zitachukuliwa. Ili kuhakikisha kuwa vitendo kama hivyo vinaepukwa siku zijazo, Tanzania itajiunga na kusimamia kikamilifu *“Kigali Principles”* ambazo ni mwongozo wa jumla kwa nchi zinazopeleka askari wa kulinda amani kwenye vikosi vya Umoja wa Mataifa.

45. **Mheshimiwa Spika**, maendeleo ya kisayansi na teknolojia yamesababisha kuongezeka kwa hali ya uhatarishi kutokana na mbinu za kiuhalifu zinazotumiwa na wahalifu wenye mitandao ya kimataifa. Mathalan, tumeshuhudia ongezeko la tishio la ugaidi Afrika Mashariki, biashara haramu ya dawa za kulevya, uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi na mzunguko wa silaha ndogondogo. Wizara yangu kupitia Jumuiya za Kikanda na Kimataifa na ushirikiano tulionao na nchi zilizondelea, tunaratibu jitihada za kitaifa za kukabiliana na uhalifu wa kimataifa. Kwa mfano, kupitia Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Nchi Wanachama wa SADC uliofanyika Gaborone, Botswana mwezi Agosti, 2015 Nchi Wanachama zilikubaliana kuandaa Mkakati wa SADC wa kukabiliana na Ugaidi, Mkakati wa SADC wa kukabiliana na ujangili na Mkakati wa SADC wa kukabiliana na uzagaji wa silaha ndogondogo.

46. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza jitihada za kupambana na uharamia baharini, Wizara iliratibu ushiriki wa Serikali katika Mkutano wa Tatu wa Majadiliano ya Bahari ya Hindi uliofanyika mwezi Machi, 2016 nchini Indonesia. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huo ulijadili changamoto zinazoukabili Ukanda huo ikiwemo vitendo vya uharamia, uhalifu wa kutumia silaha, usafirishaji haramu na ugaidi wa majini ambavyo vinaathiri maendeleo ya uchumi. Kutokana na kuwepo kwa changamoto hizo, Mkutano ulifikia Makubaliano yajulikanayo kama *Padang Consensus* yanayozitaka Nchi Wanachama kuandaa mikakati mbalimbali kwa kutumia sheria za kimataifa zilizopo katika kupambana na vitendo hivyo haramu. Tanzania imejipanga kutekeleza makubaliano hayo kupitia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Majini iliyo chini ya Uenyekiti wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu.

47. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni mhanga wa biashara haramu ya silaha ndogondogo kutokana na kuzungukwa na nchi zenye machafuko hasa kwenye Ukanda wa Maziwa Makuu. Kutokana na kuwepo kwa hali hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikichukua hatua madhubuti za kukabiliana na changamoto hiyo ikiwemo kutunga sheria na kanuni za kudhibiti

biashara hiyo haramu; kuweka alama silaha zinapoingizwa nchini na kuzisajili; na kuchoma silaha haramu. Jitihada hizi pia zinafanyika kimataifa ikiwemo kusaini mikataba mbalimbali kama vile Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Biashara ya Silaha. Aidha, jitihada hizi zinapewa nguvu zaidi na lengo la 16 la Agenda 2030 ya Maendeleo Endelevu ambalo linazitaka nchi kupunguza ufadhili na usambazaji haramu wa silaha ndogondogo ifikapo mwaka 2030.

Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Paris

48. **Mheshimiwa Spika**, katika miaka ya hivi karibuni tumekuwa mashuhuda wa athari za mabadiliko ya Tabianchi yanayosababisha kuwepo kwa ongezeko la ukame; mvua nyingi zinazoleta mafuriko; kuzama kwa baadhi ya visiwa; vimbunga na tufani kubwa; kupotea kwa baadhi ya mimea na wanyama na kuongezeka kwa kina cha bahari. Hali hii sio tu inapoteza maisha ya binadamu wengi na mali zao, bali pia inaturudisha nyuma kwenye jitihada zetu za maendeleo na kutokomeza umaskini. Ni kwa msingi huo, Tanzania kama ilivyo nchi nyingi zinazoendelea imeunga mkono kupatikana kwa Mkataba mpya unaolenga kudhibiti mabadiliko ya tabianchi. Mkataba huo ulikubaliwa wakati wa Mkutano wa 21 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Paris, Ufaransa mwishoni mwa mwaka 2015. Mkataba huo tofauti na mingine iliyopita una mamlaka ya kisheria kuzibana nchi zilizoendelea na zenye viwanda vingi kupunguza gesijoto.

49. **Mheshimiwa Spika**, Mkataba huo uliokubaliwa na nchi zote, ulitiwa saini tarehe 22 Aprili, 2016 kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, New York na nchi 175 zikiwemo zile kubwa ambazo zilikuwa zikipinga Mikataba iliyopita. Tanzania ilikuwa ni miongoni mwa nchi zilizotia saini Mkataba huo. Naomba nichukue fursa hii kuzisihi nchi zote hasa zile zilizoendelea na zinazotoa gesijoto kwa wingi kuheshimu makubaliano hayo ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kuitunza dunia yetu kwa manufaaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Aidha, ninawaasa Watanzania wote kulinda misitu yetu, uoto asilia na wanyamapori wetu kwa manufaa ya Taifa letu.

50. **Mheshimiwa Spika**, sitaweza kuhitimisha hoja hii ya Mkataba wa Paris bila kumpongeza binti wa Kitanzania, Getrude Clement, mwenye umri wa miaka 16 ambaye alipata nafasi ya kulihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa niaba ya vijana duniani wakati wa hafla ya utiaji saini Mkataba huo. Ninaona fahari kuwa nafasi hiyo alipewa mtoto wa Kitanzania miongoni mwa vijana wengi duniani kutokana na uwezo mkubwa alionao. Binti huyo ameliletea heshima Taifa na napenda kutumia nafasi hii kuwasihia watoto na vijana wengine hapa nchini kuweka jitihada kwenye masomo na shughuli zao wanazozifanya ili siku moja nao wapate nafasi kama hizi na kupeperusha vizuri bendera ya Taifa. Mtoto huyu awe mfano kwa kizazi kipya cha Watanzania ambao watakuwa makini katika kulinda urithi wa mazingira yetu.

Uteuzi wa Watanzania kwenye Mashirika na Taasisi za Kimataifa

51. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na mahusiano mazuri tuliyonayo na nchi nyingine, Watanzania wameendelea kupewa nafasi muhimu kwenye mashirika na taasisi za kimataifa. Suala linalozidi kuipa sifa nchi yetu na kuthibitisha imani iliyowekwa na Jumuiya ya Kimataifa kwa nchi hii na watu wake.

52. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Februari 2016, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa na Bw. Ban Ki-moon, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuwa mmoja wa wajumbe wa Jopo la Ngazi za juu la kumshauri Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Masuala ya Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi. Aidha, mwezi Januari 2016, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa kuwa Mwakilishi wa Umoja wa Afrika kwenye utatuzi wa mgogoro wa Libya. Uteuzi wa Mhe. Kikwete unalenga kusaidia juhudi za Umoja wa Afrika katika kurejesha amani na utulivu nchini Libya kwa kutumia uzoefu wake. Pia katika mwezi huo wa Januari, Mhe. Kikwete, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti mwenza wa Jopo la Watu Mashuhuri la Umoja wa Mataifa lenye jukumu la kutoa mwongozo wa agenda ya kina mama na watoto wakati huu wa mpito kutoka Malengo ya Milenia kwenda Malengo ya Maendeleo Endelevu.

53. **Mheshimiwa Spika**, uteuzi haukuishia tu kwa viongozi hawa wa Kitaifa, Watanzania wengine pia wameendelea kuchaguliwa na kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali kubwa kwenye Mashirika na Taasisi za Kimataifa. Hawa ni pamoja na Dkt. Agnes Kijazi, Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani; Bw. Gabriel Rugalema ambaye ameteuliwa kuwa Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani nchini Sierra Leone; Profesa Kennedy Gastorn ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam Kitivo cha Sheria, alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Mashauriano ya Masuala ya Kisheria katika nchi za Asia na Afrika nafasi ambayo ataanza kuitumikia mwezi Agosti 2016; na Balozi Wilfred Ngirwa alichaguliwa kuendelea na nafasi yake ya Mwenyekiti Huru wa Baraza la Shirika la Chakula na Kilimo Duniani. Pia, Bw. Donatius Kamamba, alichaguliwa kuwa Mjumbe kwenye Kamati ya Urithi wa Dunia ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni na Dk. Frannie Leautier alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Kuratibu Masuala ya Ushirikiano Barani Afrika Umoja wa Afrika

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Ubalozi wetu wa Addis Ababa, Ethiopia, imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika shughuli

mbalimbali za Umoja wa Afrika. Mwezi Januari 2016, Tanzania ilishiriki kwenye Mkutano wa 26 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo. Kaulimbiu ya mkutano huo ilikuwa ni “Mwaka wa Haki za Binadamu Afrika, hususan Haki za Wanawake”. Wakati wa uzinduzi wa kaulimbiu hiyo, Nchi Wanachama zilihimizwa kuridhia na kutekeleza Itifaki na sera mbalimbali zilizoundwa na Umoja huo kwa lengo la kulinda, kukuza na kutekeleza haki za wanawake Afrika. Itifaki hizo ni pamoja na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Sera ya Umoja wa Afrika kuhusu Masuala ya Jinsia. Mkutano huo pamoja na masuala mengine pia ulijadili ripoti ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kuhusu hali ya amani na usalama Barani Afrika.

55. **Mheshimiwa Spika**, mwezi Novemba, 2015 Tanzania iliteuliwa na Umoja wa Afrika kusimamia uzinduzi wa Jeshi la Pamoja la Afrika la Kulinda Amani Barani Afrika. Mimi mwenyewe nilisimamia uzinduzi huo. Tanzania vilevile iliendelea kutoa mchango wake katika kutafuta suluhu ya migogoro barani Afrika. Tanzania ikiwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ilieleza hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutatua mgogoro wa Burundi. Mchango wa Tanzania katika Umoja wa Afrika kuhusu mgogoro wa Burundi kwa kiasi kikubwa uliweza kusaidia Umoja huo kuwa na taswira mpya ya namna ya kutafuta suluhu ya kudumu ikiwemo kutoa kipaumbele katika mazungumzo yanayohusisha pande zinazohasimiana nchini Burundi chini ya usimamizi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki badala ya uamuzi wa awali wa kupeleka majeshi ya Umoja huo nchini Burundi.

56. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa vipindi viwili mfululizo kuanzia mwaka 2012 hadi mwezi Januari, 2016. Hii inatokana na mchango wake mkubwa katika kusuluhisha migogoro barani Afrika. Katika uchaguzi wa wajumbe wapya wa Baraza hilo uliofanyika mwezi Januari 2016, Kenya, Rwanda na Uganda zilichaguliwa kuwakilisha ukanda wa Afrika Mashariki.

Mkutano wa Tatu wa Ushirikiano kati ya Afrika na India

57. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Tatu wa Ushirikiano kati ya Afrika na India, uliofanyika New Delhi, India mwezi Oktoba, 2015. Katika Mkutano huo, pamoja na masuala mengine, India iliahidi kuisaidia Afrika katika kuendeleza miundombinu; umwagiliaji; kuongeza thamani ya rasilimali; kuanzisha viwanda; na teknolojia ya habari na mawasiliano. Aidha, Serikali ya India iliahidi kutoa mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za Marekani bilioni 10, ruzuku ya misaada ya Dola za Marekani milioni

600 na kuchangia Dola za Marekani milioni 100 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo. Vilevile, India iliahidi kutoa nafasi 50,000 za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Afrika nchini India kwa miaka mitano ijayo. Ili kunufaika na fursa hizi, nchi za Afrika zinatakiwa kuwasilisha andiko la miradi mbalimbali ya vipaumbele kwa Serikali ya India.

58. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kufuatia mkutano huo, tayari Serikali imeandaa na kuwasilisha miradi ya kipaumbele ikiwemo miradi 17 ya maji pamoja na Mradi wa Serikali Mtandao. Aidha, miradi mingine itakayowasilishwa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa atamizi kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati katika kila mkoa; mradi wa ujenzi wa reli itakayotumika kusafirisha abiria katika Jiji la Dar es Salaam; na mradi wa kilimo cha umwagiliaji – Zanzibar.

Mkutano wa Sita wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika

59. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Sita wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika uliofanyika mwezi Desemba 2015, Jijini Johannesburg, Afrika Kusini. Katika mkutano huo Serikali ya China ilitangaza mpango mpya wa miaka mitatu kuanzia 2016 hadi 2018 wa ushirikiano kati ya China na Afrika ambao umeweka kipaumbele katika kuendeleza sekta ya viwanda barani Afrika. Tanzania ni miongoni mwa nchi nne za mfano zilizochaguliwa na China kwa ajili ya kujenga viwanda vya mfano. Nchi nyingine zilizomo kwenye mpango huo ni Afrika Kusini, Ethiopia na Kenya.

60. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Mpango huo, Serikali ya China imetangaza kutenga Dola za Marekani bilioni 10 kwa ajili ya kuendeleza sekta ya viwanda barani Afrika. Aidha, China itatoa nafasi 40,000 za mafunzo ya kuwajengea waafrika stadi za ufundi nchini China na nafasi 200,000 kwenye nchi zao; kutuma wataalam wa China katika nchi za Afrika kwa ajili ya kutoa ushauri wa namna ya kutekeleza programu ya viwanda; na kujenga vyuo vya ufundi vya kikanda kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa viwandani.

61. **Mheshimiwa Spika**, ili kunufaika na Mpango huo, Serikali ya Tanzania imebainisha na kuwasilisha miradi ya kipaumbele ambayo ni Ujenzi wa Reli ya Kati katika kiwango cha kimataifa; ujenzi wa miundombinu wezeshi ya reli, barabara, kina cha bandari, umeme, gesi na maji katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bagamoyo; Ujenzi wa mtandao wa kusambaza gesi katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani (Bagamoyo na Mkuranga); Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume – Zanzibar; na Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri – Zanzibar.

Kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda

Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu

Mikutano ya Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu.

62. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika Livingstone, Zambia mwezi Agosti, 2015. Mkutano huo ulipokea taarifa kutoka Nchi Wanachama kuhusu hatua zilizofikiwa katika kuridhia na kutekeleza Itifaki za Jumuiya ya nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu hususan Itifaki nne zinazopewa kipaumbele katika utekelezaji wake kwa sasa. Itifaki hizo ni; Itifaki ya Ushirikiano wa Kiulinzi; Itifaki ya Ushirikiano wa Kimahakama; Itifaki ya Kuzuia Uvunaji Haramu wa Maliasili na Itifaki ya Kuzuia Unyanyasaji wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto. Mkutano huo ulibaini itifaki hizo hazijatekelezwa kikamilifu na nchi zote wanachama. Hivyo, nchi wanachama zilikubaliana kutekeleza itifaki hizo kikamilifu.

63. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Itifaki hizo Serikali imechukua hatua mbalimbali zikiwemo kutunga Sheria ya kudhibiti uhalifu wa njia ya mawasiliano; Sheria ya kurudishiana wahalifu waliokimbilia nchi nyingine; kuanzisha vitengo maalum katika viwanja vya ndege vya Kimataifa nchini ili kudhibiti usafirishaji holela wa Maliasili; kuanzisha Mpango wa Mataifa wa kuwalinda wanawake na watoto dhidi ya unyanyasaji wa kujinsia na kuanzisha kitengo maalum katika vituo vya polisi Wilaya zote nchini kushughulikia kesi za uonevu wa kijinsia.

64. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia iliratibu ushiriki wa wataalamu wa Tanzania katika Mkutano wa Jumuiya ya Nchi za Maziwa Makuu uliofanyika Luanda, Angola mwezi Januari, 2016. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika Mkutano huo ni kutathmini hali ya ulinzi na usalama katika nchi za eneo la Ukanda wa Maziwa Makuu hususan katika nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Sudan Kusini. Pamoja na mambo mengine Jumuiya hiyo imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na Taasisi za Kikanda katika kuratibu shughuli za kutatua migogoro. Kwa mfano, mgogoro wa Burundi kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki, mgogoro wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa kushirikiana na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika pamoja na mgogoro wa Sudan Kusini kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ushirikiano wa Maendeleo ya Nchi za Mashariki na Pembe ya Afrika.

65. **Mheshimiwa Spika**, Jumuiya hiyo ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu ambayo Tanzania ni mwanachama inatambua uhusiano mkubwa uliopo kati ya uvunaji haramu wa rasilimali na kushamiri kwa migogoro. Hivyo, nchi wanachama zimesaini Itifaki ya Ulinzi, Usalama na Maendeleo pamoja na

Itifaki ya Kupinga Uvunaji Haramu wa Rasilimali ambazo kwa pamoja zinazitaka nchi zote 12 wanachama kutii taratibu zinazotambulika kikanda za uvunaji rasilimali ambapo Cheti ya Kikanda cha kuthibitisha uvunaji huo hutolewa. Hii kwa kiasi kikubwa imesaidia kudhibiti makundi ya waasi kujipatia fedha kwa njia za uvunaji haramu wa rasilimali kwa lengo la kufadhili shughuli zao.

66. **Mheshimiwa Spika**, jitihada hizo za pamoja zimepelekea kutengamaa kwa hali ya ulinzi na usalama katika nchi za maziwa makuu. Kwa mfano, idadi ya wakimbizi wanaoingia nchini imepungua kutoka kati ya wakimbizi 200 hadi 300 kwa siku kwa mwezi Novemba, 2015 hadi kufikia wakimbizi kati ya 100 hadi 120 kwa siku kwa mwezi Mei, 2016. Hadi sasa Tanzania inahifadhi jumla ya wakimbizi 136,000 kutoka Burundi na wengine 2,360 kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Bado idadi hii ni kubwa na Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wengine katika jitihada za kutatua migogoro katika ukanda wetu wa Maziwa Makuu ili hatimaye wakimbizi hao waweze kurejea nchini mwao.

Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika

Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika

67. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika mwezi Agosti 2015 Gaborone, Botswana. Mkutano huo ulijadili masuala ya siasa, uchumi, uwekezaji, kijamii, ulinzi na usalama katika Kanda.

68. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Mkutano huo kuiteua Tanzania kuwa Makamu Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama wa Jumuiya hiyo, Nchi Wanachama ziliazimia yafuatayo:-

i. Serikali ya Lesotho pamoja na washirika wengine wa kisiasa nchini humo kuandaa mapema iwezekanavyo mpango wa utekelezaji wa mabadiliko ya Katiba na Sekta ya Ulinzi;

ii. Kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ongezeko la uwakilishi wa wanawake katika nafasi mbalimbali za maamuzi ya juu Serikalini na sekta binafsi;

iii. Kutekeleza kikamilifu Sera ya Kilimo ya Kanda na Itifaki zingine ili kusaidia kuongeza kasi ya uzalishaji, biashara na ushindani katika sekta ya kilimo; na

iv. Sekretariati kufuatilia kwa karibu kwa kushirikiana na Nchi Wanachama kuhakikisha UKIMWI na magonjwa mengine ya kuambukiza hayaendelei kuwa tishio kwenye Sekta ya Afya katika Kanda.

69. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na nchi yetu kujijengea sifa ya umahiri na weledi katika masuala ya siasa, ulinzi na usalama barani Afrika na katika Kanda, katika mkutano huo, Tanzania iliteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Asasi ya SADC ya Siasa, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha mwaka 2015/2016. Kutokana na uteuzi huo, Tanzania kwa mara nyingine itakuwa Mwenyekiti wa Asasi hiyo katika kipindi cha Agosti 2016 hadi Agosti 2017 ikiwa ni mara ya tatu kupewa wadhifa huo. Uteuzi huu unaonyesha imani ya wanachama wa SADC waliyonayo kwa Tanzania katika kutatua migogoro na kusimamia amani katika kanda hiyo na unaendelea kujijengea nchi yetu heshima kubwa na kuiweka juu katika medani za Kikanda na Kimataifa.

Mkutano wa dharura wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika wanaosimamia Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama

70. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania ilishiriki kwenye Mkutano wa Dharura wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika wanaosimamia Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama uliofanyika Gaborone, Botswana tarehe 18 Januari, 2016 kwa ajili ya kujadili hali ya kisiasa nchini Lesotho. Ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huo ulielekeza Serikali ya Jamhuri ya Lesotho kutoa kwa umma ripoti ya Tume Huru ya Uchunguzi ya SADC na kuhakikisha kuwa inatekeleza kwa uadilifu mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo ili kuboresha hali ya siasa, ulinzi na usalama nchini humo. Vilevile, Viongozi Wakuu walisisitiza umuhimu wa kusimamia kwa dhati utekelezaji wa Mikataba yote mitatu ya amani iliyosainiwa kwa ajili ya kurejesha amani nchini humo. Taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo katika ripoti hiyo itawasilishwa kwenye Mkutano wa 36 wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliopangwa kufanyika mwezi Agosti, 2016 Mbabane, Swaziland.

Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

71. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ambao ulifanyika Gaborone, Botswana mwezi Machi, 2016. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo ulijadili hatua ya utekelezaji ya Mpango wa Kikanda wa Maendeleo 2015 - 2020; hatua ya utekelezaji wa Mpango wa Kikanda wa Maendeleo ya Viwanda; na Mtangamano wa Utatu wa Eneo Huru la Biashara la COMESA-EAC-SADC. Mkutano huo pia ulipokea taarifa ya utekelezaji wa

maamuzi ya vikao vya Baraza la Mawaziri ambayo ilihusisha jumla ya maeneo kumi. Taarifa hiyo inaonyesha kuwa utekelezaji wa maeneo hayo unaendelea vizuri.

72. **Mheshimiwa Spika**, Mkutano huo pia, ulipokea maombi ya Serikali ya Visiwa vya Comoro na Serikali ya Burundi ya kutaka kujiunga na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Hivi sasa Sekretarieti inaendelea na zoezi la kutathmini maombi ya nchi hizo kulingana na taratibu, kanuni na sheria za Jumuiya za kuwa mwanachama. Taarifa ya tathmini hiyo itatolewa kwenye Mkutano wa 36 wa Wakuu wa Nchi ambao umepangwa kufanyika mwezi Agosti, 2016, Mbabane, Swaziland.

Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi

73. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania imeendelea kuwa mwanachama wa mstari wa mbele katika kuimarisha ushirikiano wa nchi zilizo katika mwambao wa Bahari ya Hindi kupitia Jumuiya ya Nchi hizo.

Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri kuhusu 'Blue Economy'

74. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri wa Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi kuhusu *Blue Economy* uliofanyika mwezi Septemba, 2015 nchini Mauritius. Mkutano huo ulijadili maeneo manne ya kipaumbele kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali zitokanazo na bahari. Maeneo hayo ni *Fisheries and Aquaculture; Renewable Ocean Energy; Seaport and Shipping; na Seabed Exploration and Minerals*. Mkutano huo pia ulidhamiria kuunda mifumo madhubuti yenye Sera, Sheria na Mikakati ya Matumizi Endelevu ya Rasilimali za Bahari na kusimamia Dhana ya Uchumi wa Bahari ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu kwa Nchi Wanachama.

75. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza maazimio ya mkutano huo, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania inaendelea kufanya utafiti wa kutambua maeneo yenye samaki wengi hususan aina ya Jodari pamoja na majaribio ya kuweka vifaa vya kuvutia samaki katika Bahari ya Hindi. Utafiti huu unaohusisha maeneo ya Mafia, Zanzibar na Bagamoyo unalenga kuwapunguzia wavuvi muda wa kutafuta samaki, kupunguza gharama za mafuta na kuwaongezea kipato. Vilevile, taarifa za utafiti huo zitatolewa kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili waje kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu ya Tanzania.

Kulinda na kuendeleza Maslahi ya Taifa ya Kiuchumi na Mengineyo nje ya nchi

Mkutano wa 70 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa

76. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa 70 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika New York, Marekani, mwezi Septemba, 2015 ambapo Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipata nafasi ya kulihutubia Baraza hilo na kueleza msimamo wa nchi kwenye masuala mbalimbali duniani, yakiwemo ya kiuchumi na maendeleo, amani na usalama, pamoja na mahusiano yetu na nchi nyingine. Aidha, Mheshimiwa Kikwete alifanya mazungumzo na nchi marafiki na washirika wetu wa maendeleo na kukubaliana masuala mbalimbali yenye manufaa kwa nchi ikiwemo ufadhili wa miradi ya maendeleo.

Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola

77. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola uliofanyika Malta mwezi Novemba, 2015. Tanzania ilishiriki kikamilifu kwenye majadiliano mbalimbali yaliyofanyika na hivyo tamko la mwisho ya mkutano liliakisi maslahi ya nchi hususan kwenye masuala ya amani na usalama; haki za binadamu na utawala bora; maendeleo endelevu; mabadiliko ya tabianchi; biashara na usawa wa kijinsia na kumwezesha Mwanamke.

78. **Mheshimiwa Spika**, kwa mara ya kwanza baada ya miaka 66, Jumuiya ya Madola ilimchagua mwanamke mwenye asili ya Afrika, Mheshimiwa Baroness Patricia Scotland mzaliwa wa Dominica na mwenye uraia pacha wa Dominica na Uingereza kuwa Katibu Mkuu wa sita wa Jumuiya hiyo ambapo alianza kazi tarehe 1 Aprili, 2016. Vipaumbele alivyodainisha Mheshimiwa Scotland ni pamoja na kushughulikia unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto wa kike; athari za mabadiliko ya Tabianchi; biashara na utawala bora; na kuanzisha majadiliano na nchi wanachama kuhusu kutokufanya suala la mahusiano/mapenzi ya jinsia moja kuwa kosa la jinai. Alisisitiza kuwa nchi haziwezi kulazimishwa kufuata suala hili lakini ataanzisha majadiliano na lazima pawepo na makubalino ya pande zote. Wizara itaendelea kufuatilia kwa makini ajenda zake ili kuhakikisha masuala ambayo yanapingana na sheria, mila na desturi za nchi yetu hayawi sehemu ya majadilino ya Jumuiya.

Mkutano wa 10 wa Nchi Wanachama wa Shirika la Biashara Duniani

79. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa 10 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Shirika la Biashara Duniani

uliofanyika mwezi Desemba 2015, Nairobi, Kenya. Katika Mkutano huo Tanzania ilitetea maslahi yake hasa kuhusu masuala ya biashara ya kilimo na mazao yake ikiwemo pamba kwa kushirikiana na makundi ya Afrika; Nchi Masikini zaidi Duniani; Kundi la 77 na China; na Kundi la Afrika, Karibiani na Pasifiki, hivyo kuwa na ushawishi kwenye matokeo ya Mkutano huo yanayojulikana kama *Nairobi Package*. Makubaliano yaliyofikiwa kwenye Mkutano huo ni pamoja na nchi zilizoendelea kusitisha ruzuku ya kuuza nje mazao ya kilimo na kuimarisha soko kwa nchi zinazoendelea. Makubaliano haya ni muhimu zaidi kuwahi kufanyika ndani ya miaka 20 ya uhai wa Shirika hilo.

Ushiriki wa Watanzania waishio Ughaibuni katika Maendeleo ya Nchi

80. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na juhudi za kuwahamasisha na kuwashirikisha Diaspora wa Tanzania waishio maeneo mbalimbali duniani katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu. Jitihada hizo zimeleta mafanikio katika nyanja za uwekezaji, biashara na kubadilishana uzoefu, elimu na ujuzi. Diaspora waliopo katika nchi mbalimbali kama vile, Australia, Botswana, Marekani, Oman na Thailand wamekuwa mstari wa mbele katika kutafuta fursa za biashara, elimu pamoja kuutangaza utalii wa nchi yetu. Kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa kupitia Balozi zetu, Watanzania waishio nje ya nchi wanakadiriwa kuwa zaidi ya milioni moja kote duniani. Kitaaluma wapo Wahandisi, Madaktari, Wachumi, Wahadhiri na Wakufunzi katika nyanja mbalimbali na pia wafanyabishara; ambao wote hawa wametawanyika sehemu mbalimbali duniani.

81. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Pili la Diaspora lililofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Agosti, 2015. Lengo la Kongamano hilo lilikuwa ni kuhamasisha Diaspora kushiriki katika kukuza sekta ya biashara ndogondogo na za kati na kuboresha mahusiano kati ya Diaspora na Wajasiriamali waliopo nchini. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu makongamano mengine ya kibiashara na uwekezaji yanayofanyika nje ya nchi kama yale yanayoandaliwa na Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchini Marekani.

82. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ziara ya kitabibu ya Madaktari Watanzania kwa kushirikiana na madaktari wenzao wa kiasia waishio nchini Marekani mwezi Julai 2015. Madaktari hao walitoa huduma za matibabu na ushauri katika hospitali za Mwananyamala (Dar es Salaam) na Mnazi Mmoja (Zanzibar) kwa magonjwa ya moyo, saratani na kinywa. Aidha, walitoa msaada wa madawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Dola za Marekani 300,000 kwenye hospitali hizo na kukabidhi mashine ya kupima saratani ya matiti yenye thamani ya Dola za Marekani 200,000 katika Hospitali ya Lugalo.

83. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru madaktari hao kwa moyo wao wa dhati wa kujitolea. Aidha, ningependa kuwahamasisha Diaspora wengine kuiga mifano hiyo. Wizara yangu iko tayari kushirikiana nao wakati wote.

84. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kuitikia wito wa kuchangia maendeleo ya nchi yetu, uwekezaji wa Diaspora katika Benki ya CRDB, Mfuko wa Pensheni wa PSPF na Mfuko wa Mitaji wa UTT umefikia Shilingi Bilioni 26 mwaka 2015. Aidha, uwekezaji wa Diaspora katika mifuko mingine ya hifadhi za jamii, sekta za afya, viwanda na utalii umeongezeka.

85. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira wezeshi kwa Diaspora, Wizara yangu imekamilisha hatua za awali za kutengeneza Sera ya Diaspora kwa ushirikiano na Mfuko wa Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki. Sera hii itatoa mwongozo kwa wadau na kuleta uelewa wa pamoja kuhusu mikakati bora ya kuwatambua Diaspora na kuwawezesha kuchangia maendeleo ya nchi. Rasimu ya Sera hiyo itawasilishwa kwa wadau kwa ajili ya maoni na ushauri. Ni matarajio ya Serikali kuwa ushirikishwaji wa Diaspora kama moja ya wadau wa maendeleo utawawezesha kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu kwa kuleta teknolojia mpya; na kuongeza uwekezaji kwenye sekta mbalimbali kama vile viwanda, masoko ya mitaji, kilimo na utalii. Ushirikishwaji huo wa Diaspora utaiwezesha nchi kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

86. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania na wadau wengine inaandaa mfumo sahihi wa kutambua na kurahisisha uingiaji wa fedha kutoka kwa Diaspora ili kuwa na takwimu sahihi za mchango wa Diaspora kwenye kuongeza Pato la Taifa.

Kusimamia masuala yanayohusu Kinga na Haki za Kibalozi kwa Wanadiplomasia waliopo nchini kulingana na Mkataba wa Vienna wa mwaka 1961

87. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushirikiana na mamlaka mbalimbali nchini ili kuhakikisha kuwa, jamii ya wanadiplomasia waliopo nchini wanapata haki zao kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Vienna Kuhusu Mahusiano ya Kidiplomasia wa mwaka 1961. Wizara inasimamia kikamilifu utekelezaji wa Mkataba huo kwenye vipengele muhimu vya kinga na haki za kibalozi na wategemezi wao. Pamoja na jamii ya kibalozi kuwa na kinga na upendeleo maalum, Wizara inahakikisha kuwa jamii hizi zinaheshimu na kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi yetu.

Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Itifaki na Uwakilishi

88. **Mheshimiwa Spika**, mara baada ya kuundwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano, nilikutana na Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa waliopo nchini. Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, nilitumia fursa hiyo kuwapatia taarifa ya masuala mbalimbali yanayohusu umuhimu wa ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine na kutoa Dira ya Serikali ya Awamu ya Tano. Wizara yangu itaendelea kuwa na vikao vya mara kwa mara na wanadiplomasia hawa kwa lengo la kuimarisha zaidi ushirikiano.

89. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ziara za Viongozi wa Kitaifa wa Awamu ya Nne nje ya nchi ambao ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Makamu wa pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baadhi ya ziara za Viongozi hao zilifanywa katika nchi za Uswisi, Australia, Marekani, Misri, India, Kenya, Uganda, Botswana, Vietnam, Uingereza na Italia. Vilevile, Wizara iliratibu ziara za Viongozi wa Kitaifa wa Awamu ya Tano nje ya nchi zilizofanyika katika nchi za Afrika Kusini, Botswana, Ethiopia, Rwanda, Uganda, Uingereza Zambia, Comoro na Papua New Guinea.

90. **Mheshimiwa Spika**, ziara hizo zimekuwa na mafanikio ikiwa ni pamoja na kukuza na kuimarisha mahusiano kati ya nchi yetu na nchi hizo, zimetangaza fursa za uwekezaji, biashara, utalii na kuwahamasisha Diaspora kuwekeza nyumbani. Pia zinaimarisha uhusiano kati ya sekta binafsi za hapa nchini na taasisi mbalimbali za nje.

91. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu na kufanikisha uwasilishaji wa hati za utambulisho za Mabalozi kutoka nchi mbalimbali. Katika kipindi hiki Mabalozi waliowasilisha hati zao za utambulisho ni pamoja na Qatar, Argentina, India, Denmark, Uswisi, Uturuki, Finland, Sweeden, Ubelgiji, Hispania, Msumbiji, Uganda, Misri, Israeli, Ufilipino, Jamhuri ya Korea, Umoja wa Ulaya, Palestina, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Namibia, Brazil, Jamhuri ya Czech na Jamhuri ya Sudan Kusini.

Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli

92. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa huduma za kikonseli kwa kurahisisha upatikanaji wa viza kwa maafisa na watendaji wa Serikali, Vyama vya Siasa na Taasisi nyingine zinazostahili huduma hiyo. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu matumizi ya Ukumbi wa Watu Mashuhuri wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, kwa watu wanaostahili wakiwemo Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa, viongozi wa Serikali na baadhi

ya Wafanyabiashara hapa nchini. Vilevile, Balozi zetu nje zimeendelea kutoa Viza kwa raia wa nje wanaoitembelea Tanzania na kushirikiana na mamlaka nyingine kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayowakabili Watanzania waishio nje ya nchi.

93. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara yangu imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya Watanzania wanaofanya kazi katika Balozi na mashirika hayo kutokuwa na mikataba ya ajira. Hivyo, natoa rai kwa ofisi za Kibalozi na Mashirika ya Kimataifa yaliyopo hapa nchini kutoa mikataba kwa waajiriwa wao ili kukidhi matakwa ya kisheria. Vilevile, nawaasa Watanzania wanaofanya kazi katika Balozi na Mashirika ya Kimataifa wahakikishe wana mikataba ya ajira ili kulinda maslahi yao.

94. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa huduma za kikonseli kwa Watanzania waliopo nje ya nchi. Naomba kutumia fursa hii kuwasihi Watanzania hao kuhakikisha wanajisajili katika Balozi zetu na Konseli, na pale ambapo hatuna ofisi za ubalozi wajisajili katika ofisi za ubalozi wa Uingereza kama ilivyoainishwa kwenye hati za kusafiria.

95. **Mheshimiwa Spika**, niruhusu nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba miaka ya karibuni pamejitokeza wimbi la Watanzania wanaokwenda nje ya nchi kwa ahadi za kupatiwa ajira. Kwa upande wa India, Thailand, Malaysia na China, ahadi hizo za ajira zimekuwa zikitolewa na watu wasio waaminifu ambao wana mtandao wa biashara ya kusafirisha binadamu. Mtandao huo unahusisha raia wa Tanzania waliopo ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na raia wa kigeni waliopo kwenye nchi hizo. Watu hao wanachofanya ni pamoja na kuwatafuta wasichana wenye umri kati ya miaka 18 na 24, kuwatafutia vibali vya safari na kuwalipia nauli za kuwafikisha kwenye nchi husika kwa kuwalaghai kuwa wanakwenda kufanya kazi katika hoteli, migahawa, maduka makubwa au kazi za nyumbani. Matokeo yake, wanapofika kwenye nchi hizo wasichana hao wanakuta kuwa ahadi walizo ahidiwa sio za kweli na badala yake wanalazimishwa kukubali kufanya kazi za ukahaba ili kurejesha fedha walizogharimiwa kufika huko. Kwa taarifa tulizonazo, mtandao huo wa biashara ya ukahaba huwataka wasichana hao kurejesha kiasi cha Dola za Marekani kati ya 5,000 hadi 6,000 kiasi ambacho sio rahisi kupata kwa kazi hizo ikizingatiwa kwamba mapatano na malipo ya kazi hiyo hayafanywi na wahusika bali madalali wa mtandao huo. Madalali waliowapeleka vijana hao kwenye nchi hizo huwanyang'anya hati zao za kusafiiria ili kuwadhibiti wasitoroke hadi kipatikane kiasi cha fedha walizogharimwa. Kwa kuwa hawana fedha na namna nyingine ya kuishi wasichana hao wamelazimika kukubali kufanya biashara hiyo.

96. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya vijana hao, waliweza kuwatoroka madalali hao, na kukimbilia kwenye ofisi zetu za Ubalozi kutafuta msaada. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Spika, Balozi zetu hazina fungu la kuhudumia Watanzania wanaopata shida ughaibuni na matokeo yake maafisa wa Ubalozi kwa moyo wa kibinadamu wamekuwa wakitoa fedha zao wenyewe kusaidia kununua tiketi za kuwarejesha Watanzania waliofanikiwa kuchomoka kwenye makucha ya makuadi wa ukahaba. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hilo, Wizara imeanzisha mazungumzo na Shirika la Kimataifa la Uhamaji ili wasaidie kuwarudisha nyumbani vijana hao.

97. **Mheshimiwa Spika**, ni wazi kwamba vitendo hivyo ni vya kinyama na vinakiuka haki ya binadamu. Ifahamike pia kwamba usafirishaji wa binadamu ni uhalifu kwa mujibu wa makosa ya kupangwa ya Azimio la Umoja wa Mataifa NA. 55/25 la mwaka 2003 la kuzuia, kukomesha na kuadhibu usafirishaji wa binadamu hasa kwa wanawake na watoto chini ya Itifaki yake.

98. **Mheshimiwa Spika**, Kutokana na ushirikiano kutoka kwa Jumuiya za Watanzania waishio nchini Thailand na India, pamoja na baadhi ya wahanga wa biashara hiyo haramu, Serikali imepata majina ya baadhi ya wahusika wa mtandao huo na tayari mawasiliano na Serikali za nchi hizo yamefanyika ili kuwakamata wahusika wote na kuwafikisha katika mkondo wa sheria. Kwa hapa nyumbani, uchunguzi unaendelea kwa kushirikiana na Balozi za nchi ambazo wasichana wetu wanapelekwa ili kubaini watu wote walio sehemu ya mtandao huo hususan wale wanaowezesha upatikanaji wa vibali vya kusafiria kwenye Balozi hizo ili kuwakamata na kuwachukulia hatua kali za kisheria. Pia tumeziomba Balozi hizo ziwe makini zaidi kudhibiti uombaji wa vibali vya kusafiria kwa shughuli mbalimbali na kuwataka wahusika kuthibitisha uwezo wa kifedha zitakazo wawezesha kutalii, kufanya shughuli ama kuishi katika nchi wanazokwenda ili kuudhibiti mtandao wa biashara ya watu.

99. **Mheshimiwa Spika**, Vilevile, kupitia Bunge hili, ninatoa wito kwa Watanzania wote, tuwe makini pale tunapopata fursa za kazi nje ya nchi. Kama nilivyosema hapo awali, ni muhimu kuzingatia na kujiridhisha na masuala yote ya msingi yanayohusiana na ajira za nje, ikiwa ni pamoja na; kuwepo na mkataba rasmi wa ajira unaotambuliwa na Mamlaka husika zilizopo nchini na za Nchi unayotaka kwenda, kujisajili kweye ofisi za Ubalozi wa Tanzania uliopo katika nchi hizo na kutokubali kuweka hati yako ya kusafiria kama rehani.

100. **Mheshimiwa Spika**, nasikitika kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa bado kuna Watanzania kadhaa wanatumikia vifungo na wengine kati yao wanakabiliwa na adhabu ya kifo katika magereza ya nchi mbalimbali duniani baada ya kukutwa na hatia ya makosa ya kujihusisha na biashara haramu ya madawa ya kulevya. Idadi yao ni kama ifuatavyo: Brazil (41), China (266), Iran

(68), India (9), Nepal (4), Oman (3), Thailand (14) na Umoja wa Falme za Kiarabu (3). Naomba kuchukua nafasi hii kuwasili Watanzania kujiepusha na biashara hiyo kwa kuwa hasara zake ni kubwa kwa familia zao na Taifa kwa ujumla.

Kuratibu shughuli za Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano

101. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu Mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano ambazo kimsingi hutoa fursa kwa nchi zetu kujadiliana kwa kina kuhusu masuala muhimu katika nyanja zote za mahusiano na kuweka mikakati ya pamoja ya maendeleo.

102. **Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2016, Wizara ilifanya kikao cha Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Zambia kilichofanyika hapa nchini. Katika kikao hicho, pande zote mbili zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya Ulinzi na Usalama Mipakani; kuanzisha Mashauriano ya Kidiplomasia; Kupunguza Msongamano wa magari katika mpaka wa Tunduma/Nakonde; na kuanzisha majadiliano ya kutotoza kodi mara mbili kwenye bidhaa zinazotoka na kuingia katika nchi hizo.

103. **Mheshimiwa Spika**, Vilevile, mwezi Aprili 2016, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Kikao kingine cha Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Rwanda kilichofanyika Mjini Gisenyi, Rwanda. Katika kikao hicho nchi hizi zimekubaliana kushirikiana katika kukamilisha mapema ujenzi wa miundombinu ya ushoroba wa kati kama vile ujenzi wa reli ya kati katika kiwango cha kimataifa kwa kushirikiana na wadau, kukuza ushirikiano katika sekta ya anga hususan baina ya Shirika la Ndege la Rwanda na Shirika la Ndege la Tanzania, kuimarisha ushirikiano katika sekta za sayansi na teknolojia, afya, kilimo, ufugaji, utalii na elimu. Mkutano huo umezidi kuimarisha urafiki na ushirikiano kati ya Tanzania na Rwanda kufuatia ziara ya kirafiki ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda mwezi Aprili, 2016.

104. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeratibu na kushiriki vikao vya Ujirani Mwema kati ya Tanzania na nchi za Msumbiji, Uganda na Zambia. Vikao hivyo ni muhimu katika kukuza mahusiano katika sekta mbalimbali kati ya Tanzania na nchi husika. Aidha, Vikao hivyo vinasaidia kutatua matatizo mengi ya mpakani na kurasimisha biashara baina ya nchi yetu na nchi tunazoshirikiana nazo.

Kusimamia utawala na Maendeleo ya Utumishi Wizarani na kwenye Balozi zetu

105. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki Wizara iliajiri watumishi 42, ambapo maafisa 30 kati ya hao walipelekwa katika mafunzo maalum ya Jeshi la Kujenga Taifa yenye lengo la kuwajengea uwezo, uadilifu na uzalendo katika kazi; mtumishi mmoja alibadilishwa kada; iliwapandisha vyeo watumishi 59; na

iliwathibitisha kazini watumishi 15. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kipindi hiki ulifanyika uteuzi wa mabalozi kuiwakilisha nchi yetu katika nchi za Uholanzi, Malawi, Kuwait, Japan, Uingereza na Zimbabwe. Vilevile, Wizara imejaza nafasi za Wakurugenzi zilizokuwa wazi.

106. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza mpango wa mafunzo wa miaka mitatu 2013/2014 - 2015/2016. Katika kipindi hiki jumla ya watumishi 43 walihudhuria mafunzo ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, Watumishi 24 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 19 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Wizara imeshaanza kuandaa mpango mwingine wa mafunzo wa miaka mitatu ambao utaanza kutekelezwa kuanzia mwezi Julai 2016 baada ya mpango wa sasa kuisha muda wake mwezi Juni 2016.

107. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki Wizara imewarejesha nyumbani Mabalozi watano na watumishi tisa baada ya kustaafu na wengine kumaliza muda wao wa kufanya kazi Ubalozini. Aidha, Wizara iliwapeleka vituoni Naibu Mabalozi watatu na watumishi thelathini. Zoezi la kuwarudisha Mabalozi na watumishi wanaostaafu na wanaomaliza muda wao na kupeleka mbadala wao ni endelevu na Wizara itaendelea kutekeleza kadri inavyopata fedha.

TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

108. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inasimamia taasisi tatu ambazo ni Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Jijini Dar es Salaam, Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha, ambacho pia kinasimamia Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Dar es Salaam.

Chuo cha Diplomasia

109. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaaluma na kendesha kozi fupi kwenye nyanja za diplomasia na uhusiano wa kimataifa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Chuo kimejizatiti katika kutimiza na kutekeleza viwango vilivyowekwa na Baraza la Taifa la Ithibati la Mafunzo ya Ufundi linalosimamia elimu ya mafunzo na ufundi kama vile kuwa na wanataaluma wenye vigezo vinavyotambulika, kuboresha shughuli za kitaaluma, kuboresha majengo na miundombinu ya kitaaluma pamoja na matumizi ya teknolojia katika taaluma na utawala.

Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha

110. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 2015, Kituo kiliweza kuwa mwenyeji wa mikutano 150 ya kitaifa na 57 ya kimataifa iliyoingiza nchini wageni wanaokadiriwa kufikia 35,288. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 kituo kimeweza kuwa mwenyeji wa Mikutano 82 ambapo 10 ni ya Kimataifa na 72 ya kitaifa.

111. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara nyingine tena, Kituo kimeendelea kupata hati safi ya hesabu zake zilizoandaliwa na kukaguliwa kwa wakati kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2015.

112. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kituo kimepanga kuingiza mapato ya shilingi 15,778,162,803.00 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ikiwemo Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Dar es Salaam ambacho kinatarajiwa kukusanya mapato ya Shilingi 3,051,000,000.00.

113. **Mheshimiwa Spika**, Kituo kinategemea kukopa shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya ujenzi wa jengo la maonesho na upanuzi wa Hospitali. Miradi yote inayotekelezwa imeombewa kibali cha Msajili wa Hazina.

114. **Mheshimiwa Spika**, Kituo kinaendelea kufanya taratibu za kuwezesha kujengwa kituo mahsusi cha mikutano kitakachoitwa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mlima Kilimanjaro. Taarifa ya upembuzi yakinifu ya mradi wa ujenzi wa Kituo hicho iliandaliwa na Wataalamu Washauri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taarifa hiyo ilionyesha kwamba mradi huo ni muhimu na wenye manufaa kiuchumi na kijamii kwa taifa. Aidha, makadirio ya awali ya ujenzi wa kituo hicho ni Dola za marekani milioni 248. Kwa hivi sasa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha kinaendelea na mazungumzo na mifuko ya hifadhi ya jamii iliyopo nchini ili iweze kushiriki katika kutekeleza mradi huo. Ni matarajio ya Wizara kuwa kuwepo kwa Kituo hicho kutakuwa suluhisho sahihi la mahitaji ya mikutano ya kimataifa na maonesho hapa nchini.

Mpango wa Kijitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika

115. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika kwa upande wa Tanzania wenye lengo la kuzisaidia nchi za Kiafrika kuhakikisha kuwa changamoto zinageuzwa kuwa fursa za maendeleo na mambo mazuri ya kuendelezwa kwa faida ya nchi yenyewe na hata kuwa mfano wa kuigwa na nchi nyingine.

Mpango huo unaratibiwa kwa mujibu wa miongozo ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa nchi za Afrika.

116. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, Taasisi ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika kwa upande wa Tanzania imeendelea kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kusimamia utekelezaji wa Mpango kazi wa kuondoa changamoto za utawala bora zilizobainishwa kwenye ripoti ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika kwa upande wa Tanzania. Taasisi imeendelea kupokea na kuchambua taarifa mbalimbali za utekelezaji kutoka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali zilizoguswa na Ripoti ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika kwa upande wa Tanzania;

ii. Kuandaa taarifa ya utekelezaji ya mwaka kuhusu hatua zilizochukuliwa ili kutatua changamoto zilizojitokeza kwenye ripoti ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika kwa upande wa Tanzania. Taarifa hiyo inatarajiwa kuwasilishwa kwenye vikao vya Wakuu wa Nchi za Kiafrika wanaoshiriki kwenye mchakato wa Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika;

iii. Kuendelea kutoa taarifa kwa wananchi juu ya matokeo ya tathmini ya utawala bora kwa nchi yetu kupitia vyombo mbalimbali vya habari na majukwaa mengineyo; na

iv. Kutafsiri ripoti ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika kwa upande wa Tanzania katika lugha ya Kiswahili na kuandaa chapisho la muhtasari.

ILİYOKUWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

117. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuelezea utekelezaji wa majukumu ya iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba sasa nilieleze Bunge lako Tukufu utekelezaji wa majukumu ya iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Wizara hiyo ilikuwa na majukumu yafuatayo:-

- I. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake;
- II. Kuratibu, kushiriki na kusimamia utekelezaji wa Mtangamano wa Afrika Mashariki hususan majadiliano na utekelezaji wa hatua za Mtangamano ambazo ni Umoja wa Forodha; Soko la Pamoja; Umoja wa Fedha; na Shirikisho la Kisiasa;

III. Kutoa elimu ya Mtangamano wa Afrika Mashariki ili Wananchi waweze kuelewa na kutumia fursa za Mtangamano huo; na

IV. Kuimarisha utendaji na kujenga uwezo wa Wizara.

118. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara hiyo iliidhinishiwa Shilingi 26,666,436,300.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 24,047,468,300.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 2,618,968,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi. Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kimejumuisha mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki wa kiasi cha Shilingi 18,570,055,300.00.

119. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2016, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 19,003,440,860.00, sawa na asilimia 71.26 ya fedha zote zilizotengwa. Kati ya fedha hizo Shilingi 15,506,375,000 zilitumika kulipa mchango wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Shilingi 1,689,936,160.00 zilitumika kulipa mishahara ya watumishi na Shilingi 1,807,129,700.00 zilitumika kutekeleza shughuli za Wizara.

Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake

120. **Mheshimiwa Spika**, kama unavyofahamu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umepiga hatua kubwa ambapo Nchi wanachama wa Jumuiya zimefikia makubaliano na kuendelea kuyatekeleza makubaliano hayo kwenye nyanja zote za kiuchumu, kijamii, kiutamaduni na kwa kiasi fulani kisiasa pia na hivyo kutufanya tusilale na kutakiwa kuwa makini katika kila hatua tunazopiga. Itakumbukwa kuwa Jumuiya yetu ilianzishwa rasmi Julai 2000 baada ya Nchi Wanachama kukamilisha kuridhia Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliotiwa saini na Wakuu wa Nchi Wanachama tarehe 30 Novemba, 1999. Aidha, hivi sasa Nchi zote Wanachama zinatekeleza Mkataba huu na Itifaki zake kubwa tatu (3) na zile mbalimbali za kisekta. Maeneo yaliyobaki ambayo tunaendelea na majadiliano ni Umoja wa Fedha na Shirikisho la Kisiasa.

121. **Mheshimiwa Spika**, juhudi hizi sasa zinamaanisha kuwa eneo lote la nchi sita (6) za Jumuiya ya Afrika Mashariki kimsingi limeungana katika nyanja mbalimbali na hivyo kutoa motisha ya ushindani mkubwa wa ndani ya Jumuiya kiuchumi na kimaendeleo. Kwa kutambua kuwa Tanzania ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Wizara yangu ameelekeza Wimbo na Bendera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki zitumike hapa nchini.

122. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito wa kuongezwa kwa matumizi ya Bendera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye Ofisi zote za Umma nchini zikiwemo za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma (tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge kwenye Magari yetu na ofisi zetu Majimboni) na zile za sekta binafsi sambamba na Bendera ya Taifa letu Tukufu. Aidha, natoa rai kwa Taasisi za Serikali na vyombo vya habari viweze kuutumia Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pale ambapo Wimbo wa Taifa letu Tukufu unapigwa.

123. **Mheshimiwa Spika**, ni imani yangu kuwa hatua hii itasaidia kuwajengea Watanzania uelewa, kuifahamu vyema Jumuiya yetu na hatimae waweze kujiandaa, kushiriki na kupata manufaa yanayoendana na fursa zilizopo kibiashara, kiuchumi, kiuzalishaji, kijamii na kiutamaduni kwa kuzingatia uwepo wa Soko kubwa la Afrika Mashariki na fursa zinginezo.

124. **Mheshimiwa Spika**, wito huu ni moja ya utekelezaji wa Mkakati wetu wa mawasiliano wa Wizara ambao unalenga kuwapa fursa Wananchi wetu ya kujiandaa, kuiendesha, kuitumia Jumuiya yao na kutimiza matakwa ya Ibara ya 7(a) ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo inasisitiza kuwa "Jumuiya yetu hii imejengwa katika Wananchi na ushirikiano wa kimasoko". Aidha, hatua hizi zinalenga katika kuendeleza juhudi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuhakikisha kuwa Jumuiya hii inakuwa kweli ni Jumuiya ya Wananchi wetu, kutambua uwepo wake na wanufaika nayo katika kubadilisha maisha yao.

Mkutano wa 17 wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama na Mikutano ya 32 na 33 ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki

125. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 17 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Machi 2016 Jijini Arusha, Tanzania. Katika Mkutano huo Tanzania iliteuliwa kwa mara ya pili mfululizo kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi mwezi Novemba 2016. Aidha, Mkutano huo uliridhia Jamhuri ya Sudan Kusini kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo tarehe 15 Aprili, 2016 nchi hiyo ilisaini Mkataba wa Kujiunga na Jumuiya hiyo.

126. **Mheshimiwa Spika**, kadhalika, katika mkutano huo Wakuu wa Nchi walizindua rasmi Pasi mpya ya kielektroniki ya Kusafiria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuelekeza matumizi ya hati hii mpya kuanza rasmi tarehe 1 Januari, 2017. Pasi hii inaipandisha hadhi Pasi ya sasa ya Afrika Mashariki kutumika kusafiria nje ya Afrika Mashariki. Nchi Wanachama zimekubaliana kuziondoa hati za kusafiria zilizopo sasa katika kipindi cha miezi 24 kuanzia tarehe 1 Januari, 2017 hadi tarehe 31 Desemba, 2018. Hati hizo zitakuwa na alama za jumla za

kiusalama na kila Nchi Mwanachama imeruhusiwa kuongeza alama zake za kiusalama katika Pasi hizo. Idara za Uhamiaji katika nchi wanachama zitaendelea na jukumu la utoaji wa hati hizo kwa raia wa nchi zao.

127. **Mheshimiwa Spika**, Mkutano wa 32 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifanyika tarehe 14 Agosti, 2015 na kufikia maamuzi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuidhinisha ajira kwa Mwanasheria Mkuu wa Jumuiya, Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usalama wa Anga na Mkurugenzi wa Mipango katika Jumuiya.

Umoja wa Forodha

128. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa hatua ya kwanza ya Mtangamano ambayo ni Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki kama ifuatavyo:

Kanuni Mpya za Utambuzi wa Uasili wa Bidhaa

129. **Mheshimiwa Spika**, katika kuziwezesha Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kunufaika zaidi na hatua hii ya Umoja wa Forodha, mabadiliko yamefanywa katika kanuni za utambuzi wa uasili wa bidhaa. Katika mabadiliko hayo, Nchi Wanachama zimeacha kutumia vigezo sawa kwa bidhaa zote, na sasa zitatumia vigezo tofauti kulingana na bidhaa husika. Mabadiliko haya ni fursa kubwa kwa viwanda vya Tanzania ambavyo vingi bado ni vidogo na vilikuwa haviwezi kufikia vigezo vya uasili wa bidhaa. Aidha, katika kipindi hiki, nchi Wanachama wa Jumuiya zilikamilisha mwongozo wa kutumika katika kurahisisha utekelezaji wa kanuni hizo.

Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha

130. **Mheshimiwa Spika**, katika kuweka mazingira wezeshi ya biashara katika Jumuiya, Wizara imeendelea kuratibu uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha kupitia Kamati ya Kitaifa na Kikanda ya uondoaji wa vikwazo hivyo. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 vikwazo 16 viliripotiwa vimeondolewa, kati ya hivyo vinne (4) viliihusu Tanzania. Vikwazo hivyo ni tozo ya Dola za Marekani 200 kwa kila kontena la kemikali; kutopewa upendeleo wa ushuru wa forodha kwa chumvi na bidhaa za plastiki kutoka Kenya; na upimaji wa malori matupu.

131. **Mheshimiwa Spika**, ili kuharakisha uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha, Wizara imekuwa na utaratibu wa kuitisha mikutano ya pande mbili husika. Katika kipindi hiki Wizara ilifanya mikutano na Kenya na Burundi ambayo ilichangia kuharakisha uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha vikiwemo vile vilivyotajwa hapo juu. Vilevile, tumekubaliana na Kenya kufanya utafiti juu ya

tozo zinazotozwa na mamlaka za Serikali za mitaa za nchi zetu zinazoathiri biashara baina yetu kwa lengo la kurazinisha tozo hizo.

Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa kati ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

132. **Mheshimiwa Spika**, nafasi ya Tanzania katika Soko la Jumuiya imeendelea kupanda kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia 26 mwaka 2014 na tunategemea kufanya vizuri zaidi kutokana na juhudi zinazoendelea za kudhibiti ulanguzi wa mazao na bidhaa mipakani, utekelezaji wa sheria mpya ya uasili wa bidhaa, kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha na kuimarisha uzalishaji viwandani. Kwa mujibu wa Taarifa ya Biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2014, biashara ndani ya Jumuiya imekua na kufikia Dola za Marekani bilioni 5.63 kwa mwaka 2014 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 3.72 kwa mwaka 2010. Aidha, biashara baina ya Tanzania na Nchi Wanachama imeendelea kuimarika na kuongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 0.69 mwaka 2010 na kufikia Dola za Marekani bilioni 1.49 mwaka 2014. Kwa mwaka 2013 kiwango cha biashara kiliongezeka zaidi kulingana na hali ya mahitaji ya soko na kupanda kwa uzalishaji kwenye sekta mbalimbali. Tanzania imeendelea kuwa na urari chanya wa biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1**.

133. **Mheshimiwa Spika**, wafanyabiashara wa Tanzania wamendelea kuchangamkia fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Wafanyabiashara hao wamefanikiwa kuuza kwa wingi katika Soko la Afrika Mashariki bidhaa za viwandani kama vile transfoma, waya za umeme, vyandarua, saruji na magunia; na bidhaa za kilimo kama vile mahindi, mchele, katani, mbogamboga, asali na chakula cha mifugo. Hii inaashiria kuendelea kuimarika kwa biashara ya bidhaa za viwandani na mazao ya kilimo.

134. **Mheshimiwa Spika**, bidhaa zilizounuliwa kwa wingi kutoka Nchi Wanachama ni pamoja na kemikali kwa ajili ya viwanda vya nguo, vipodozi na sabuni; dawa za binadamu na mifugo; vipuri vya magari; vifuniko vya chupa za vinywaji; sabuni; vifaa vya kufanyia usafi; vifungashio; mabanda maalum ya kilimo cha mbogamboga na maua (green house); na vyumba vya baridi kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa mbalimbali.

Umoja wa Fedha

135. **Mheshimiwa Spika**, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kutekeleza Mpangokazi wa Miaka Kumi wa Kuelekea katika Eneo la Sarafu Moja ulioanza kutekelezwa mwaka 2014 na utakaokamilika mwaka 2024. Katika kutekeleza Mpangokazi huo, Nchi Wanachama zimekamilisha majadiliano ya Muswada wa Sheria ya uanzishwaji

wa Taasisi ya Fedha ya Afrika Mashariki na Taasisi ya Takwimu ya Afrika Mashariki. Maandalizi ya majadiliano ya muswada wa Kamisheni ya Ufuatiliaji na Usimamizi ya Afrika Mashariki yataanza katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha.

136. **Mheshimiwa Spika**, matarajio ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuifikia hatua hii muhimu ya kuanzisha matumizi ya sarafu moja kwenye eneo la Jumuiya ifikapo mwaka 2024. Hatua hii itafikiwa mara baada ya Nchi Wanachama angalau watatu (3) kufikia vigezo vya kiuchumi vilivyoainishwa kwenye Itifaki ya Umoja wa Fedha. Aidha, hatua hiyo itatanguliwa na uanzishwaji wa Benki Kuu ya Afrika Mashariki ambayo pamoja na majukumu mengine itakuwa na majukumu ya kuchapisha na kusambaza sarafu hiyo ya Afrika Mashariki.

Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki

137. **Mheshimiwa Spika**, Shirikisho la Kisiasa ni hatua ya nne na ya mwisho katika mtangamano wa Afrika Mashariki ambayo inategemea sana misingi imara itokanayo na utekelezaji wa hatua za mwanzo za mtangamano. Katika kipindi cha mwaka fedha 2015/2016, Nchi Wanachama ziliendelea na majadiliano ya modeli ya shirikisho ambayo itatumika katika kuandaa Rasimu ya Katiba ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

138. **Mheshimiwa Spika**, rasimu hiyo, inatarajiwa kutumika katika kuelimisha na kuhamasisha wananchi wa Afrika Mashariki kuhusu aina ya Shirikisho linalotarajiwa kuundwa ili kuleta uelewa wa pamoja na uungwaji mkono wa hatua hiyo wakati ukifika. Aidha, kwa kuwa Shirikisho la Kisiasa ni mchakato, Nchi Wanachama zimeendelea na utekelezaji wa shughuli zinazounda msingi wa Shirikisho hilo ikiwemo masuala ya utawala bora, uimarishaji wa demokrasia na utawala wa sheria.

Ushirikiano na Kanda nyingine za Kiuchumi

Majadiliano ya Kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

139. **Mheshimiwa Spika**, juhudi za kuziunganisha Jumuiya za COMESA, EAC na SADC ili kuwa eneo moja huru la kibiashara zimefika hatua nzuri. Mkutano wa Tatu wa Wakuu wa Nchi za COMESA, EAC na SADC uliofanyika tarehe 10 Juni, 2015 Jijini Sharm El Sheikh, Misri ulihitimishwa kwa Wakuu wa Nchi na Serikali kutia saini Azimio la Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara; na Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara.

140. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia kusainiwa kwa mkataba huo, Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya hizo walikubaliana kukamilisha majadiliano ya maeneo yaliyosalia katika kipindi cha miezi 6 hadi 12 baada ya uzinduzi rasmi wa eneo huru la biashara. Maeneo hayo ni uondoshwaji wa kodi kwenye bidhaa, utambuzi wa uasili wa bidhaa, usuluhishi wa migogoro ya kibiashara na kupunguziana ushuru.

Majadiliano ya Uhuru wa Wafanyabiashara kusafiri katika Eneo la Utatu

141. **Mheshimiwa Spika**, ili kurahisisha na kuwezesha wafanyabiashara kusafiri katika Eneo hilo la Utatu, Nchi Wanachama zimeendelea na majadiliano ya kuandaa Mkataba wa Uhuru wa Wafanyabiashara kusafiri kwenye eneo hilo. Mkataba huo unatarajiwa kuidhinishwa ifikapo Desemba, 2016.

Majadiliano ya Uendelezaji wa Viwanda katika Eneo la Utatu

142. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika kukamilisha Rasimu ya Mpango wa Maeneo ya Ushirikiano katika Maendeleo ya Viwanda; na Mpangokazi kwa ajili ya Utekelezaji wa utaratibu wa Ushirikiano katika eneo la Utatu. Maeneo yaliyoboreshwa ni Sera na Mikakati kutoka Kanda zote tatu; Uzingatiaji wa uendelezaji wa viwanda unaojali utunzaji wa mazingira; na Utambuaji Kisheria na Umiliki wa Haki zinazotokana na Uvumbuzi na Ubunifu katika maendeleo ya Viwanda. Aidha, Nchi Wanachama zimekubaliana kushirikiana katika maeneo ya uratibu na uhamasishaji wa pamoja wa sera ya maendeleo ya viwanda na uongezaji thamani bidhaa baina ya nchi Wanachama; na Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na vya Kati na kujenga uwezo wa utaalam katika kuendeleza Viwanda.

Ubia wa Kiuchumi kati ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya

143. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya. Malengo ya ubia huu ni kuimarisha ushirikiano wa kikanda, kuleta maendeleo endelevu na kuziwezesha nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki kupata misaada ya kimaendeleo ili kukabiliana na changamoto za uzalishaji na kuweka muda wa kuondoa vikwazo vya biashara.

144. **Mheshimiwa Spika**, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya zilikamilisha mapitio ya kisheria ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi baina ya nchi hizo. Hatua inayoendelea ni Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutafsiri mkataba huo katika lugha ya Kiswahili wakati Umoja wa Ulaya unatafsiri mkataba huo katika lugha 21 zinazotumiwa na Jumuiya ya Ulaya. Baada ya kukamilika kwa mchakato wa kufanya tafsiri, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya

Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya zitasaini Mkataba huo, pamoja na kuuridhia ili utekelezaji wake uanze.

145. **Mheshimiwa Spika**, ili kuweka mazingira wezeshi ya kukuza na kuendeleza viwanda vya nguo na ngozi ndani ya Jumuiya, Mkutano wa 17 wa Wakuu wa Nchi Wanachama ulielekeza Nchi Wanachama kuhakikisha zinapunguza uingizaji wa nguo na viatu vilivyotumika kutoka nje ya Jumuiya na kusitisha uagizaji wake katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka huu wa fedha. Aidha, Wakuu wa Nchi walielekeza Nchi wanachama kupiga marufuku utaratibu wa kuuza ngozi na bidhaa za ngozi ghafi nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kujengea uwezo na upatikanaji wa masoko kwa Wajasiriamali wadogo

146. **Mheshimiwa Spika**, Maonesho ya 16 ya Juakali/Nguvukazi yaliyofanyika tarehe 30 Novemba hadi 6 Disemba 2015 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam katika maonesho hayo jumla ya wajasiriamali 734 kutoka Nchi zote wanachama walishiriki. Kati ya hao, wajasiriamali 395 walikuwa ni washiriki kutoka Tanzania. Lengo la maonesho hayo ni kujenga uwezo wa wafanyabiashara wadogo kupata masoko ya bidhaa zao katika Nchi Wanachama. Napenda kutoa rai kwa wajasiriamali wa Tanzania kushiriki katika Maonesho ya 17 ya Juakali/Nguvukazi yaliyopangwa kufanyika mwezi Novemba 2016 nchini Kenya.

Uendelezaji wa Miundombinu ya Kiuchumi

147. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu na miradi ya kitaifa yenye sura ya Kikanda iliyoainishwa katika Mipango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Kiuchumi. Hatua zilizofikiwa katika uendelezaji wa programu na miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

Ujenzi wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani

148. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu ujenzi wa vituo vya kutoa huduma kwa pamoja mipakani. Hadi sasa vituo viwili (2) kati ya saba (7) vinavyojengwa kwa uratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki vimekamiliwa na kuzinduliwa. Vituo hivyo ni kituo cha Holili/Taveta mpakani mwa Tanzania na Kenya; na kituo cha Rusumo mpakani mwa Tanzania na Rwanda.

149. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara iliratibu ukamilishaji wa Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Jumuiya ya Kusimamia Uendeshaji wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani. Kanuni hizo zimepitishwa na Mkutano wa 33 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya uliofanyika mwezi Februari, 2016. Ili kupata

uelewa wa pamoja kuhusu Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani, Wizara iliratibu na kushiriki katika mafunzo kwa maafisa wa Serikali, sekta binafsi na wawakilishi wa jamii kwa Vituo vya Horohoro na Sirari. Taarifa kuhusu vituo vingine na hatua zilizofikiwa ili kuwezesha kuanza kutoa huduma stahiki ni kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 2**.

150. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu ukamilishaji wa ujenzi wa Daraja la Kimataifa la Rusumo ikiwa ni sehemu ya kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na kuimarisha vituo vya kutoa huduma za pamoja mipakani katika ushoroba wa kati. Daraja hilo lenye uwezo wa kupitisha magari manne kwa wakati mmoja yenye uzito wa tani 56 kila moja lilizinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda tarehe 6 Aprili, 2016.

Uendelezaji wa Mtandao wa Barabara

151. **Mheshimiwa Spika**, hatua zilizofikiwa katika uendelezaji wa mtandao wa barabara za Kikanda katika mwaka 2015/2016 ni kama ifuatavyo:

Mradi wa Barabara ya Arusha – Holili/Taveta – Voi

152. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu uendelezaji wa mtandao wa barabara unaoziunganisha nchi za Tanzania na Kenya kupitia mpaka wa Holili/Taveta yenye urefu wa kilomita 234.3. Kwa upande wa Tanzania, awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami unahusisha upanuzi wa sehemu ya kutoka Arusha hadi Tengeru yenye urefu wa kilomita 14.1 kuwa njia nne na barabara ya mzunguko wa kusini mwa Jiji la Arusha yenye urefu wa kilomita 42.41. Aidha, kwa upande wa Kenya mradi unahusisha ujenzi wa barabara mpya ya lami yenye urefu wa kilomita 100 kutoka Taveta hadi Mwatate. Gharama za mradi kwa upande wa Tanzania ni takriban Shilingi bilioni 209.61 ambapo kati ya hizo Benki ya Maendeleo ya Afrika itatoa Shilingi bilioni 190.21 na Serikali ya Tanzania itatoa Shilingi bilioni 19.4.

153. **Mheshimiwa Spika**, Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Barabara hiyo liliwekwa mwezi Machi, 2016 na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya.

Uwianishaji wa Uzito wa Magari Katika Barabara

154. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Mwaka 2013 iliyopitishwa na Bunge la Afrika Mashariki imeridhiwa na Nchi zote Wanachama. Nchi Wanachama zimekamiliisha majadiliano ya kuandaa Kanuni

za kuwezesha utekelezaji wa Sheria hizo ambazo zilipitishwa katika Mkutano wa 33 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya uliofanyika Jijini Arusha mwezi Februari, 2016.

Mkakati wa Kuwezesha Sekta ya Uchukuzi

155. **Mheshimiwa Spika**, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeidhinisha utekelezaji wa Mkakati wa Kuwezesha Sekta ya Uchukuzi. Mkakati huo unazitaka Nchi Wanachama pamoja na masuala mengine kuwianisha mitaala ya mafunzo ya udereva wa magari ya biashara; usajili wa vyombo vya moto; na madaraja ya leseni. Nchi Wanachama zimekamilisha rasimu za mitaala ya mafunzo ya udereva wa magari ya biashara.

Sekta ya Mawasiliano

156. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kutatua Changamoto ya Gharama Kubwa za Maunganisho ya Simu za Mkononi katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ulivyoridhiwa na Wakuu wa Nchi wa Jumuiya hiyo mwezi Februari, 2015. Katika kutekeleza mpango huo, yamefanyika mapitio ya Kanuni zinazotumika katika mfumo wa kuongoza sekta ya mawasiliano nchini. Wizara ya kisekta inafanya tathmini ya changamoto zilizoibuliwa na wadau kuhusu mpango huo.

Sekta ya Hali ya Hewa

157. **Mheshimiwa Spika**, Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Ushirikiano katika Huduma za Hali ya Hewa ilisainiwa na Mawaziri wanaosimamia masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka Nchi Wanachama katika Mkutano wa 33 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Februari, 2016. Itifaki hiyo inatoa mwongozo wa ushirikiano wa Nchi Wanachama katika kubadilishana taarifa na ujuzi katika masuala ya hali ya hewa. Nchi Wanachama zimekubaliana kuridhia Itifaki hiyo kabla ya mwezi Julai, 2016.

Sekta ya Bandari na Usafiri Majini

158. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kurahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zinaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Usafiri wa Majini wa Afrika Mashariki. Katika kutekeleza azma hiyo, Utafiti wa Awali wa Hali ya Usafiri wa Majini na Sekta ya Bandari umekamilika. Ripoti ya Utafiti huo, pamoja na mambo mengine, imebainisha changamoto katika utekelezaji wa miradi ya kuendeleza Bandari katika mwambao wa Bahari ya Hindi, Maziwa na Uanzishaji wa Bandari Kavu.

Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa rasilimali fedha zinazohitajika katika kutekeleza Miradi iliyodainishwa katika Mipango Mkuu ya kuendeleza Bandari za Nchi Wanachama na haja ya kuwianisha Mifumo ya Kitaasisi na Udhibiti katika Sekta ya Usafiri wa Majini miongoni mwa Nchi Wanachama ili kuwa na viwango vinavyofanana katika udhibiti wa vyombo vya majini. Maoni ya Ripoti hiyo yatasaidia katika maandalizi ya Mkakati wa Afrika Mashariki wa Usafiri wa Majini.

Sekta ya Nishati

159. **Mheshimiwa Spika**, wakati wa Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Machi 2016, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Jamhuri ya Uganda walifanya Kikao cha pamoja kujadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda mpaka bandari ya Tanga litakalokuwa na urefu wa kilometa 1,410.

160. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia Kikao hicho cha Marais wawili, wataalam wa pande zote mbili waliendelea na majadiliano yaliyopelekea Serikali ya Uganda kutoa tamko rasmi kwenye Mkutano wa 13 wa Ushoroba wa Kaskazini uliofanyika mwezi Aprili, 2016 Jijini Kampala kuwa bomba hilo litajengwa kupitia Tanzania. Mradi huo utagharimu Dola za Marekani bilioni nne na kukamilika baada ya miaka mitatu hadi minne. Mradi huo unatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja takriban 1,500 na ajira zisizo za moja kwa moja 20,000. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika imeidhinisha msaada wa kiasi cha Dola za Marekani 1,691,130 kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Mradi mwingine wa Bomba la Mafuta la Mbarara - Mwanza - Isaka - Dar es Salaam. Fedha za nyongeza Dola za Marekani 95,600 zinahitajika ili kukamilisha upembuzi yakinifu huo. Hivyo, kila Nchi Mwanachama imetakiwa kuchangia kiasi cha Dola za Marekani 19,120 kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2016 ili kukamilisha upembuzi yakinifu wa Mradi huo.

Ushirikiano Katika Sekta za Huduma za Jamii

Sekta ya Elimu, Utamaduni na Michezo

Urazinishaji wa Mitaala

161. **Mheshimiwa Spika**, Waziri wa Maendeleo na Uratibu wa Zoezi la urazinishaji wa Mitaala kwa ngazi zote za Elimu pamoja na mafunzo ya ualimu kwa shule za awali, msingi na sekondari.

Shindano la Insha la Jumuiya

162. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika shindano la uandishi wa Insha la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililoshirikisha wanafunzi wa shule za sekondari kutoka nchi tano (5) Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kijana Mtanzania Simon Mollel Sabaya kutoka Shule ya Sekondari ya Mzumbe alilibuka mshindi wa kwanza katika shindano hilo. Huu ni ushahidi kuwa vijana wetu wanaweza na wanauelewa wa Jumuiya yetu. Naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi kwa kijana huyu na kuwatia moyo vijana wengine waendeleo kushiriki kwenye mashindano haya ili waweze kuliletea sifa Taifa letu. Natoa wito kwa walimu na wazazi kuwahamasisha wanafunzi kushiriki katika shindano hilo ili kukuza uelewa wao katika masuala ya Jumuiya. Wizara yangu kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki; Wizara za Elimu, Sayansi na Teknolojia; na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo itaanzisha kampeni ya kuongeza uelewa wa Jumuiya katika shule na vyuo.

Mdahalo wa Nne wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu

163. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ushiriki wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Tanzania katika mdahalo wa Nne (4) wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Desemba 2015, Kampala, Uganda. Lengo la mdahalo huo ni kupata washindi wawili kutoka kila Nchi Mwanachama wa Jumuiya ambao watakuwa Mabalozi wa Nchi zao katika masuala ya Jumuiya. Kwa upande wa Tanzania, washindi wa mwaka 2015 ni Raphael Kambamwene wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Lucy Peter Funja wa Chuo Kikuu cha Ardhi. Aidha, Wizara inaendelea na jukumu la kuwapatia taarifa Mabalozi hao zitakazowawezesha kutoa elimu kwa umma hususan kwa vijana wenzao.

Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki

164. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki imeshahamia rasmi katika Makao Makuu yake yaliyopo Zanzibar. Hii ni kufuatia kusainiwa kwa Mkataba wa Uenyaji baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 28 Desemba, 2015.

Mradi wa Hifadhi ya Mazingira Katika Bonde la Ziwa Victoria Awamu ya Pili

165. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na athari za mazingira zinazotokana na shughuli za binadamu katika Bonde la Ziwa Victoria zilizosababisha pamoja na mambo mengine kupungua kwa kina cha maji na samaki katika ziwa, Wizara imeendelea na uratibu wa utekelezaji wa shughuli za

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria. Katika kipindi hiki, Benki ya Dunia iliongeza muda wa miaka miwili na nusu kuanzia mwezi Juni 2015 hadi mwezi Desemba 2017 na mkopo wa Dola za Marekani milioni 10 ambazo zitatumika kukamilisha miradi ambayo ilikuwa haijakamilika katika Awamu ya Pili ya Mradi iliyofikia ukomo wake mwezi Juni 2015 na kuandaa Awamu ya Tatu. Vilevile, udhibiti wa magugumaji katika Ziwa Victoria umeendelea ambapo magugumaji yamepungua Ziwani kutoka hekta 520 mwezi Septemba, 2009 hadi hekta 104 mwezi Novemba, 2015. Mradi umeendelea na shughuli za udhibiti wa utupaji taka na uhamasishaji wa uzalishaji bora viwandani ambapo Jumla ya viwanda 118 sawa na asilimia 86 vimepata mafunzo ya uzalishaji bora viwandani.

Programu ya Hifadhi ya Mazingira kwa Kuboresha Sera, Mabadiliko ya Tabianchi, Utafiti na Maendeleo ya Kiuchumi

166. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kunakuwa na matumizi endelevu ya rasilimali maji katika Bonde la Mto Mara, Wizara yangu imefanikisha utiaji saini wa Hati ya Makubaliano ya Usimamizi wa pamoja wa rasilimali maji katika Bonde la Mto Mara kati ya Tanzania na Kenya. Makubaliano hayo yatasaidia kupunguza athari za mazingira zinazosababishwa na shughuli za binadamu katika bonde hilo.

Mradi wa Idadi ya Watu, Afya na Mazingira wa Jumuiya

167. **Mheshimiwa Spika**, ili kujenga uelewa wa pamoja kwa wananchi katika masuala ya idadi ya watu, afya na mazingira kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika maandalizi ya Mpango Mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Masuala ya Idadi ya Watu, Afya na Mazingira. Mpango huo utakapokamilika utatoa mwongozo wa kuzingatia masuala ya idadi ya watu, afya na mazingira katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Nchi Wanachama.

Sekta ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii

168. **Mheshimiwa Spika**, nafasi ya wanawake, watoto na vijana imeendelea kupewa kipaumbele katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa muktadha huo, Wizara imeendelea kuratibu programu na miradi inayolenga kuyajengea uwezo makundi hayo ili kunufaika na fursa mbalimbali zinatokanazo na Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, programu hizi zimetoa fursa kwa makundi hayo kutoa maoni yao ya namna bora ya kuendeleza mtangamano. Vilevile, Jumuiya ya Afrika Mashariki inakamilisha Sera ya Watoto ya Jumuiya.

Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama

169. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imepata Katibu Mkuu mpya Balozi Libérat Mfumukeyo kutoka Jamhuri ya Burundi atakeyeiongoza Jumuiya kwa Kipindi cha miaka mitano ijayo. Aidha, naomba kumshukuru Balozi Dkt. Richard Sezibera kutoka Jamhuri ya Rwanda kwa mchango wake mkubwa katika kuiendesha Jumuiya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Ushirikiano katika Siasa

170. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki tumeendelea kushuhudia kushamiri kwa demokrasia katika Nchi Wanachama wa Jumuiya. Kwa kuzingatia kwamba demokrasia ni moja ya misingi mikuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara yangu imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika timu ya waangalizi wa uchaguzi mkuu kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki kushiriki katika uangalizi wa uchaguzi mkuu katika Nchi Wanachama. Katika kipindi hiki, Nchi tatu Wanachama wa Jumuiya zilifanya uchaguzi mkuu wa Rais na Wabunge. Nchi hizo ni Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda. Jamhuri ya Burundi ilifanya Uchaguzi wake mwezi Julai, 2015 ambapo Rais Pierre Nkurunziza aliibuka mshindi wa Uchaguzi huo. Aidha, kwa upande wa Uchaguzi Mkuu wa Tanzania, Wizara iliratibu ushiriki wa waangalizi wa uchaguzi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki waliokuja kufanya uangalizi ambapo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipata ushindi katika uchaguzi huo.

171. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia iliratibu ushiriki wa Tanzania katika timu ya waangalizi wa uchaguzi wa Jumuiya kwenye uchaguzi mkuu wa Uganda uliofanyika mwezi Februari, 2016. Katika uchaguzi huo, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili alipewa heshima ya kuwa Kiongozi wa timu hiyo kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Mheshimiwa Rais Yoweri Kaguta Museveni aliibuka mshindi.

172. **Mheshimiwa Spika**, katika kuwashirikisha zaidi wananchi wa Afrika Mashariki kuchangia maoni yao katika maamuzi mbalimbali ya uendeshaji wa Jumuiya, Wizara yangu iliwawezesha Wananchi wa Tanzania kupitia asasi zao kushiriki katika Mkutano wa Katibu Mkuu wa Jumuiya na Asasi Zisizo za Kiserikali na Sekta Binafsi uliofanyika mwezi Machi, 2016 Dar es Salaam, Tanzania. Maazimio ya Mkutano huo yalikuwa ni pamoja na kuliomba Baraza la Mawaziri la Jumuiya kuharakisha matumizi ya vituo vya utoaji wa huduma kwa pamoja mipakani, utekelezaji wa himaya moja ya forodha; na kushirikisha sekta binafsi katika ngazi zote za mchakato wa uchaguzi ili kuweka mazingira mazuri ya kufanya shughuli zao.

Bunge la Afrika Mashariki

173. **Mheshimiwa spika**, Wizara iliratibu na kushiriki katika mikutano ya Bunge la Afrika Mashariki, ambapo Bunge hilo lilijadili na kupitisha Miswada ya Sheria za Jumuiya, Maazimio na Taarifa mbalimbali. Miswada iliyopitishwa ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Kupunguza na Kukabiliana na Majanga wa mwaka 2012; Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Miamala ya Kielektroniki wa mwaka 2014; Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Tasnia ya Ubunifu na Utamaduni wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2015; na Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usimamizi na Uhifadhi wa Misititu wa mwaka 2015.

174. **Mheshimiwa spika**, aidha, Miswada iliyosomwa Bungeni kwa mara ya kwanza ni: Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usawa wa Jinsia na Maendeleo wa mwaka 2016; Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kulinda Watoa Taarifa wa mwaka 2016; Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mafao ya Kustaafu kwa baadhi ya Wakuu wa Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2016; Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki wa mwaka 2016; na Muswada wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa mwaka 2016.

175. **Mheshimiwa spika**, Vilevile, Bunge lilitoa Maazimio kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kusisitiza Kuridhia Itifaki ya Umoja wa Afrika ya kuanzisha Bunge la Afrika; Kuridhia Itifaki ya Sheria ya Ushauri ya Umoja wa Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika; Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi wake katika uchaguzi Mkuu pamoja na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kudumisha Amani na Demokrasia wakati wa Uchaguzi; Azimio la Bunge la Kuzitaka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuchukua hatua za haraka katika kudhibiti Usafirishaji haramu wa binadamu; na Azimio la Bunge la kuwashukuru Wake wa Viongozi wa Nchi Waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

176. **Mheshimiwa spika**, Kamati ya Bunge la Afrika Mashariki ya Masuala ya Kikanda na Utatuzi wa Migogoro ilifanya ziara ya Uangalizi na tathmini ya changamoto za utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja katika Kanda ya Kati mwezi Novemba 2015. Kamati hiyo na Uongozi wa Wizara ilijadili hali halisi ya utekelezaji wa makubaliano ya Itifaki hiyo hususan katika kanda ya kati ambapo kati ya masuala yaliyoibuliwa ni kuhusu afya ya Wananchi katika kutumia uhuru wa watu wa Jumuiya kuingia na kutoka Nchi za Jumuiya ambapo walisisitiza kuhusu umuhimu wa Chanjo ya Homa ya Manjano ili kuzuia uambukizaji wa ugonjwa huo.

177. **Mheshimiwa Spika**, Kamati mbalimbali za Bunge la Afrika Mashariki zilifanya mikutano ya kukusanya maoni ya wadau kuhusu utungwaji wa sheria mbalimbali za Jumuiya ambapo Kamati ya Mawasiliano, Biashara na Uwekezaji ilikusanya maoni ya Muswada wa Sheria ya *Sectional Properties Bill*, 2016, Kamati ya Kilimo, Maliasili na Mazingira ilikusanya maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Misituta wa Afrika Mashariki wa mwaka 2015 na Kamati ya *General Purpose* ilikusanya maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu wa mwaka 2015.

178. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu Programu ya Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Jumuiya ya kutoa elimu kwa umma iliyohusisha Vyombo vya Habari, Taasisi za Elimu, Asasi za Kiraia, Wabunge na Maafisa wa Serikali mwezi Aprili, 2016. Lengo la programu hiyo pamoja na mambo mengine ni kuhamasisha umma juu ya fursa zitokanazo na Jumuiya ili kunufaika nazo.

Ushirikiano katika Ulinzi

179. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha uwezo wa vyombo vya ulinzi na usalama vya Nchi Wanachama katika urejeshaji amani wakati wa machafuko, kukabiliana na ugaidi, uharamia na majanga, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika zoezi la kijeshi kwa vyombo vya ulinzi na usalama kutoka nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki la Vituo vya Kamandi Ijulikanalo kama '*Ushirikiano Imara 2016*'. Zoezi hilo lilifanyika mwezi Machi 2016 nchini Kenya.

Ushirikiano katika Usalama

180. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa amani na usalama ni nguzo kuu kwa maendeleo ya kijamii na uchumi katika Jumuiya, Wizara yangu iliratibu ushiriki wa Tanzania katika mkutano wa Wakuu wa Upelelezi toka Jeshi la Polisi, Wasajili wa Magari, Wakuu wa Kupambana na Madawa ya Kulevywa na Wakuu wa Vitengo vya Kupambana na Biashara Haramu ya Watu uliofanyika mwezi Desemba 2015 Nairobi, Kenya. Mkutano huo ulitoa fursa kwa wakuu hao kubadilishana uzoefu na taarifa za mienendo ya uhalifu katika maeneo yao na kupanga mpango wa pamoja wa operesheni za kupambana na uhalifu. Aidha, Nchi Wanachama zinaendelea kutekeleza Mkakati wa Kikanda wa Amani na Usalama.

181. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jamhuri ya Sudan Kusini imejiunga rasmi na Jumuiya na hivyo kuifanya idadi ya Nchi Wanachama kuongezeka kutoka tano hadi sita. Nchi ya Sudan Kusini, iliwasilisha rasmi maombi ya kujiunga na Jumuiya mwezi Novemba, 2011. Nchi Wanachama zilikamilisha mchakato wa uhakiki kuthibitisha iwapo nchi hiyo inakidhi vigezo kulingana na matakwa ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya

ya Afrika Mashariki. Mkutano wa 17 wa Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika mwezi Machi 2016 jijini Arusha uliridhia nchi hiyo kujiunga na Jumuiya.

182. **Mheshimiwa Spika**, Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya walimpa heshima Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya kusaini Mkataba wa Jamhuri ya Sudan Kusini kujiunga na Jumuiya kwa niaba yao. Zoezi la utiaji saini Mkataba huo, lilifanyika Dar es Salaam tarehe 15 Aprili, 2016.

183. **Mheshimiwa Spika**, kujiunga kwa Jamhuri ya Sudan Kusini kumeifanya Jumuiya kuwa na jumla ya watu zaidi ya milioni 160, hii ni fursa ya kipekee kwa sekta binafsi hapa nchini katika kuendeleza na kukuza biashara zao. Naomba kuchukua nafasi hii kuishauri sekta binafsi hapa nchini kuchangamkia fursa zitokanazo na kupanuka kwa soko la Jumuiya.

Kutoa elimu ya Mtangamano wa Afrika Mashariki ili Wananchi waweze kuelewa na kutumia fursa zitokanazo na Mtangamano

184. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wake wa Mawasiliano kwa kutoa Elimu kwa Umma kuhusu fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na jinsi ya kunufaika nazo. Wizara ilitumia maonesho mbalimbali kama vile ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Saba Saba, Nane Nane, Maonesho ya Biashara Zanzibar, maonesho ya Siku ya Mara, Maonesho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani na Juakali/Nguvu Kazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoa elimu kwa Umma. Jumla ya nakala za machapisho 11,046 yenye taarifa muhimu na fursa zipatikanazo kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki yalisambazwa na jumla ya wananchi 7,387 walitembelea Mabanda ya Wizara ili kupata taarifa na ufafanuzi wa masuala ya mtangamano. Taarifa za maonesho hayo zilisambazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo Luninga, tovuti na blogu ya Wizara. Vilevile, makala ya Televisheni yenye ujumbe wa fursa mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki ilioneshwa katika Luninga za TBC1, Star TV, Channel 10 na Clouds TV.

185. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu iliweka mabango saba katika mipaka ya Namanga, Horohoro, Holili, Sirari, Mutukula, Rusumo na Kabanga yenye kuelezea taratibu za kufuatwa na wafanyabiashara wakati wa kuuza na kununua bidhaa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

186. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliendesha mikutano ya elimu kwa umma katika Mikoa ya Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Mara, Kagera, Mtwara, Lindi na katika mipaka ya Mutukula, Rusumo, Kabanga, Holili na Namanga. Aidha, Wizara iliendesha warsha ya Waandishi wa Habari wa

Zanzibar kwa lengo la kuwaelimisha juu ya fursa na masuala ya Mtangamano ili waweze kufikisha taarifa sahihi za Mtangamano kwa wananchi.

Kuimarisha Utendaji wa Kujenga Uwezo wa Wizara

187. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliendelea kuimarisha uwezo wa kiutendaji kwa kupandisha vyeo watumishi 20 baada ya kukidhi Vigezo vya Kisheria kama vilivyoainishwa katika Miundo yao ya Utumishi pamoja na kutengewa fedha katika Makisio ya Ikama na Bajeti ya Mishahara ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, Wizara iliwabadilisha kada jumla ya watumishi watatu wa kada tofauti baada ya kujiendeleza kitaaluma wakiwa kazini na kupata sifa stahiki. Vilevile, watumishi 29 wamethibitishwa kazini na watumishi 15 wa kada mbalimbali walithibitishwa katika vyeo vyao vipya baada ya kukidhi vigezo.

188. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa Wizara inawajengea uwezo wa kitaaluma watumishi wake ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi, Wizara iliandaa na kutekeleza mpango mdogo wa mafunzo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambao hadi kufikia mwezi Februari 2016 watumishi wawili (2) walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi tisa (9) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Mpango huu mdogo ni utekelezaji wa mpango wa mafunzo wa Wizara wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2017/2018.

USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI

189. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika Mapato na Matumizi ya Fedha za Umma kwa kuzingatia sheria na kanuni za fedha za umma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imeendelea kupata Hati Safi ya Ukaguzi wa Hesabu. Kwa mujibu wa ripoti ya Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15, Fungu 34 na 97 pamoja na balozi 34 zilizokuwepo kwa wakati huo zimepata Hati Safi. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza watendaji wa Wizara na kuwahimiza waendeleo kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya matumizi ya fedha za Serikali.

CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

190. **Mheshimiwa Spika**, Changamoto ambazo Wizara imekabiliana nazo katika utekelezaji wa majukumu yake ni kama ifuatavyo:

i. Kasi ndogo ya ubadilishaji wa Sheria za Nchi ili kuendana na matakwa ya Itifaki ya soko la pamoja la Afrika Mashariki;

ii. Kasi ndogo ya sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki na masoko ya kimataifa; na uelewa mdogo wa Watanzania kuhusu masuala ya Mtangamano;

iii. Kasi ndogo ya Watanzania kuchangamkia fursa za ajira zilizopo kwenye taasisi za kikanda na kimataifa;

iv. Kuendelea kuibuka kwa vikwazo vipya visivyo vya kiforodha ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

v. Wigo mdogo wa uwakilishi nje. Hadi hivi sasa, Tanzania ina Balozi 35 na Konseli Kuu 3 duniani. Uwakilishi huu ni mdogo kuweza kukidhi mahitaji ya nchi hususan katika kipindi hiki ambacho fursa mbalimbali zinaibuka kila kona ya dunia.

191. **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu Wizara yangu imejipanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kuendelea kuzihimiza sekta husika kutoa kipaumbele na kuongeza kasi ya ubadilishaji wa sheria zilizoinishwa ili kuwawezesha Watanzania kunufaika ipasavyo na fursa za soko la pamoja;

ii. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusiana na fursa zitokanazo na ushiriki wa nchi yetu katika Jumuiya za kikanda na kimataifa, na kupitia makubaliano na mikataba mbalimbali kwa lengo la kuhamasisha Watanzania kuzitumia ipasavyo;

iii. Kuendelea kuhamasisha Watanzania kujitokeza pindi fursa za ajira zilizopo kwenye taasisi za kikanda na kimataifa zinapotangazwa;

iv. Kuendelea kuratibu uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha nchini ili kuwavutia wafanyabiashara kutoka ndani ya Jumuiya kununua bidhaa zinazozalishwa nchini na kutumia bandari zetu kikamilifu; na

v. Wizara itaendelea kuimarisha Balozi zetu na kufungua ofisi za uwakilishi kwenye maeneo yenye maslahi kwa taifa.

SHUKRANI

192. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kutekeleza sehemu ya majukumu yaliyotajwa hapo juu kwa ushirikiano na washirika wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kitaifa, kikanda, kimataifa pamoja na sekta binafsi. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Australia, Brazil, Canada, China, Cuba,

Denmark, Finland, India, Italia, Ireland, Japan, Korea Kusini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Malta, Norway, Oman, Poland, Qatar, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno, Urusi, Uswisi, Uturuki, Umoja wa Ulaya, AfDB, African Capacity Building Facility, FAO, IAEA, ILO, IMF, IOM, Investment Climate Facility for Africa, UNDP, UNEP, UN-HABITAT, UNWTO, UNHCR, UNICEF, UNFPA, UNESCO, UNIDO, WHO, TradeMark East Africa, The Association of European Parliamentarians with Africa, World Bank na WWF kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Diplomasia ya uchumi.

MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

193. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na mambo mengine, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imepanga kutekeleza malengo makuu muhimu kulingana na majukumu yake kama ifuatavyo:-

i. Kuitangaza nchi yetu kama moja ya nchi duniani zenye mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji kutokana na historia yake ya miaka mingi ya amani, umoja, utulivu na mshikamano wa kitaifa;

ii. Kuongeza uwakilishi wetu nje ya nchi kwa kufungua Balozi mpya, Ofisi za Kikonseli na kuimarisha rasilimali watu na fedha;

iii. Kuendelea kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosainiwa kati ya nchi yetu na nchi nyingine na ile ya mashirika ya kikanda na kimataifa;

iv. Kukamilisha mchakato wa kuitambua jumuiya ya watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya taifa;

v. Kuratibu majadiliano kuhusu maeneo ya ushirikiano katika uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi, kijamii na kuendeleza ushirikiano katika sekta za uzalishaji;

vi. Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa miaka kumi wa Umoja wa Fedha katika kuelekea kwenye eneo la Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

vii. Kuratibu majadiliano na kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za Kikanda kuhusu kuanzisha Eneo Huru la Kibiashara na Kiuchumi;

viii. Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano na utekelezaji wa makubaliano katika maeneo ya siasa, ulinzi na usalama;

ix. Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano na utekelezaji wa hatua za Mtangamano wa Afrika Mashariki; na

x. Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zinazopatikana katika Jumuiya hiyo.

MAKADIRO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

194. **Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imepangiwa bajeti ya kiasi cha shilingi 151,396,775,000.00 Kati ya fedha hizo shilingi 143,396,775,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 8,000,000,000.00 ni kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo.

195. **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017, shilingi 133,056,021,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 10,340,754,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara. Kati ya fedha za Matumizi Mengineyo shilingi 720,160,000.00 ni kwa ajili ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Tanzania, shilingi 3,154,721,000.00 ni kwa ajili ya fedha za Mishahara na Matumizi Mengineyo ya Chuo cha Diplomasia na shilingi 686,298,378.00 ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

196. **Mheshimiwa Spika**, katika fedha za bajeti ya maendeleo za kiasi cha shilingi 8,000,000,000.00 zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kiasi cha shilingi 2,375,250,000.00 zitatumika kufanikisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ambalo ni sehemu ya Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Julius Nyerere; shilingi 1,316,435,000.00 zitatumika kukamilisha ukarabati jengo la ghorofa tisa (9), makazi ya Balozi na Mkuu wa Utawala Ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji; shilingi 2,172,880,000.00 zitatumika kukarabati makazi ya Balozi na watumishi yaliyopo Stockholm, Sweden; shilingi 1,813,871,000 zitatumika kukarabati majengo mawili yanayomilikiwa na Serikali yaliyopo Khartoum, Sudan na shilingi 321,564,000.00 kwa ajili ya kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Wizara na Balozi za Tanzania nje.

197. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Balozi zake, inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 24,001,150,000.00 kama maduhuli ya Serikali.

HITIMISHO

198. **Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyotajwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya Shilingi 151,396,775,000.00. Kati ya fedha hizo Shilingi 143,396,775,000.00. ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 8,000,000,000.00. ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

199. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

200. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Tunaendelea. Sasa tupate taarifa ya Kamati iliyofanya kazi hiyo kwa niaba ya Bunge. Nani anawasilisha kwa niaba ya Kamati? Makamu Mwenyekiti, karibu. (Makofi)

MHE. KAN. MST. MASOUD ALIY KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu; nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mfenesini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji na malengo ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu ya Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na JKT. Aidha, kwa kuzingatia Kifungu cha 7(1) na ya (2) ya nyongeza hiyo, Kamati inalo jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (7) cha Nyongeza ya Nane kimeainisha jukumu la Kamati hii, pamoja na mambo mengine ni kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) Kamati ilipaswa kutumia siku zisizozidi tisa kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii ilifanyika tarehe 14 Aprili, 2016 katika Ukumbi wa GEPF Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inalenga kufafanua kuhusu mambo manne yafuatayo:-

- (i) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2015/2016;
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mapato ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017; na
- (iv) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara hii Fungu 34 kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufanya ulinganisho kati ya bajeti inayoekelezwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2016/2017, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016. Wakati wa kutekeleza shughuli hiyo, Kamati ililinganisha na kuhoji masuala kadhaa kama yalivyoorodheshwa katika ukurasa namba nne na tano wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa – Fungu 34, liliidhinishiwa jumla ya shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya Mradi Namba 391 uliojulikana kama *Acquisition, Expansion and Rehabilitation of Mission's Building* ambao ni Mradi wa Ununuzi, Ujenzi na Ukarabati wa Majengo Balozini na Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya mradi huu yalikuwa ni:-

- (i) Makao Makuu ya Wizara;
- (ii) Ubalozi wa Tanzania, Maputo;

- (iii) Ubalozi wa Tanzania, Stockholm – Sweden; na
- (iv) Jengo la Kitega Uchumi, Nairobi – Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu haikuwahi kukagua miradi ya maendeleo ya Wizara hii kama inavyotakiwa na Kanuni ya 98(1) ya kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kutokana na baadhi ya changamoto zilizojitokeza, ikiwemo ya miradi kutopatiwa fedha zozote kutoka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaamini kuwa kutokana na juhudi zinazoendelea, itawezeshwa ili kwenda kutembelea na kukagua miradi pamoja na kazi nyingine zinazotekelezwa na Wizara hii iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulijikita katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Wizara hii Fungu 34 ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi 20,036,019,000 kupitia Balozi 34 zilizopewa kasma 2001 hadi 2034. Katika makadirio hayo, Ubalozi uliopo Washington, Marekani, kasma 2018, uliongoza kwa kuwa na lengo kubwa la makusanyo lililofikia kiasi cha shilingi 4,169,148,876.36, sawa na 22.45% ya jumla ya makadirio ya makusanyo yaliyokadiriwa kwa Balozi zote 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, haikupangiwa kukusanya maduhuli yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, mwisho wa robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti, jumla ya shilingi 13,354,340,715 zilikusanywa katika Ofisi za Balozi zetu mbalimbali, kiasi cha asilimia 66.6 ya makadirio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, kiwango cha makusanyo kingetakiwa kufikia siyo chini ya asilimia 75, hivyo kiwango kilichokusanywa cha asilimia 66.65 kipo nyuma kwa asilimia 8.55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 110,877,655,389 kati ya shilingi 146,958,917,246. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 75.4 ya bajeti yake kwa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, Wizara iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya shilingi 8,000,000,000. Uchambuzi unaonyesha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, Wizara ilikuwa haijapokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufafanuzi huo, Kamati imebaini kuwa katika bajeti ya uendeshaji na mishahara, mwenendo wa upatikaji wa fedha ulikuwa mzuri. Changamoto kubwa ilikuwa kwenye upatikanaji wa fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni dhahiri kuwa kwa namna hii ya upatikanaji wa fedha, siyo rahisi kufanikisha malengo ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitaka kujiridhisha zaidi kuhusu mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha kwa kasma mbalimbali za Wizara hii. Ili kufanikisha azma hiyo, ulinganisho ulifanyika kwa kasma za mishahara, matumizi mengineyo na matumizi ya maendeleo kama inavyonekana katika jedwali Na. 1 la taarifa hii. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa uzito wa miradi ya maendeleo wakati wa bajeti ulikuwa asilimia 5.4 lakini katika upatikanaji wa fedha kutoka Hazina uzito ulikuwa ni 0%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwonekano huo, ni dhahiri kuwa nguvu zaidi zinahitajika ili kupata ufanisi katika azma ya Serikali kuwa na bajeti ya miradi ya maendeleo na kuweza kukabiliana na changamoto za Wizara hii kwa nia ya kuleta mtazamo mzuri katika jicho la Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti hizo na uzito unaowekwa kwenye miradi ya maendeleo wakati wa bajeti na wakati wa utekelezaji, zinaonyeshwa katika taarifa hii kwa kutumia chati ya duara Na. 1 na Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa asilimia 6.4 ya kiasi cha fedha zilizotolewa na Hazina hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 ni mishahara na 93.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja lisilopendeza ni kuwa fedha za matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazikupatikana kabisa. Kwa kuwa fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa baadhi ya majengo ya Balozi zetu nje ya nchi, tafsiri ya kutopokelewa fedha za miradi ya maendeleo ni kuwa kwa mwaka mzima wa 2015/2016, haikuwepo juhudi ya kuboresha au kununua majengo kwa ajili ya Balozi zetu. Kwa mwenendo huu, Kamati ina maoni kuwa hali hiyo inahitaji hatua za uamuzi mahsusi wa kunusuru hali mbaya ya majengo ya Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, utekelezaji wa majukumu ya iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na sasa Wizara

hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016, ilitegemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha ambao kwa upande wa miradi ya maendeleo haukuwa mzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa iliyokuwa Wizara ya Afrika Mashariki, uchambuzi unaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, kilipokelewa kiasi cha shilingi 16,886,897,117 kati ya shilingi 22,102,756,303 sawa na asilimia 76.4 ya bajeti yake ya matumizi. Aidha, hakuna kiasi chochote kilichokuwa kimeidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 umezingatia rejea zilizoainishwa katika ukurasa wa 15 na 16 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa rejea hizo, Kamati ilichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makadiro yaliyowasilishwa kwenye Kamati, ilielezwa kuwa ofisi zetu za Balizi zinakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 24,001,257,737 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kiasi hiki ni asilimia 15.85 ya bajeti ya Wizara inayokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ikilinganishwa na kiasi cha asilimia 13.63 ya bajeti ya Wizara hii kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujiridhisha na mwenendo wa ukadiriaji, Kamati ililinganisha makadirio hayo ya maduhuli na makadirio ya mwaka wa fedha 2015/2016. Uchambuzi ulibainisha kuwa makadirio ya mwaka 2016/2017 ni ongezeko la asilimia 16.52 ikilinganishwa na makusanyo yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Serikali inaonesha kuwa makadirio ya maduhuli ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa maana ya utekelezaji wa bajeti hayakujumuishwa kama sehemu ya bajeti ya matumizi mengineyo ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huo ambao unatofautiana kidogo na ule wa miaka iliyopita ya 2014/2015 na 2015/2016, fedha zinazotarajiwa kuidhinishwa na Bunge zote zinatakiwa zipatikane moja kwa moja kutoka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaomba kuidhinishwa kiasi cha shilingi 151,396,775,000. Kamati ililinganisha makadirio hayo na jumla ya bajeti iliyoidhinishwa kwa iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa

Kimataifa pamoja na iliyokuwa Wizara ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2015/2016. Uchambuzi umebainisha kuwa kiuhalisia makadirio hayo yamepungua kwa kiasi cha shilingi 17,664,898,549 sawa na upungufu wa asilimia 10.4. Mchanganuo huo umeainishwa katika jedwali Na. 3 katika ukurasa namba 18 na 19 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya tofauti hiyo inaweza kuwa ni kuongezeka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani ikilinganishwa na mwaka 2015/2016 au kupungua kwa uzito unaowekwa katika shughuli zinazotekelezwa na Wizara hii ikilinganishwa na mwaka 2016/2017. Hali halisi ya thamani ya fedha ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani kwa sasa haioneshi kuongezeka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Ni dhahiri kuwa uzito wa kibajeti kwa masuala ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki umepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi wa makadirio ya matumizi ulifanyika kwa kuoanisha kasma za matumizi ya Balozi zetu 35 zenye vifungu (*subvotes*) 2001 hadi 2035 na kubaini kuwa kasma za Balozi hizo kwa ujumla zimeombewa jumla ya shilingi 109,884,906,000. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 72.58 ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika Bajeti inayoombwa ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya Balozi za Tanzania nje ya nchi asilimia 76.6 inaombwa kugharamia shughuli za kawaida za Balozi wa Tanzania nje ya nchi. Ni wazi kuwa shughuli za msingi za Wizara hii zinatekelezwa na Balozi zetu kwa gharama ambayo ni asilimia 76.6 ya gharama ya utekelezaji wa jumla majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uwiano wa matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishwa jumla ya shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo Balozi na Makao Makuu ya Wizara chini ya Mradi Namba 6391 ambao katika Kitabu cha Nne cha Bajeti, *Supply Votes, Volume IV*, unasomeka *Acquisition Expansion and Rehabilitation of Mission's Buildings*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hicho ni sawasawa na kiasi kilichoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ingawa fedha hazikupatikana kabisa. Aidha, fedha hizi zinazombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni asilimia 5.3 ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzito wa umuhimu wa bajeti ya kugharamia mradi wa maendeleo kitaifa ni asilimia 40, wakati uzito huo kwa Wizara hii ni asilimia 5.3 tu. Ni maoni ya Kamati kuwa uwiano huo ulipaswa kuboreshwa zaidi na hasa ikizingatiwa kuwa hali ya Balozi zetu nje ya nchi si ya kuridhisha. Kwa

mfano, majengo, magari na zana nyingi za kutendea kazi kwa Balozi zetu mbalimbali nje ya nchi zinahitaji kuboreshwa, jambo ambalo likipangwa vizuri, uwiano huu utabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi huo, Kamati ilirejea sera na miongozo mbalimbali inayotumika katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pamoja na matarajio ya wananchi kwa Bunge lao katika kuisimamia na kuishauri Wizara hii na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mafunzo ya Diplomasia;

(i) Wizara iweke uzito katika vifungu vinavyohusu watumishi kupatiwa mafunzo katika Balozi zake zote duniani ili kukuza weledi wa utekelezaji wa kazi zao za uwakilishi wa nchi yetu;

(ii) Kwa kuwa ujenzi wa Chuo cha Kidiplomasia – Bagamoyo ulishindikana kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kushindwa kulipa fidia ya eneo; na kwa kuwa Wizara imetoa eneo mbadala la Lakilaki, Mkoani Arusha kwa ajili ujenzi wa Chuo hicho, Serikali itoe kipaumbele katika kuliimarisha eneo hilo kwa njia mbalimbali ikiwemo kuingia ubia na wawekezaji wenye masharti nafuu;

(iii) Kutokana na mwelekeo wa dunia ulivyo hivi sasa kuhusu uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa, Serikali kupitia Chuo cha Diplomasia, iweke mitaala ambayo itazalisha wataalamu wengi wa fani ya Diplomasia za Kiuchumi. Aidha, chuo hicho kijitawanye na kujipanua kwa kuandaa mafunzo ya Kidiplomasia katika sehemu mbali mbali za ndani na nje ya nchi.

Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje;

(i) Serikali itoe ukomo wa Bajeti ya Wizara hii ambao ni wa uhalisia katika utekelezaji wa kazi zake ili kufanya kazi hizo kwa kiwango kinachotakiwa cha Kimataifa na kuepuka aibu inayoweza kujitokeza kwa nchi yetu;

(ii) Kamati inasisitiza kuendelea kutekelezwa kwa ushauri uliotolewa mwaka 2015/2016 kuhusu kuongeza juhudi za uboreshaji wa majengo ya Ofisi na makazi ya watumishi Balozini pamoja na kuzipatia Balozhi hizo vitendea kazi vya kisasa;

(iii) Serikali itafute fedha kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na Taasisi nyingine za kifedha duniani kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Kibalozi ambazo zikijengwa vizuri zitaweza kutumika kama vitega uchumi kama vile linavyotumika jengo la Ubalozi wa Tanzania lilioko Umoja wa Mataifa,

New York – Marekani. Aidha, zile Balozi ambazo bado zinakodisha nyumba, mikakati ianze kwa kuanza kuwa na nyumba zetu wenyewe;

(iv) Wizara iangalie upya watumishi walioko katika Balozi mbalimbali duniani na kufanya marekebisho yatakayohakikisha wanaopelekwa na kubakishwa ni wale wenye fani na uwezo wa kushika nafasi zinazohusu shughuli za Ubalozi ili kuleta ufanisi katika diplomasia ya uchumi;

(v) Kwa kuwa Sera ya Mambo ya Nje haijafanyiwa mapitio tangu mwaka 2001, Wizara ifanye mapitio ya sera hiyo ili iendane na mazingira ya sasa kiuchumi, kisisasa na kijamii; *(Makofi)*

(vi) Serikali itoe fedha kwenye Balozi zetu nje ili kueneza Sera ya Diplomasia ya Uchumi ambayo itatuongezea wawekezaji na watalii; *(Makofi)*

(vii) Serikali itoe fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo katika Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, Serikali ihakikishe Balozi ambazo zinakodisha nyumba na ofisi zinajengewa majengo yake; *(Makofi)*

(viii) Serikali ipeleke fedha Ubalozi kwa ajili ya kuwarejesha Maafisa wote waliomaliza muda wao katika Balozi. Aidha, Wizara iangalie uwezekano wa kuacha kutoa barua kwa maafisa kurejea nyumbani kama fedha kwa ajili ya shughuli hiyo hazijatolewa; *(Makofi)*

(ix) Wizara itume fedha mapema kwa ajili ya malipo ya kodi ya pango la nyumba za watumishi Ubalozi ili kuepusha usumbufu unaojitokeza; *(Makofi)*

(x) Balozi za Heshima zifunguliwe katika sehemu ambazo ni muhimu kwa faida ya nchi hususan nchi zenye wawekezaji na watalii wengi. Hii ifanyike kwa kuanzia katika nchi jirani;

(xi) Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka Waambata wa Biashara na Utalii kwa Balozi maalum ambazo zina muono wa kuleta wawekezaji na watalii kwa wingi. Aidha, Waambata hao wagharamiwe na Wizara zao ili kupunguza gharama zinazoelekea Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

(xii) Serikali ihakikishe kuwa viwanja ambavyo vimenunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Balozi zetu nje ya nchi vijengwe kabla havijachukuliwa na nchi husika. Mfano, kiwanja cha Ubalozi wa Tanzania; Oman, Rwanda na Uingereza. *(Makofi)*

Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Kimataifa:-

(i) Wizara iendelee kukuza mahusiano na nchi za Afrika Mashariki na Kimatatifa. Aidha, Kamati inaisifu Wizara ambayo ilishirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kufanikisha zabuni ya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Bandari ya Tanga;

(ii) Wananchi wa Tanzania kwa ujumla bado hawajaelewa dhana nzima ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuwa hali hii imewafanya wananchi walio wengi kutojikusisha katika biashara zenye manufaa kwa kuitumia Jumuiya hiyo, Serikali ichukue hatua maalum ya kuwaelimisha wananchi kuhusu faida na hasara ya Jumuiya hiyo;

(iii) Kwa ujumla Tanzania imekuwa ikinunua zaidi bidhaa za nchi nyingine za Afrika Mashariki kuliko kuuza. Wizara ishirikiane na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuwawezesha wafanyabiashara wakubwa na wadogo kushiriki katika mifumo ya kibiashara ya Jumuiya hii;

(iv) Kwa kutumia njia mbadala, Wizara kwa kushirikiana na taasisi za kijamii iandae mfumo wa kutoa elimu zaidi kwa umma kuhusu soko la pamoja kwani hivi sasa wanaofaidika zaidi ni wafanyabiashara wakubwa na wale wadogo wanahisi haliwahusu;

(v) Wizara ifanye juhudi katika kuzishawishi nchi wanachama kuchukua hatua za haraka kurekebisha sheria ambazo zimependekezwa kurekebishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki hususan zinazohusu fursa za kibiashara na zile zenye tija kwa nchi yetu;

(vi) Katika kuiwakilisha nchi yetu kwenye Jumuiya hiyo, Wizara iwasilishe hoja ya kufanyika kwa uchambuzi kuhusu Jumuiya nyingine za Kimataifa zinazohitaji kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na kushirikiana tu na zile Jumuiya zenye mwelekeo wa kutuletea maslahi ya watu wa Afrika Mashariki;

(vii) Serikali ihakikishe kuwa utekelezaji wa lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kuwa na soko la pamoja hausababishi upungufu wa chakula na bidhaa nchini;

(viii) Serikali ihakikishe inalinda umiliki wa ardhi ya nchi yetu katika mikataba na kisheria za ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(ix) Serikali ihakikishe usalama wake wa ndani katika utekelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia nchi zinazotaka na zinazoendelea kujiunga katika Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe

Joseph Magufuli kwa kazi nzuri ya kuendeleza heshima ya Tanzania katika diplomasia na mahusiano na nchi nyingine duniani kwa kipindi kifupi cha uongozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ili niwasilishe taarifa hii pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Namshukuru pia Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mahiga, Mbunge, kwa ushirikiano aliutoa wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namshukuru Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba, Mbunge; nawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Aziz Mlima na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhan Muombwa kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo hivi karibuni. Nawashukuru watendaji wengine wote wa Wizara hii walioshiriki kutoa ufafanuzi uliotakiwa na Kamati wakati wa vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa ushirikiano wao wakati wa kupitia, kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kuthamini michango yao, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu - Mwenyekiti

MWENYEKITI: Mwenyekiti, usisome hayo majina.

MHE. KAN. MST. MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuhakikisha kuwa Kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Ramadhan Abdallah, Ndugu Grace Bidya na Ndugu Hamisi Mwinyimkuu wakisaidiwa na Ndugu Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu kuwa liipokee taarifa hii pamoja na kuyajadili na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Fungu 34 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.
(Makofi)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA
USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE,
USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA KWA MWAKA WA
FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMZI YA WIZARA
HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 -
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa inatokana na kuunganishwa kwa Wizara mbili ambazo ni iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na JKT. Aidha, kwa kuzingatia Kifungu cha 7 Fasili ya (1) na ya (2) cha Nyongeza hiyo, Kamati inalo jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge, ilizitaka Kamati za kisekta, ikiwemo Kamati hii, kutembelea na kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na baada ya kutembelea miradi hiyo kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7 cha nyongeza ya nane kimeainisha jukumu la Kamati hii pamoja na mambo mengine, ni kushughulikia Bajeti ya Wizara ya

Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa. Kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) Kamati ilipaswa kutumia siku zisizozidi tisa kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kazi hii ilifanyika tarehe 14 Aprili, 2016 katika Ukumbi wa GEPF Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inalenga kufafanua kuhusu mambo manne yafuatayo:-

- (i) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2015/2016;
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji ya mpango wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017; na
- (iv) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa kazi za Wizara hii Fungu 34 kwa Mwaka 2016/2017.

2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kufanya ulinganisho kati ya bajeti inayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016. Wakati wa kutekeleza shughuli hiyo, Kamati ilizingatia mambo yafuatayo:-

- i) Malengo ya bejeti yaliyopangwa kutekelezwa na iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;
- ii) Majukumu ya msingi ya Wizara hii kwa mwaka 2015/2016;
- iii) Dhamira ya Bunge la kumi wakati wa kuidhinisha Bajeti ya mwaka 2015/2016; na
- iv) Hali halisi ya mwenendo wa utekelezaji;

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilitaka kujua mambo yafuatayo:-

- i) Namna Serikali ilivyozingatia maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge la Kumi ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;
- ii) Kiasi cha fedha za maduhuli kilichokusanywa ikilinganishwa malengo yaliyowekwa; na
- iii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ikilinganishwa na majukumu yaliyotekelezwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016.

2.1 Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2015/2016

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa – Fungu 34, iliidhinishiwa jumla ya **ShT. 8,000,000,000/=** kwa ajili ya Mradi Namba 6391 uliojulikana kama “*Acquisition, Expansion and Rehabilitation of Mission's building*” ambao ni Mradi wa Ununuzi, ujenzi na ukarabati wa Majengo Balozini na Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1004 – Sera na Mipango (Policy and Planning) cha Fungu 34, kwa Kasma kubwa mbili, ambazo ni 411000 – *Rehabilitation and other civil works* na 411100 – “*Acquisition and other civil Works*”. Maeneo ya mradi huu yalikuwa ni

- (i) Makao Makuu ya Wizara;
- (ii) Ubalozi wa Tanzania Maputo – Msumbiji;
- (ii) Ubalozi wa Tanzania Stockholm – Sweden; na
- (iii) Jengo la Kitega Uchumi, Nairobi – Kenya.

2.2 Ukaguzi wa Miradi

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu haikuwahi kukagua miradi ya maendeleo ya Wizara hii kama inavyotakiwa na Kanuni ya 98(1) ya kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 kutokana na baadhi ya changamoto zilizojitokeza, ikiwemo ya miradi kutopatiwa fedha zozote kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati inaamini kuwa kutokana na juhudi zinazoendelea, itawezeshwa ili kwenda kutembelea na kukagua miradi hiyo pamoja na kazi nyingine zinazotekelezwa na Wizara hii iwezekanavyo.

2.2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Mapato na Matumizi ya mwaka 2015/2016

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2015/2016 Kamati ilitoa mapendekezo kumi na nne (14) ambayo nane (8) yalitakiwa kutekelezwa na iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na sita (6) yalikuwa ya iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba uniruhusu kuliarifu Bunge lako tukufu kuhusu hatua za utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati hadi kufikia mwezi Aprili 2016 wakati ilipokuwa ikipokea taarifa ya utekelezaji kutoka kwa Wizara kama ifuatavyo:-

a) Ushauri uliozingatiwa na kufikia hatua nzuri

Mheshimiwa Spika, Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati inaonesha kuwa ushauri uliozingatiwa na ambao upo katika hatua nzuri ni pamoja na ushauri kuhusu mafunzo ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa Wizara inaendelea kutekeleza Mpango wa Mafunzo wa Miaka Mitatu ulioanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 na unaotarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha wa 2015/2016.

b) Ushauri ambao utekelezaji wake unaendelea na michakato

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara inaonesha kuwa upo ushauri ambao utekelezaji wake unaendelea na mchakato. Hii ni pamoja na ushauri kuhusu kuboresha majengo ya Ofisi za ubalozi na makaazi ya watumishi na kuwapatia vitendea kazi vya kisasa.

c) Ushauri ambao utekelezaji wake bado haujazingatiwa

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati ilipokea taarifa kuhusu ushauri ambao utekelezaji wake bado haujazingatiwa. Hii ni pamoja na ushauri wa Kamati kuhusu Serikali kupitia sheria za Tanzania ambazo zinatakiwa kufanywa marekebisha ili ziendane na utekelezaji wa mambo ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

2.3 Uchambuzi wa Mapitio ya utekelezaji wa mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya utekelezaji wa mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulijikita katika

makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Njia zilizotumika katika uchambuzi ni pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati, mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na maoteo (Projection).

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa uchambuzi umefanywa kwa kutumia njia mbali mbali kama vile majedwali, ulinganisho wa asilimia, grafu na nyenginezo kama ifuatavyo:-

2.3.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Wizara hii katika Fungu 34 ilitarajiwa kukusanya jumla ya **ShT. 20,036,019,000.00** kupitia balozi thelathini na nne zilizopewa Kasma 2001 hadi 2034. Katika makadirio hayo, Ubalozi uliopo Washington, Marekani, Kasma 2018, uliongoza kwa kuwa na lengo kubwa la makusanyo lililofikia kiasi cha **ShT. 4,169,148,876.36/=**, sawa na asilimia 22.45 ya jumla ya makadirio ya makusanyo yaliyokadiriwa kwa balozi zote thelathini na nne.

Mheshimiwa Spika, iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki haikupangiwa kukusanya maduhuli yoyote.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, mwisho wa robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti, jumla ya **ShT. 13,354,340,715.00** zilikusanywa na ofisi za Balozi zetu mbalimbali. Kiasi hicho ni asimili 66.6 ya makadirio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida kiwango cha makusanyo kingelitakiwa kufikia sio chini ya asilimia 75, hivyo kiwango kilichokusanywa cha asilimia 66.65 kipo nyuma kwa asilimia 8.55.

2.3.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Sote tunafahamu kuwa ukadiriaji wa bajeti ya matumizi ni jambo moja na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa ni jambo jingine. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Mipango ya Bajeti, kwa kulinganisha fedha zilizopatikana hadi kufikia mwisho wa robo ya tatu ya mwaka wa fedha na kiasi cha fedha iliyokadiriwa kwa matumizi ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilikuwa imepokea **ShT. 110,877,655,389/=** kati ya **ShT. 146,958,917,246/=**, kiasi hiki ni sawa na asilimia 75.4 ya bajeti yake ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo Wizara iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya **shs. 8,000,000,000/=**. Uchambuzi unaonyesha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, Wizara ilikuwa haijapokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa ufafanuzi huo, Kamati imebaini kuwa katika Bajeti ya uendeshaji na Mishahara mwenendo wa upatikaji wa fedha ulikuwa mzuri. Changamoto kubwa ilikuwa kwenye upatikanaji wa fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni dhahiri kuwa kwa namna hii ya upatikanaji wa fedha si rahisi kufanikisha malengo ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa spika, Kamati ilitaka kujiridhisha zaidi kuhusu mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha kwa Kasma mbalimbali za Wizara hii. Ili kufanikisha azma hiyo ulinganisho ulifanyika kwa Kasma za Mishahara, Matumizi mengineyo na Matumizi ya maendeleo kama inavyonekana katika Jedwali Na. 01 la Taarifa hii.

Jedwali Na. 01

Ulinganisho wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2015/2016


BAJETI ILIYODHISHWA			UPATIKANAJI WA FEDHA		
MGAWANYO	BAJETI	% YA JUMLA	MGAWANYO	BAJETI	% YA JUMLA
OC	130,289,930,246	89	OC	103,219,972,979	93
Mishahara	8,668,987,000	6	Mishahara	7,657,682,410	7
Maendeleo	8,000,000,000	5	Maendeleo	0	0
Jumla	146,958,917,246		Jumla	110,877,655,389	

Chanzo: Randama ya Wizara

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwa uzito wa miradi ya maendeleo wakati wa Bajeti ulikuwa asilimia 5.4 lakini katika upatikanaji wa fedha kutoka Hazina uzito ulikuwa ni asilimia 0.

Mheshimiwa Spika, kwa muonekano huo ni dhahiri kuwa nguvu zaidi zinahitajika ili kupata ufanisi katika azma ya Serikali kuwa na Bajeti ya Miradi ya maendeleo na kuweza kukabiliana na changamoto za Wizara hii kwa nia ya kuleta mtazamo mzuri katika jicho la kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tofauti hizo za uzito unaowekwa kwenye Miradi ya Maendeleo wakati wa Bajeti na wakati wa utekelezaji zinaonyeshwa hapa chini kwa kutumia chati duara Na. 01 na Na. 02 kama ifuatazo:-



Chanzo: Randama ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa asilimia 6.4 ya kiasi cha fedha zilizotolewa na Hazina hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016 Mishahara na asilimia 93.6 ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida. Jambo moja lililopendeza ni kuwa fedha za matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo hazikupatikana kabisa. Kwa kuwa fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa baadhi ya Majengo ya Balozi zetu nje ya nchi, tafsiri ya kutopokelewa fedha za miradi ya Maendeleo ni kuwa kwa mwaka mzima wa 2015/2016, haikuwepo juhudi ya kuboresha au kununua majengo kwa ajili ya Balozi zetu.

Kwa mwenendo huu, Kamati ina maoni kuwa hali hiyo inahitaji hatua za uamuzi mahsusi wa kunusuru hali mbaya ya majengo ya Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla utekelezaji wa majukumu ya iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na sasa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulitegemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha ambao kwa upande wa Miradi ya maendeleo haukua mzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa iliyokuwa Wizara ya Afrika Mashariki, uchambuzi unaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, kilipokelewa kiasi cha **ShT. 16,886,897,117/=** kati ya **ShT. 22,102,756,303/=**, sawa na asilimia 76.4 ya bajeti yake ya matumizi. Aidha, hakuna kiasi cha fedha kilichokuwa

kimeidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 umezingatia rejea zifuatazo:-

- i) Maelezo ya Serikali kuhusu Ukomo wa Bajeti ya Mwaka 2016/2017;
- ii) Maelezo ya Serikali kuhusu Mwelekeo wa Mipango kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017;
- iii) Majukumu ya msingi ya Wizara kama hizi (Wizara za Mambo ya Nje) kwa Dunia nzima kwa mujibu wa Hati Idhini (The Ministers (Assignment of Ministerial Functions) Notice 2016) iliyochapishwa katika Gazeti la Serikali Toleo Na. 16); na
- iv) Hali halisi ya Ofisi na majengo balozini.

Mheshimiwa Spika, kwa rejea hizo, Kamati ilichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Katika Makadiro yaliyowasilishwa kwenye Kamati, ilielezwa kuwa ofisi zetu za balozi zinakadiriwa kukusanya jumla ya **Sh. 24,001,257,737/=** kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kiasi hiki ni asilimia 15.85 ya bajeti ya wizara inayokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ikilinganishwa na kiasi cha asilimia 13.63 ya bajeti ya wizara hii kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika kujiridhisha na mwenendo wa ukadiriaji, Kamati ililinganisha makadirio hayo ya maduhuli na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2015/2016. Uchambuzi ulibainisha kuwa makadirio ya Mwaka 2017/2017 ni ongezeko la asilimia 16.52 ikilinganishwa na makusanyo yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali inaonesha kuwa Makadirio ya Maduhuli ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti hayakujumuishwa kama sehemu ya Bajeti ya Matumizi mengineyo ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu ambao unatofautiana kidogo na ule miaka iliyopita ya 2014/2015 na 2015/2016, fedha zinazotarajiwa kuidhinishwa na Bunge zote zinatakiwa zipatikane moja kwa moja kutoka Hazina.

3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Randama inaonesha kuwa, ili kuweza kutekeleza malengo ishirini na tisa (29) yaliyoelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara inaomba kuidhinishwa kiasi cha **ShT. 151,396,775,000.00**. Kamati ililinganisha Makadirio hayo na jumla ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa iliyokuwa Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2015/2016. Uchambuzi umebainisha kuwa, Kiuhalisia Makadirio hayo yamepungua kwa Kiasi cha **ShT. 17,664,898,549.00** sawa na punguzo kwa asilimia 10.4.

Mchanganuo huo umeoneshwa katika Jedwali Na. 03 hapa chini;

Jedwali Na. 03

Ulinganisho wa Makadirio kati ya Mwaka 2015/2016 na 2016/2017

WIZARA	MWAKA		TOFAUTI
	2015/2016	2016/2017	
(a) Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	146,958,917,246	-	
(b) Ushirikiano wa Afrika Mashariki	22,102,756,303	-	
JUMLA (a) + (b)	169,061,673,549	151,396,775,000	17,664,898,549
Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa	-	151,396,775,000	17,664,898,549

Chanzo: Randama ya Wizara

Mheshimiwa Spika, Tafsiri ya tofauti hiyo inaweza kuwa ni kuongezeka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani ikilinganishwa na Mwaka 2015/2016 au kupungua kwa uzito unaowekwa kwa shughuli zinazotekelezwa na Wizara hii ikilinganishwa na Mwaka 2016/2017. Hali halisi ya thamani ya fedha ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani kwa sasa haioneshi kuongezeka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Ni dhahiri kuwa uzito wa Kibajeti kwa Masuala ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kikanda na Kimataifa umepungua.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi zaidi wa Makadirio ya Matumizi ulifanyika kwa kuwianisha Kasma za Matumizi ya Balozi zetu thelathini na tano zenye vifungu (Subvotes) 2001 hadi 2035 na kubaini kuwa Kasma za Balozi hizo kwa Ujumla zinaombewa jumla ya **ShT. 109,884,906,000/=**. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 72.58 ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017.

Aidha, katika Bajeti inayoombwa ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya Balozi za Tanzania nje ya nchi, asilimia 76.6 inaombwa kugharamia shughuli za kawaida za Balozi za Tanzania nje ya nchi. Ni wazi kuwa shughuli za msingi za Wizara hii zinatekelezwa na Balozi zetu kwa gharama ambayo ni 76.6 ya gharama ya utekelezaji wa jumla majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, kwa Upande wa Uwiano wa Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishwa jumla ya ShT. 8,000,000,000 kwa ajili ya ununuzi, Ujenzi na Ukarabati wa Majengo Balozini na Makao Makuu ya Wizara chini ya Mradi Namba 6391 ambao katika Kitabu cha Nne cha Bajeti (*Supply Votes, Volume IV*) unasomeka "*Acquisition Expansion and Rehabilitation of Mission's buildings*". Kiasi hicho ni sawasawa na Kiasi kilichoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ingawa fedha hazikupatikana kabisa.

Mheshimiwa Spika, masharti ya Kanuni ya 98(2) yanazitaka Kamati za Sekta kufanya Uchambuzi wa Makadirio. Kwa sababu hiyo, Kamati ilichambua kwa kuwianisha kiasi hicho na Jumla ya Bajeti ya Wizara ili kulinganisha uwiano huo na uwiano katika Bajeti Kuu ya Taifa. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Makadirio ya Gharama za miradi ya Maendeleo chini ya Wizara hii ni asilimia 5.3 ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Uzito wa umuhimu wa Bajeti ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kitaifa ni asilimia 40, wakati uzito huo kwa Wizara hii ni asilimia 5.3 tu. Ni moani ya Kamati kuwa Uwiano huo ulipaswa kuboreshwa zaidi na hasa ikizingatiwa kuwa hali ya Balozi za Tanzania nje ya nchi si ya kuridhisha. Kwa mfano, Majengo, Magari na zana nyingi za kutendea kazi kwa Balozi zetu mbalimbali nje ya nchi zinahitaji kuboreshwa, jambo ambalo likipangwa vizuri, uwiano huu utabadilika.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na Matokeo yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Mradi Na. 6391 chini ya Fungu 34 la Wizara hii, Kamati ilichanganua Kasma nne za Wizara hii kama inavyoonesha katika Mchoro Na. 3 wa Taarifa hii. Kasma hizo zinahusu mambo yafuatayo:-

- (i) Gharama za Usafiri nje ya nchi – Kasma 221100
- (ii) Gharama za Ushauri elekezi – Kasma 410700

(iii) Gharama za Ukarabati wa Majengo, Maputo, Stockholm na Mfumo wa Mawasilino Wizarani – Kasma 411000

(iv) Gharama ya Ujenzi jengo la Khartoum – Kasma 411100


Uwiano wa Makadirio hayo umeoneshwa katika Chati Na.4 ya Taarifa hii.

MAELEZO YA KASMA	MAKADIRIO	ASILIMIA
Usafiri nje ya nchi	375,833,000.00	4.6
Ushauri elekezi	75,000,000.00	1
Ukarabati	3,573,046,000.00	44.7
Ujenzi	3,976,121,000.00	49.7
JUMLA	8,000,000,000.00	

Chanzo: RANDAMA UK 176

Chati Namba 4

Uwiano wa Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo



Chanzo: Randama ya Wizara

Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa Bajeti ya kugharamia Miradi ya Maendeleo katika chati Na.4 ya Taarifa hii, unadhihirisha kuwa asilimia 94.4 ya Makadirio ya Mradi huu imeelekezwa katika matokeo halisi yanayotarajiwa kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambayo ni Majengo mapya na Majengo yaliyokarabatiwa. Kiasi cha asilimia 5.6 ya gharama za mradi kinakadiriwa kugharamia upembuzi yakinifu na Ushauri elekezi. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati iliridhishwa na Uwiano huu. Hata hivyo ni maoni ya Jumla kuwa Kasma mbili chini ya Mradi huu zinapaswa kuangaliwa vema Kibajeti. Kasma hizo ni Kasma 411000 inayohusu Ukarabati ambayo inasomeka “*Rehabilitation and other civil works*” na Kasma 411100 inayohusu ujenzi ambayo inasomeka “*Construction and other civil works*.”

4.0 MAONI NA USHAURI

Mheshimwa Spika, baada ya uchambuzi huo, Kamati ilirejea Sera na Miongozo mbalimbali inayotumika katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa pamoja na matarajio ya wananchi kwa Bunge lao katika kuisimamia na kuishauri Wizara hii na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

4.1 Mafunzo ya Diplomasia

i) Wizara iweke uzito katika vifungu vinavyohusu watumishi kupatiwa mafunzo katika balozi zake zote duniani ili kukuza weledi wa utekelezaji wa kazi zao za uwakilishi wa nchi yetu;

ii) Kwa kuwa ujenzi wa Chuo cha Diplomasia – Bagamoyo ulishindikana kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kushindwa kulipa fidia ya eneo, na kwa kuwa Wizara imetoa eneo mbadala la Lakilaki Mkoani Arusha kwa ajili ujenzi wa Chuo hicho, Serikali itoe kipaumbele katika kuliimarisha eneo hilo kwa njia mbalimbali ikiwemo ya kuingia ubia na wawekezaji wenye masharti nafuu; na

iii) Kutokana na mwelekeo wa Dunia ulivyo hivi sasa kuhusu Uhusiano na Ushirikiano wa Kimataifa, Serikali kupitia chuo cha Diplomasia, iweke mitaala ambayo itazalisha wataalamu wengi wa fani ya Diplomasia ya Kiuchumi. Aidha, chuo hicho kijitawanye na kujipanua kwa kuandaa mafunzo ya Kidiplomasia katika sehemu mbali mbali za ndani na nje ya nchi.

4.2 Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje

i. Serikali itoe ukomo wa Bajeti ya Wizara hii ambao ni wa uhalisia katika utekelezaji wa kazi zake ili kufanya kazi hizo kwa kiwango kinachotakiwa cha kimataifa na kuepuka aibu inayoweza kujitokeza kwa nchi yetu;

ii. Kamati inasisitiza kuendelea kutekelezwa kwa ushauri uliotolewa mwaka 2015/2016 kuhusu kuongeza juhudi za uboreshaji wa majengo ya Ofisi na makaazi ya watumishi balozini pamoja na kuzipatia balozi hizo vitendea kazi vya kisasa;

iii. Serikali itafute fedha kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na taasisi nyingine za kifedha Duniani kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Kibalozi ambazo zikijengwa vizuri zitaweza kutumika kama vitega uchumi kama vile linavyotumika jengo la Ubalozi wa Tanzania lilioko Umoja wa Mataifa, New York – Marekani. Aidha, zile Balozi ambazo bado zinakodisha nyumba, mikakati ianze kwa kuanza kuwa na nyumba zetu wenyewe;

- iv. Wizara iangalie upya watumishi walioko katika Balozi mbalimbali Duniani na kufanya marekebisho yatakayohakikisha wanapelekwa na kubakishwa wale wenye fani na uwezo wa kushika nafasi zinazohusu shughuli za ubalozi ili kuleta ufanisi katika Diplomasia ya Uchumi;
- v. Kwa kuwa Sera ya Mambo ya Nje haijafanyiwa mapitio tangu mwaka 2001, Wizara ifanyie mapitio ya Sera hiyo ili iendane na mazingira ya sasa kiuchumi, kisisasa na kijamii;
- vi. Serikali itoe fedha kwenye Balozi zetu nje ili kueneza Sera ya Diplomasia ya Uchumi ambayo itatuongezea wawekezaji na watalii;
- vii. Serikali itoe fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo katika Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, Serikali ihakikishe Balozi ambazo zinakodisha nyumba na Ofisi zinajengewa majengo yake;
- viii. Serikali ipeleke fedha ubalozini kwa ajili ya kuwarejesha maafisa wote waliomaliza muda wao katika Balozi. Aidha, Wizara iangalie uwezekano wa kuacha kutoa barua kwa maafisa kurejea nyumbani kama fedha kwa ajili ya shughuli hiyo hazijatolewa;
- ix. Wizara itume fedha mapema kwa ajili ya malipo ya kodi ya pango ya nyumba za watumishi ubalozini ili kuepusha usumbufu unaojitokeza;
- x. Balozi za Heshima zifunguliwe sehemu ambazo ni muhimu kwa faida ya nchi hususan nchi zenye wawekezaji na watalii wengi. Hii ifanyike kwa kuanzia katika nchi jirani;
- xi. Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka waambata Biashara/ Utalii kwa Balozi Maalum ambazo zina muono wa kuleta wawekezaji na watalii kwa wingi. Aidha, waambata hao wagharamiwe na Wizara zao ili kupunguza gharama zinazoelekea Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa; na
- xii. Serikali ihakikishe kuwa viwanja ambavyo vimenunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Balozi zetu nje ya nchi vijengwe kabla havijachukuliwa na nchi husika mfano Kiwanja cha Ubalozi wa Tanzania- Oman, Rwanda na Uingereza.

4.3 Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Kimataifa

- i. Wizara iendeele kukuza mahusiano na nchi za Afrika Mashariki na Kimatatifa. Aidha, Kamati inaisifu Wizara ambayo ilishirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kufanikisha zabuni ya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Bandari ya Tanga;

- ii. Wananchi wa Tanzania kwa ujumla wao bado hawajaelewa dhana nzima ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuwa hali hii imewafanya wananchi walio wengi kutojikusisha katika biashara zenye manufaa kwa kuitumia Jumuiya hiyo, serikali ichukue hatua maalum ya kuwaelimisha wananchi kuhusu faida na hasara ya Jumuiya hii;
- iii. Kwa kuwa Tanzania imekuwa ikinunua zaidi bidhaa za nchi nyingine za Afrika Mashariki kuliko kuuza, Wizara ishirikiane na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuwawezesha wafanyabiashara wakubwa na wadogo kushiriki katika mifumo ya kibiashara ya Jumuiya hii;
- iv. Kwa kutumia njia mbadala Wizara kwa kushirikiana na taasisi za kijamii iandae mfumo wa kutoa elimu zaidi kwa umma kuhusu soko la pamoja kwani hivi sasa wanaofaidika zaidi ni wafanya biashara wakubwa na wale wadogo wanahisi haliwahusu;
- v. Wizara ifanye juhudi katika kuzishawishi nchi wanachama kuchukua hatua za haraka kurekebisha Sheria ambazo zimependekezwa kurekebisha na Jumuiya ya Afrika Mashariki hususan zinazohusu fursa za kibiashara na zile zenye tija kwa nchi yetu;
- vi. Katika kuiwakilisha nchi yetu kwenye Jumuiya hiyo Wizara iwasilishe hoja ya Kufanyika kwa uchambuzi kuhusu Jumuiya nyingine za kimataifa zinazohitaji kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na kushirikiana tu na zile jumuiya zenye mwelekeo wa kutuletea maslahi ya watu wa Afrika Mashariki;
- vii. Serikali ihakikishe kuwa utekelezaji wa lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kuwa na soko la pamoja hausababishi upungufu wa chakula na bidhaa nchini;
- viii. Serikali ihakikishe inalinda umiliki wa ardhi ya nchi yetu katika mikataba na Sheria za Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- ix. Serikali ihakikishe usalama wake wa ndani katika utekelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia nchi zinazotaka na zinazoendelea kujiunga katika Jumuiya hiyo.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri ya kuendeleza heshima ya Tanzania katika diplomasia na mahusiano na nchi nyingine Duniani kwa kipindi kifupi cha Uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ili niwasilishe taarifa hii pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Namshukuru pia Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mahiga, (Mb) kwa ushirikiano alioutoa wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza kazi zake.

Aidha, Namshukuru Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba, (Mb) na nawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Aziz Mlima Na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ramadhan Muombwa Mwinyi kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo hivi karibuni. Nawashukuru watendaji wengine wote wa Wizara hii walioshiriki kutoa ufafanuzi uliotakiwa na Kamati wakati wa vikao.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Ushirikiano wao wakati wa kupitia, Kujadili na Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kuthamini michango yao, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb, **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kanali (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Capt. (Mst) George H. Mkuchika, Mb, Mjumbe
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb, “
5. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb, “
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa, Mb, “
7. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb, “
8. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb, “
9. Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb, “
10. Mhe. Allan Joseph Kiula, Mb, “
11. Mhe. Cosato David Chumi, Mb, “
12. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb, “
13. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb, “
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb, “
15. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb, “
16. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb, “
17. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb, “
18. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb, “
19. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb, “
20. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb, “
21. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb, “
22. Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb, “
23. Mhe. Stephen J. Masele, Mb, “
24. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb, “

Mheshimiwa Spika, Namshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuhakikisha kuwa Kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mwisho, lakini si kwa umuhimu nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah, Ndg. Grace Bidya na Ndg. Hamisi Mwinyimkuu wakisaidiwa na Ndg. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu kuwa liipokee Taarifa hii pamoja na kuyajadili na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa- **Fungu 34** kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Balozi Adadi Mohamed Rajab, (Mb)

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO
YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

Mei, 2016

MWENYEKITI: Ahsante kwa wasilisho lako zuri na ndani ya muda, tunashukuru. Tunaendelea. Sasa tupate Taarifa au Hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu irekodiwe yote kwenye *Hansard*; nitasoma sehemu ya hotuba na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hotuba yangu ya kwanza ya bajeti nikiwa Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Namshukuru Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa wajibu mzito alionipa wa kushughulikia masuala nyeti ya nchi katika viwango vya Kimataifa. Ninaahidi kuipa Serikali ushirikiano wenye tija katika kujenga Tanzania mpya yenye kuheshimika na yenye kunufaika vya kutosha na Diplomasia ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namtukuza Mungu wangu asiyeshindwa kamwe; ukuu wake, umetuma ujumbe kwa Wana-CCM ambao walidhani sitarudi kwenye Bunge hili la Kumi na Moja. Walitoa kebehi nyingi wakidhani nilikuja hapa kwa kubahatisha. Wengine walikwenda mbali zaidi

wakidai kuwa isingekuwa makosa ya uteuzi wa ndani ya CCM, nisingeshinda mwaka 2010. Leo hii ni dhahiri wamejionea Msigwa kuwepo Bungeni hapa ni mpango wa Mungu na siyo jambo la kuigiza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nasimama kwa jeuri ya Mungu nikiwashukuru sana watu wa Iringa Mjini kwa upendo wao mzito juu yangu. Mwenyezi Mungu kawatuma kuonesha umma kuwa mbeba maono hafi mpaka mpango wa Mungu utimie. Kwa sababu hiyo, ushindi wa Iringa ni ujumbe tosha kwa kila mwanasiasa na kwa mtu yeyote anayekatishwa tamaa na kauli za watu. Ikumbukwe kuwa *your value does not decrease based on someone's inability to see your worth or potential*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo Iringa ninayojua mimi; Iringa ya watu wanaojitambua, jasiri na wenye rekodi ya kipekee ya kuduwaza dunia. Naam, Iringa tunaita *intellectual habitat, center of education; the home of knowledge; the land of Mkwawa*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hukusoma Tosamaganga, basi ulisoma *Mkwawa High School*; kama hukusoma Lugalo, ulisoma Ifunda; kama hukusoma Ifunda, Malangali au *Iringa Girls*. Najivunia kuwa Mbunge wa Iringa Mjini. Wanairinga sitawaangusha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyuma ya mafanikio yangu kuna Kissa Msigwa. Huyu ndio Mama Mchungaji, Malkia wangu wa nguvu, rafiki yangu, mke wangu, mama watoto wangu. Tumepitia mengi magumu, namshukuru kwa thamani yake kuu kwangu na kwa watu wa Iringa Mjini. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee namshukuru Naibu wangu, Waziri Kivuli Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali kwa ushirikiano alioutoa katika kuhakikisha hotuba inasheheni mawazo mbadala na yenye kutoa dira na kulisaidia Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili uhusiano wa Kimataifa tukiwa katika zama mpya. Zile enzi za kupigania uhuru na ukombozi wa Bara la Afrika zilizoipa Tanzania hadhi na heshima kubwa Kimataifa zimeshapita; na wala Tanzania yetu haiwezi tena kutegemea sifa hizo za kihistoria kujijenga Kimataifa. Hizi ni zama mpya, ni zama za kusaka maendeleo ya kiuchumi kwa diplomasia ya kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza Sera ya Mambo ya Nje na Diplomasia ya Kiuchumi. Ni miaka 15 sasa tangu Serikali ianze kutekeleza sera mpya ya Mambo Nje ya mwaka 2001 inayolenga kusukuma mbele diplomasia ya uchumi. Mwanadiplomasia mahiri na Waziri wa Mambo ya Nje wa 38 wa Australia, anayeitwa Julie Bishop, katika moja ya hotuba zake anasema, nami

nanukuu: *"Just as traditional diplomacy aims for peace, so economic diplomacy aims for prosperity", not just as an end in itself but also as a vital support for peace in the region and for global peace and security. In this regard effective economic diplomacy must translates into economic growth, job creation and new sources of investment to further build on the quality of life and standards of living that people enjoy"* mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyosema Mwanadiplomasia huyu mashuhuri; "wakati diplomasia ya kizamani ililenga amani, diplomasia ya kiuchumi inalenga ustawi kwa kukuza ustawi wa maisha ya watu. Diplomasia ya kiuchumi inakuwa ndiyo msingi muhimu wa kudumisha amani. Ikitekelezwa vizuri, diplomasia ya kiuchumi ni lazima ilete matokeo ya kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa ajira na kufunguka kwa vyanzo vipya vya uwekezaji wa ndani na wa Kimataifa kuchochea ubora wa maisha ya watu wa nchi husika." Kinyume na hayo, diplomasia ya uchumi ya Tanzania itabaki kuwa ni neno la kuiga na kubandika (copy and paste) kutoka kwenye nchi zinazojua nini hasa maana ya diplomasia ya uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 15 iliyotumika kutekeleza sera hii ni sawa na muda uliotumika kutekeleza Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) kutoka mwaka 2000 – 2015. Pia miaka 15 ndiyo muda ambao unatumia kutekeleza Malengo yote ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (Sustainable Development Goals –SDGs) kutoka 2015 - 2030. Aidha, kwa miaka yote 15, Bunge hili lilishaidhinisha mabilioni ya shilingi kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa sera hiyo. Hakuna kisingizio cha muda tena, wala hakuna kisingizio cha pesa tena. Huu ni wakati wa Serikali kutupa matokeo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanataka kujua na Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua:-

(i) Ni mafanikio gani makubwa na ya maana ambayo Serikali ya CCM imeyaleta kwa kutekeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi? (Makofi)

(ii) Je, ni ajira ngapi mpya zimetengenezwa kwa kutumia fursa za uwekezaji wa Kimataifa, ikiwa hadi leo Watanzania wengi bado hawana ajira? (Makofi)

(iii) Sera hii imeongeza ubora gani kwenye maisha ya Watanzania, ikiwa watu wengi bado wapo kwenye umaskini uliopitiliza? (Makofi)

(iv) Wizara hii inapata wapi uhalali wa kuomba tena mabilioni mengine ya bajeti ikiwa kwa miaka 15 mfululizo imeshindwa kuleta mafanikio yanayoonekana na yanayoendana na uhalisia wa mabilioni yanayotengwa kila mwaka kwa ajili ya Wizara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani umebaini kuwa Serikali haiko *serious* katika kufukuzia fursa za kiuchumi na kusukuma maslahi ya nchi katika siasa za Kimataifa. Diplomasia ya kiuchumi inataka utaalumu, inahitaji, viongozi wenye maono, wenye ushawishi na mikakati madhubuti yaani nikimaanisha *visionary leadership, strong negotiators, lobbyists and smart strategies* ndipo nchi ipate mafanikio. Tanzania tumepungukiwa vyote hivyo. Nchi haina maono, haina mikakati na haina wataalam wa kutosha kusukuma sera hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, katika nchi yoyote ile duniani, mkuu wa nchi ndiye Mwanadiplomasia namba moja na ndiye anayepaswa kutoa dira na msukumo wa kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje kwa maslahi ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi inayojua kila kitu na hakuna kiongozi anayejua kila kitu. Hii ni dunia ya kutegemeana, hii ni dunia ya kujifunza na kubadilishana mikakati na uzoefu wa kushughulikia maendeleo ya watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii, nchi yoyote ile duniani inayoongozwa na kiongozi *local*, asiye na *interest* na masuala ya Kimataifa, anayekimbia Mabalozi wa nchi rafiki, anayeogopa na asiyependa kushiriki mikutano muhimu ya Kimataifa, asiyejua nini kinaendelea katika ajenda za Kimataifa na asiyependa kujifunza kutoka kwa viongozi wa mataifa mengine, basi nchi hiyo haiwezi kufanikiwa kamwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuongoza nchi inayotafuta fursa za uchumi wa dunia, halafu unajifungia Ikulu. Maendeleo ya nchi hayawezi kuja tu kwa kutumbua majipu ya ndani, bali kwa kutekeleza mikakati makini ya kiuchumi ambayo kufanikiwa kwake kunahitaji ushirikiano wa mataifa mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu haipo *serious* na diplomasia ya uchumi. Ukitaka kuuthibitisha ukweli huu, tazama aina ya Mabalozi wanaoteuliwa. Uchunguzi unaonyesha kuwa chini ya Serikali hii ya CCM Ubalozi hutolewa kama zawadi kwa makada waliosaidia kampeni; hutolewa kama pole kwa Wanajeshi wastaafu wenye uswahiba wa karibu na CCM na pia hutolewa kama adhabu kwa wanasiasa wanaoonekana kuwa tishio kwa vigogo wa CCM wakati wa kuwania nafasi mbalimbali, hasa zile za Kiserikali. Ni nadra sana kukuta fulani kapewa Ubalozi kwa sababu ana sifa za msingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makada hawa wa CCM wasiokua na weledi kuhusu diplomasia ya uchumi, ndio wanaokabidhiwa dhamana ya kuhakikisha

eti Tanzania inafanikiwa Kimataifa. Kambi Rasmi ya Upinzani inazitambua juhudi za Mheshimiwa Rais za kuwarudisha nyumbani baadhi ya Mabalozzi. Kwa dhamira njema kabisa tunaishauri Serikali kutumia vizuri fursa hiyo kwa kufanya kwanza *performance appraisal* ya Mabalozzi ili kuwabaini vizuri wale wasio na sifa, Mabalozzi wasioendana na wakati tulionao, waondolewe katika nafasi hizo. Wengi wao wangeweza kuwa Mabalozzi wazuri sana wa nyumba kumi kumi lakini siyo kutuwakilisha nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozzi wana wajibu mkubwa katika kubaini fursa za kiuchumi zilizopo kwenye Mataifa mengine na kuiongoza Serikali katika kushawishi na kuzitumia fursa hizo. Katika zama hizi mpya, tunahitaji Mabalozzi wenye uwezo wa kijasusi wa kiuchumi (*economic espionage*) ili wawe na tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni chombo gani hasa kinachotumika kama kiunganishi kati ya Balozi zetu na Wizara hii na hata Wizara nyingine ili nao Mabalozzi waweze kujua na kujifunza mambo mengine mazuri yanayofanywa katika Wizara mbalimbali?

Je, ni namna gani wananchi wanaweza kupata ripoti za Balozi mbalimbali kwa njia rahisi ili wahamasike katika kutafuta fursa za kiuchumi katika nchi wanazoziwakilisha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina uhaba mkubwa sana wa wataalam wa diplomasia ya kiuchumi. Randama ya Wizara inathibitisha ukweli huu. Wakati Serikali inaanza kutekeleza sera hii mwaka 2001 ilikwishajua vizuri kuwa haina Wanadiplomasia wa kutosha, cha kusikitisha iliichukua Wizara hii miaka 12 ndipo ikaanza kutoa mafunzo ya muda mfupi na ya muda mrefu mwaka 2013 kwa ajili ya kuzalisha *Economic Diplomats*. Matokeo yake hadi kufikia mwezi Mei, 2015 ni watumishi 32 tu ndio waliokuwa wamehitimu mafunzo ya muda mfupi ya diplomasia ya uchumi. Tuache mzaha, tuache ukada, tuliokoe Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kufika kwa mwendo huu wa konokono. Tunaposema CCM imeshindwa kuliongoza Taifa hili huwa tuna maana kuwa mambo madogo madogo mnayoyafanya hayalingani hata kidogo na muda mwingi mnaotumia wala fedha nyingi mnazotengewa. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge hili jinsi Serikali ilivyojipanga kukabiliana na uhaba huu mkubwa wa Wanadiplomasia na jitihada zinazokusudiwa kuchukuliwa kumaliza tatizo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Wizara hii kuvutia wawekezaji, lakini Wizara haipaswi tu kuvutia wawekezaji, pia inapaswa kuhakikisha wawekezaji wanafanya shughuli zao katika namna isiyoathiri maslahi ya nchi na wananchi.

Tathmini ya Kambi ya Upinzani inaonyesha kuwepo kwa udhaifu mkubwa wa Wizara hii katika kutekeleza jukumu hili. Matokeo yake makampuni ya Kimataifa, hasa ya Madini, yamekuwa chanzo kikuu cha malalamiko na migogoro isiyokwisha miongoni kwa wananchi wetu na kuleta hali ya hofu, vifo na kukata tamaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano mingi ya aina hii ya migogoro na uonevu unaofanywa na makampuni makubwa ya nje (*multinationals*). Mfano ni migogoro isiyoisha katika migodi ya Nyamongo huko Tarime ambapo wananchi wamekuwa wakilalamikia kudhulumiwa haki zao na Kampuni ya *Acacia Mining (Barrick Gold)* huku Wizara husika, ikiwemo Wizara ya Mambo ya Nje ikifumbia macho mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni hii ya *Acacia Mining (Barrick Gold)* imeendeleza tabia yake ya kukandamiza haki za wazawa kwa kusaidiwa na baadhi ya Maafisa wa Serikali kukiuka taratibu za sheria ya nchi yetu. Tunazo taarifa za Kampuni ya *Acacia* kudhulumu kampuni nyingine ya wazawa iitwayo *Bismark Hotel Mining Ltd.* ya Mwanza, kwa kupora na kudhulumu kitalu cha kampuni hiyo kilichopo Geita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia hii ya makampuni ya nje kuyadhulumu makampuni ya wazawa bila Wizara kuingilia kati, ni hatari kwa maslahi ya wananchi wetu na ni hatari pia kwa uhusiano wetu na Mataifa ya nje. Wizara ichukue hatua madhubuti za kutatua migogoro yote iliyosababishwa na makampuni ya nje. Wizara ianze na mgogoro ya Kampuni ya *Acacia Mining*, ukiwemo huu wa kudhulumu kitalu cha Kampuni ya *Bismark Hotel Mining Ltd.*, kwa kuruhusu wazawa kudhalilishwa na makampuni makubwa ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imetoa maelekezo kupitia mawasiliano yake na Mabalozi (*NoteVerbale*) kuelekeza kuwa kabla ya Mabalozi au Maofisa wa Ubalozi kukutana na asasi zisizo za kiserikali au vyama vya siasa, ni lazima kwanza waombe kibali cha Serikali kupitia Wizara ya Mambo Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu wa kuwataka Mabalozi kuomba kibali Serikalini unaminyu uhuru wa Mabalozi na wanadiplomasia mbalimbali wa Kimataifa kufanya kazi zao hapa nchini. Kimsingi amri hiyo ya Serikali inakiuka utamaduni uliokuwepo awali, inakiuka Masharti ya Mkataba wa Vienna kuhusu Mahusiano ya Kibalozi Duniani. Huu ni ushahidi mwingine kuwa Serikali hii ya Awamu ya Tano imeamua kudhibiti uhuru wa habari nchini na imevuka mipaka kiasi cha kuingilia uhuru wa Mabalozi na Wanadiplomasia wanaofanya kazi zao hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Kimataifa wa Vienna unaoshughulika na masuala ya mahusiano ya kidiplomasia na kibalozi ya nchi mbalimbali duniani, kwenye ibara yake ya 27(1) unatoa masharti ya nchi inayopokea Mabalozi, kuwalinda na kuwapa uhuru wa mawasiliano yao yote na kutokuyaingilia kwa namna yoyote ile. Katika Mkataba wa Vienna Ibara ya 41(1) inasema kuwa bila kuathiri masharti ya haki na kinga, Mabalozi wana jukumu la kuheshimu sheria na taratibu za nchi zinazowapokea na wanatakiwa kutoingilia mambo ya ndani ya nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya bila kuathiri (*without prejudice*) katika uandishi wa sheria, yana maana kubwa sana. Hii ni kwa sababu Serikali imekuwa ikitumia ibara hii kuwabana Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini katika kutekeleza majukumu yao. Hii ina maana kuwa pamoja na Mabalozi kuwa na jukumu la kuheshimu sheria za nchi yetu, bado jukumu hilo haliondoi uhalali, uwepo wa haki na kinga walizonazo za kutoingiliwa wajibu wa Mkataba wa Vienna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno bila kuathiri (*without prejudice*) kwa tafsiri ya Kiingereza lina maana ya “*without detriment to any existing right or claim, without any loss or waiver of rights or privilege.*” Ni wazi kuwa Serikali haitatumia kifungu hiki kama utetezi kwa namna yoyote ile ya kuwabana Mabalozi kwa kutumia utaratibu wa sasa wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuondoa utaratibu huu inaotumia kwa sasa kwa sababu inanyima na kuua uhuru wa mawasiliano wa Mabalozi na Wanadiplomasia mbalimbali waliopo nchini. Hali hii inapelekea Taifa letu kuwa na sifa mbaya kwenye medani za Kimataifa. Kambi ya Upinzani haioni msingi wowote wa kuwanyima Mabalozi hawa waliotumwa na nchi zao kufanya mawasiliano halali na taasisi, vyama vya siasa, wadau wengine bila kuathiri sheria za nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayoogopa Mabalozi wa nchi za kigeni wasiwasiliane kwa uhuru na vyama vya siasa na taasisi nyingine hadi itoe kibali, ni Serikali isiyojiamini. Mabalozi ni wawakilishi halali kwa mujibu wa sheria; na vyama vya siasa vipo kihalali kwa mujibu wa sheria. Hii hofu inatoka wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutengua amri hiyo mara moja. Aidha, natoa wito kwa Mabalozi wote nchini kuwa huru. Aidha, natoa wito kwa Mabalozi wote kuwa huru kuwasiliana na vyama vya siasa na taasisi mbalimbali kwani wanalindwa na Mkataba wa Vienna ambao Tanzania imeuridhia. Watanzania tunaoheshimu diplomasia, haki na uhuru wa kuwasiliana tupo tayari kushirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Kimataifa katika

kuhakikisha Serikali ya Tanzania inaheshimu Mkataba huu wa Vienna, ikiwa itaendeleza udikteta katika hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanauawa nchi za nje, wanabaguliwa na kudhalilishwa huku Serikali ya CCM ikikaa kimya bila kuchukua hatua madhubuti. Miongoni Watanzania waliouawa kikatili hivi karibuni huko ughaibuni ni Marehemu Andrew Sanga, maarufu kama King Drew, aliyepigwa risasi tena na mtu aliyefahamika, na baadaye kupoteza maisha yake baada ya kupata majeraha makubwa; Marehemu Robert John Mpwata aliyeuawa kwa sumu nchini Ujerumani; Marehemu Caroline Mmari aliyeuawa huko Los Angeles, Marekani; Marehemu Imran Mtui aliyeuawa huko India; Marehemu Jerry Issack Mruma aliyeuawa huko Kenya; Marehemu Method Clemence Mengi aliyeuawa kwa kuchomwa visu huko nchini Marekani pamoja na wengine wengi ambao sijawataja hapa. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hawa mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na mauji hayo, yuko binti wa Kitanzania aliyefanyiwa vitendo vya udhalilishaji kwa kuvuliwa nguo zake kisha kutembezwa uchi mitaani. Serikali isiyopaza sauti kulaani mauaji ya raia wake, inayoshindwa kulinda uhai wa raia wake, ni Serikali iliyopoteza uhalali wa kuongoza. Jukumu la kwanza la Serikali yoyote duniani ni kulinda uhai wa raia na mali zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitegemea Serikali ikemee vikali kitendo cha Serikali iliyohusika ikiwa ni pamoja na kuwakamata wahusika. Je, kuna uhalali gani wa Mabalozi wetu kuwa katika nchi hizo endapo wanashindwa kuchukua hatua kali dhidi ya nchi zinazohusika kwa kuwa zimeshindwa kutoa ulinzi kwa watu wetu? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliambia Bunge lako ni nini inategemea kufanya endapo tabia hizi zinazokiuka haki za binadamu zitaendelea kufanywa dhidi ya wananchi wetu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ifanye uchunguzi wa kina juu ya sababu za mazingira yaliyosababisha kushamiri kwa mauaji ya Watanzania katika miezi na miaka ya hivi karibuni. Aidha, kwa kuzingatia matokeo ya ripoti hiyo, Bunge lako lijadili na kushauri hatua za kuchukua na Serikali na Balozi zetu ili kuepusha mauaji ya raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa walisaini Azimio la Kutetea na Kulinda Haki za Binadamu na kwa kuwa mauaji na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaowadhuru Watanzania hufanyika miongoni mwa nchi rafiki zilizoridhia Azimio hilo, Kambi ya Upinzani inashauri pia Serikali yetu ivunje ukimya, ipaze sauti kuzitaka nchi husika ziongeze

juhudi za kulinda usalama wa raia wa Tanzania na wa nchi nyingine dhidi ya mauaji na ukiukwaji wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia sasa inatambua mchango mkubwa wa uchangiaji uchumi unaofanywa na watu mbalimbali wanaoishi nchi za nje *(Diaspora)*. Hatuna budi kama Watanzania kuendelea kutambua na kuthamini mchango huo mkubwa unaofanywa na kaka na dada zetu wanaoishi nje ya nchi kwani uwepo wao huko unachangia kukuza jina la nchi yetu na kuboresha mahusiano ya nchi hizo. *(Makofi)*

(Hapa Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa alikunywa maji)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi na dawa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna takwimu za Kitaifa zinazoonyesha idadi kamili ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi na taarifa za kile wanachokifanya huko. Umuhimu wa kuwa na taarifa ni kubaini kwa wepesi idadi na aina ya watu wenye ujuzi na uzoefu ambao Serikali inaweza kuutumia kwa maslahi ya nchi.

Aidha, kujua idadi ya wananchi waliopo nje ya nchi kutapelekea kutengeneza milango ya kiuchumi kati yao na nchi *(economic gateway)*, kutafungua fursa za kibiashara ikiwa ni pamoja na soko la nje *(export market)* kwa bidhaa zetu za Kitanzania na hivyo kutuachia fursa kwa soko la ndani kuboresha bidhaa zao ili ziweze kupata masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa *database* hiyo pia yenye kila Mtanzania aliopo nje ya nchi kutasaidia kupunguza idadi ya raia wa nchi nyingine wanaotumia jina la nchi yetu vibaya huko nje ya nchi kwa kujifanya ni wakimbizi kutokea Tanzania. Tutaweza kuwatambua na kuwabaini kwa kutumia Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa jambo hili la kutengeneza *database* linazingatiwa kwa uzito wake kwa kuwa lina manufaa kwa wananchi wetu walio katika kila pembe ya dunia na pia manufaa ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanaoishi nje wamekuwa wakifanya jitihada kubwa sana za kuchangia uchumi wa nchi hii, japo Serikali imekuwa haiwapi ushirikiano wa kutosha. Hii ni kwa sababu Serikali kuwa imejitenga na watu wake wanaoishi nje ya nchi, basi hata michango inayoingia

nchini imekuwa ni kidogo tofauti na matakwa au matamanio ya ndugu zetu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo linashangaza sana, Mtanzania anapotaka kutuma kiasi chochote cha pesa kwenda nje ya nchi imekuwa ni rahisi sana, lakini anapotaka kuingiza fedha ndani ya nchi kutoka nje inakuwa ni vigumu sana kwa sababu kuna urasimu mkubwa na wenye kukatisha tamaa. Yote hii ni kwa sababu Serikali haijajiweka utaratibu wa kuwasaidia Watanzania kutafuta mbinu za kuingiza fedha nchini.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ya CCM ijifunze kwa majirani zetu Somalia, Ethiopia, Kenya na Rwanda wanavyofanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 mwezi Novemba Serikali ya Kenya ilizindua taasisi inayotoa elimu kuhusu masuala ya *remittances* chini ya Tume ya Umoja wa Afrika (*African Union Commission*). Taasisi hiyo inayojulikana kama *African Institute for Remittances (AIR)* ilizinduliwa ili kutoa fursa kwa Wakenya wengi kujifunza masuala ya *remittances* na kuona ni kwa namna gani nchi hiyo itanufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/2015 Benki ya Taifa ya Ethiopia (*National Bank of Ethiopia*) ilikusanya *remittances* kutoka dola bilioni 1.5 mpaka dola bilioni mbili, kwa kipindi cha mwaka mmoja pekee, fedha zilizochangia kwa kiasi kikubwa kupanda kwa uchumi wa nchi hiyo. Ni vyema sasa na sisi Tanzania tuanze kubuni mbinu za kunufaika na michango hii kwa faida ya uchumi wa nchi yetu na kuwakwamua Watanzania wengi katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutambua, kuthamini na kuheshimu michango ya wananchi wanaoishi nje ya nchi ikiwa ni pamoja na shughuli zote za kimaendeleo wanazozifanya kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Hivyo basi, pamoja na yote yaliyopendekezwa na Kambi Rasmi katika kipindi chote cha Bunge la Kumi kuhusu *remittances*, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda hautoshi Mheshimiwa Waziri na Serikali, mtasoma ushauri wangu uko hapo, kuhusu wageni wa nje. Niende kwenye suala la Afrika Mashariki, ambalo ni la muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka 16 tangu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, lakini bado Tanzania haina Sera yake ya Utengamano kwenye Jumuiya hii kama ilivyo kwa nchi za Kenya na Uganda. Kwa kukosa sera hii muhimu, Tanzania inakuwa haina dira ya nini hasa tunasimamia au tunataka kwa maslahi ya nchi yetu kwenye Jumuiya hii. Kwa kutokuwa na sera hii, Wabunge wetu wa Afrika Mashariki wanakuwa hawana mwongozo wowote

muhimu wa kusimamia maslahi ya nchi wanapokuwa kwenye vikao vya Bunge hilo. Nadhani wako pale watakuwa mashahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kielelezo kingine cha kuwa na Serikali isiyo *serious* katika kusimamia masuala ya msingi ya nchi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ijieleze, ni kwanini hadi leo hatuna Sera ya Utengamano? Ni lini Serikali itahakikisha sera hiyo inakamilika? Serikali pia imeonyesha udhaifu mkubwa katika kuwasaidia na kuwatumia Wabunge wetu wa Afrika Mashariki kutekeleza vizuri wajibu wao kwenye jumuiya hiyo:-

(i) Serikali hii imeshindwa kuwapatia Ofisi Waheshimiwa Wabunge wetu wa *East Africa* kiasi cha kulazimika kufanyia shughuli zao za kibunge nyumbani kwao au hotelini. (Makofi)

(ii) Serikali hii imeshindwa kuwapatia usafiri Wabunge wetu wa *East Africa* licha ya kuombwa kupatiwa mikopo ya magari isiyolipiwa kodi kama ilivyokuwa kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

(iii) Serikali hii imeshindwa kuwatumia Waheshimiwa Wabunge wetu wa *East Africa* katika kuhamasisha wananchi kuzifahamu faida na fursa za jumuiya hii. Matokeo yake miaka 16 tangu kuanzishwa kwa jumuiya hii, uelewa wa Watanzania bado ni mdogo sana kiasi kwamba, hawawezi kuziona fursa za kiuchumi. (Makofi)

(iv) Serikali hii imeshindwa kuwapatia mtafiti (*researcher*) Waheshimiwa Wabunge wetu wa *East Africa* na kuwaacha wakichangia mjadala kwa kutegemea tu utashi wao badala ya ushahidi wa kitafiti. Serikali zilizo *serious* duniani huwa hazifanyi uzembe kama huo. (Makofi)

(v) Kambi ya Upinzani imebaini kuwa mpaka sasa Waheshimiwa Wabunge wetu wa *East Africa* hawajui wako chini ya nani? Wanapaswa kuripoti kwa nani hasa? Kwa Wizara au kwa Bunge? Huu ni udhaifu mwingine wa Serikali wa kushindwa kutoa miongozo na kufanya kazi kwa karibu na Wabunge wetu. (Makofi)

(vi)ambi ya Upinzani inazo taarifa kuwa Serikali ya Tanzania ndiyo inayoongoza kwa urasimu na uzembe wa kushindwa kufanya maamuzi kwa wakati kwa masuala yanayoihusu Tanzania. Udhaifu huu umekuwa ukichelewesha kufikiwa kwa maamuzi kadhaa ya Bunge la Afrika Mashariki katika kupitisha Miswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakaporudi aje na majibu. Upungufu huu wote unathibitisha jinsi Serikali yetu isivyo *serious* katika kusukuma maslahi ya nchi kwenye *East Africa*. Aidha, huu ni ushahidi kuwa

Tanzania bado haijajiandaa na wala haina wataalam wa kuiongoza vizuri Serikali katika kusukuma diplomasia ya kiuchumi hata kwa nchi jirani za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upungufu huu, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni tija yoyote ya fedha ambazo Serikali imekuwa ikitengwa na Bunge hili kwa ajili ya shughuli za Afrika Mashariki. Kwa udhaifu huu, Wizara hii inabaki kuwa ni Wizara ya safari, vikao na mikutano, isiyokuwa na tija yoyote kwa maendeleo ya nchi kwa sababu ya Serikali kushindwa kujipanga na kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ijitathmini, ijipange upya, itupe mkakati makini na endelevu kuhusu ushiriki wake wenye tija wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Burundi ilifanya Uchaguzi wake mnamo mwezi Julai, 2015 na Uganda tarehe 18 Februari 2016. Makundi ya wanasiasa na wanaharakati mbalimbali wa haki za binadamu waliishutumu Tume za Uchaguzi, walishuhudia ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi, mauaji ya viongozi wa upinzani na kila alama ya udikteta dhidi ya wananchi wa nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini Uganda, viongozi wa Upinzani akiwemo Kiongozi Mkuu wa Upinzani nchini humo, Kizza Besigye, aliwekwa korokoroni katika kipindi cha uchaguzi na hata baada ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania ilipaswa kukemea uovu huo waziwazi kama alivyokuwa akifanya Mwalimu Nyerere alipokuwa akikemea vitendo vya ki... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA MHESHIWIWA PETER SIMON MSIGWA (MB) KUHUSU BAJETI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

(Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016)

KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, hii ni hotuba yangu ya kwanza ya bajeti nikiwa Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Namshukuru Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mhe. Freeman Mbowe (Mbunge) kwa wajibu huu mzito alionipa wa kushughulikia masuala nyeti ya nchi katika viwango vya kimataifa. Ninaahidi kuipa serikali hii ushirikiano wenye tija katika kuijenga Tanzania mpya, yenye kuheshimika na yenye kunufaika vya kutosha na diplomasia ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namtukiza Mungu wangu asiyeshindwa kamwe. Ukuu wake umetuma ujumbe kwa wana -CCM ambao wallidhani sitarudi kwenye bunge hili la 11. Walitoa kebehi nyingi wakidhani nilikuja hapa kwa kubahatisha. Wengine walikwenda mbali zaidi wakidai kuwa isingekuwa makosa ya uteuzi wa ndani ya CCM nisingeshinda mwaka 2010. Leo hii ni dhahiri wanajionea Msigwa kuwepo Bungeni hapa ni mpango wa Mungu na sio jambo la kuigiza.

Mheshimiwa Spika, leo nasimama kwa jeuri ya Mungu nikiwashukuru sana watu wa Iringa Mjini kwa upendo wao mzito juu yangu. Mwenyezi Mungu kawatumia kuonyesha umma kuwa mbeba maono hafi mpaka mpango wa Mungu utimie.

Kwa sababu hiyo, Ushindi wa Iringa ni ujumbe tosha kwa kila mwanasiasa na kwa mtu yoyote anayekatishwa tamaa na kauli za watu; akumbuke kuwa **"Your value does not decrease based someone's inability to see your worth and potentials"**

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo Iringa ninayojua Miye. Iringa ya watu wanaojitambua, jasiri na wenye rekodi ya kipekee ya kuiduwaza Dunia. Naam – Iringa - **intellectuals' habitat, center of education, the home of knowledge, the land of Mkwawa**. Kama hucusoma Tosamaganga basi ulisoma Mkwawa High School, au ulisoma Lugalo, Ifunda, Malangali au Iringa girls. Najivunia kuwa Mbunge wa Iringa Mjini. Sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, nyuma ya mafanikio yangu kuna mke wangu Kisa Msigwa ambe ananipa moyo wakati wowote. Tumepitia mengi magumu, namshukuru kwa thamani yake kuu kwangu na kwa watu wa Iringa Mjini.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani kwa Naibu Waziri kivuli Mheshimiwa Riziki Shahali Mgwali kwa ushirikiano wake aliutoa ili kuhakikisha kuwa hotuba hii inasheheni mawazo mbadala ya kuweza kutoa dira na kulisaidia taifa.

Mheshimiwa Spika, leo tunajadili uhusiano wa kimataifa tukiwa katika zama mpya. Zile enzi za kupigania uhuru na ukombozi wa Bara la Afrika zilizoipa Tanzania hadhi na heshima kubwa kimataifa zimeshapita; na wala Tanzania yetu haiwezi tena kutegemea sifa hizo nzuri za kihistoria kujijenga kimataifa. Tupo kwenye zama mpya, zama za kusaka maendeleo endelevu ya kiuchumi kwa diplomasia ya kiuchumi.

2. SERA YA MAMBO YA NJE NA DIPLOMASIA YA KIUCHUMI

Mheshimiwa Spika, ni miaka 15 sasa tangu serikali ianze kutekeleza sera mpya ya mambo nje ya mwaka 2001 inayolenga kusukuma mbele diplomasia ya uchumi. Mwanadiplomasia mahiri na Waziri wa Mambo ya Nje wa 38 wa Australia - Julie Bishop – katika moja ya hotuba zake anasema, nanukuu: ***“Just as traditional diplomacy aims for peace, so economic diplomacy aims for prosperity’ – not just as an end in itself but also as a vital support for peace in the region and for global peace and security. In this regard effective economic diplomacy must translates into economic growth, job creation and new sources of investment to further build on the quality of life and standards of living that people enjoy”***, mwisho wa kunukuu

Mheshimiwa Spika, kama anavyosema Mwanadiplomasia huyu mashuhuri ***“wakati diplomasia ya kizamani ililenga amani, diplomasia ya uchumi inalenga ustawi, kwa kukuza ustawi wa maisha ya watu diplomasia ya kiuchumi inakuwa ndiyo msingi muhimu wa kudumisha amani. Ikitekelezwa vizuri, diplomasia ya kiuchumi ni lazima ilete matokeo ya kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa ajira na kufunguka kwa vyavyo vipya vya uwekezaji wa ndani na wa kimataifa kuchochea ubora wa maisha ya watu wa nchi husika”***. Kinyume na matokeo hayo, diplomasia ya uchumi ya Tanzania itabaki kuwa ni neno la kuiga na kubandika tu (copy and paste) kutoka kwenye nchi zinazojua nini hasa maana ya diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, miaka 15 iliyotumika kutekeleza sera hii ni sawa na muda uliotumika kutekeleza **Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs kutoka mwaka 2000 -2015)**; pia miaka 15 ndio muda ambao Dunia imeamua kuutumia kutekeleza Malengo yote ya Maendeleo Endelevu ya Dunia **‘Sustainable**

Development Goals –SDGs - kutoka 2015-2030. Aidha, kwa miaka yote 15, Bunge hili lilishaidhinisha mabilioni ya shilingi kila mwaka kwaajili ya utekelezaji wa sera hiyo. Hakuna kisingizio cha muda tena, wala hakuna kisingizio cha pesa tena. Huu ni wakati wa serikali kutupa matokeo ya maana.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanataka kujua na Kambi ya Upinzani inataka kujua;

- ☐ Ni mafanikio gani makubwa na ya maana ambayo Serikali ya CCM imeyaleta kwa kutekeleza sera ya diplomasia ya uchumi?
- ☐ Je, ni ajira ngapi mpya zimetengenezwa kwa kutumia fursa za uwekezaji wa kimataifa, ikiwa hadi leo Watanzania wengi bado hawana ajira?
- ☐ Sera hii imeongeza ubora gani kwenye maisha ya Watanzania, ikiwa watu wengi bado wapo kwenye umaskini uliopitiliza?
- ☐ Na Wizara hii inapata wapi uhalali wa kuomba tena mabilioni mengine ya bajeti ikiwa kwa miaka 15 mfululizo imeteketeka mabilioni ya shilingi bila kuleta mafanikio yanayoonekana na yanayoendana na uhalisia wa mabilioni yanayotengwa kila mwaka kwa ajili ya Wizara hii?

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kambi ya Upinzani umebaini kuwa Serikali **haiko serious** katika kufukuzia fursa za kiuchumi na kusukuma maslahi ya nchi katika siasa za kimataifa. Diplomasia ya kiuchumi inataka utaalumu, inahitaji, viongozi wenye maono, wenye ushawishi, na mikakati madhubuti yaani nikimaanisha (**visionary leadership, strong negotiators, lobbyists, and smart strategies**) ndipo nchi ipate mafanikio. Tanzania tumepungukiwa vyote hivyo. Nchi haina maono, haina mikakati na haina wataalam wa kutosha kusukuma sera hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, nchi yoyote ile Duniani inayoongozwa na Kiongozi local, asiye na interest na masuala ya kimataifa, anayekimbia Mabalozi wa nchi Rafiki, anayeogopa na asiyependa kushiriki mikutano muhimu ya kimataifa, asiyejua nini kinaendelea katika ajenda za kimataifa, na asiyependa kujifunza kutoka kwa viongozi wa mataifa mengine, basi nchi hiyo haiwezi kufanikiwa kamwe. Huwezi kuongoza nchi inayotafuta fursa za uchumi wa dunia, halafu unajifungia Ikulu. Maendeleo ya nchi hayawezi kuja tu kwa kutumbua majipu ya ndani, bali kwa kutekeleza mikakati makini ya kiuchumi ambayo kufanikiwa kwake kunahitaji kushirikiana na mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, serikali yetu **haipo serious** na diplomasia ya uchumi. Ukitaka kuuthibitisha ukweli huu, tazama aina ya mabalozi wanaoteuliwa. Uchunguzi unaonyesha kuwa chini ya serikali hii ya CCM ubalozi hutolewa kama zawadi kwa makada waliosaidia kampeni; hutolewa kama pole kwa wanajeshi wastaafu wenye uswahiba wa karibu na CCM; na pia hutolewa kama adhabu

kwa wanasiasa wanaoonekana kuwa tishio kwa vigogo wa CCM wakati wa kuwania nafasi mbalimbali, hasa zile za kiserikali. Ni nadra sana kukuta fulani kapewa ubalozi kwasababu ana sifa za msingi.

Mheshimiwa Spika, makada hawa wa CCM wasiojua kitu kuhusu diplomasia ya uchumi, ndio wanaokabidhiwa dhamana ya kuhakikisha eti Tanzania inafanikiwa kimataifa. ***Kambi ya Upinzani inazitambua juhudi za Mhe. Rais Magufuli za kuwarudisha nyumbani baadhi ya mabalozi. Kwa dhamira njema kabisa tunaishauri Serikali kuitumia vizuri fursa hiyo kwa kufanya kwanza performance appraisal ya mabalozi*** ili kuwabaini vizuri wale wasio na sifa. Mabalozi wasioendana na wakati tulionao, waondolewe katika nafasi hizo. Wengi wao wangeweza kuwa mabalozi wazuri sana wa nyumba kumi-kumi lakini sio kutuwakilisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mabalozi wana wajibu mkubwa katika kubaini fursa za kiuchumi zilizopo kwenye mataifa mengine na kuiongoza serikali katika kushawishi na kuzitumia fursa hizo. Katika zama hizi mpya, tunahitaji mabalozi wenye uwezo wa kijasusi wa kiuchumi (economic espionage), ili wawe na tija kwa taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni chombo gani hasa kinachotumika kama kiunganishi kati ya balozi zetu na wizara hii na hata wizara nyingine ili mabalozi hao waweze kujua na kujifunza mambo mengine mazuri yanayofanywa katika Wizara mbalimbali? Je, ni namna gani Wananchi wanaweza kupata ripoti za Balozi mbalimbali kwa njia rahisi ili wahamasike katika kutafuta fursa za kiuchumi katika nchi hizo zenye wawakilishi wetu?

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina uhaba mkubwa wa wataalam wa diplomasia ya uchumi. Randama ya Wizara inathibitisha ukweli huu. Wakati serikali ilianza kutekeleza sera hii mwaka 2001 ina maana ilikwishajua vizuri kuwa haina wanadiplomasia wa kutosha. Cha kusikitisha, iliichukua wizara hii miaka 12 ndipo ikaanza kutoa mafunzo ya muda mfupi na ya muda mrefu (mwaka 2013) kwaajili ya kuzalisha economic diplomats. Matokeo yake, hadi kufikia mwezi Mei mwaka jana (2015) ni watumishi 32 tu ndio waliokuwa wamehitimu mafunzo ya muda mfupi ya diplomasia ya uchumi. Tuache mzaha, tuache ukada, tuliokoe taifa.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kufika kwa mwendo huu wa Konokono. Tunaposema CCM imeshindwa kuliongoza Taifa hili huwa tuna maana kuwa mambo madogo-madogo mnayoyafanya hayalingani hata kidogo na muda mwingi mnaotumia wala na fedha nyingi mnazotengewa. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge hili jinsi Serikali inavyojipanga kukabiliana na

uhaba huu mkubwa wa wanadiplomasia na jitihada inazokusudia kuzichukua kumaliza tatizo hili kwa haraka.

3. UONEVU WA MAKAMPUNI YA KIMATAIFA

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Wizara hii kuvutia wawekezaji. Lakini wizara haipaswi tu kuvutia wawekezaji, bali pia inapaswa kuhakikisha wawekezaji wanafanya shughuli zao katika namna isiyoathiri maslahi ya nchi na wananchi. Tathmini ya Kambi ya upinzani inaonyesha kuwepo kwa udhaifu mkubwa wa Wizara hii katika kutekeleza jukumu hili. Matokeo yake, makampuni ya kimataifa, hasa ya Madini, yamekuwa chanzo kikuu cha malalamiko na migogoro isiyokwisha miongoni kwa wananchi wetu na kuleta hali ya hofu, vifo, na kukata tamaa.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano mingi ya aina hii ya migogoro na uonevu unaofanywa na makampuni makubwa ya nje (multinationals). Mfano ni migogoro isiyoisha katika migodi ya Nyamongo huko Tarime ambapo wananchi wamekuwa wakilalamika kudhulumiwa haki zao na kampuni ya Acacia Mining (Barrick Gold) huku wizara husika, ikiwamo wizara ya mambo ya nje ikifumbia macho mambo haya.

Mheshimiwa Spika, kampuni hii ya Acacia Mining (Barrick Gold) imeendeleza tabia yake ya kukandamiza haki za wazawa kwa kusaidiwa na baadhi ya maafisa wa serikali kukiuka taratibu na sheria za nchi yetu. Tunazo taarifa za kampuni ya Acacia kuidhulumu kampuni nyingine ya wazawa iitwayo Bismark Hotel Mining Ltd ya Mwanza, kwa kupora na kudhulumu kitalu cha kampuni hiyo kilichopo Mgusu Geita.

Mheshimiwa Spika, tabia hii ya Makampuni ya Nje kuyadhulumu Makampuni ya Wazawa bila Wizara kuingilia kati, ni hatari kwa maslahi ya wananchi wetu na ni hatari pita kwa uhusiano wetu na Mataifa ya Nje. Wizara ichukue hatua madhubuti za kutatua migogoro yote inayosababishwa na makampuni ya nje. Wizara ianze na migogoro ya kampuni ya Acacia Mining (Barrick Gold), ukiwemo huu wa kuidhulumu kitalu cha Kampuni ya Bismark Hotel Mining Ltd, kwani kuuacha ni kuruhusu Wazawa kudhalilishwa na Makampuni makubwa ya Nje.

4. MAHUSIANO YA KIMATAIFA

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni serikali imetoa maelekezo kupitia mawasiliano yake na Mabalozi (*Note Verbale*) kuelekeza kuwa kabla ya Mabalozi au Maofisa wa Ubalizi kukutana na asasi zisizo za kiserikali au vyama vya siasa ni lazima kwanza waombe kibali cha serikali kupitia Wizara ya Mambo Nje.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kuwataka mabalozi kuomba kibali serikalini unaminyu uhuru wa mabalozi na wanadiplomasia mbalimbali wa kimataifa kufanya kazi zao hapa nchini. Kimsingi, amri hiyo ya serikali inakiuka utamaduni uliokuwepo awali na inakiuka Masharti ya Mkataba wa Vienna kuhusu Mahusiano ya Kibalozi Duniani. Huu ni ushahidi mwingine **kuwa serikali hii ya Awamu ya Tano imeamua kudhibiti uhuru wa habari nchini na imevuka mipaka kiasi cha kuingilia uhuru wa mabalozi na wanadiplomasia wanaofanya kazi zao hapa nchini.**

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Vienna unaoshughulika na masuala ya mahusiano ya kidiplomasia na kibalozi ya nchi mbalimbali Duniani, kwenye ibara yake ya 27 (1) inatoa masharti ya nchi inayopokea mabalozi kuwalinda na kuwapa uhuru wa mawasiliano yao yote na kutoyaingilia kwa namna yoyote ile. Katika Mkataba huo wa Vienna Ibara ya 41(1) inasema kuwa bila **kuathiri** masharti ya haki na kinga, Mabalozi wanajukumu la kuheshimu sheria na taratibu za nchi zinazo wapokea na wanatakiwa kutoingilia mambo ya ndani ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, maneno haya bila kuathiri (without prejudice) katika uandishi wa Sheria yana maana kubwa sana, hii ni kwa sababu serikali imekuwa ikitumia ibara hii kuwabana mabalozi wanaozikilisha nchi zao hapa nchini katika kutekeleza majukumu yao. Hii ina maana kuwa pamoja na Mabalozi kuwa na jukumu la kuheshimu sheria za nchi yetu bado jukumu hilo haliondoi uhalali au uwepo wa haki na kinga walizonazo – za kutoingiliwa - kwa mujibu wa Mkataba wa Vienna.

Mheshimiwa Spika, neno “**bila kuathiri**” (without prejudice) kwa tafsiri ya Kingereza lina maana ya “**without detriment to any existing right or claim**” “**without any loss or waiver of rights or priveleges**”. Ni wazi kuwa serikali haitatumia kifungu hiki kama utetezi wa namna yoyote ile ya kuwabana Mabalozi kwa kutumia utaratibu wa sasa wa serikali

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuondoa utaratibu huu inaotumia kwa sasa kwa sababu inaminyu na kuua uhuru wa mawasiliano kwa Mabalozi na wanadiplomasia mbalimbali waliopo nchini na hali hii inapelekea Taifa letu kuwa na sifa mbaya kwenye medani za kimataifa. Kambi ya Upinzani haioni msingi wowote wa kuwanyima mabalozi hawa waliotumwa na nchi zao kufanya mawasiliano halali na taasisi, vyama vya siasa au wadau wengine bila kuathiri sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, *Serikali inayoogopa mabalozi wa nchi za kigeni wasiwasiliane kwa uhuru na vyama vya siasa na taasisi nyingine hadi itoe kibali, ni serikali isiyojamini. Mabalozi ni wawakilishi halali kwa mujibu wa sheria, na vyama vya siasa viko kihalali kwa mujibu wa sheria, hii hofu inatoka wapi?*

Kambi ya Upinzani inaitaka serikali kutengua amri hiyo mara moja. Aidha, natoa wito kwa mabalozi wote nchini kuwa huru kuwasiliana na vyama vya siasa na taasisi mbalimbali kwani wanalindwa na Mkataba wa Vienna ambao Tanzania imeuridhia. Watanzania tunaoheshimu diplomasia, haki na uhuru wa kuwasiliana tupo tayari kushirikiana kwa karibu na jumuiya ya kimataifa katika kuhakikisha serikali ya Tanzania inaheshimu Mkataba muhimu wa Vienna, ikiwa itaendeleza udikteta katika hili.

5. PASI YA KUSAFIRIA YA KIDIPLOMASIA (DIPLOMATIC PASSPORT)

Mheshimiwa Spika, hatua ya serikali kutoa diplomatic passport kwa viongozi na kuwabagua wake au waume zao, haina mantiki katika dunia ya sasa inayohubiri usawa wa kijinsia na umuhimu wa kuimarisha familia. Umefika wakati sasa serikali irejee upya kanuni zake za kutoa diplomatic passport, hakuna sababu ya msingi ya kwanini wake au waume za viongozi wanyimwe wakati ni jambo jema kwa kiongozi kusafiri na mwenza wake. Utaratibu wa sasa hautoi tafsiri nzuri kwa Tanzania inayopinga uzinzi na kusesitiza upendo baina ya wanandoa. Umefika wakati serikali iache kusita, ilitazame upya suala hili. Taifa linaloamini katika nguvu ya ndoa na familia haliwezi kamwe likajaribu kuwatenganisha wanandoa hao kwa kitu kama diplomatic passport. Hizi ni zama mpya.

6. PROGRAMU YA KUTAFUTA FURSA ZA AJIRA NJE YA NCHI

Mheshimiwa Spika, wako wafanyakazi wengi wanaoajiriwa Tanzania wakitokea nje ya nchi kwa kigezo cha utaalamu (expertise). Wataalamu hawa wanalipwa pesa nyingi tena kwa kiwango cha kimataifa na wanalipwa kwa dola za kimarekani tofauti kabisa na wataalamu wetu wa hapa nchini hata kama wataalamu wetu wana uwezo kuzidi hao. Wafanyakazi wengi wa namna hii huja kupitia makampuni yanayopata tenda mbalimbali hapa nchini kama ya uchimbaji madini, kutengeneza barabara, makampuni ya simu n.k. Na nchi zao zimekuwa zikiwapa ushirikiano wa kutosha katika kuhakikisha wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, wakati wageni wengi wanaokuja nchini wanapewa kazi za ngazi za juu za kiutawala yaani managerial positions, Watanzania wanapokwenda katika nchi zao wanaishia kupata kazi kama za usafi, kubeba mizigo, kusambaza magazeti, kazi za viwandani na za majumbani, hata kama Watanzania hao wanataaluma nzuri na wana uzoefu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kupitia balozi zetu kwenye nchi mbalimbali duniani na kupitia wizara nyingine za kisekta, ihakikishe inatafuta fursa za ajira kwenye nchi hizo kwaajili ya Watanzania. Kinyume na hivyo, wizara hii na balozi zake itaendelea kupoteza

umuhimu kwa kushindwa kufanya mambo yenye tija na yanayomgusa mwananchi wa Tanzania. Aidha, serikali ijifunze kutoka nchi nyingine jinsi zinavyotafuta fursa za ajira kwaajili ya wananchi wao na kuhakikisha wanaojiriwa wanashika nafasi za juu pia (managerial positions) pale viwango vya elimu na uzoefu vinaporuhusu.

7. USALAMA WA WATANZANIA WANAISHI NJE YA NCHI

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanauwawa nchi za nje, Watanzania wanabaguliwa na kudhalilishwa huku serikali hii ya CCM ikikaa kimya bila kuchukua hatua zozote. Miongoni Watanzania waliuwawa kikatili hivi karibuni huko ughaibuni ni; marehemu Andrew Sanga maarufu kama “King Drew” aliyepigwa risasi - tena na mtu aliyefahamika - na baadaye kupoteza maisha baada ya kupata majeraha makubwa; marehemu Robert John Mpwata aliyeuawa kwa sumu nchini Ujerumani; marehemu Caroline Mmari aliyeuawa huko Los Angeles Marekani; marehemu Imran Mtui aliyeuawa huko India; marehemu Jerry Issack Mruma aliyeuawa huko Kenya; marehemu Method Clemence Mengi aliyeuawa kwa kuchomwa visu huko nchini Marekani pamoja na wengine wengi ambao sijawataja hapa.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote hao mahali pema peponi – Amina. Mbali na mauji hayo yuko binti wa Kitanzania aliyefanyiwa vitendo vya udhalilishaji kwa kuvuliwa nguo zake na kisha kutembezwa uchi mitaani. **Serikali isiyopaza sauti kulaani mauaji ya raia wake na inayoshindwa kulinda uhai wa raia wake, ni serikali inayopoteza uhalali wa kuongoza. Jukumu la kwanza na la msingi la serikali yoyote ile duniani ni kulinda uhai wa raia na mali zao.**

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitegemea serikali ikemee vikali kitendo cha serikali iliyohusika ikiwa ni pamoja na kuwakamata wahusika. Je, kuna uhalali gani wa mabalozi wetu kuwa katika nchi hizo endapo wanashindwa kuchukua hatua kali dhidi ya nchi zinazohusika kwa kuwa zimeshindwa kutoa ulinzi kwa watu wetu ? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuliambia bunge lako ni nini inategemea kufanya endapo tabia hizi zinazokiuka haki za binadamu zinaendelea kufanywa dhidi ya wananchi wetu?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka serikali ifanye uchunguzi wa kina juu ya sababu na mazingira yaliyosababisha kushamiri kwa mauaji ya Watanzania katika miezi na miaka ya hivi karibuni. Aidha, kwa kuzingatia matokeo ya ripoti hiyo, Bunge lako lijadili na kushauri hatua za kuchukuliwa na serikali na balozi zetu ili kuepusha mauaji ya raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa walisaini Azimio la Kutetea na Kulinda Haki za Binadamu; na kwa mauaji na ukiukwaji

mkubwa wa haki za binadamu unaowadhuru Watanzania hufanyika kwenye miongoni mwa nchi rafiki zilizoridhia Azimio hilo; Kambi ya Upinzani inashauri pia serikali yetu ivunje ukimya, ipaze sauti kuzitaka nchi husika ziongeze juhudi za kulinda usalama wa raia wa Tanzania na wa nchi nyingine dhidi ya mauaji na ukiukwaji wa haki za binadamu.

8. KANZI DATA YA WATANZANIA WAISHIO NJE YA NCHI (DIASPORA DATABASE)

Mheshimiwa Spika, Dunia sasa inatambua mchango mkubwa wa uchangiaji uchumi unaofanywa na watu mbalimbali wanaoishi nje ya nchi zao (yaani Diaspora).Hatuna budi kama Watanzania kuendelea kutambua na kuthamini mchango huu mkubwa unaofanywa na kaka na dada zetu wanaoishi nje ya nchi kwani uwepo wao huko unachangia kukuza jina la nchi yetu na kuboresha mahusiano na nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, hakuna takwimu za kitaifa zinazoonyesha idadi kamili ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi na taarifa za kile wanachokifanya huko. Umuhimu wa kuwa na taarifa ni kubaini kwa wepesi idadi na aina ya watu wenye ujuzi na uzoefu ambao serikali inaweza kuutumia kwa maslahi ya nchi. Aidha, kujua idadi ya wananchi walio nje ya nchi kutapelekea kutengeneza milango ya kiuchumi kati yao na nchi (economic gateway),kutafungua fursa za kibiashara ikiwa ni pamoja na soko la nje (export market) kwa bidhaa zetu za Kitanzania na hivyo kutaachia fursa kwa soko la ndani kuboresha bidhaa zao ili ziweze kupata masoko nje.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa database hiyo pia yenye kila Mtanzania aliyepo nje ya nchi kutasaidia kupunguza idadi ya raia wa nchi nyingine wanaotumia jina la nchi yetu vibaya huko nje ya nchi kwa kujifanya ni wakimbizi kutokea Tanzania.Tutaweza kuwatambua na kuwabaini kwa kutumia balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha kuwa jambo hili la kutengeneza database linazingatiwa kwa uzito wake kwa kuwa lina manufaa kwa wananchi wetu walio katika kila pembe ya dunia na pia manufaa kwa ya uchumi wa nchi yetu.

9. URASIMISHAJI WA FEDHA KWA WATANZANIA WANAIOISHI NJE YA NCHI (FORMALIZATION OF DIASPORA REMITTANCES)

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanaoishi nje wamekuwa wakifanya jitihada kubwa za kuchangia uchumi wa nchi hii japo serikali imekuwa haiwapi ushirikiano wa kutosha. Hii ni kwasababu serikali kuwa imejitenga na watu wake

wanaoishi nje ya nchi, basi hata michango inayoingia nchini imekuwa ni kidogo tofauti na matakwa au matamanio ya ndugu zetu hao.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo linashangaza sana. Mtanzania anapotaka kutuma kiasi chochote cha pesa kwenda nje ya nchi imekuwa ni rahisi sana, lakini anapotaka kuingiza fedha ndani ya nchi kutoka nje inakuwa ni vigumu sana kwasababu kuna urasimu mkubwa na wenye kukatisha tamaa. Yote hii ni kwasababu serikali haijajiwekea utaratibu wa kuwasaidia Watanzania kutafuta mbinu za kuingiza fedha nchini. Kambi rasmi ya upinzani inaitaka serikali ya CCM ijifunze kutoka kwa majirani zetu Somalia, Ethiopia, Kenya na Rwanda wanavyofanya.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014 mwezi Novemba serikali ya Kenya ilizindua taasisi inayotoa elimu kuhusu masuala ya remittances chini ya Tume ya Umoja wa Afrika (African Union Commission). Taasisi hiyo inayojulikana kama African Institute for Remittances (AIR) ilizinduliwa ili kutoa fursa kwa Wakenya wengi kujifunza masuala ya remittances na kuona ni kwa namna gani nchi hiyo itanufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014/2015 Benki ya Taifa ya Ethiopia (National Bank of Ethiopia) ilikusanya remittances kutoka \$1.5 bilioni mpaka dola \$bilioni 2 kwa kipindi cha mwaka mmoja pekee fedha zilizochangia kwa kiasi kikubwa kupanda kwa uchumi wa nchi hiyo. Ni vyema sasa na sisi Tanzania tuanze kubuni mbinu za kunufaika na michango hii, kwa faida ya uchumi wa nchi yetu na kuwakwamua Watanzania wengi katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutambua, kuthamini na kuheshimu michango ya wananchi wanaoishi nje ya nchi ikiwa ni pamoja na shughuli zote za kimaendeleo wanazozifanya kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Hivyo basi, pamoja na yale yote yaliyopendekezwa na Kambi hii katika kipindi chote cha Bunge la Kumi kuhusu remittances, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri yafuatayo:

- i. Serikali iagize Benki kuu ya Tanzania (BOT) kutengeneza kitengo maalumu chenye mfumo wa ufuatiliaji wa fedha yaani (tracking system), zinazoingizwa nchini kwa njia mbalimbali kutoka kwa Watanzania waishio nje ya nchi ili kuweza kujua mchango wao kwa Taifa. Hii pia itasaidia kutambua fedha zinazoingia nchini kwa njia ya utakatishwaji, au kufadhili vikundi yovyote haramu ambavyo vinaweza kuhatarisha usalama wa Taifa letu.
- ii. Serikali ije na muswada wa kutengeneza Sera ya Taifa ya Diaspora (National Diaspora Policy). Sera hii iwe mahususi kwa ajili ya kushughulikia maswala ya Wananchi wetu wanaoishi nje ya nchi,

kama nchi jirani ya Kenya ilivyotengeneza sera ya namna hii ili kulinda maslahi ya wananchi wake wanaoishi nje ya Kenya (National Diaspora Policy of Kenya).

- iii. Vilevile, serikali ije na muswada wa kuwa na sera ya uwekezaji wa Diaspora (Diaspora Investment Policy) ili kuweza kuwasaidia Wananchi wetu walio nje ya nchi kuweza kusaidiwa na serikali katika kutafuta maeneo ya uwekezaji, kutoa fursa za uwekezaji ndani ya nchi, kusaidia mazingira ya uwekezaji wa wananchi wetu nje ya nchi (Facilitation of investment abroad). Hii ni kwa sababu serikali imekuwa ikizungumzia na kutekeleza "foreign investment policy" na kusahau kuwa wananchi wetu wanahitaji msaada mkubwa wa serikali yao ili na wao waweze kuwekeza nje ya nchi na hivyo faida kurudi nyumbani. Kwa kuweza kufanikisha hili hata remittances itaongezeka.

iv. Serikali iwaagize mabalozi katika nchi husika kuratibu na kutoa semina kwa Watanzania waishio nje na kufanya kazi nje ya nchi juu ya umuhimu wa kuwekeza katika nchi yao, ili kwa kufanya hivyo waweze kuchangia Pato la Taifa na hatimaye kukuza ukuaji uchumi wa nchi yetu.

10. HADHI YA BALOZI ZETU KWENYE NCHI MBALIMBALI

Mheshimiwa Spika, balozi zetu ndio taswira halisi inayomulikwa na nchi rafiki kuhusu Tanzania. Tunatia aibu. Majengo ya balozi nyingi ni chakavu, utendaji kazi hauridhishi, na nyingi zimeonyesha uwezo finyu wa kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia na uchumi wa kidiplomasia. Hata Jengo la Wizara hii nalo linatutia aibu kama Taifa. Majengo mengi yanavuja, hayana miundombinu ya kisasa na muonekano unaokidhi hadhi ya Kimataifa. Wakati mwingine serikali inalazimika kukodi majengo ya bei rahisi ambayo kimsingi hayana hadhi ya kutumika kama balozi.

Mheshimiwa Spika, tuna maeneo mengi ambayo tumepewa viwanja ili tuweze kujenga balozi zetu na mpaka leo viwanja hivyo havijafanyiwa lolote. Pia kuna maeneo ambayo serikali ilishaweka jiwe la Msingi mpaka leo hakuna lililoendelezwa. Mfano, tarehe 17/10/2012, Mheshimiwa Rais Mstaafu Jakaya Kikwete aliweka jiwe la Msingi na kuahidi kujenga ubalozi wa Oman kabla ya hajaondoka madarakani. Mpaka sasa hakuna kilichofanyika. **Kwa udhaifu huu uliokithiri umepelekea Kambi rasmi ya Upinzani kugundua sababu ya Serikali kuizuia Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama isifanye ukaguzi wa Balozi zetu.** Huu mchezo wa kufunika Kombe Mwanaharamu unaidhalilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali iboreshe balozi zetu. Serikali iepuke kulipa fedha nyingi kupanga majengo kwa ajili ya ofisi za balozi. Serikali itumie wadau mbalimbali yakiwemo makampuni na mashirika binafsi ndani na nje ya nchi ili iweze kujenga majengo ya kudumu na kuacha kuwa wapangaji. Tunaitaka Serikali ielewe kuwa kuonekana **maskini sio sifa wala mkakati wa kuhurumiwa, bali ni fedheha inayoishushia nchi yetu hadhi na nguvu ya kiushawishi mbele ya mataifa mengine.**

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo kumekuwepo na uzembe mkubwa katika kusimamia mali za umma kwenye balozi zetu. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ya June 2015, Ubalozi wa Tanzania ulioko Kampala Uganda hauna hati miliki ya Ardhi ambayo jengo la Ubalozi limejengwa. Hali hii inaweza kuisababishia serikali kupoteza haki yake ya umiliki endapo itatokea kutokuelewana katika umiliki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutupa sababu za Kimsingi ni kwa nini mpaka leo hati ya ardhi ya ubalozi huu wa Kampala haijapatikana na inachukua hatua gani kuhakikisha hati hiyo inapatikana kwa uharaka?

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo serikali haijaona umuhimu wa kujenga au kuwa na ubalozi. Mathalani kama Lubumbashi ambapo ni eneo muhimu la kuwa na ubalozi mdogo. Eneo hili ni muhimu kwa uchumi wa Tanzania kupitia bandari ya Dar es Salam kwa usafirishaji wa biashara ya mizigo. Ni dhahiri litachochea sana shughuli za kiuchumi ambapo tuko hatarini kupoteza fursa na maeneo mengine kama Afrika Kusini na Namibia.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuweza kutambua maeneo nyeti ya kiuchumi ili tuweze kutafuta fursa za uwekezaji na fursa za kibiashara.

11. USIMAMIZI WA FEDHA KWENYE BALOZI ZA TANZANIA

Mheshimiwa Spika, balozi zetu nyingi bado hazitumii mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha kwa njia za kieletroniki za kompyuta IFMS-EPICOR, ambayo ndiyo njia bora zaidi za kusimamia matumizi ya kifedha na kuharakisha uandaji wa ripoti mbalimbali za kifedha katika Taasisi za Umma, kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya CAG 2015. Balozi ambazo bado hazitumii mfumo huo ni ubalozi wa Tanzania Cairo, Tokyo, Harare, Abuja, Brussels, London, Ubalozi wa Umoja wa Mataifa Geneva nk.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha balozi hizi kutotumia Mfumo huu kama ilivyoamriwa na serikali ni kukiuka kabisa taratibu ambazo serikali yenyewe imejiwekea. Kuendelea kutumia mfumo wa kizamani usio wa kompyuta ni kuruhusu watu wasio na nia njema kupitisha fedha zisizo halali. Jambo hili linaweza kuhatarisha imani ya nchi yetu katika mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali ichukue hatua dhidi ya mabalozi au watendaji wanaoshindwa kutekeleza maazimio na maagizo ya serikali. Aidha, tunaitaka serikali ipeleke wataalamu wenye uwezo, wanaoendana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia dunia (Global technology) ili waweze kutumia mfumo huu kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Serikali iandae mafunzo kwa ajili ya wataalamu wake katika balozi hizi ili waweze kutambua umuhimu wa kutumia mfumo huu.

12. MASLAHI YA WATUMISHI KATIKA BALOZI ZA TANZANIA

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa balozi za Tanzania kwenye nchi mbalimbali wamekuwa wakiishi kama omba-omba kwasababu ya posho zao kutokufika kwa wakati. Zipo balozi nyingine zina watumishi wachache sana (under staffing) kiasi cha kukwamisha kazi au kusababisha waliopo kuonekana hawafanyi kazi ipasavyo. Mfano ubalozi wa Oman ulikuwa na watumishi watano tu na katika hao kulikuwa na mtaalamu mmoja wa uchumi, mlinzi na msaidizi wa Balozi. Hata hivyo, mtaalamu huyo alipewa kazi nyingine na hivyo ofisi kukosa mchumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha watumishi hao wanapata stahiki zao na malipo yao yafanyike kwa wakati. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha kuwa inapeleka watumishi wa kutosha katika ofisi zetu ili pale wanaposhindwa kufanya kazi ipasavyo iweze kujipambanua na utumbuaji Majipu. Ihakikishe kuwa inapeleka wataalamu na vitendea kazi ili waweze kufanya kazi kwa moyo zaidi

13. JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Mheshimiwa Spika, ni miaka 16 tangu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), lakini bado Tanzania haina Sera yake ya Utengamano kwenye jumuiya hii kama ilivyo kwa nchi za Kenya na Uganda. Kwa kukosa sera hii muhimu Tanzania inakuwa haina dira ya nini hasa tunasimamia au tunataka kwa maslahi ya nchi yetu kwenye jumuiya hii. Kwa kutokuwa na sera hii, Wabunge wetu wa Afrika ya Mashariki wanakuwa hawana muongozo wowote muhimu wa kusimamia maslahi ya nchi wanapokuwa kwenye vikao vya Bunge hilo.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kielelezo kingine cha kuwa na Serikali isiyo **Serious** katika kusimamia masuala ya msingi ya nchi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ijieleze ni kwanini hadi leo hatuna sera ya utengamano? Na ni lini serikali itahakikisha sera hiyo inakamilika? Serikali pia imeonyesha udhaifu mkubwa katika kuwasaidia na kuwatumia wabunge wetu wa Afrika Mashariki kutekeleza vizuri wajibu wao kwenye jumuiya hiyo;

- Serikali imeshindwa kuwapatia ofisi wabunge wetu wa EAC kiasi cha kulazimika kufanyia shughuli zao za kibunge nyumbani au hotelini
- Serikali imeshindwa kuwapatia usafiri Wabunge wetu wa EAC licha ya kuombwa kupatiwa mikopo ya magari isiyolipiwa kodi kama ilivyo kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Serikali imeshindwa kuwatumia wabunge wetu wa EAC katika kuhamasisha wananchi kuzifahamu faida na fursa za jumuiya hii. Matokeo yake miaka 16 tangu kuanzishwa kwa EAC, uelewa wa Watanzania bado ni mdogo sana.
- Serikali imeshindwa kuwapatia Mtafiti (researcher) wabunge wetu wa EAC na kuwaacha wakichangia mijadala kwa kutegemea tu utashi wao badala ya ushahidi wa kitafiti. Serikali zilizo serious duniani huwa hazifanyi uzembe kama huu.
- Kambi ya Upinzani imebaini kuwa mpaka sasa wabunge wetu wa EAC hawajui wako chini ya nani na wanapaswa kuripoti kwa nani hasa, kwa Wizara au kwa Bunge? Huu ni udhaifu mwingine wa serikali wa kushindwa kutoa miongozo na kufanya kazi kwa karibu na wabunge wetu.
- Kambi ya Upinzani inazo taarifa kuwa Serikali ya Tanzania ndiyo inayoongoza kwa urasimu na uzembe wa kushindwa kufanya maamuzi kwa wakati kwa masuala yanayoihusu Tanzania. Udhaifu huu umekuwa ukichelewesha kufikiwa kwa maamuzi kadhaa ya Bunge la EAC katika kupitisha miswada.

Mheshimiwa Spika, mapungufu yote haya yanathibitisha jinsi Serikali yetu isivyo **serious** katika kusukuma maslahi ya nchi kwenye EAC. Aidha, huu ni ushahidi kuwa Tanzania bado haijajiandaa na wala haina wataalamu wa kuiongoza vizuri Serikali katika kusukuma diplomasia ya kiuchumi hata kwa nchi jirani za Afrika Mashariki. Na kwa mapungufu haya, Kambi rasmi ya Upinzani haioni tija yoyote ya fedha ambazo serikali imekuwa ikitengewa na Bunge hili kwaajili ya shughuli za Afrika Mashariki. Kwa udhaifu huu, wizara hii inabaki kuwa ni wizara ya safari, vikao na mikutano visivyokuwa na tija yoyote kwa maendeleo ya nchi kwasababu ya serikali kushindwa kujipanga na kutimiza wajibu wake. Kambi ya Upinzani tunaitaka serikali ijitathimini, ijipange upya na itupe mkakati makini na endelevu kuhusu ushiriki wenye tija wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

14. DEMOKRASIA NA HAKI ZA BINADAMU

Mheshimiwa Spika, nchi ya Burundi ilifanya Uchaguzi wake Mnamo Mwezi Julai 2015, na Uganda tarehe 18, Februari 2016. Makundi ya wanasiasa na wanaharakati mbalimbali wa haki za binadamu walishutumu tume za uchaguzi, walishuhudia ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi, mauaji ya viongozi wa Upinzani na kila alama ya udikteta dhidi ya wananchi wa nchi hizo. Nchini Uganda,

viongozi wa Upinzani akiwemo Kiongozi Mkuu wa Upinzani nchini humo, Kizza Besigye, aliwekwa korokoroni katika kipindi cha uchaguzi na hata baada ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, serikali ya Tanzania ilipaswa kukemea uovu huo waziwazi kama alivyokuwa akifanya Mwalimu Julius Nyerere alipokuwa akikemea vitendo vya kidikteta, unyonyaji na ubaguzi wa rangi kabla na baada ya kupata uhuru. Hata hivyo, kambi ya upinzani haikushangazwa na hatua ya serikali kubariki yaliyofanyika kwenye nchi hizo. Hayakuwa na tofauti yoyote na yale yaliyofanywa na CCM kwenye uchaguzi mkuu wa 2015 na ule wa marudio wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sasa ni dhahiri kuwa vyama tawala vya nchi hizi vinashirikiana katika kukandamiza wapinzani na kung'ang'ania madaraka kwa style ya kuitisha chaguzi zisizo za kidemokrasia na kujiweka madarakani. Kambi ya Rasmi ya Upinzani inaonya kuwa mchezo huo ni hatari sana kwa amani ya nchi na kwa ukanda mzima wa Afrika Mashariki. Ni vema ikazingatiwa kuwa mchezo huu wa CCM na washirika wake hauwezi kudumu siku zote bila kusababisha machafuko yatakayodhuru pande zote – upinzani na vyama tawala. Kwa hiyo, kwa mara nyingine tena naishauri serikali hii ya CCM iache kubaka demokrasia na ikome kubariki uvunjifu wa demokrasia na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, amani ya Afrika Mashariki ndio amani ya dunia. Kambi ya upinzani inatoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kupitia balozi zake zote zilizopo hapa nchini, kwamba ianze bila kuchelewa kutafuta suluhu ya kujenga demokrasia ya kweli katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki; vinginevyo upo uwezekano wa kutokea uvunjifu mkubwa wa amani katika siku za usoni utakaokuwa na athari pia kwa dunia.

15. BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 serikali imetenga kiasi cha fedha shilingi 151,396,775,000.00 ili kuendesha shughuli zote za Wizara hii. Wizara hii imekua ikikumbwa na changamoto nyingi za kifedha na hivyo kupelekea balozi kuwa hoi kifedha na kushindwa kujiendesha. Kitendo cha kutenga bajeti ndogo kunakwamisha nia ya dhati ya utekelezaji wa sera ya diplomasia ya uchumi.

16. BAJETI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Bajeti 2015/2016 fedha iliyopitishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi mengine katika wizara hii ilikuwa ni shilingi 103,219,972,979, na mishahara ilikuwa ni kiasi cha shilingi 7,657,682,410 lakini

fedha za Maendeleo zilizokuwa zimetengwa kiasi cha shilingi 8,000,000,000 hazikupelekwa katika Wizara hii. Mpaka Mwezi Machi, 2016 fedha hizo hazikuwa zimetolewa na hazina.

Mheshimiwa Spika, serikali inajua wazi umuhimu wa fedha za Maendeleo. Kutokupeleka fedha za Maendeleo katika Wizara hii kuna maanisha kuwa balozi zetu, na watumishi wake hawafanyi malengo yaliyokusudiwa na Wizara. Haya ni matumizi mabaya sana ya rasilimali watu na rasilimali fedha. Shughuli zilizopangwa kufanyika katika Wizara zinakosa kutekelezwa kabisa. Tabia ya kupanga mipango na kisha kutoitekeleza kunasababisha mrundikano wa mikakati isiyo na tija katika taifa.

Mheshimiwa Spika, hii sio mara ya kwanza kwa serikali kuonyesha udhaifu huu mkubwa. Tabia hii imetengeneza usugu ambao kimsingi usugu huu unatengeneza tabia ya watu kwenda kwenye ofisi kama utaratibu tu (formality) lakini uwepo wao katika ofisi hauna tija.

Mheshimiwa Spika, Kitendo hiki cha serikali cha kutokutoa fedha za maendeleo ni hadaa na uzushi mtupu kwa wananchi ambao kwenye kampeni waliahidiwa kuletewa maendeleo. Kambi Rasmi inaitaka serikali kuacha kabisa mtindo huu wa kutenga fedha ilhali ikijua kabisa fedha hiyo haipo. Ni bora kuwa na vipaumbele vichache vitakavyotengewa fedha na kutekelezwa kuliko kuwa na vipaumbele vingi visivyo tekelezeka.

17. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nahitimisha hotuba hii nikionya na kusisitiza yafuatayo:

Kwanza, serikali iwekeze kwenye kusomesha na kutoa mafunzo yatakayoipatia nchi wanadiplomasia wa uchumi wa kutosha. ***Investment in knowledge is the best investment.***

Pili, tabia ya kung'ang'ania madaraka ya baadhi ya Viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania itasababisha machafuko yatakayodhuru pande zote. Serikali lijifunze kutoka Zambia, Nigeria na kwingineko ambapo demokrasia inaheshimiwa. Serikali iepuke kuwa mpambe wa nchi zinazofanya siasa za kijima katika karne hii ambayo kila nchi inajitahidi kuwa na dola iliyostaarabika. ***“Let us be slow walkers, but never walk back”***

Nne, serikali itengeneze fursa kwa wananchi kushiriki kikamilifu kwenye ushindani wa kibiashara na kiuchumi ndani na nje ya nchi hususani katika nchi marafiki.

Tano, Serikali izingatie kuwa ***“uhusiano mzuri wa kimataifa wa nchi yoyote ile duniani unategemea sana ustaarabu wa ndani na mwenendo mzuri wa Serikali ya nchi hiyo kwa watu wake. Nchi yenye Serikali katili, ya kidikteta, isiyopenda***

kukosolewa, ya kifisadi, isiyoheshimu haki za binadamu, utawala wa sheria, demokrasia na inayokandamiza uhuru wa wananchi wake – kama Tanzania - haiwezi kuheshimiwa wala kuwa kivutio kwa mataifa mengine katika kujenga na kudumisha uhusiano mzuri na wenye tija kimataifa.

[Maneno “kama Tanzania” siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha

Mchungaji Peter Simon Msigwa (Mb)

**WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KARIKA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI,
KIKANDA NA KIMATAIFA.**

31 Mei, 2016

MWENYEKITI: Ahsanteni sana, Waheshimiwa Wabunge acha nifanye kazi moja ya kikanuni, ndiyo maana nimesimama.

Nimeisoma hotuba nzuri tu aliyomaliza kuwasilisha Mheshimiwa Msigwa ambayo inawakilisha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Lakini kwa mila na desturi na maamuzi ya nyuma ya Spika, ukurasa wa 32 wa hotuba hii *paragraph* ya mwisho hiyo ambayo imewekwa msisitizo *in bold*, ukiisoma hivyo ni kitu kizuri kwa sababu haya ni majukumu ambayo yanapaswa kufanywa na Serikali yoyote ambayo inayozingatia utawala bora, inayoheshimu utawala wa sheria na mengine yote kwa usatawi wa wananchi wake.

Waheshimiwa Wabunge, huwa tunaita *expositions*, na ndio maana hata ukichukua Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ile misingi mikuu inayotakiwa kuzingatiwa na Serikali na vyombo vyake vyote imeainishwa huku na ndiyo maana tunayafanya yote haya, mazuri kwa faida ya ustawi wa nchi yetu.

Lakini unapofika kusema kama Tanzania ni kama, sasa unatujumlisha sisi nchi hii kwamba yote hayo mnayoyasema hatuyafanyi. Ndiyo nasema kwa kutumbukiza maneno kama Tanzania nadhani wote mmeyaona. Sasa, inaleta sura ya kwanza, ukakasi mzito kweli kweli, ukiruhusu inaleta malumbano, inaleta uchochezi, ina maudhi. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kabisa.

MWENYEKITI: Sasa kwa kutumia mamlaka ambayo ninayo kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kanuni namba 5(1), naagiza maneno hayo kama Tanzania yaondoke na yasiwe sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Nafanya hilo kwa kuzingatia maamuzi ya nyuma yaani *precedent* ya Maspika wa Bunge hili. Baada ya kusema hayo sasa tuendeleo na wachangiaji walioko kwa asubuhi ya leo, tutajitahidi lakini tunaanza kwa uwiano wetu. *(Makofi)*

Mchangiaji wetu wa kwanza wa asubuhi ya leo sijui kama ni asubuhi, atakuwa ni Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Masele. *(Makofi)*

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa nimshukuru Mungu kwa kunipa nafasi na kunijalia zawadi ya uhai ili niweze kusimama kwenye Bunge lako Tukufu niweze kutoa mchango wangu kwa Wizara hii ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Kikanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza hii ni kwa ajili kuweka rekodi vizuri tu, nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Iringa na hasa makanda wa Chama cha Mapinduzi wa pale Iringa Mjini. Kumbe walifanya kazi nzuri sana ya kumkaba mpinzani wao mpaka leo anaonesha kwenye Bunge hili kwamba ushindi wake ni ajabu sana hakuutegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa hii ya Kambi Rasmi ya Upindani, unaona kuna vitu vimeandikwa kijinga kabisa. Moja ya kitu kulichoandikwa kijinga neno Mungu anaandikwa kwa herufi ndogo mimi sijawahi kuona mahali popote pale, ukitaka kutaja Mungu lazima uandike kwa herufi kubwa. Kwa hiyo, uchungaji wa Msigwa unanitia mashaka makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia Chuo cha Diplomasia. Chuo cha Diplomasia ni chuo kinachofanya kazi kubwa sana ya kuwaelimisha, kuwafundisha, watu, wananchi wanaoteuliwa kuwa mabalozi, wake wa viongozi, Wakuu wa Nchi, ili kuweza kujua diplomasia inafanyaje kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali itenge fedha ya kutosha kwa chuo hiki ili kiweze kufanyakazi yake kwa ufanisi na nimuombe Waziri atakaposimama hapa kutoa majibu atueleze ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya chuo hiki ili kiweze kufanya kazi yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme hizi kelele mnazosisikia kwenye Bunge hili, Wabunge wa CCM nataka niwapongezeni kwa utulivu mlionao. Tunasemwa maneno mabaya lakini tunavumilia mpaka wasemaji wamalize, lakini sisi tukitaka kujibu kidogo unasikia kelele za kuwashwa washwa upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme moja ya diplomasia kubwa iliyojengwa katika nchi yetu ni kuwa na upinzani japo kwamba upinzani wenyewe ni dhaifu. Tunao upinzani lakini ni dhaifu hata kwenye kujenga hoja. Mtu anasimama hapa kuzungumzia habari ya Mabalizi hawafanyi kazi, anasimama hapa kuzungumzia habari ya Rais haendi nje. Tulikuwa na Rais Kikwete, anasafiri kila siku. Hawa walisimama Bungeni hapa kusema kwamba Rais anasafiri sana, Rais anatumia fedha nyingi, leo tumempata Dkt. Magufuli, Rais anabana matumizi, fedha zinaelekezwa kwenye maendeleo, hawa wanasimama kupinga, watu gani hawa. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanataka tufanye nini, leo nataka niwaambie ndugu zangu kweli kazi kubwa ya upinzani ni kupinga lakini sio huu, huu ni upinzani hewa kwa sababu hakuna wanachopinga, wao wenyewe wanaingia wanasaini wanaondoka bila kufanya kazi, leo hii wanataka kusema kwamba nchi hii haina demokrasia wangekuwepo hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo upinzani wa Tanzania naufananisha kama mtoto mchanga tumboni. Mtoto mchanga tumboni haelewi ukubwa wa dunia. Kwa hiyo, anafikiria eneo la tumbo la mama yake ni eneo kubwa linalostahili hata kucheza. Hajui kwamba akitoka duniani kuna eneo kubwa mno, kuna eneo la kukimbia atachoka, kuna eneo la kucheza atachoka, kuna eneo la kulima atachoka, kuna eneo la kutembea atachoka. Hawa wanafikiria kama mtoto mchanga tumboni anayefikiria eneo la tumbo ni eneo kubwa sana. Leo unamkosoa Balozi eti kwamba tunao Mabalizi wenye hadhi ya nyumba kumi, haya ni matusi wa Mabalizi wetu. Mabalizi wetu ni Mabalizi waliochunjwa, wameiva, ukiwepo Balozi Mahiga, nani asiyejua kwamba Mahiga ni moja ya watu waliobobea katika masuala ya kidiplomasia ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanasimama hapa kutuambia as if kwamba sisi ni watoto wadogo. Hivi ingekuwa Watanzania wote au viongozi wote wa nchi hii wanatakiwa kusafiri nje ya nchi kwenda kuwasilisha masuala ya nchi hii wao wangekuwa Wabunge hapa. Si kila mwananchi wa Jimbo lao angekuja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wananchi wote kuja kwenye jengo hili ndio maana tumekuchagua Msigwa, ndio maana tumekuchagua Januari, ndio maana umechaguliwa Lusinde, kwa sababu wana nchi wa Jimbo zima hawawezi kuhudhuria katika kikao hiki. Sasa leo wanataka nchi nzima kila mtu

akajiwakilishe kule, katika kimataifa aende akazungumzie matatizo ya nchi, haiwezekani ndio maana kuna Mabalizi wameteuliwa. Jifunzeni ninyi! Kwa hiyo, nataka niwaambie, anazungumza pale mwisho, anasema nchi ya kifisadi kama hii wakati fisadi mkuu mnaye nyie. (Makofi/Vigelele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao upinzani ambao unachosema haukielewi, wanachopinga hawakielewi, walichosema mwaka jana mwaka huu wanakuja wanajijibu. Walichokataa mwaka juzi, mwaka huu wanakuja wanakikubali. Nataka nimpungeze Rais Magufuli, amewafanya wapinzani wa nchi hii hawana hoja, ndio maana mnawaona wakisimama humu hakuna lolote la msingi wanalolisema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, amewafanya wapinzani wa nchi hii hawana hoja ya msingi, sasa imekuwa moto ukiwaka wanatoka nje ya Bunge, daladala ikiungua wanatoka nje ya Bunge kwa sababu hoja ya msingi hawana maana Rais anafanya kazi vizuri. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishe Rais akienda kwa speed hii kufika mwaka 2020 hawa watakuwa hawapo ndani ya Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaitumia diplomasia ya nje kuhakikisha kwamba nchi hii inapata uchumi mkubwa utakaowafanya wananchi wanufaike, na utakaowafanya wapinzani wa nchi hii waondolewe na wananchi kwenye Bunge. (Makofi)

WABUNGE FULANI: BUUUUUU!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie, nina uzoefu wa kuongeza na hawa, nina uzoefu nao, unapowaona wanapiga kelele jua sindano zinaingia ndio maana unaona wanapiga kelele. Huwezi ukasimama kwenye Bunge hili ukiita Tanzania ni nchi ya kifisadi wakati fisadi mkuu mmemchukua, na itafika mahali nataka nikuambie, hata Mheshimiwa Mahiga hawa wakubeze vipi, siku ukijiunga kwao utakuwa mgombea Urais wa chama hicho, za kwao hawa ni kuokoteza tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namtia moyo Mheshimiwa Waziri na Naibu wako, Katibu Mkuu na Mabalizi wote wakilisheni nchi kama Rais alivyowaamini, watanzania tunawaamini, na ndio maana tuko nyuma yenu tunawaunga mkono. Chapeni kazi na hiyo kazi italeti manufaa hata kwenye Majimbo ya hawa wanaopiga kelele leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa imetosha, Waheshimiwa naomba utulivu Bungeni, naomba utulivu.

Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu unapokaa hapa nawaona wote mnaoongea huku na mnaoongea huku, wote naweza nikawataja. Sio kitu kizuri tuvumiliane, kwenye demokrasia ndio hii, tuvumiliane tu, kwa sababu ya muda jamani tuchangie maana muda sio rafiki kwetu, Mheshimiwa Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato.

MHE. STEPHEN J. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa dira ya nchi yetu inakoelekea hasa kwenye siasa za Kimataifa na diplomasia ya uchumi. Nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Waiziri Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba, Katibu Mkuu Dkt. Aziz na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kuitangaza nchi yetu na kuvutia uwekezaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina historia na ina historia kubwa hasa kwenye siasa za kimataifa. Tangu tupate uhuru chini ya uongozi wa Baba wa Taifa alijenga misingi imara ya kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa na sauti kwenye ukanda wa Kusini mwa Afrika na hasa kwenye masuala ya ukombozi wa Bara letu la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi ile ilijengwa na misingi imara na unatakiwa kuendelezwa kwa kukifanya Tanzania kuwa nchi yenye sauti kubwa na ushawishi wa kisiasa na kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na Kusini mwa Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kupongeza uongozi mzima wa Wizara pamoja na Serikali kwa kushiriki kikamilifu kusuluhisha mgogoro wa Kongo (DRC). Wote hapa tunafahamu umuhimu wa Kongo (DRC), mahusiano yetu ya kindugu, ya kijamii na kiuchumi. Kwa hiyo, uhusiano na ushiriki wa Tanzania kuhakikisha kwamba nchi ya Kongo inapata amani ya kudumu ni jambo la kipaumbele kwa Tanzania na kwa Serikali yetu. Lakini hivyo hivyo niipongeze Serikali kwa kuhakikisha kwamba Burundi inaendelea kuwa salama na Baba wa

Taifa alieleza kabisa kwamba huwezi kuwa salama kama majirani zako wote hawako salama, na wote tunatambua umuhimu wa kiuchumi wa nchi hizi zinazotuzunguka kwa maendeleo ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita zaidi kwenye diplomasia ya uchumi ambayo mwelekeo wa Wizara na Serikali kwa sasa imeweka mkazo mkubwa kwenye diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba zako zinazofuata ni vyema ukaja na takwimu uoneshe Watanzania mipango na safari na mikutano ya nje ambayo nchi yetu inashiriki imeleta faida gani kwa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa taarifa na Ripoti ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa Tanzania kwa mwaka 2014 imeongoza kwa kuwa ni Taifa la kwanza kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuingiza mapato mengi ya uwekezaji wa fedha za kigeni kwa maana ya *Foreign Direct Investments*. Leo kwa ripoti ile Tanzania iliingiza zaidi ya dola za Marekani bilioni 2.14 ukilinganisha na Taifa ambalo lina uchumi mkubwa kwenye ukanda wetu la Kenya ambalo liliingiza dola milioni 900. Uganda ilifuatiwa ya pili nyuma ya Tanzania kwa kuingiza zaidi ya dola bilioni 1.1. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio Mheshimiwa Waziri, kwa sababu haya ndio majukumu ya Wizara yako kwa shughuli zote zinazohusiana na uchumi wa Taifa hili na hasa uwekezaji kutoka nje na ukitazama katika uwekezaji huu unaona kabisa ni Sekta ya Gesi, Sekta ya Madini kwa Tanzania ndio imeongeza kwa kuingiza mapato mengi ya uwekezaji baada ya kugundua gesi asilia, Taifa letu limeingiza mapato mengi ya kigeni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ni vyema sasa kuangalia ushiriki wetu kwenye majukwaa mbalimbali ya kiuchumi kwa mfano tunaposhiriki kwenye Jukwaa la Kiuchumi la TICAD kwa mahusiano ya Japani na Afrika ama India na Afrika, ama Marekani na Afrika, na *block* zingine za kiuchumi kwa mfano *block* ya BRICS lazima tuoneshe kwa takwimu tunapata faida gani. Taifa linapata mapato kiasi gani kutoka nje kwa maana ya uwekezaji unaotoka nje. Hiyo itaweza kuonesha uhalali wa safari ambazo tunakuombeeni fedha mnazokwenda nje na huwezi kuwa mwana diplomasia ambaye unaishia kwenda Shinyanga badala ya kwenda nje kutafuta uwekezaji kwa faida ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima niseme kwamba ukitazama kama nilivyoieleza awali, Sekta ya Nishati kwa maana ya utafiti na gunduzi za gesi na madini ndio zimeongeza mapato mengi ya kigeni hasa katika uwekezaji. Je, Wizara inajipangaje sasa kuhakikisha kwamba sekta zingine kama Sekta ya Kilimo na Viwanda inafanya vizuri kuwekeza, kuingiza fedha nyingi za kigeni.

Ukitazama kama Ethiopia imefanikwa sana kwenye viwanda hasa kwenye maeneo ya kilimo, imefanikiwa sana kuvutia uwekezaji kwenye kilimo na viwanda ambayo imechangia mapato makubwa ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kama Afrika Kusini ambayo ndio inaongoza kwa Afrika kwa zaidi ya dola bilioni 145 za uwekezaji ambazo imepokea, imewekeza zaidi kwenye Sekta ya Viwanda, Biashara pamoja na Madini. Sasa Sekta zingine zinasubiri nini! Je, wizara yako inawezaje kusaidia kutafuta wawekezaji zaidi wa kuongeza mapato na uwekezaji katika sekata za Kilimo, biashara pamoja na viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Rais amesema anataka Tanzania iwekeze zaidi kwenye viwanda. Je, Wizara yako inafanya nini na hawa wawekezaji wanaokuja kuwekeza hapa baada ya kuwekeza je, Wizara yako inafuatilia kuona wanaendeleaje? Maana wawekezaji wengine wanakuja kwenye sekta hizi mbalimbali lakini wanaishia kuchanganyikiwa, wanaishia kuwa *frustrated* na mazingira mengine ya uwekezaji. Je, Wizara hii inafuatilia kujua wanaendeleaje? Na kama kuna changamoto ambazo zinawakabili mnafanya nini kuhakikisha kwamba mnashirikiana na sekta zingine kuhakikisha changamoto hizi mnazitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba Taifa lolote duniani haliwezi kuendelea bila uwekezaji, hasa uwekezaji wa fedha zinazotoka nje. Marekani yenyewe inashika nafasi ya tatu kwa kupokea fedha nyingi za uwekezaji kutoka mataifa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, China imeendelea kwa sababu imepokea fedha nyingi za uwekezaji kutoka mataifa mengine, na kutoka ndani ya China wenyewe. Lakini Tanzania tunapovutia wawekezaji lakini tunatumia muda mwingine kuwa-*frustrate* wawekezaji na kuona kama ni maadui ama wezi wa mali za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wetu kuwa na sheria nzuri, ni wajibu wetu kusimamia vizuri rasilimali zetu, lakini taifa hili linahitaji kuendelea, Taifa hili linahitaji kuwa Taifa la uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hatuwezi kuwa na uchumi wa kati mwaka 2025 kama dira ya Taifa ya uchumi ya maendeleo inavyoelekeza kama hatutoweza kuvutia uwekezaji kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, badala ya kufanya siasa, badala ya maelezo mengi, *next time* uje na *data*, uje na *figures* uoneshe faida, ya kushiriki kwenye mikutano hii yote, Taifa linapata nini. Uoneshe fedha tunazopokea kutoka Asia, Marekani, Uingereza katika uwekezaji, wala sio fedha za misaada, nazungumzia fedha za uwekezaji ambazo zinaongeza mzunguko wa uchumi katika Taifa letu. Leo katika mradi

wa bombo la gesi tu, tulipokea zaidi ya dola bilioni 1.2, dola bilioni 1.2 imetumika hapa Tanzania, na makampuni ya kitanzania yamepata fedha, na mzunguko wa fedha umemfikia kila mwananchi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja, na nampongeza Waziri na Wizara yake. Yeye ni mzoefu nina uhakika kwamba atalisaidia Taifa hili, kuhakikisha heshima ya Tanzania, kwenye nyanja za kimataifa inaendelea kuwepo. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana tunaendelea, Mheshimiwa Chumi Cosato atafuatiwa kwa muda Mheshimiwa Fakharia.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii, kuna mengine sikupanga kuyasema lakini kutokana na maelezo ya Waziri Kivuli, nimejikuta kwamba nawajibika kuyasema. Sisi wengine *background* zetu zinatuongoza kusema hivi ambavyo nitasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme moja tu kwamba tujifunze kua-*appreciate, the way* Waziri Kivuli amewasema Mabalozi, kwa kweli kwanza kitendo cha kuwafananisha na Mabalozi wa Nyumba Kumi, maana yake ni kwamba ni kama vile Mabalozi wa Nyumba Kumi wao sio watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninaamini Mheshimiwa Msigwa, ili atambulike popote lazima aende kwa Balozi wa Nyumba Kumi. Lakini pia Mabalozi hawa wameisha fanyakazi nzuri ya kuwakilisha Taifa letu, hii ni nchi ambayo hakuna kiongozi mkubwa duniani hajafika katika nchi hii, haya ni matokeo ya kazi nzuri ya hawa Mabalozi. Clinton ameisha fika hapa, Obama katika utawala wake mpaka sasa hivi amefanya jumla ya ziara 46, katika nchi zaidi ya 150 duniani, katika hizo 46 amefika hapa, ni kutokana na kazi nzuri ya hawa Mabalozi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Marais wa nchi kubwa kama China, Hu Jintao ameondoka alikuja hapa, ni kazi nzuri ya hawa hata huyu wa sasa. Sasa ndio maana nasema tujifunze ku-*appreciate* na kutiana moyo kuliko kusemana semana kwa namna ambayo haitusaidii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme tu kama alivyosema Mheshimiwa Lusinde, yaani kweli kuna *time* ya kupinga lakini sio kupinga tu. Mheshimiwa Dkt. Jakaya alikuwa anasafiri anapingwa, huyu sasa hivi hasafiri ameamua kutanua wigo kwa Mabalozi unapinga, *where are you standing you guys? Anyway* niendeleo kujilinda na *background* yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite sasa kwenye Sera ya Mambo ya Nje, hii *economic diplomacy*. Nimshauri Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla,

hebu tujaribu kuona je, sera hii inaendana na *current situation*? Wakati sera hii inapoanzishwa mwaka wa 2001, je, changamoto kwa mfano kama mambo ya *global warming*, mambo kama ya vikundi vya kigaidi, mambo ya kuibuka kwa jumuiya nyingine mpya za kiuchumi, kama *the BRICS* yalikuwepo, na kama hayakuwepo sera imejipanga vipi, au Wizara imejipanga vipi ku-accommodate hali kama hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeshauri Wizara iwe na kitengo au na idara maalum ambayo kazi yake itakuwa ni kusimamia utekelezaji na kufanya tathmini ya diplomasia ya kiuchumi. Nijikite katika suala la EAC, ni kweli kwamba katika siasa za kimataifa za sasa hivi *you can't work alone*, lazima uwe katika *economic integration*, katika *economic blocks*. Lakini pia na sisi kwenye hizi *blocks* tujitizame, hebu tuangalie pia ni namna gani tunaweza ku-benefit nje ya EAC. Nitatoa mfano kwa mfano, *DRC trade wise* mizigo ambayo tunasafirisha kwenda *DRC volume wise* inazidi ya Rwanda, Burundi na Uganda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata kama tutajenga reli, tutaimarisha bandari, kama hatutailinda *DRC*, *strategically* kama huyu ni *partner* wetu kibiashara, kwa sababu ya kwenda na mkumbo wa *Single Custom Territory* nawaambia tutapoteza na ili tufanikiwe na kulinda soko la *DRC* kibiashara, lazima Lubumbashi tufungue ubalozi mdogo, hili halikwepeki, kusudi tulinde maslahi ya Kongo.

Lakini pia sisi tunashiriki *Congo Peace Keeping* na kadhalika, *we are not going there* kama *shopping* hapana, nchi zote duniani Amerika unaona wanaenda Iraq, na kadhalika baada ya pale ni kuulinda na kung'amua fursa za kibiashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa zilizoko Kongo, hebu tujaribu kuzilinda. Lakini pia Mheshimiwa Waziri hata hii *Single Custom Territory*, leo hii nasikia kwamba tumekubaliana na wenzetu kwamba *after sometimes* tutapiga marufuku mitumba. Je, ndani hapa viwanda vya nguo tumejipanga sisi, au tutakuwa soko la wa Kenya, kama ambavyo leo hii maziwa ukienda kwenye maduka yanatoka Kenya, ukienda walimu katika kila shule tano, tatu unakuta ni walimu kutoka nje. Sawa tunaonesha *spirit* ya EAC lakini pia na sisi kama hii Wizara ya ku-coordinate mambo kama hayo, tunajipanga vipi, Mheshimiwa Waziri ningependa katika kujumuisha, uje na masuala kama hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine la muhimu *JPC*. *JPC* zetu kwa kweli zimekuwa tu za kinadhalia. *JPC* ni muhimu katika kutatua changamoto na kuchochea uhusiano hasa uhusiano wa kiuchumi. Hebu tutenge fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafanya hizi *JPC (Joint Permanent Commission)* maana yake ndio mwanzo na chemchem ya mahusiano. Lakini hayo yote

Mheshimiwa Waziri utakapoyajumuisha, ili haya yote tuweze kuyafanikisha vizuri lazima tuangalie *staff welfare*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanadhani wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Nje wanalipwa mishahara *in terms of dollar*, Kumbe maskini ya Mungu wanalipwa ni *terms of TGS shillings*. Lakini sio hivyo tu hata Balozi zetu Mheshimiwa Rais katika kubana matumizi, amesema kwamba kazi nyingi zitafanywa na Balozi zetu, tumezi-equip kwa kiasi gani na tunazi-facilitate kwa kiasi gani? Je, zina *staff* wa kutosha? Sio mtumishi yuko nje ughaibuni, lakini nyumba kila mwisho wa mwezi unapofika, roho yake iko juu kwamba mwenye nyumba atakuja kudai pango, unategemea huyu mtu *ata-derive*? Unategemea huyu mtu *ata-perform*? Maendeleo ni gharama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuje na mipango ambayo pia itaangalia *staff welfare*. Hata pale Makao Makuu Wizara ya Mambo ya Nje, mimi nimetoka pale nafahamu, watu wanafanya kazi usiku na mchana, Mheshimiwa Waziri hili unalifahamu, kwa hiyo tuangalie ni kwa namna gani tutaenda, lakini pia katika *diplomacy* ili uwe a *good diplomatic person*, lazima pia u-save *abroad*. Sasa huwezi kuwa a *good diplomat* unakaa *headquarter* miaka kumi, kumi na tano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie pia suala la *posting*, kwa sababu kama tunakusudia watu hawa wafanye kazi ipasavyo lazima tuwa-expose. Lazima tuangalie *welfare* yao, lazima tuwatafutie *short training* za mambo ya diplomasia ya kiuchumi ili kweli tuendane na kasi ya mambo ya dunia ya sasa inavyokwenda. Namshukuru Mheshimiwa Rais, amempa Wizara mtu ambaye ni nguli wa mambo haya, huyu mtu ameongoza ushauri katika mgogoro wa Somalia mpaka leo hii Somalia ina Serikali, jambo ambalo hata wa Marekani walishindwa. Leo hii mnawasema eti Mabalizi hawafanyi kazi, maana yake huyu katoka katika kitu cha aina hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe utakapokuwa unajumuisha, tafadhali ili tuenende sambamba na demokrasia ya kiuchumi, tuzingatia kufufua *JPC* kivitendo sio kwa maneno. Lakini tuangalie *welfare* ya watumishi katika Balozi zetu, lakini pia na watumishi pale *headquarter*, lakini kuhakikisha pia watumishi wanakwenda *posting*.

Napenda kuishukuru Wizara, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote, kwa kazi inayofanyika nzuri na tunaendelea kuwatia moyo, msikatishwe tamaa na maneno ya kukatisha tamaa. Sisi tusonge mbele Mungu awabariki sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako, tunaendelea na Mheshimiwa Fakharia na kama muda utaruhusu, atafuatiwa Mheshimiwa Musukuma.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, na viongozi wote wa Wizara hii, kwanza kwa hotuba nzuri waliotusomea imeifunika hotuba ya Kambi ya Upinzani, ndio maana mkawaona wamekuja na jazba kubwa mpaka mwisho mtu anakunywa maji, ili kutafuta sauti akwamue, aifunike speech ya Mheshimiwa Waziri, lakini ameshindwa na vilevile nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani wamezungumza kwamba Mheshimiwa Rais anajifungia Ikulu, anashindwa kutoka nje. Nawaambia Mheshimiwa Dkt. Magufuli ndiye Rais bora duniani na ambaye ameweza kutekeleza sera zake, kwa Watanzania na hivi sasa ana sifika Tanzania nzima na nje ya nchi kwa sababu ya uwezo wake, na hapo anapokuwepo Ikulu si kwamba anakaa anafanya kazi, anatafakari nini cha kuwafanyia Watanzania kuwaondoshea madhila, lakini mimi ninajua wenzetu ninyi kazi yenu ni kupinga tu kila kilichokuwa kizuri kazi yenu ninyi kupinga, kila kinachotendeka kikiwa kimekaa sawa imekuwa sawasawa na mke mwenza, amelisifia kaburi la mke mwenzie, hili kaburi la nani zuri limependeza, alipambwa na mke mwenzie, ndio maana nikaona limekaa upande, ndio upinzani huo, wakati ameshalisifia anakuja analiponda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mabalozi. Mabalozi wetu wanafanya kazi nzuri, hata wao wanapokwenda nchi za nje, wanahemea kwa Mabalozi. Sasa leo imekuwaje maana yake baniani mbaya kiatu chake dawa, jamani hebu tuwe makini katika masuala yetu tunapozungumza. Maana yake wakati mwingine mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni, tusiwe kwa sababu kuna upinzani, ndio upinge kila kitu mengine mshukuru kwa sababu yanawafaeni na ninyi wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na suala lingine, kuna siku alisimama Mbunge akazungumza kwamba Zanzibar utalii wao kama hauna uendelezo wala hauna faida nao upo upo tu. Namwambia huyo Mheshimiwa kwamba Zanzibar hivi sasa bajeti yake anatumia pesa za ndani, hategemei za nje na kinachofanya hivyo ni kwa sababu utalii unaenda vizuri, karafuu anauza vizuri na ndio maana ikaweza kujitosheleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utamkuta mtu anakurupuka anakuambia, Seif ndio atakuwa Rais atauweza uchumi, unajidanganya. Seif alitia mpira kwapani na Bwana Jecha alimpa uhuru mkubwa tu wa kugombea na alimuambia tarehe 20 Machi, 2016 uchaguzi kashindwa. Katia mpira kwapani,

kaondoka kamuachia Mheshimiwa Shein kachukua Serikali kwa ulaini, na sasa hivi mazungumzo yaishe, Mheshimiwa Shein ndio kiongozi wa Zanzibar na ninawaambieni msilolijua ni sawa na usiku wa kiza, tulieni Mheshimiwa Shein akamate madaraka aendelee nayo. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mtu mzima hovyoy.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa uchaguzi mwaka 2020, mwaka 2020 kama hamkuja basi tena tunaendelea, tunapiga *more* waliyojionea vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nitajikita katika diplomasia ya kiuchumi. Ninajua Wizara imejipanga katika kukuza diplomasia ya kiuchumi na kwenye kitabu chenu nimeona kwamba tayari mmejikita na mnakwenda vizuri. Nilikuwa nataka kusema hivi, kwa sababu Tanzania hivi sasa inataka kujikita katika viwanda, je, Wizara imejipanga vipi kutafutia masoko ya biashara ambapo kwa sababu tutakapojiingiza kwenye viwanda, lazima tuwe na masoko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namtaka Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujumuisha, uniambie masoko ya nje tumejikita vipi ili kwa bidhaa zetu tuweze kuuza. Kwa kweli Tanzania inajikita katika mambo ya utalii, kwa sababu tunavyo vitu vinavyotufanya ili tuweze kuvutia watalii wetu. Kuna Mlima Kilimanjaro, kuna fukwe za Bahari za Zanzibar, kuna bustani ndani ya Bahari ya Hindi na hiyo wanakuja wanapoenda kuangalia, vilevile tuna mbuga za wanyama. Sasa ningekuomba na haya sasa myafanyie kazi ya kuyatangaza, msiwaachie Kenya ambao wakitoka wao ndio Tanzania wakatutangazia, wakati sisi tuna uwezo na uwezo huo najua Mheshimiwa Waziri unao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia ambalo sikuliona kwenye kitabu chake, mwaka jana tulizungumza kwamba kuna vijana Wazanzibari 13 mliwasomesha, ili baadae muwaajiri katika Wizara zenu au vitengo vyenu. Lakini kwenye kitabu chako sijaona hao vijana ambao wameajiriwa au hawakuajiriwa, umetuambia kwamba kuna watu wamestaafu, kuna watu wamemaliza muda wao, lakini hujasema vijana gani ambao tayari umewaajiri kama kutoka Tanzania Bara au Tanzania Visiwani. Sasa hivyo Mheshimiwa Waziri ningependa pia ukija unijulishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kuhusu kitabu chako cha mwaka jana ukurasa wa 61; mlisema Wizara mnajikita katika kuweka vitega uchumi, kufanya wafanyakazi watakaokuwa nje ya taasisi yenu ambao watakua Ubalozi kupata sehemu zao za kukaa na ofisi zao za kukaa. Lakini sijaona kwenye kitabu chako maendeleo yake yamekuwaje kama kweli, maana ulisema mpaka mtakuwa na mapato katika sehemu za vitega uchumi, kwa kupata viwanja na majengo

ambayo mengine mtaweza kukodisha. Sasa na hilo ningependa utakapokuja Mheshimiwa Waziri nipate kujua maendeleo yake yakoje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki makao makuu yake yako Zanzibar. Sasa hili lazima nitoe pongezi kwamba Zanzibar ambayo mmeipa kitengo kama mlivyosema kwamba Kamisheni ya Kiswahili Makao Makuu yake yatakuwa Zanzibar, ni katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ilianza kuanzia mwaka 2014. Sasa hili kwangu ni pongezi na ninashukuru, na tutaendelea kuilinda, na tutaendelea kuilea kama tunavyoilinda na kuilea CCM, kwa maelezo hayo naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Jaku unaweza kuchangia kwa dakika nne. Huwezi haya.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, unapokuta maji yakoge, mwanzo hujui mbele kama utayakuta tena.

Kwanza nichukue fursa hii kukushukuru wewe kunipa hizi dakika nne au tano hizi zilizobaki kumaliza ngwe hii iliyobaki na nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeniwezesha kusimama hapa na kuvuta pumzi zake na kurudi tena kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo Mheshimiwa Waziri kipindi kilichopita mwaka jana, nilikigusia sana na nikazuia shilingi, na hii leo hii nafikiri Mheshimiwa Waziri kuna vijana 13 kutoka Zanzibar. Nazungumza kuhusu maslahi ya Zanzibar kuhusu Wizara hii, kutokana na mambo yanayohusu masuala ya Muungano.

Kuna vijana 13 mmewasomesha Chuo cha Diplomasia, bahati mbaya mkawachukua saba, lakini kwa masikitiko makubwa na unyonge na huruma kubwa mpaka hii leo vijana hao saba hamjawaajiri. Mwaka jana nilihoji kwenye bajeti na Mwenyezi Mungu si Athumani kanirudisha tena leo hii, nipo hapa, kwa hiyo, nitahitaji maelezo ya vijana saba hawa wa Zanzibar mpaka leo hamjawaajiri na hii ilikuwa si hisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni makubaliano katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Vijana hawa hamjawaajiri hadi hivi leo, nataka maelezo ya kina kuhusu suala hili na umri wao unakwenda, na mmechukua barua Zanzibar kama kuwaazima, si kitu kizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoka hapo kwa haraka haraka nitahitaji maelezo lakini haya vilevile ni ya kusikitisha, Wizara hii huko nyuma au uzoefu

unaonesha Waziri anatoka Bara, Naibu Waziri kutoka Visiwani. Lakini kwa masikitiko Wizara hii wote wazee mmekalia kiti chenu, lakini si maamuzi yangu ni maamuzi ya Mheshimiwa Rais. Lakini kama hapatoshi hapo, hata Wizara ya Fedha haya mambo ya Muungano tulikuwa tupokezane, hapatoshi hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa umakini wake na Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu, alikuwa akijitahidi katika safari za nje, kuwachukua Mawaziri kutoka Zanzibar katika safari zake, je, mpango huu utaendelea tena vilevile au utalala? (Makofi)

WABUNGE FULANI: Haendi. (Kicheko)

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke hapo nataka kuulizia haya maslahi ya Mabalozi wangapi wa Zanzibar waioajiriwa, huu ni wimbo wa Taifa wa muda mrefu. Wimbo huu umekuwa wa muda mrefu, kuhusu ajira katika Wizara hii nataka kujua Mabalozi kutoka Zanzibar ni wangapi wanaowakilisha hivyo? Vilevile *senior officer* kutoka Zanzibar, katika Mabalozi wako wangapi, wimbo huu umekuwa ni wa muda mrefu lakini hautoshi... (Makofi)

(Hapa kengelele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Musukuma aliomba achangie mchana ndio maana niliona niliache.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi ya leo asubuhi ndio hii, wachangiaji ndio hao, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

Aah kweli nitende haki eti eeh. Ili tu-*balance* jamani huwa napenda *debate* inakuwa ni nzuri, huwezi kulalia upande mmoja kwa kusudi hilo tunasema hivi. Kiti lazima ki-*balance* unachukua watu ambao unajua watasaidia kuleta kidogo uhai wa haraka ndani ya nyumba. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa mchana tutaanza na Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud, halafu tutaendelea sasa kiti kinavyoona mambo yanavyotiririka hawa watatu, watatusaidia kufungua dimba. Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni. (Makofi)

(Saa 07.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. (Makofi)

Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wabunge ambao walitajwa asubuhi, tunaanza na Mheshimiwa Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi lakini nasikitika naenda kuchangia wakati Waziri mwenyewe hayupo; kwa sababu ilibidi hivi vitu avibebe Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe ndio tungeenda sawa zaidi, lakini sio mbaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na kuna Wabunge wapya humu wanashangaa suala la sisi kutoka Bungeni sijui tunasaini, sijui tunafanya nini; niwataarifu tu wanatakiwa kabla hujalingia kwenye kitu upate elimu kuhusu utendaji wa hicho chombo au taasisi. Kutoka Bungeni ni suala la kawaida kabisa kwa sababu hata tunavyotoka sio kwamba tunatoka tunakwenda nyumbani; kwa sababu kuna wakati ni heri uwe nje unatumia simu kuongea na watu Jimboni kuliko kukaa humu ndani kusikia watu wanavyo zomea zomea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niwataarifu tu kwamba tutaendelea kutoka hatua hii mpaka pale kiti anapokaa Naibu Spika aache *tendency* za udikteta ndani ya Bunge kwa sababu tupo humu tunataka *freedom* kwa ajili ya masuala yanayohusu hili Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la diplomasia, Wizara hii ni muhimu sana na imefika mahali tunatakiwa tuweke mbele diplomasia ya uchumi; naongea hivi nikiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Msigwa, Waziri Kivuli kwa sababu tunatakiwa tutoke sasa tuachane na diplomasia ya enzi za *cold war*. Diplomasia hiyo imepitwa na wakati, lakini *unfortunately* sisi ndio tunabaki nayo na afadhali hata zamani tulikuwa na misimamo. Sasa hivi hata misimamo hatuna, Wizara ya Mambo ya Nje kazi yake ni pamoja na kusimamia, kuwa

custodian wa *our foreign policy* (Sera yetu ya Mambo ya Nje) na ndio maana kwa kutumia platform hiyo Serikali hii ya Tanzania chini ya Mwalimu Nyerere ilifunga Ubalozi wa Israel hapa Tanzania kwa madai kwamba kwa ku-support Palestina ipate uhuru na Palestina haijapata uhuru mpaka leo msimamo ule wa Mwalimu upo hapa ndio maana mnahanya hanya katika kujaribu kurudisha Ubalozi wa Israel; ilikuwa ni msimamo wenye hoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa angalia leo hii tumo humu ndani tunatambulishwa kwamba kuna Balozi wa Libya nchi ambayo Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi wakati Waziri akiwa Bernard Membe alisimama pale kwenye *podium* akasema kwamba kamwe Tanzania haitakaa itambue mapinduzi ya Gaddafi. Sasa najiuliza leo hii kuna Balozi wa Libya yupo humu ndani je, Gaddafi amerudi? Naomba nipate jibu wakati Waziri atakaporudi lakini vinginevyo nisistize kwamba Wizara hii ndio *custodian* wa sera zetu za nje, *foreign policy* ni muhimu tunavyokuwa na misimamo basi idumu na ieleweke na ndio namna tulivyopata heshima na ndio namna Nyerere alituletea heshima katika eneo hilo ndugu zangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje ni nyeti sana kwa Taifa kisiasa na kiuchumi. Wizara hii ingeweza kutoa mchango mkubwa hata kwenye masuala ya ajira ndani ya nchi iwapo ingekuwa na mbinu za kutafuta masoko nje na pia zaidi mbinu za kutangaza utalii wetu nje ya nchi kupitia Balozi zetu, lakini ndio hivyo Balozi zimechoka. Kuna mwaka fulani miaka sita saba iliyopita nilienda Ubalozi wetu wa DC Washington, bendera niliikuta nusu sasa upo Marekani unakuta bendera imepepea mpaka imechanika mpaka imebaki nusu, je, hali ya wafanyakazi humo ndani na mifuko yao kiuchumi inakuwaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatakiwa kwa wazi kabisa kucheza na diplomasia ya uchumi na katika hili tungeweza kufanya vizuri sana kama tungetumia kundi linaloitwa *diaspora* (Watanzania wanaoishi nje ya nchi). Kundi hili nina uhakika nisiseme sina uhakika hata Serikali haijui ni Watanzania wangapi wanishi nchi za nje wala haijui ni mchango kiasi gani wa fedha kupitia *remittances* yaani fedha wazotuma nyumbani ni kiasi gani kwa mwaka. Sasa watu kama hao huwezi kuwaingiza katika utaratibu wa mipango ya nchi wakati kimsingi tuna-miss kitu fulani kutokana na mchango wao huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wenzetu wapo vizuri wana rekodi. Kwa mujibu wa *World Bank report* ya Machi 2016 Kenya kwa mwezi wanapokea kutoka *diaspora* yao Ulaya na Marekani, *North America* dola milioni 133 kwa mwezi na wanapokea kwa mwaka 1.4 bilioni USD hizo kwa hela za Tanzania piga hesabu ni karibu shilingi trilioni tatu, ungeziingiza katika bajeti ya nchi zingesaidia Wizara ngapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndio diplomasia inayotakiwa kufanyika sasa hivi lakini hatuna rekodi; angalia kama Ethiopia wanavyojaribu kuwashirikisha *diaspora* yao katika masuala ya uchumi. Walianzisha mradi mkubwa sana wa umeme pale unaitwa *Ethiopian Grand Millennium Dam* kutokana na mgogoro wa chanzo Nile na *support* inayopata Egypt baadhi ya mataifa wakakataa kui-*support* Ethiopia kifedha kwenye ule mradi; walichofanya Serikali ya Ethiopia wakawahusisha watu wao wa *diaspora Worldwide*, wakawatengenezea *bond* maalum, wakawawekea utaratibu wale mabwana wanachangia sasa dola kwenye ule mfuko na Ethiopia sasa hivi ule mradi nilikuwa naangalia jana umefikia asilimia 70 ya kutengenezwa, wamebaki asilimia 30 tu kutengeneza bila fedha za nje kwa kutumia fedha za *diaspora* ya Ethiopia inayoishi *North America* na Uingereza ndugu zangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa sisi tumekaa tu Ethiopia wanatumia *diaspora* wanakwenda kuwa na bwawa kubwa, wanaenda kutengeneza historia, wana bwawa kubwa la umeme kuliko yote Afrika kwa kutumia *diaspora*. Sisi *diaspora* hatuwashirikishi; huwezi kuwashirikisha watu kwenye uchumi; Watanzania hawa huwezi kuwashirikisha kwenye uchumi wakati hautaki kutambua uraia wao, uzalendo wao na utaifa wao. Hapa nazungumzia *diaspora* maana yake tunafika mahali tunachanganya mambo, ninyi mnachanganya kati ya utaifa na uraia. Utaifa ni kitu *natural*, uraia ni kitu cha *documentation* yaani *paper work*, kama mimi ningeamua kufanya *paper work* sasa hivi ningekuwa raia wa Marekani, lakini utaifa ni kitu *by nature*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuwezi kwenda mbele bila kuwashirikisha hawa watu; mnawadanganya watu mnaenda mnawaambia rudini nyumbani wakirudi nyumbani hawawezi kuacha mambo yao waliyoyatengeneza kule miaka yote eti aache uraia wa Marekani aje hapa akitaka kibali hichi *corruption*, akitaka hichi *corruption* na pia aje kama mgeni. Anatakiwa mnatambua mnawapa *dual citizenship* ili wanavyokuja hapa wanakuja kama Watanzania sio Mtanzania yupo Marekani mmemnyang'anya utaifa wake kwa sababu ya makaratasi ya uraia halafu anakuja hapa mnamzuia kabisa mnataka awe mwekezaji kama mgeni na sio kama Mtanzania wa hapa, sasa hii ni mbaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kwa nini mnaogopa sana *diaspora*, kwa nini mnaogopa sana *dual citizenship* mnajua ni hasara kiasi gani mnalipa hili Taifa kwa kutokujua tu *remittances* zinaingizwa nchini kiasi gani hiyo ni upungufu mkubwa sana na tunaitaka hii Serikali sasa hivi ifanye mkakati walete *dual citizenship* ili watanzania waliopo nje walete *input* na sio tu *input* ya kiuchumi *exposure* waliyoipata wale mabwana kule hata katika masuala ya utawala tukiwaleta na kuwaingiza katika mfumo wa uendeshaji nchi hivi vitu vidogo vidogo vya uzembe uzembe, rushwa rushwa

ndogo ndogo hizi havitakuwepo kwa sababu *good governance* itaenda kutamalaki pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tumekaa, Serikali haiwajali diaspora wakiwa hai na hata wakiwa wamekufa; Watanzania wanauwawa huko kama niki-refer hotuba ya Waziri Kivuli, niende kwenye mauaji ya juzi juzi tu Watanzania wawili katika mwezi mmoja mwezi wa nne wamepigwa risasi hakuna tamko lolote mpaka tupige kelele Bungeni humu ndio Waziri atakuja baadaye atajifanya anatoa tamko wakati alitakiwa walishughulikie hili suala na naunga mkono *petition* ya Watanzania wanaoishi Marekani ambao wanataka Balozi wa Marekani Washington DC aondolewe mara moja arudishe nyumbani kwa sababu ameshindwa kuwatumikia Watanzania kule Marekani. Ameshindwa kutambua hata pole hajatoa kwenye misiba hii iliyotokea. Umetokea msiba wa Andrew Sanga, Afrika nzima imelia; Serikali haina habari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Andrew Sanga amepigwa risasi amekufa Serikali hii haina habari; Balozi wa Marekani anapigiwa simu kuna msiba Houston ameacha kwenda kwenye msiba Houston anasema nina udhuru, udhuru wenyewe yupo Dallas, Dallas na Houston ni kama Dar es salaam na Morogoro. Amekwenda Dallas kwenye *party* ameacha kwenda kwenye msiba ambao umetingisha Marekani nzima na yeye angeenda pale angeenda kuleta *harmony* kidogo na kuwatuliza wale watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Waziri atuambie na aliambie Bunge lako Tukufu Serikali hii imefikia wapi kufuatilia uchunguzi wa mauaji ya Andrew Sanga kwa sababu Marekani usipo-push na wao wana-relax kwa sababu wanajua...

(Hapa kengelele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi muda umemalizika naomba ukae.

Tunaendelea na Mheshimiwa Msukuma na baadae Mheshimiwa Masoud Abdallah na Mheshimiwa Raisa Abdallah kwa dakika tano tano ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya mambo ya nje.

Kwanza nianze kwa kumpa taarifa tu kidogo mzungumzaji aliyemaliza kwa kutambua umuhimu wa Wabunge makini wa CCM wageni...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Tulieni...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma naomba uendelee.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Kwa kutambua kwamba kuna Wabunge makini CCM, vijana ambao watawafuatilia kila mnapotoka tutawaambia Watanzania mnasaini pesa mnaenda kula jojo huko nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana pia naomba mtambue niliwahi kuzungumza hapa, sasa hivi ni saa kumi, saa kumi hii kwa kawaida mzungumzaji mnaelewa alikotokea, kwa hiyo sio kitu cha ajabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusiana na hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Mheshimiwa Mahiga Waziri ukiona watu wanakupiga mawe *style* hiyo wanakuogopa, Taifa hili linakuheshimu na linatambua uchapa kazi wako, haya wanayoyasema yasikukatishe tamaa hawa ni kawaida yao na hawana cha kusema lazima wazungumze hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme pia nilivyokuwa sijaingia Bungeni nikiwa kijana nilikuwa namuona Kingunge akiapa pale alikuwa anaapa hashiki Biblia wala hashiki *Quran* nilikuwa najiuliza sana kwanini huyu mzee anaapa bila kushika vitabu vya dini. Leo nimethibitisha kama msomaji wa taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kweli ni mchungaji mimi nipo tayari kubadilisha dini niwe mpagani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika miiko ya uchungaji na mimi nimesoma uchungaji japo sikumaliza ni kusema uongo. Nataka niseme ukweli, Mheshimiwa amesema uongo ambao sijawahi kuona; ukisoma ukurasa wa tisa anasema Kampuni ya *Bismark Hotel Mining Limited* ya Mwanza imedhulumiwa eneo lake na Acacia Geita. Mimi ni Mwenyekiti wa Mkoa, Geita hakuna kampuni ya Acacia, wewe unawaambia watu hawajafanya *research* wewe unatoa taarifa za *research* umeipata wapi hii? Acacia ipo Kahama, nani anakuletea hizi taarifa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tujue kwamba hao ndio wachungaji wetu na wanachunga kondoo waliowasafi, hawachungi waliopotea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mahiga nakuomba ujue tu kwamba hawa wapinzani wanakuogopa na uendelee kufanya kazi na Mungu atakusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze pia aliyezungumza Kambi ya Upinzani amesema Rais wetu anajifungia Ikulu kwa maelezo ya hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiwa na Rais Kikwete nimemshuhudia Msigwa mara nyingi akisema Rais wetu anamaliza muda wote *honeymoon* kwenye ndege, sasa huyu hasafiri umegeuza tena unataka kumlazimisha asafiri. Tarehe 24 Julai, Mheshimiwa Godbless Lema na boss wake walikuja Geita wakasema sisi Geita tuna rasilimali zote lakini nchi hii ni maskini bado

tunategemea kwenda kuomba Marekani, ameingia kigogo hataki kwenda Marekani mnamlazimisha kusafiri, hela zipo hapa hapa. Na nataka niwaambie ninyi ndio makuwadi wa wezi wa hela za Tanzania na mtabanwa mpaka mtaleleweka tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia umezungumza ukasema kwamba kuna watu wanapewa Ubalozi kama shukrani, huko kwenu huko watu wamepewa Ubunge kama shukrani hawajawahi kusimama hata kwenye jukwaa mbona husemi? Mbona husemi kwamba kwenu kuna watu wameokotwa hawajui hata CHADEMA ikoje wamepewa Ubunge; wewe umetoa mapovu miaka mitano umekuja kupambana Jimboni kuna watu wamepewa bure kule, hebu bisheni tuwataje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa tumewazoea hawana jipya, watu hawa wanatuchonganisha na Mabalozi; wanasema Mabalozi wetu ni sawa na Mabalozi wa Nyumba Kumi... *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Taarifa Mwenyekiti.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Ngojeni mje muugue mkienda India ndio mtajua...

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Tuna Mabalozi waliosoma wala hawakupewa shukrani, achana na taarifa Mzee acha nimalize... *(Makofi)*

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Taarifa Mwenyekiti.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni mwenzetu pengine anataka kuniongezea nondo...

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mwenyekiti taarifa!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema Mheshimiwa Msigwa ili utambue...

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mwenyekiti taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Kama ni muongo anasema Wabunge wa East Africa...

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Taarifa Mwenyekiti.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Hawapewi mikopo ya magari sijui...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma naomba ukae.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia kwa muda mrefu Mheshimiwa Mbunge anayechangia naomba umuelekeze atumie lugha yenye staha; sisi ni Wabunge sio hawa watu na jinsi anavyo-address Wabunge kwa mujibu wa Kanuni kuna namna ya ku-address Wabunge.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msukuma taarifa hiyo unapokea?

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea, Mheshimiwa lakini message imeenda. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa amesema Wabunge wetu wa *East Africa* hawapewi magari, pengine hana kumbukumbu sahihi na aliwataja nilitaka wangukwepo pale wakamdhahirishia Wabunge hawa wa *East Africa* wanapewa mikopo ya magari kama tunavyopewa sisi na wana *exemption* ya magari mawili na ndio maana gari zao zinaandikwa namba za Ubalozi, wewe msomi gani huelewi? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma naomba uongee na kiti huku jamani.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia kusema kwamba kwa hali ilivyo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli ilivyojipanga hawa hawana cha kusema zaidi ya kutoka nje. Na mnasema kila anaposimama Mheshimiwa Dkt. Tulia, Mheshimiwa Naibu Spika mtatoka nje, tokeni; kama mlizoea Spika ambaye hafuati kanuni mlizitunga wenyewe wenyeji sisi wengine ni wageni. Tunakuomba Mheshimiwa Naibu Spika simamia Kanuni hawa watoke nje; tunawataka watoke nje kila siku tena ukae asubuhi tu kile kipindi cha *live* wafyatuke wakae wenyewe humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi naomba kuishia hapo. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea Mheshimiwa Masoud, dakika tano.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza nataka Watanzania ambao wanatusikiliza waelewe kwamba sisi kama Kambi ya Upinzani tutaendelea kushikilia misimamo yetu dhidi ya ukandamizaji wa demokrasia na sisi tuko makini kweli kweli, hiyo ya kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wakati alipokuwa akitoa hotuba yake alisema miongoni mwa taasisi ambazo anaziongoza tatu ni APRM (*African Peer Review Mechanism*) mpango ni wa kujitathmini wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huu mpango Tanzania inajitathmini yenyewe ningependa nimuulize Mheshimiwa Waziri atueleze, kwa sababu huu ni mpango wa utawala bora, huu mpango wa Bunge kutooneshwa *live* mmejithathmini kiasi gani? Mpango huu wa Bunge kutooneshwa *live* ni kiasi gani mmejithathmini ninyi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, viongozi wetu kukatwa katwa mapanga na kupigwa na kuumizwa na wengine kuuawa kama kwa kamanda Alphonse Mawazo ambaye yeye ni Mwenyekiti wa Mkoa wa CHADEMA, kiasi gani mmejithathmini na nani waliohusika katika mpango huu wa utawala bora? Pia sambamba na hilo ningependa kuelewa kupigwa na kukatwa katwa na kuuawa kwa Diwani wetu kule Muleba, Faustine Mlinga, Kata ya Kimwani, kiasi gani mmejithathmini na kujua nini cha kufanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuelewa kuvamiwa kwa viongozi mbalimbali wa dini kule Mwanza juzi na kupigwa. Je, katika mfumo huu wa utawala bora ni kiasi gani mmejithathmini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuuawa kwa vikongwe, walemavu, wale *albinism*, kiasi gani mpango huu wa kujitathmini wenyewe mmeweza kukaa kitako na mkaona njia gani mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya ili tuelewe sasa kiasi gani APRM, kwa sababu haina vote yake yenyewe hampewi fedha, kwa hivyo sasa ionekane kiasi gani katika kujitathmini ninyi wenyewe kama uwezo wenu ni mdogo, hamna fedha, mimi naishauri Serikali, APRM (*African Peer Review Mechanism*) ipewe vote yake yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna masikitiko makubwa, Watanzania ambao wanataka kwenda Uingereza viza zao zamani walikuwa wanazipata Kenya, sasa mpaka Afrika ya Kusini. Mheshimiwa Waziri, tuambie tatizo gani la figisu figisu baina ya Tanzania kutoaminiwa na Uingereza mpaka viza hizi kutoka sasa kwenda kutoa Kenya sasa unazipata Afrika ya Kusini, tatizo ni nini? Mna tatizo gani la kidiplomasia na hawa wenzetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni diplomasia ya kiuchumi. Nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri ingawa anaongea ongea pale, katika kuongeza kasi hii ya diplomasia ya kiuchumi baadhi ya nchi zimeweza ku-*present credentials*, kupeleka hati za utambulisho hapa kwetu, na sisi inaonekana bado kuna nchi mbalimbali hatujaweza kuwasilisha hati za utambulisho. Tanzania

hapa Balozi wa Namibia na Botswana wako Tanzania lakini sisi Balozi wetu kule Botswana na Namibia naona kama sisi hatuna Balozi.

Lakini tarehe 05 Januari, 2016 kuna nchi tatu ambazo waliweza ku-present *credentials* hapa. Jamhuri ya Korea, Jumuiya ya Ulaya na Taifa la Palestina. Je, sisi tumejipanga vipi? Wakati wao tarehe tano walileta hiyo hati ya utambulisho kwa Rais John Pombe Magufuli, sisi je, kwa nchi ambazo nimezitaja. Jamhuri ya Watu wa Korea, Jumuiya ya Ulaya na Taifa la Palestina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba Mheshimiwa Waziri ukija unieleze, ni kwa nini sisi tunachelewa kuwasilisha hati za utambulisho? Mfano Balozi wetu pale Berlin, Ujerumani, nchi ambazo anaziwakilisha ni Ujerumani, Uswiss, Jamhuri ya Czechoslovakia, Poland, Hungary, Bulgaria, Romania, Australia na Vatican, lakini hati ambazo zimewasilishwa na Ujerumani, Uswiss, Austria na Vatican, nyingine zote mpaka leo hatujawasilisha hati za utambulisho, tatizo ni nini na hii ni diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo Cairo, pale Misri Balozi wetu nchi ambazo anaziwakilisha ni Misri, Israel, Lebanon, Palestina, Libya, Iraq, Syria na Jordan. Lakini hati ambazo zimewasilishwa ni Misri peke yake, nyingine zote bado hatujawasilisha hati za utambulisho na hapa uchumi wetu utakuwa ukiendelea kudorora siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri, utakapokuja uniambie...

(Hapa hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Masoud, dakika tano zako zimekwisha, tunaendelea na Mheshimiwa Raisa.

MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara hii muhimu kwa nchi yetu ya Tanzania. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii kuwepo hapa katika Bunge hili Tukufu la Tanzania. Pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kumpa subira kiongozi wangu Maalim Seif Sharif Hamad na Mwenyezi Mungu azidi kumpa subira kwa mikiki yote anayoipata katika Serikali ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Na ieleweke kwamba Chama cha CUF hakikutia mpira kwapani, badala yake ni chama kinacholinda Katiba na sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika suala zima la mada iliyopo mbele yetu. Napenda niseme kwamba Wizara hii ni Wizara ambayo CAG aliilalamikia sana wakati wa kujadili fungu hili wakati tuko kwenye

Kamati. ninashangaa sana, kwamba mjumbe wa Kamati ya PAC ambaye alikuwepo siku tuliyojadili fungu hili na malalamiko yaliyotolewa na CAG pale kwamba katika Wizara ambazo zinakosa mafungu basi moja ni hii, kukosa pesa ambazo zinaingizwa na Hazina. Leo anasimama hapa, badala ya kuchangia Wzara hii muhimu, tukamsaidia Mheshimiwa Waziri bado anakwenda kulalamikia hotuba ya upande wa upinzani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshauri au kumpa mawazo Mheshimiwa Waziri kutokana na Balozi zetu za Tanzania zilizoko nchi za nje. Nchi ya Tanzania katika balozi ambazo ziko dhaifu basi ni nchi ya Tanzania, mpaka inafikia ofisi ya ubalozi kuvuja na kuna Mheshimiwa mmoja katika Kamati yetu alisema yeye katembelea nchi ya Msumbiji, akakuta ofisi ya Balozi watu wanaingia kuuza chai, kauza nini, haina hadhi kama Balozi ya Tanzania. Leo hii tumefikia Watanzania, ukiiangalia Balozi ya nchi za nje iliyoko Tanzania ina hadhi, tunavyowanyenyekea wenzetu, lakini ni tofauti kabisa na mabalozi wetu walioko nchi za nje, jinsi ofisi zetu zilivyo kama Tanzania.

MBUNGE FULANI: Mnakandika dari, nyumba inavuja paa.

MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA: Mnakandika dari na nyumba inavuja mapaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie suala hili la Watanzania ambao wanakutwa na matatizo wakiwa nchi za nje, Balozi zetu wanawasaidia vipi watu hawa? Kuna watu wanaokamatwa na dawa za kulevya na mambo mengine, hasa nchi za Bara la Asia. Wizara haioni umuhimu wa watu wale, ikaundwa mbinu mbadala ambapo wale vifungo vyao wakaja wakavitumikia Tanzania kuliko kunyanyasika kule? Na je, Wizara ya Mambo ya Nje imeshughulikia vipi kwenda kukagua magereza ambayo yako nchi za nje? Watanzania wako kule na hatujui wako katika hali gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri uje utuambie suala hili, na tunaomba ulifuatilie kwa kina suala la Watanzania walioko kule. Hatujui mateso yao na tuna uhakika wanateseka kwa sababu mtu kwao ndiyo ngao. Leo wako nje ya Tanzania, vipi watu wetu kule watapata haki au kutetewa? Sisi tunaona nchi za nje zote Balozi zao anapokamatwa mtu nje ya nchi yake Serikali ya nchi ile inasimamia kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba watu wake wanarejeshwa katika nchi yao kwenda kuhukumiwa. Na wanapata haki zao za kibinadamu kama inavyotakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba...

MBUNGE FULANI: Hapo hapo.

MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika ripoti yake alituambia kwamba Watanzania waliokamatwa huko nje ni 108, kama ufahamu wangu unaniambia hivyo kwa mujibu wa alivyosema katika kitabu chake hiki. Sasa watu hawa wanashughulikiwa vipi na Serikali ya Tanzania? Ni miongoni mwa haya niliyotanguliza kuyasema kwamba Watanzania 108 ni wengi, wana watoto, wana familia wana wazee, je, Serikali imewasimamia vipi watu hawa 108? Na unatuthibitishia vipi kwamba hawa Serikali ya Tanzania inawashughulikia na inawasimamia haki zao za kibinadamu kama Watanzania wengine, ututhibitishie suala hili, kwamba makosa yao ni yapi mpaka wakafika kufunguliwa mashitaka nchi za nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Raisa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. RAISA ABDALLA MUSSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa na baadaye Mheshimiwa Masoud Ali Khamis pamoja na Mheshimiwa Mattar ajiandae.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa nichangie Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninampongeza sana mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu. Licha ya kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais mwanamke, lakini vile vile Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa amemteua kuwa kwenye jopo la juu kabisa la ushauri jinsi gani ya kuweza kumuwezesha mwanamke. Ninaamini kwa njia hii wanawake wa Tanzania tutanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo mimi naomba nianze yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni *sovereign state*, lakini cha ajabu ukiangalia nchi kama Israel, Australia, Uingereza, Canada masuala yote ya viza unapoyahitaji hayapatikani hapa Tanzania. Sasa nilikuwa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, shemeji yangu, ninayemuheshimu sana, suala la *bilateral* limefikia hatua gani mpaka visa hazitolewi hapa nchini kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala zima la diplomasia ya kiuchumi. *Foreign Minister* wa Australia by then Julie Bishop aliwahi kusema, *just as traditional diplomacy aims for peace and security, so economic diplomacy aims for prosperity*. Kwa nini ninasema haya? Hii diplomasia ya kiuchumi ilianza nchini kwetu mwaka 2001, lakini nilikuwa nahitaji sana Mheshimiwa Waziri atuambie, *as of to date*, sera hii ya kiuchumi imefikiwa vipi na imefanikiwaje na tumei-utilize namna gani kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Masele pale, maana hii *economic diplomacy* ndiyo injini ya sasa hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa kuna changamoto za pesa, lakini kuna suala zima la *commercial attaché*, niliwahi kuuliza hapa swali, tatizo la *commercial attachés* wetu kazi zao hazionekani vizuri na wengine wako *inactive* ama hawapo kabisa kwenye Balozi zetu. Lakini ajabu nikajibiwa kwamba Wizara hii ni mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapozungumzia *economic diplomacy* kwa misingi hii sijui ni nini kifanyike. Ushauri wangu kwa Serikali, ni kama huu ufuatao; pamoja na kwamba *diplomacy is expensive but in order to move* tunatakiwa tufanye nini? La kwanza tunatakiwa tuwe na *various capacity building* kwa *foreign staff* wetu ili waweze kujua wanaweza wakaitangaza nchi yetu namna gani kule nchi za nje pamoja na vivutio vyake. Na hawa ndugu zetu ma-*foreign staff* wanatakiwa pia wawe ma-*lobbyists* wazuri, wawe *negotiators* wazuri, wawe *smart*, waweze ku-*strategize* waweze kuwa *innovative*. Na ndiyo maana ninazungumzia tuweze kuwa na *capacity building* za mara kwa mara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile *performance appraisal* inatakiwea kufanyika, wapewe *marbles*, wapewe *goals* ili tuweze kuwa na *deliverables* ziweze kuonekana, vinginevyo tutakuwa tunafanya *business as usual*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika hizi Balozi zetu tunatakiwa tuwe na *tourists experts* kama wale wa uhamiaji wanaoshughulikia viza. Lakini hawa *tourists experts* wetu ambao tunakiwa tuwe nao katika zile Balozi zetu na wenyewe wajaribu kuwa *strategists*, kwa maana ya kwamba wawe katika zile nchi ambazo tunaweza tukafanya ubalozi wetu na biashara ya utalii kwa vizuri. Kwa mfano, nchi ya China sasa hivi wote ni mashahidi, ni nchi ambayo inakua kwa kasi na vilevile inaweza ikaleta ndege tukawa na uwekezaji; ukizingatia pia Watanzania wengi wanafanya biashara kule China, na vilevile tukaweza kuwa na *consulate pale* Guangzhou na tukafanya utaratibu wa Watanzania hawa kuweza kuwa na *partnership* pamoja na wale wenzetu wa China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala zima la *shuttle diplomacy*. Katika Bunge lililopita jambo hili nililizungumzia sana. Ninatoka Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Mbeya kuna Ziwa Nyasa na tunajua upande wa Ziwa Nyasa kuna suala zima la Heligoland, maana hii ni tangu enzi za Kamuzu Banda. Lakini

Mheshimiwa Waziri hapa kwenye taarifa yake hajazungumzia mgogoro wa mpaka wa Ziwa Nyasa mpaka leo hii imekuwa vipi. Sisi tunaotoka katika Ziwa Nyasa na wenzangu wengine wote tungependa kujua mpaka leo hii suala hili llimefikia wapi na suala zima za *shuttle diplomacy* limefikia wapi kwa sababu wakati ule Mzee wetu Chissano na wenzake walikuwa wanajaribu kulizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la *conference diplomacy*. Hii ninajua ina gharama zake na sasa hivi tunajua wengi hawasafiri sana na ndiyo maana nikazungumzia masuala ya *foreign staff* wapewe ile *capacity building*, lakini vilevile katika suala zima la *bilateral na multilateral* basi tujaribu kuangalia sana kama tunaweza tukawa na *forums* za aina mbalimbali kuweza kufanyika hapa nchini kwetu ili tuweze kuongeza Pato la Taifa, tuweze kutangaza nchi na vivutio vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni majengo yetu katika Balozi zetu. Waheshimiwa wengi hapa wamezungumzia, ukweli majengo yetu katika balozi yanatia aibu sana, hakuna fedha. Sasa tufanyeje ili majengo haya yaweze kufanyika katika njia itakayokuwa bora na ya ufanisi? Kwanza yanatakiwa kukarabatiwa; ama tuweze kujenga majengo ya *staff* wetu, vinginevyo tusipoangalia gharama zitakuwa ni kubwa sana zile za kupangisha. Kwa maana hiyo tujenge balozi zetu, vile vile tuimarisha au tuboreshe makazi ya *staff* maana na wenyewe wanakuwa hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mawazo yangu kwa leo yalikuwa ni machache, nisingependa nigongewe kengele, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mary kwa kujali muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Kanali Masoud dakika tano na Mheshimiwa Mattar pia itakuwea dakika tano.

MHE. KAN. MST. MASOUD ALI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru nafasi hii na mimi ya kuchangia mambo machache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa maombi tu kwa Wizara hii ya Mambo ya Nje. Kwa kipindi kifupi ambacho tunaambiwa tunataka kujiunga na mtengamano wa Afrika ya Mashariki wasi wasi wangu mkubwa bado elimu hii haijafika kwa wananchi wa Tanzania. Na kama tukienda hivi itakuwa ni kama wale abiria tunaodandia gari lilishaondoka. Tumeona uzoefu, hasa kwetu hapa Tanzania na Zanzibar zaidi, sehemu nyingi za ajira wafanyakazi wengi wanatoka Kenya. Na tatizo si kwamba nafasi hizi Watanzania hawaombi, Watanzania wanaomba nafasi, sifa za kuajiriwa hawana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kwenye mtangamano huu wa Afrika ya Mashariki wasiwasi wangu tutakuja kukuta hapa sasa Wizara zote, sehemu zote za biashara na mambo mengine yamechukuliwa na wenzetu kwa sababu tayari walishajipanga. Ninaomba sana Wizara hii ijitahidi, kwanza ifikishe elimu, tena tujipange sasa sisi wenyewe tunaingiaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tunakokwenda ni kugumu kwa mawazo yangu nadhani tutakwenda kuanguka huko. Hatujajipanga, kama tuliodandia gari vile. Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara ijitahidi kufanya uwezo wanaouweza wao walionao kuhakikisha vijana wetu nao wanakuwa na sifa; kwanza kwa kuajiriwa lakini pili tupunguze na sisi kununua bidhaa kutoka nchi za wenzetu, tujitahidi na sisi kuzalisha kupeleka kwa wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kupeleka bidhaa nje ya nchi Serikali yetu ijitahidi kuondoa vikwazo, bado *corruption* ipo Tanzania. Wafanyabiashara wetu wanapata vikwazo vingi, wanapotaka kupeleka bidhaa zao nje ya nchi wanapata vikwazo tofauti na wenzetu. Bidhaa zinazokuja tunapokea vizuri tu, lakini zetu sisi tukitaka kuzipeleka humo njiani mtu anakwama mpaka anaamua kuziua njiani. Ninaomba sana Serikali hii ijitahidi na Wizara hii isimamie biashara na sisi tuwe tunanufaika na wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninataka kuzungumza kidogo. Tunapokuja hapa Bungeni kuna watu wanazungumza mambo mengi, wengine hatujasafiri, tumesafiri kidogo nje ya nchi. Sasa tunalinganisha wenzetu na sisi, lakini ninasema tulinganisha wenzetu na sisi katika baadhi ya mambo. Baadhi ya mambo Tanzania tuko mbele sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengine, kweli, wala tusikatae, ziko nchi kubwa zimetushinda lakini yako mambo sisi tuko mbele. Yule anayesema amekwenda *Washington DC* mimi pia nimeshafika huko, na si mara moja. Lakini ukisema maendeleo wanaangalia watu wanavyotembea mitaani, maendeleo wanayaona mitaani kwa zile sura za mitaa. Mimi nilishawahi kufika *Washington DC* nanikakuta barabara ina shimo, katikati ya barabara. Barabara yetu ya Kimara ni nzuri. Kwa hiyo, bado tuseme tu, yako mambo tumezidiwa, lakini yako mambo wenzetu bado wametushinda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu, ndugu yangu mmoja hapa, Mheshimiwa Msigwa, sijui kama ni mchungaji maana hajawahi kuniambia na ni rafiki yangu sana lakini hajawahi kuniambia. Amesema, sitaki kulijibu lakini sijafanya kazi sana *foreign*, nilikuwa nayaona mambo mengine ambayo yanafuatwa, hasa suala la Mabalozi. Anapozungumza Mabalozi wanakatazwa, sijafahamu, labda atakuja kunifahamisha nikikutana naye nje. Nina vyofahamu mimi Balozi kama Balozi, hakatazwi kukutana na mtu, isipokuwa kuna taratibu lazima Balozi azifuate. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti Balozi atakapo kwenda kwenye Taasisi au kuonana na mtu yoyote, lazima Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje ielewe. Lazima atoe taarifa na taarifa zifikishwe kule anakokwenda, sio kukutana naye tu halafu useme. Mimi sidhani kama Balozi anakatazwa kukutana na mtu, tunakutana na watu binafisi hiki kitakuwa chama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu, tunachozungumza utaratibu ukifuatwa, sidhani kama Balozi anakatazwa kukutana na mtu. Naomba tu wanapotaka kukutana na watu kama hao, si wafuate utaratibu tu! Wasiogope kwa sababu utaratibu upo, umepangwa na wautekeleze, hakuna haja ya kuleta mambo mengine hapa ambayo kwa kweli ni kupotosha, si kweli! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tunapokuja Bungeni, hasa Bunge letu la Tanzania hili, tukitaka liwe na heshima, sisi wote kwanza tuheshimiane. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Mattar na baadaye Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Balozi Adadi na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako wajiandae.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia siku ya leo. Lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze watendaji wake wote wa Wizara hii ya Mambo ya Nje na vilevile, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri, ambayo anaifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze Mabalozi wetu kwa kazi nzuri, ambayo wanaifanya wakiwa katika kazi zao huko nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, Mabalozi wetu walioko nje, hawa Mabalozi wetu wa Tanzania, wafanye kazi nzuri, tuwatumie katika kazi ya kutangaza utalii wetu tukiwatumia Mabalozi hawa katika kazi ya kutangaza utalii na kazi ya kutafuta Wawekezaji katika nchi yetu, basi naamini hata sekta ya utalii katika nchi yetu hii itakua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaamini katika sekta ya utalii ikikua, basi ni chanzo cha uchumi wetu kukua, kwa kuwa, tunaamini uchumi wetu, hii

sekta ya utalii inachangia asilimia kubwa katika suala kuongezeka uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri tufanye kazi ya ziada tuhamasishe Mabalozzi wetu na tuwaambie Mabalozzi wetu wahakikishe kwamba wanatangaza utalii wetu wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatembelea Balozzi za wenzetu, basi ni kazi kubwa wanayoifanya, unapofika Mheshimiwa Waziri jambo la kwanza wanakuonyesha utalii wa nchi za zao. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri tuweze kufanya kazi hizi na Balozzi zetu ziweze kufanya kazi hizi kwa maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kufanya Mabalozzi wetu tunawapenda sana. Vilevile wahamasishie katika kuwatafuta wawekezaji ili kuhakikisha kwamba, nchi yetu inatumia njia hii ya Mabalozzi. Sio Mabalozzi hawa kuwepo kule, ikawa ndiyo imemaliza kazi tu. Tunawatumia Mabalozzi wetu kuhakikisha kama wanahangaika na kazi ya kuwatafuta wawekezaji ili nchi yetu ipate maendeleo kwa kuwatumia Mabalozzi hawa, tusiwe na Mabalozzi tumewaweka tu wakati kazi haifanyiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mabalozzi hawa wafanye kazi ya ziada ili wafahamu kwamba nchi yetu tukiwapeleka kule na sisi tunawategemea kwa hali na mali, tunawategemea wafanye kazi kwa huruma zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, jambo kubwa linasikitisha sana hili. Jambo la makazi, jambo la majengo ya ofisi za Balozzi zetu, hizi hali zimekuwa mbaya, haziridhishi kabisa haya majengo. Mabalozzi wetu na watendaji wetu, wanafanya kazi katika wakati mgumu, na wanakaa pahala pabaya, zinafika hatua hata nyumba nyingine, zinafika hatua ya kuvuja na tukitegemea majengo haya yatafika hatua ya kuporomoka tutapata hasara kubwa katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la watendaji wetu. Watendaji wetu katika sekta hii, jambo kubwa sana wanatakiwa wapewe mafunzo ya kutosha. Inaonekana wafanyakazi wetu, watendaji wetu bado mafunzo yetu katika ufanyaji wao wakazi, umekuwa uko duni sana. Naiomba Wizara yako, naamini Waziri wewe ni msikivu utafanya hii kazi, hawa wafanyakazi wetu waweze kupata mafunzo bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wafanyakazi wanapopata mafunzo ya uhakika, basi hata utendaji wao wa kazi, utakuwa wa kuboresha sana katika kazi hii ya kutangaza utalii wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wetu tukiwapeleka wanakuwa kama si wafanyakazi tofauti na Balozi wa nchi za wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mattar. Tunaendelea na Mheshimiwa Allan Kiula kwa dakika tano na Mheshimiwa Balozi Adadi kwa dakika tano halafu tutakwenda na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Ninayo mambo manne na mambo yenyewe ni mafupi mafupi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Sera ya Mambo Nje inabidi ifanyiwe marekebisho, tunajua ni ya mwaka 2001 kwa sababu sera ndiyo inatoa mwelekeo, tunakoelekea, inaweka *priority* zetu, hilo ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, tunasema mtengamano, fursa zilizopo, tumepata machapisho mengi, lakini ni jambo la ajabu hata sisi Wabunge tunauliza, hatujaujua sawasawa huu mtangamano. Sasa ni wakati muafaka wenzetu hawa wakachukuwa hatua za makusudi kuwaelimisha jamii inayozunguka, watu walioko mipakani waelimishwe na sisi Wabunge tuelimishwe ili tuweze kutumia fursa hizo. Kwa sababu fursa hizi zinafahamika tu kwa Wabunge wa Afrika Mashariki, zinafahamika na baadhi ya watu tu, lakini Mwananchi wa kawaida; katika nchi yetu tuna utaratibu wa utawala, tuna wenyeviti wa vitongoji, tuna wenyeviti wa vijiji wanaweza wakatumiwa hasa mipakani kuhakikisha kwamba, elimu hii inawafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la *Diaspora* limezungumziwa sana, watu walioko huko. Mimi najua kwamba, iko *diaspora*, kuna *forum* ya *diaspora* na huwa wanakusanyika wanatambuana katika nchi mbalimbali wanazoishi licha ya mchango wanaopaswa kuuleta huku kwetu, lakini pia wao wanatakiwa kutambuana. Ni ukweli usiopingika kwamba watu wengi wamekwenda kule wamejilipua, hawatambuliki katika Balozi zetu, kama hautambuliki katika Balozi zetu zilizoko huko, utapataje huduma hiyo? Kwa hiyo, ni wakati muafaka sasa waliojificha huko watoe taarifa kwenye Balozi ili waweze kupata huduma zinazohitajika badala ya kuendelea kulalamika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine limezungumziwa hapa, suala la Rais kusafiri nje ya nchi; kuna *leadership style*, *leadership style* ni muhimu, kiongozi anaweza akawa anasafiri nje na ikawa sawa lakini yuko kiongozi mwingine, yuko anafanya *strategic planning* nyumbani. maadamu nchi inakwenda, inasonga mbele na tunaona matokeo, kama tunaona matokeo

hana sababu ya kusafiri. Atasafiri itakapo kuwa ni lazima, huo ni utaratibu wa uendeshaji wa nchi yake. Hata wenzetu hawa wakipata nchi watapanga utaratibu wao wa kuendesha nchi, huu ndiyo utaratibu unaonekana ni utaratibu bora. Kwa hiyo, inabidi tuheshimu utaratibu huo, tuone nchi inaendeshwaje na sisi Wabunge hapa tushauri ili tuweze kuona kwamba tunatoa mchango katika uendeshaji wa nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mabalazi; suala la Balozi kuzuiwa, limesemwa wanazuiwa kuwasiliana na maeneo mbalimbali, amesama msemaji wao mmoja. Uko utaratibu, hapa ni Tanzania na hapa ni kwetu na sisi ndiyo Watanzania. Balozi hawezi kuja hapa akafanya mambo anavyotaka yeye, lazima Balozi akija hapa anakuwa *Monitored* na asipofuata taratibu hizo tunamchukulia hatua na tunaweza kumrudisha alikotoka. Na hii imeshaonekana ni *practice World Wide*, inafanyika na sisi hatuwezi kwenda tofauti na hivyo. Lazima tulinde nchi yetu, lazima tuwe na uchungu wa nchi yetu, tuweze kuona kwamba Taifa letu linakuwa salama na hao Mabalazi wanafanya kazi walizotumwa sio wanafanya kazi, ambazo wanafikiria wao kichwani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ya kwangu yalikuwa ni hayo machache tu, asante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi dakika tano na baadaye Mheshimiwa Nsanzugwako ajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii, kuchangia hoja hii ya Mambo ya Nchi za Nje. Nashukuru sana kwa sababu Wizara hii ni Wizara ambayo ni muhimu sana, Wizara ambayo inatuunganisha na mambo yetu huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kukuhakikishia kwamba Mabalazi ambao wako nje, Mabalazi ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais huko nje wanafanyakazi nzuri sana. Wanafanya kazi nzuri na wanajenga, wanatoa sifa kubwa kwa nchi yetu ya Tanzania. Sisi ambao tumekuwa Mabalazi huko nje tunaelewa uthamini ambao tulikuwa tunapewa, heshima ambayo tulikuwa tunaipata huko nje na *consultation* nyingi nchi ya Tanzania, Mabalazi ambao wako nje walikuwa wanakuwa *consulted* kwa ushauri na kwa kila kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemshangaa sana Mheshimiwa Waziri Kivuli, anapotupiga *critic* na kutulinganisha na Wajumbe wa Nyumba Kumi Kumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli unaweza ukanilinganisha mimi na Mjumbe wa Nyuma Kumi Kumi? Unaweza kumlinganisha Balozi Mahiga na Mjumbe wa

Nyumba Kumi Kumi, amekuwa Balozi wetu kwenye Umoja wa Mataifa kwa miaka kemkem mpaka Katibu Mkuu mwenyewe Ban Ki -Moon, akasema kwamba, hapana wewe umefanya kazi nzuri akampa kazi Somalia. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa Balozi na kiongozi wa Mabalozi Zimbambwe kwa miaka chungu nzima, Mheshimiwa Msigwa unaweza kusema hivyo kweli? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi Mheshimiwa Msigwa nilikuonya nikakwambia kwamba, ushauri ambao tunakupa kwenye Kamati, usiuchukuwe ushauri huo ukaugeuza kwamba ndiyo *critic* na ndiyo ulichokifanya hicho. (Makofi/ Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingi ambao umezungumza hapa ni ushauri ambao tumeupa Wizara kwamba vitu gani muhimu ambavyo wanatakiwa kuvifanya. Sasa yeye kazigeuza kwamba ndiyo *critic*, ndiyo madongo ya Wizara, hapana hivyo, hatuendi hivyo Mheshimiwa Msigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, kazi ambayo wanafanyika huko ni kubwa na heshima ambayo tunaipata huko nje ni kubwa na Mabalozi hawa msiwakatishe tamaa, wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia diplomasia ya uchumi, wameleta wawekezaji chungu nzima hapa. Mimi mwenyewe nimeshaleta wawekezaji chungu nzima hapa, wamekuza biashara chungu nzima na nchi yetu na nchi za nje. Jamani tusiwakatishe tamaa, tuzidi kuwaunga mkono, Mabalozi hawa kazi wanayofanya ni kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokisema sasa hivi, *Foreign Policy* ya kwetu inabidi ibadilike kwamba zamani *foreign policy* ilikuwa *politically*, inakwenda *politically*, lakini sasa hivi ni lazima twende na hali halisi inavyokwenda duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tumeishauri Wizara kwamba, ni lazima waangalie wanapoanzisha Balozi sasa hivi waanzishe balozi sio *politically*, waangalie kwamba tunaweza kufaidika vipi kiuchumi na ndiyo maana sasa hivi unakuta kwamba Balozi wana mipango, ambayo tumeshauri, sisi tumeishauri Kamati kwamba ni lazima wahakikishe kwamba wanaanzisha Balozi kwenye zile nchi, ambazo wanaona kwamba tunaweza kupata wawekezaji, kukuza biashara zetu na tunaweza pia kuleta watalii wengi hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana sasa hivi Wizara ina malengo makubwa sana ya kuanzisha ubalozi kule Uturuki, Qatar, *South Korea* na

sehemu nyingine nyingi. Kwa hiyo, ni suala ambalo tunatakiwa tuwaunge mkono na tuhakikishe kwamba, wanapata fedha za kutosha kwa sababu diplomasia.... aaha! (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi. Tunaendelea na Mheshimiwa Nsanzugwako na baadaye Mheshimiwa Lucy Magereli na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali pamoja na Mheshimiwa Khatib Said Haji wajandae.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kwa namna ya pekee kabisa nikupe hongera sana Balozi Mahiga na Naibu wako. Na kweli tuwape hongera sana Mabalozi wetu wanaofanya kazi nchi za nje katika mazingira magumu. Wengine wanafanya kazi katika mazingira ambayo sio rafiki sana, hawana vitendea kazi, hawana staff wa kutosha, lakini wameendelea kufanya kazi kwa moyo mmoja, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba nianze na hili moja na Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba ulisikie hili. Lipo tatizo, nilikuwa nafikiri ni muhimu Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, Wabunge wa Upinzani, tuwe na mafunzo maalum ya diplomasia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama ni ya siku mbili, siku tatu. Unajua Mheshimiwa Msigwa kuna mambo mengine hayasemwi hadharani. Kuna mambo mengine hayasemwi hadharani na kuna mambo mengine yanasemwa hadharani. Katika utamaduni wa diplomasia kuna mambo ambayo unaweza ukayasema tu hadharani na mengine yanazungumzwa ndani, *under camera*. Kwa hiyo, niombe, huko ndani nyuma kulikuwa na utamaduni huu kwamba Bunge linakaa, Balozi Mahiga na uzoefu wako unakuja na wenzako mnatupiga shule sawasawa, tunaelewa. Hata makatazo mnatueleza kwamba hiki usifanye na hiki ufanye. Maana haitoshi tu kwamba, wewe ni Mbunge unakwenda kukutana na Mabalozi, unakutana nao kuzungumza kitu gani? Kuna mambo mengine ambayo yanagusa uhai wa Taifa letu yana namna yake ya kuyazungumza na hata Bunge la mwaka 2005, Bunge la mwaka 2000 yote yalifanyika mafunzo yaliendeshwa na Wabunge walifundishwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kujifunza hakuishi, unaweza ukakaa unasema sema maneno hapa kwa sababu tu pengine hujui vizuri au unafikiri kila kitu lazima kisemwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Mheshimiwa Balozi nikurudishe kwenye kitabu chako ukurasa wa 118, nianze na kuzungumzia ujenzi wa Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja na pia nimeona imeambana na kipeperushi hiki hapa ambacho kinazungumzia Vituo vya Pamoja na Utoaji wa Huduma Mipakani. Naomba nikukumbushe tu, umeorodhesha vituo saba, lakini katika kipeperushi hiki umeongezea habari ya Vituo vya Kasumulu kule Songwe, Malawi na Mtambaswala na kwenye *border* ya Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nikukumbushe kitu kimoja kwamba kuna vituo muhimu sana umevisahau. Kuna kituo muhimu sana cha forodha, kiko kwenye mpaka wetu wa Burundi, sehemu ya Manyovu na Burundi, ni *border post* ya muda mrefu sana na Serikali ya Tanzania kimkakati ilishajenga barabara ya lami kutoka bandari ya Kigoma mpaka kwenye *border* na wenzetu wamejenga barabara ya lami kuanzia *border* pale kwenda Bujumbura. Sasa kituo kile ni cha siku nyingi sana, sasa katika orodha hii sikioni. Nilikuwa nafikiri kama sio *oversight* basi mkiongeze na kiweze kupewa fedha kikarabatiwe vizuri. Mpaka wa Manyovu ni mpaka wa siku nyingi na ni mpaka wa kihistoria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kingine cha forodha, ambacho umekisahau Mheshimiwa Waziri ni Kituo cha Forodha cha Mabamba na Burundi ni Kituo cha Forodha cha muda mrefu, kiko katika Wilaya ya Kibondo, hiyo Manyovu iko Wilaya ya Buhigwe. Nilikuwa naomba katika vituo vile ambavyo vinahitajiwa kufanyiwa ukarabati, Mheshimiwa Waziri ni vyema mkavitazama vituo hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba, swali langu la pili Mheshimiwa Waziri, naomba Balozi unisaidie utakapokuwa unahitimisha, ni vigezo gani mnavitumia tunapoanzisha Ubalozi mpya? Ningependa kujua vigezo, ambavyo vinatumika kwa mfano, mimi mpaka leo sielewi ni kwa nini hatuna Ubalozi Seoul - Korea ya Kusini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Burundi ina Ubalozi pale, nchi ya Zambia ina Ubalozi pale. Niliishi pale Seoul, kwa nini sisi Tanzania hatuna Ubalozi pale? Na mnajua wenzetu Wakorea hawa na katika diplomasia ya kiuchumi ndiyo wametujengea Daraja la Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akikuuliza moja ya vitu halisi vya kuonyesha ni kwamba Daraja la Mto Malagarasi na viunga vyake limejengwa kwa sababu ya ushirikiano ulioanzia *Foreing Affairs* kwa kweli na ni jitihada za Mheshimiwa Kikwete akiwa Waziri wa *Foreign Affairs*, ambaye alizungumza na wenzetu wale, hatimaye tukapa daraja lile. Sielewi kwa nini hatuna Ubalozi pale. Seoul - Korea ya Kusini mnajua ni nchi, ambayo imepiga hatua kubwa katika TEHAMA, katika

ujenzi, katika kilimo, ni muhimu Mheshimiwa Waziri utakapohitimisha unieleze ni kwa nini hatuna ofisi pale Seoul?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ambalo ningependa niliseme ni kuhusu Wakimbizi. Sisi Mkoa wa Kigoma tumepokea wakimbizi tangu uhuru, lakini bado wakimbizi wanaingia katika nchi zetu. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri kupitia ofisi yako pale ofisini kwako kwenye *Foreign Services* anzisheni kitengo cha wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kitengo cha wakimbizi kilichopo Mambo ya Ndani kina *deal* na usalama zaidi wa wakimbizi. Lakini sisi ambao tumeathirika na ujio wa wakimbizi, ambao Mabalози wengi wanakuja Kigoma pale, Mabalози wengi wanakuja Kasulu pale, Mabalози wengi wanakwenda Kibondo pale hatuna namna ambayo tuna kiunganishi cha kwamba Mabalози hawa sasa wanaokuja kuhudumia wakimbizi kuwe na jitihada maalum hasa ya kusaidia maeneo, ambayo yameathirika na ujio wa wakimbizi.

Mheshimiwa Balozi, mwezi Januari nilibahatika kukutana na Mabalози sita waliokuja kutembelea kambi za wakimbizi, tumezungumza mengi sana nikahisi ni wakati sasa kwenye ofisi yako au ofisi yako muwe na uhusiano wa karibu kati ya Kitengo cha Wakimbizi Mambo ya Ndani na Kitengo cha Wakimbizi katika ofisi zako ambacho kitakuwa kina-raise masuala haya na hasa huduma kwa maeneo ambayo yameathirika na ujio wa wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie suala la migogoro. Alisema ndugu yangu mmoja suala la Kongo, Mheshimiwa Balozi Mahiga, lazima tuilinde Kongo ya Mashariki, lazima tuilinde DRC kimkakati, wale ni *partners* wetu katika biashara. Kwa sababu tuna askari wetu kule ambao wanafanya kazi nzuri sana na nimwombe Waziri wa Ulinzi wale askari wasitoke Kongo wanatufanyia kazi nzuri sana, naomba tuilinde DRC kimkakati kama *partners* wetu wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono kwamba wakati umefika pale Lubumbashi angalau tuwe na Ofisi ndogo ya Kibalozi kwa ajili ya kulinda maslahi yetu kama nchi. Ie ni nchi kubwa, nchi yenye utajiri mkubwa na kusema kweli tunaweza tukanufaika nayo kwa msingi huo, naomba uyazingatie hayo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Nsanzugwanko. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Magereli.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa ya kuchangia katika Wizara ya Mambo ya Nje. Kwa utangulizi tu, nianze kwa kuonesha masikitiko yangu juu ya ukandamizwaji wa demokrasia unaofanywa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hili Bunge sasa limegeuka kuwa mwiba mkali sana kwa ustawi wa demokrasia ya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono jitihada zote zilizofanyika siku ya jana kuhakikisha kwamba tunaleta *attention* ya kuwasaidia vijana wetu ambao hawakutendewa sawa. *Whether* mliikubali au mliikataa lakini ulimwengu unajua ya kwamba hapo mmekosea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Msigwa umefanya kazi yako vizuri, hongera sana. Naomba pia kuunga mkono hotuba ya Kamati ya Mambo ya Nje, mmefanya kazi nzuri, mmetendea haki mlichokiona na huo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ku-*declare* kwamba ni mjumbe wa Kamati hii na katika kutekeleza majukumu yetu ya Kamati, nieleze tu masikitiko yangu kwamba hii ndiyo Wizara ambayo tulikuta hata cha kuzungumzia hakipo, kila unakogusa tabu, shida, karaha, fadhaha. Ukizungumzia shughuli za utendaji wa watendaji katika Wizara ya Mambo ya Nje yaliyoko kule fadhaha, ukitazama Balozi zetu zilizoko nchi za nje fadhaha, bajeti ya maendeleo waliyotengewa hawakupata hata senti moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika kwa kweli kuona hotuba hii ambayo nimeisoma mwanzo mwisho, sijajua Waziri anaogopa, ana hofu au ana mashaka, lakini nilitarajia aje na hotuba ambayo ni ya kitaalam, ina mikakati na ina mipango lakini Mheshimiwa Waziri amekuja na hotuba ya kisiasa. Nikajiuliza yale tuliyoyaona wakati wa Kamati, japo sawa Waziri mpya kwa *this time*, nikajua atayaona na kwenye hotuba yake ndiko atakakokuja na yale ambayo aliyaona ni upungufu na ataonesha mikakati yake na *way forward* lakini Mheshimiwa Waziri ameandika siasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye hotuba yake ukurasa wa 111, amesema malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017, nimeyasoma yote ni siasa. Nisome mawili ya mwanzo tu, la kwanza kutangaza nchi yetu kama moja ya nchi duniani zenye mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji kutokana na historia yake ya miaka mingi ya amani, umoja, utulivu na mshikamano wa kitaifa, kwa kufanyaje?

Lla pili, anasema kuongeza uwakilishi wetu nchi za nje kwa kufungua Balozi mpya ofisi za Kiconseli na kuimarisha rasilimali watu na fedha wakati haya ndiyo ambayo kwenye Kamati tumezunguka tukiyatazama, hizo Balozi tulizonazo tu ziko hohehahe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia Mheshimiwa Mbunge, mama wa CUF anasema alikwenda Msumbiji akakuta katika Ofisi ya Balozi mama ntilie anaingia anauza chai, hakuna hadhi. Mimi iko Balozi tulifika tukakutana na mende, panya na popo. Sasa akituambia tu kwa maneno mepesi kama alivyosema katika lengo lake la pili kwamba anataka kufungua Ofisi za Balozi wakati viwanja tulivyonunua havijajengwa, viwanja vilivyotolewa havijajengwa, nyumba tulizopewa kwa ajili ya Ubalozi ziko hoi, ndiyo hizo zenye popo na mende, sasa anafunguaje Balozi nyingine mpya wakati zilizopo hii ndiyo hali yake? Basi *fine*, tulitegemea aseme *at least* kwa *details* kwamba tutafanya moja, mbili, tatu, tutakarabati lakini tutaongeza na hili yaani tulitaka hata kuona nyingi ngapi? Ndiyo maana nasema hii ni siasa kwamba tutafungua Balozi mpya, ngapi, wapi na kwa gharama ipi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni huduma za kibalozi. Watendaji wetu katika Balozi zetu mbalimbali wana hali mbaya, huduma ni shida lakini hata vipindi vyao vya kuhudumia vinapokwisha fedha ya kuwarejesha nyumbani ni tatizo. Badala yake, kama alivyosema Mheshimiwa Msigwa, uteuzi wa nafasi za Balozi katika nyakati fulani zimeonekana ni adhabu kwa wale watu ambao wanaonekana ni *threat* kwa wanasiasa fulani. Kilicho kibaya ni kwamba unapigwa jina Ubalozi halafu unaachwa hapo. Kwa hiyo, pale *Foreign Affairs* kuna watu wenye *titles* za Ubalozi wengi tu, wakiona unakerakera kwa kuweko hapa basi wanakutafutia mahali wanakwenda kukuficha pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakaporejea ningetamani haya ninayoyazungumzia atuoneshe kimkakati hasa kwamba anakwenda kuchukua hatua gani na atupe na *time frame*. Kwa sababu hata suala la Sera ya Mambo ya Nje, hii ambayo imetumikiwa kwa miaka kadhaa sasa ya *Economic Diplomacy*, hakuna tulicho-*achieve*. Kwa sababu kingekuwapo angekuja nacho akatuonesha kwamba kwa kipindi kilichopita tumefanya yafuatayo lakini hotuba yake imeongea siasa mwanzo mwisho na hakuna ambacho kiukweli amemudu kutupatia kama takwimu za kuonyesha *achievement* na *if so, what is next?* Je, tunakuja na sera nyingine au bado tunaendelea kutumikia hiyo hiyo iliyoshindwa? Mchangiaji mmoja amesema tumeleta wawekezaji wa kutosha. Sawa, walipotosha wakafanya nini? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utangazaji wa vivutio na fursa za uwekezaji Tanzania, kama alivyosema Mheshimiwa Mwanjelwa, natamani sana labda tungeweka sasa *goals* na kila Afisa wa Balozi aliyeko Ubalozi ambaye ana wajibu wa kutekeleza haya mwisho wa bajeti ya mwaka mmoja atuambie ame-*achieve* nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hawauwezi kumdai ame-*achieve* nini kwa sababu hawawa-*finance*, hawawa-*facilitate* wale watu, kwa hiyo hawa-

perform. Wamekaa kule wanaendelea ku-enjoy diplomatic securities lakini kiukweli najua hawawezi kukubali ku-set goals na kuanza kufanya assessment ya performance kwa sababu hawajawa-facilitate maafisa wetu walioko maeneo ya Balozi ili waweze kutekeleza wajibu wao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niombe Serikali itusaidie katika Wizara ya Mambo ya Nje, bajeti wanayopewa haikidhi haja hasa kwenye miradi ya maendeleo. Ile ndiyo sura ya Tanzania katika maeneo ambayo tuna uwakilishi lakini kama kweli tuna Balozi ambazo mapaa yanavuja na umekaa *sitting room* mende anapita, kiukweli hata kama tungetaka wafanye nini isingewezekana kwa sura ile. Mwaka jana wametengewa bajeti ya shilingi bilioni nane lakini hawakupata hata senti moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia. Kama kweli majukumu tuliyokipatia Chuo cha Diplomasia ndiyo tunayotaka kitekeleze, basi Serikali inatakiwa kuja na kauli ituambie kwamba hicho chuo kweli ni Chuo cha Diplomasia au wameshabadilisha ajenda. Kile chuo kwa miaka mitatu mfululizo hawajapata senti moja ya pesa za maendeleo halafu tunasema wawafundishe Mabalozi wetu, wake wa Marais na kadhalika, hiyo haiwezekani *unless* tuwe na mkakati mwingine. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Magereli.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali kwa dakika tano.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri naomba anisikilize kwa makini ili nimshauri, ingawa tuko wachache huku lakini tuna ushauri mzuri kweli, huko usione wingi huo, hakuna kitu watakachokushauri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwenye hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 112 ameelezea malengo ya Wizara yake. Kwenye lengo namba tatu, anasema kuendelea kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mikataba, naishia hapo hapo kwa sababu nina dakika tano. Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekubaliana na wamesaini mikataba kwamba kila nchi itakuwa na Wizara maalumu inayoshughulikia Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wana Waziri wa Mambo ya Afrika Mashariki na wana Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje; Uganda hali kadhalika; Rwanda hali kadhalika na sisi Rais Kikwete alikuwa na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Waziri wa Afrika Mashariki. Ndiyo, Mheshimiwa Mwakyembe anasikitika nini, alikuwa Waziri wa Afrika Mashariki. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hajui kama kuna mkataba wa Afrika Mashariki kwamba lazima kuwe na Waziri Maalum anayehusika na mambo ya Afrika Mashariki au huyu Mwanasheria anamshauri nini Rais sasa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nilirejeshe kwa sababu Mheshimiwa Waziri ndiye anayehusika, suala la mabaki ya mjusi wa Tendegulu yaliyopo Ujerumani. Aibu! Watu wa Ethiopia walikuwa na mnara wao ulikaa Italia miaka 68, wameurejesha. Leo tuna mabaki ya mjusi yamechukuliwa Tanzania ninyi mnakaa hapa kuja kusifia tu, tani 70, sijui alikuwa na urefu wa mita 60, Tanzania tunanufaika na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeandika barua nimewaitea kwenye Wizara hii, Makatibu Wakuu walichonijibu sikielewi, mara mpaka leo wanafanya *calculation*, hawajui Tanzania inanufaika na nini. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hapa aje atuambie Tanzania inanufaika na nini na mabaki ya mjusi wa Tendegulu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mjusi huyu mkubwa anaijengea historia Ujerumani, yuko pale Hamburg, watalii wanakwenda kuangalia wanaingiza pesa Ujerumani, leo alikotoka mjusi maji ya kunywa hawana, barabara hakuna, Wazungu wanakwenda pale Tendegulu tunawabeba mgongoni. Mheshimiwa naomba majibu na niliwaambia wananchi wangu na Mheshimiwa Magufuli alisema wakati wa kampeni alipokuwa Jimbo la Mchinga kwamba atashughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiona Waziri anashindwa kulishughulikia nitawachukua wananchi 112,000 wa Jimbo la Mchinga, nitampelekea Mheshimiwa Magufuli awajibu alichowaahidi wakati wa uchaguzi. Haiwezekani kama Taifa tunakaa tu, vitu vyetu viko nje vinawanufaisha watu wengine, sisi wenyewe tuko bwerere tunafurahifurahi tu hapa. Tunaomba majibu, mabaki ya mjusi wa Tendegulu tunayapata na kama hatuyapati tunanufaika na nini? Tunaomba majibu juu ya hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala la Chuo cha Diplomasia. Limezungumzwa sana. Hiki chuo wamekitelekeza au hiki chuo sasa hivi kazi yake ni nini? Miaka mitatu Chuo cha Diplomasia hawapeleki bajeti ya maendeleo na ni chuo ambacho kina-*train* wanadiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Waziri na nivishauri vyama, kuna umuhimu wagombea wa Urais waanze kupitia pale kwa sababu tunaingia kwenye matatizo ya kidiplomasia kwa sababu viongozi wetu wengine hawajui hata maana ya diplomasia ni nini. Ndiyo maana leo unakuta tunazuia hela za MCC shilingi trilioni moja, kiongozi mkubwa wa nchi anasema yeye haoni kama ni tatizo. Mheshimiwa Waziri nataka atakapokuja hapa atuambie tumewakosea nini, tatizo nini, diplomasia yetu imeyumba kwa kiasi gani mpaka pesa za MCC zimezuwa, aje ajibu hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda tu, lakini nilitaka nimshauri mambo mengi. Nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib Said Haji na baadaye Mheshimiwa Nagi Kaboyoka ajiandae.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nikuelezee tu kwamba moyo wangu unasikia burudani sana unapokaa kwenye Kiti hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu sana kunijalia na mimi leo kusema hapa. Pia nataka nimwombe dua zaidi kiongozi wetu wa Chama cha Wananchi CUF, Katibu Mkuu, Seif Sharif Hamad kwa majaribu anayokumbana nayo Wazanzibari na Watanzania wapenda haki wako sambamba na yeye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kila aliaye anashika kichwa chake, hashiki kichwa cha mwenzie. Tarehe 25 Julai, kama sikosei, mwaka 2011, nilisimama kwenye Bunge hili wakati huo ikiwa Wizara ya Afrika Mashariki nikilalamikia kitendo cha Jamhuri ya Kenya wanachowafanyia wananchi wetu wa Zanzibar wanaokuwepo Kenya wakishiriki katika shughuli za kujitafutia rizki kupitia njia ya uvuvi. Nililalamika hilo na Waziri aliyekuwepo wakati ule alifuatilia kiasi chake mambo yale yalitulia kwa kiasi lakini katika miaka ya karibuni masuala ya askari wa Kenya kuwakamata wavuvi kutoka Kisiwani Pemba kule Kenya ni suala ambalo linaonekana ni jambo la kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamekuwa yakitokea, hivi karibuni tu, nadhani miezi mitatu iliyopita, wananchi karibu 100 kutoka Visiwa vya Pemba, wengi wao wakitoka katika majimbo yetu ya Kaskazini, Wilaya ya Micheweni, Wete walishikiliwa pale na sababu za msingi za kuwashikilia watu wale hawana, tumekuwa tukilalamika sana. Balozi wetu wa Kenya, Balozi mdogo aliyeko Mombasa amekuwa akifuatilia mambo haya na wakati mwingine amekuwa akiambiwa hakuna hasa shtaka la kuwashtaki watu wale badala yake wanapigwa faini ambazo kwa bahati mbaya sana tunalazimika Wabunge sisi kutoka Zanzibar hasa kutoka Pemba, tuchangishane mifukoni mwetu kwenda

kuwagomboza watu wale kwa kuwalipia faini kubwa sana, haya mambo hayafai. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar tuko kwenye Muungano, hatuna Wizara wala hatuna utetezi wa moja kwa moja, lazima tupitie kwenu. Mliyafanya, mnayaweza lazima muyaweze. Kule Zanzibar asilimia 90 ya watandika vitanda kwenye hoteli za kitalii ni Wakenya, wala hawanyanyaswi. Kwa nini Wapemba wanapata tabu katika Jamhuri ya Kenya? Naomba sana, Mheshimiwa Waziri akija atuambie tumekosea nini, wavuvi wetu wanapokuwa katika Jamhuri ya Kenya wanapata matatizo makubwa na yanajirudia kila mwaka. Hili haliwezekani na hatutakubali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tufike mahali tuseme kunyanyasiwa watu wetu imetoshwa, raia wa Tanzania ana thamani sana. Kwa hiyo, kuwaacha Wazanzibari ambao sasa ni Watanzania wakiendelea kuteseka na Balozi yupo, Mheshimiwa Waziri afuatilie jambo hili, linatukera sana. Kama wameshindwa wafikirie upya Zanzibar kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki waone tutakavyotetea haki zetu kule. Hilo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka nizungumzie suala lingine la mahusiano. Tanzania imezuka aibu sana hasa kwa viongozi na watu wanaosimamia usalama wa nchi hii. Jambo dogo ugaidi, kuna ugaidi, kuna magaidi Amboni, kuna ugaidi Zanzibar, hii hatujengi! Neno ugaidi ukilitaja kwa watu wengine huko macho yao yanakaa hivi. Leo pale Zanzibar imetajwa ni kisiwa ambapo kuna magaidi yako mahakamani wakati hakuna tendo la ugaidi ambalo limewahi kufanyika Zanzibar, kama lipo litajeni! (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Sio sifa kutaja ugaidi wakati hakuna ugaidi. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Khatib. Tunaendelea na Mheshimiwa Nagi Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri Kivuli kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mimi naomba nizamie katika diplomasia ya kiuchumi. Naona nchi yetu tumeongelea hili tangu 2001 mpaka leo na inaelekea hata Mabalozi wetu hawajui katika diplomasia kiuchumi wanatakiwa wafanye nini. Tunaongea juu juu tu hatuzamii kusema diplomasia ya kiuchumi maana yake ni nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Waziri ni mwanadiplomasia sana lakini nasikitika kusema hotuba yake yote au sehemu kubwa imeenda katika mambo ya kisiasa kwa maana na diplomasia ya kiisiasa. Kwanza tuanzie karibu hapa nyumbani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, inasikitisha sana kuona Wabunge wetu wa Afrika Mashariki hawajui wanaripoti kwa nani au wako chini ya nani? Je wako chini ya Bunge hili au wako chini ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi hawana hata ofisi. Sasa unampaje mtu jukumu kubwa kuitwa Mbunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini hana hata Ofisi nyumbani kwake. Nchi ndogo kama Burundi wana ofisi za Wabunge wao wa Afrika Mashariki hata Rwanda na Kenya lakini Tanzania hatuna. Hii inaonesha jinsi Tanzania ambavyo tunachukulia mambo yetu kwa urahisi rahisi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu tuangalie, angalia shilingi yetu ya Tanzania na shilingi ya Kenya. Mpaka jana shilingi yetu ishirini na mbili ya Tanzania ndiyo unapata shilingi moja ya Kenya. Hivi wenzetu wametuzidi nini na tunazungumzia diplomasia ya kiuchumi. Mabalozi wetu wa East Africa wanajifunza nini au wanatuambia kwa nini wenzetu Kenya wanapiga hatua? Wakenya wako mbali sana angalia *supermarket* tu hata iliyoko Dar es Salaam, Mkenya ndiyo anaiendesha hata Kenya *Commercial Bank*, Tanzania Kenya tuna nini, Uganda tuna nini na Rwanda tuna nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ninachoshangaa kama tunazungumzia mambo ya diplomasia kiuchumi, nakumbuka Awamu ya Pili kule Saudia walieleza kwamba wanataka mbuzi wengi kwa vile watu wakienda Hija wanatumia sana nyama ya mbuzi. Watu wakaja hapa (Waarabu), Ubalozi wetu sijui ulifanya kazi yoyote kufuatilia suala lile lakini *foreign officers* wakapigapiga ikaishia hapo. Sasa hivi wenzetu wa Comoro ndiyo wanapeleka Uarabuni ng'ombe na mbuzi kutoka Tanzania. Tunaongelea diplomasia ya kiuchumi, uko wapi uchumi wetu tunaouzungumzia hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie wawekezaji, wanakuja wawekezaji sijui *Foreign Ministry* yetu inasaidiaje kuonyesha hawa wawekezaji kule kwao wana uwezo kiasi gani ili waweze kutushauri kwamba hao muwakubali kama wawekezaji au msiwakubali? Unakuta wawekezaji wengine wanakuja kukopa kwenye benki zetu hizi hizi, halafu unaambiwa ni mwekezaji huyu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi angalieni migodi yetu wageni kutoka nje wametawala migodi yetu Watanzania tunabakia kufanya kazi za vibarua. Wizara yetu ingeshauri kwamba hawa wawekezaji labda tuwape *position* moja, mbili hizi nyingine zote zibanwe na Watanzania. Watanzania mali yetu (*contribution*) yetu iwe ardhi yetu na wale wawekezaji waje na hela ili tuwe *equal partners*. Leo tunaongelea uchumi wa kidiplomasia lakini migodi yetu watu wetu ni kupigwa risasi kila siku na wageni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalieni hoteli zetu mfano Hoteli ya Serena na iliyokuwa inaitwa Kilimanjaro sijui sasa hivi imeshabadilishwa jina au bado.

MBUNGE FULANI: Inaitwa Hyatt.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Haya Hyatt. Hawa wenzetu wanapewa *grace period* kwamba msilipe kodi muangalie kwanza biashara, miaka mitano wakimaliza wanabadilisha jina leo Sheraton, kesho Serena sijui keshokutwa wataitwa nani? Tumekaa kimya, hiyo diplomasia kweli ya uchumi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie wawekezaji wanapewa umiliki wa mashamba kwa muda wa miaka 99, mwananchi sisi mpaka na watoto wetu hamna atakayekaa kushuhudia mkataba umeisha, tunawapa wawekezaji. Huko nchi za nje, je, kuna Mtanzania anakwenda apewe ardhi miaka 99? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa kwamba tumejivunia tunaletewa msaada wa pikipiki na Wachina, jamani juzi sijui miaka kumi iliyopita tuliletewa baiskeli wanakuja ku-*assemble* pikipiki kiwanda chetu cha jeshi pale Nyumbu ambacho kilikuwa kinatengeneza magari pale Kibaha, kingeombewa hela wangukuwa mbali siye tunarudi kwenye pikipiki. Pikipiki zitabeba mizigo gani, ndiyo diplomasia ya uwekezaji huo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vyuo vya ufundi, tumeenda kuomba hela, wakati nafanya *Danish Embassy* tulitengeneza Chuo cha Chang'ombe na Dodoma kwa *grant* leo tunaenda kuomba mikopo kurudi tena kutafuta *technical assistance* kutoka nje. Tunajivunia Italia wanatusaidia, hivi *Engineers* wetu wote kutoka chuo kikuu kutoka iliyokuwa *technical college* wameshindwa kusaidia kutengeneza VETA kweli mpaka twende tukaombe huko Italia? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba USD milioni 55 kujenga maghala, maghala mangapi tunayo yamewekwa uchafu hayawekwi hata mazao? Leo tunaomba USD milioni 55 msaada wa kujenga maghala, hivi kweli hata kujenga maghala jamani tushindwe nchi hii? Wenzetu wanatengeneza ndege wako mbali sisi bado tunatafuta msaada wa kujenga maghala? Hii diplomasia ya

kwamba tuna marafiki siyo urafiki siye ni ombaomba, hakuna urafiki na ombaomba. Ukiwa na rafiki kila siku yuko mlangoni kwako anaomba utasema huyo ni rafiki yangu siyo rafiki. Tumekuwa nchi ya ombaomba hata vile vitu tunavyoweza kutengeneza wenyewe, inatuaibisha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, anafuata Mheshimiwa Emmanuel Papien na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ajiandae.

MHE. EMMANUEL J. PAPIAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nampongeza Waziri mwenye dhamana na Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Mahiga kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia nawapongeza Mabalozi wetu kwa kazi nzuri wanazofanya huko nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu machache ni ushauri tu. Napenda kushauri Wizara ya Mambo ya Nje wakae na Mifuko ya Jamii. Vile viwanja vyetu vilivyoko nje ambavyo vinahitaji kujengwa wakae na Mifuko ya Jamii wapate pesa wajenge zile nyumba halafu zile pesa wanazolipa kwa maana ya zile nyumba wanazokodi waweze kulipa hiyo Mifuko na kurejesha ili tuweze kuwa na nyumba zetu kwenye Balozi zetu kote duniani ambapo tuna Balozi. Hilo ni jambo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili naomba Mheshimiwa Mahiga ajaribu kuhakikisha kwamba Mabalozi wetu tulionao nje ambao wanatusemea sisi wajitahidi kutafuta nafasi kwa ajili ya vijana wetu watoke nje waende kusoma, kutafuta washirika, misaada, matajiri walioko nje waweze kutu-support kusomesha watoto wetu katika vyuo vikuu vya nje ili waweze kutusaidia. (Makofi)

*(Hapa kulikuwa na mwangwi kutoka
kwenye kipaza sauti cha mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba uhamie sehemu nyingine.

MBUNGE FULANI: Hamia hapa.

MHE. EMMANUEL J. PAPIAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nataka kuzungumzia Chuo cha Diplomasia, napenda kushauri Wizara ijitahidi kuona ni namna gani inaweza kufanya *training* kwa ajili ya viongozi wetu hata wale wa kisiasa ambao tuko humu Bungeni. Watuletee wataalam tuelimishwe tujue namna gani ya kuishi kwenye mazingira haya ya kidiplomasia kwa maana tujue namna gani ku-behave kwenye *community* nje ya hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine nataka kushauri Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, soko letu la *East Africa* ni kubwa sana, lakini naomba niseme kuna *challenge* kubwa sana kwenye *East Africa* ambayo Tanzania haiendani na nchi nyingine. Ukiangalia kwa mfano Kiwanda cha Maziwa Musoma kilikuwa kinapeleka maziwa Kenya, kilipigwa mizengwe mpaka kikafa lakini leo Kenya ina-import maziwa Tanzania na tunakunywa. Unaweza ku-imagine ni namna gani nchi nyingine ndani ya *East Africa* zinajaribu kuhakikisha kwamba wawekezaji wao, biashara zao, sisi Tanzania ni *market* kwao lakini sisi kupeleka kwao inakuwa ni ngumu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo ukipeleka mahindi Kenya lazima upitishie kwa mtu mmoja anunue hayo mahindi hakuna mtu mwingine mpaka yeye anunue. Mkenya akitoka Kenya kuja hapa lazima aingie Kiteto anunue kwa mkulima aende Hanang, Simanjiro, Iringa hakuna *control*, *it means* wao wako aware.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Wizara hii ijaribu ku-create watu ambao ni *business attaché* kwenye hizo *embassies*, wawe aware, waangalie ni namna gani ya ku-control wale watu wanaokuja lakini na wale watu ambao wako kule ili wananchi wetu waweze kupeleka biashara huko na sisi bidhaa zetu ziuzike huko kama ambavyo bidhaa zao zinavyoweza kuuzika hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa Wizara hii wanafanya lakini liko jambo moja nimejiuliza nikashindwa kupata majibu. Kama miaka miwili iliyopita magari yetu mengi yalikuwa yanapeleka mizigo Congo, Rwanda na Burundi. Leo naomba niwape swali moja jepesi, ukitoka Dar es Salaam kukanyaga Dodoma unakutana na magari ya Rwanda zaidi ya mia, nimejiuliza ni kwa nini? Sisi wakati tunapeleka ile mizigo madereva wetu walikuwa wana kazi, *turnboy* kazi, magari yetu yanakunywa mafuta hapa, *creation* ya *employment* ipo, sasa leo kwa sababu ya kushindwa kukabiliana na uwezo wa kupeleka mizigo, kuleta mizengwe mizengwe hapa katikati tumesababisha na kuwaamsha wale sasa wako kikazi zaidi. Hebu jiulizeni tumepoteza shilingi ngapi kwenye nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe na kuwashauri mjaribu kuwa watu wa kukabiliana na hali ya soko, tuko kwenye *East Africa*, soko linatosha, *opportunities* zilizopo nyie ndiyo mnatakiwa mtuambie kuna hili, fanyeni hili ili Watanzania wetu waweze ku-benefit kwenye hizi nchi ambazo sisi ni Wanajumuiya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri jambo lingine. Huko nje Mabalozi wetu wanazo kazi lakini kazi kubwa ambayo wanatakiwa kuifanya sasa ni ya ku-market Tanzania kwa maana ya uwekezaji, kwa maana ya kututafutia mashirika makubwa na ku-monitor pesa zao zinakuja kufanya nini

hapa. Hawa watu wanaokuja kwa kujipenyeza tutashtukia siku nyingine watu wanaingiza pesa hapa, wananyonya uchumi wetu na hatujui na wanajiita wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *laundry money* zitatembea hapa, uchumi na shilingi yetu itashuka, Watanzania tutabaki maskini wenzetu wakichakachua pesa. Niombe Waziri mwenye dhamana na Mabalizi wetu wajaribu kusimamia hili, waliangalie kwa ukaribu na wajitahidi kuhakikisha kwamba nchi yetu haipotezi na sisi tuna-benefit kutokana na hizo nchi ambazo wao wanaziwakilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niwashukuru sana, niwaombe kwa jinsi wanavyoweza wajitahidi kufanya kazi hiyo. Watu wanabeza kwamba Tanzania haijafanya kitu, hatuwezi ushirikiano, hatuwezi umoja, hebu angalieni siku ya kukumbuka Uhuru wetu wageni wa kimataifa wanaokuja kushangilia nchi yetu. Hii ni *indication* kwamba Tanzania ina heshima ndani ya Afrika, ina heshima ndani ya dunia, kubali usikubali Tanzania kuna kitu imefanya katika *investment* ya umoja na *diplomacy* ndani ya dunia hii. Niwaombe mnaotubeza na nyie njooni na njia mbadala ya kutuambia tutoke hapa twende vipi badala ya kubeza yale ambayo tumekwishayafanya, hongereni sana kama Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na Mheshimiwa Susan Lyimo ajiandae.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje ina mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi, ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Wizara hii ina wajibu mkubwa sana wa kutafuta wawekezaji walio makini, kutafuta wataalam na kujenga mahusiano kati ya nchi yetu na Mataifa ya nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza jambo hili kwa sababu kama kuna tishio kubwa la usalama wa Taifa letu na usalama wa Mataifa basi umaskini duniani ndiyo tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, tunaitarajia Wizara ya Mambo ya Nje itekeleze wajibu huo kwa weledi ili nchi yetu iweze kupata matarajio hayo tunayoyatarajia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje imejitahidi kuwaunganisha na kuwashajihisha Watanzania wanaoishi nchi za nje kuwekeza ndani ya nchi yetu, kuleta utaalum na kutoa ushauri katika mambo ya kitaalam.

Kwa bahati mbaya kidogo, mchango wa Watanzania hao waliutoa si mkubwa wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa na ametueleza mchango ambao Watanzania walio nje waliutoa kwa nchi yetu ni takribani shilingi za Tanzania bilioni 36. Fedha hizi kwa maoni yangu ni kidogo sana ukilinganisha na wenzetu. Labda nitoe mfano wa wenzetu wa Kenya, mchango wa Wakenya wanaoishi nje ya nchi yao ni takribani dola bilioni moja. Kwa mnasaba huo basi nasema tunayo kazi ya ziada ya kuifanya ili kuwashajiisha Watanzania hawa waweze kutoa mchango mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa katika Bunge hili katika Bunge lililopita, moja ya malalamiko makubwa sana ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaeleza ni mikataba yetu mingi ambayo tunaingia si mizuri. Kwa utafiti usio wa kina sana inaelekea utaalamu wetu katika kuingia makubaliano ya mikataba si wa kiwango cha juu sana. Kwa hiyo, naishauri Wizara ya Mambo ya Nje ifanye kila linalowezekana kukisaidia Chuo chetu cha Diplomasia ili kiweze kutoa mafunzo mazuri ya *international negotiation*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikifuatilia mara nyingi utendaji wa Mashirika ya Kimataifa, najua Waheshimiwa Mabalozi wamefanya kazi nzuri sana nje ya nchi huko, lakini kama tutafanya ulinganisho wa mchango ambao Watanzania tumeutoa katika Mashirika ya Kimataifa, ukilinganisha na nchi kama Ghana, Senegal na Kenya, wataalam wanaofanya kazi katika mashirika hayo Watanzania ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, ukiwa huna wana diplomasia wa kutosha kwenye mashirika hayo, itakuwa vigumu sana kuweza kuwavutia watu wengine ndani ya nchi hata nafasi hizo zikitoka Watanzania wanakuwa hawapati taarifa za kutosha. Kwa hiyo, naishauri Wizara ifanye kila linalowezekana, kwanza tuwape Watanzania mafunzo ya kutosha lakini tuhakikishe kwamba Watanzania wengi zaidi wanafanya kazi katika Mashirika ya Kimataifa ili wawe chachu na wafungue milango kwa Watanzania wengine ambao wangependa kupata fursa hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kwa bahati nzuri mimi ni miongoni mwa wanafunzi ambao walipitia Chuo cha Kidiplomasia na Mheshimiwa Shahari ni miongoni mwa Walimu ambao walitufundisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana inaonekana kama Chuo cha Diplomasia pamoja na mchango wake katika kuandaa Mabalozi na Maafisa wa Ushirikiano wa Kimataifa, Serikali haikiendelezi kiasi cha kutosha. Serikali na Wizara ya Mambo ya Nje imekuwa ikishauriwa kwa miaka mingi kukiimarisha Chuo cha Diplomasia kwa kukipatia vifaa na wataalam lakini pia

kukipatia eneo ambapo chuo hiki kinaweza kikatanuliwa ili kiweze kutoa fursa nyingi zaidi. Kwa bahati mbaya takriban miaka kumi na tano eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya chuo hicho bado halijaendelezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Mambo ya Nje ikiunganishe Chuo cha Kidiplomasia na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kunyanyua hadhi yake. Kama ilivyo Taasisi ya Diplomasia na Ushirikiano wa Kimataifa Nairobi ilivyounganishwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Lyimo na baadaye Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Hafidh Ali, dakika tano tano wajiandae.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana. Awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Msigwa kwa hotuba yake nzuri sana pamoja na kwamba wengine imewakwaza lakini kwetu ni nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na jambo ambalo limezungumzwa sana na niseme kwamba *last time* nilikuwa kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, suala la Chuo cha Diplomasia ni la msingi sana, wamezungumza wengi lakini naomba niende kwa maswali tu. Chuo hiki kilikuwa kipanuliwe na eneo walikuwa wanafuatilia kule Bagamoyo. Nataka Waziri anapokuja kujumuisha atuambie suala hilo limeishia wapi maana silioni mahali popote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la *diaspora*, ni jambo la kusikitisha sana. Bahati nzuri nimeangalia hotuba ya mwaka juzi, ya mwaka jana, hotuba ya mwaka 2014 inaonesha kwamba walikuwa wanafanya utafiti kujua Watanzania wangapi wanaishi nchi za nje, *two years ago*. Leo Mheshimiwa Waziri anatuletea taarifa kwamba Watanzania waishio nchi za nje wanakadiriwa kuwa zaidi ya milioni moja. Tulitaka kujua idadi kamili ni wangapi ili tujue ni kiasi gani wanaweza kuleta nchini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Nigeria leo inaingiza dola za kimarekani bilioni 21. Sawa Nigeria ina watu wengi lakini Kenya jirani zetu, bilioni 1.4 mwaka 2015, Tanzania wanaingiza kiasi gani, hatuna kiasi. Kwa hiyo, kama walivyosema wenzangu nadhani hii Wizara diplomasia iko kisiasa zaidi lakini haiko kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine na tulilizungumza sana ni suala la kuhakikisha kwamba Mabalizi wetu wote walioko nje ya nchi wanakuwa angalau na mkutano mmoja ili wajue huko kwingine kuna fursa kiasi gani wakae pamoja wapeane taarifa. Nina taarifa kwamba nchi nyingine wanafanya hivyo, nimekuwa Finland nimeona kila tarehe fulani Mabalizi wa nchi zote wa Finland wanarudi nyumbani ili kutoa *feedback* ya mambo gani au changamoto gani wanakutana nazo na fursa gani wanakutana nazo. Hapa Tanzania tuna utaratibu gani, ni mwaka gani Mabalizi wetu wote wamewahi kuitwa wakakutana ili angalau wazungumzie fursa na changamoto wanazozikabili ili tuone nchi yetu inaendelea kiuchumi zaidi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha, nimepitia kitabu cha maendeleo, Wizara kubwa namna hii ina shilingi bilioni nane (8) tu fedha za maendeleo, *unless* kuna fedha nyingine. Ukiangalia hotuba ya Waziri anazungumzia suala la kupanua Balozi, kwa fedha zipi? Hizi ambazo tunazo tumeshindwa, ukienda kwenye Ubalizi wa Zambia ni matatizo, ukienda kwenye Balozi nyingine nyingi ni matatizo, bahati nzuri tumekwenda, ni matatizo makubwa, mpaka hata Ubalizi wetu Marekani ni shida. Kama mwenzetu Idd Amin aliweza kujenga jengo kubwa sana pale New York Tanzania tumeshindwa na alijenga miaka ile, ni jambo la kusikitisha, tunaendelea kupanga. Tulisema ni kwa nini makampuni kama *NSSF*, *NHC* wasiingie ubia na Serikali kupitia Wizara hii ili waweze kujenga nyumba huko nje lakini naona jambo hili nalo limekufa kifo cha kishujaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma akiwa Waziri Membre mwaka 2014 na huko nyuma tuliongelea sana suala la *dual citizenship* (uraia pacha) lakini leo halionekani mahali popote na ni kama vile limekufa. Mheshimiwa Waziri anajua watu kwenye *Diaspora* walilalamikia sana suala hili la uraia pacha na tukawa tumeambiwa na Mheshimiwa Membre kwamba jambo hili linafanyiwa utafiti, litaendelea kushughulikiwa na litaingizwa kwenye Katiba iliyokuwa inapendekezwa lakini leo hakuna kitu, sasa tuwaeleweje jamani? Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba tujue *status* ya uraia pacha ikoje sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumza ni kwenye masuala ya ndoa. Tunajua kwamba ukiwa mwanaume Mtanzania, ukioa raia wa nje *automatically* yule mama anakuwa raia wa Tanzania lakini mwanamke wa Kitanzania akiolewa na mzungu au mtu mwingine ni tatizo kubwa. Sasa tunaomba kujua hii *double standard* inakuwaje kwa sababu hawa akinamama wananyimwa haki yao ya msingi. Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la mji (dinosaur). Wizara hii pamoja na mambo mengine inashughulikia pia masuala ya kiutalii, huduma za jamii, elimu na kila kitu. Tuliambiwa kwamba yule *dinosaur* akiletwa hapa kwenye hili jengo hataenea, hiyo siyo *issue* yetu wala

siyo hoja. Hoja ya msingi tunataka kujua, toka huyu mjusi amepolekwa huko Ujerumani ameingiza kiasi gani na Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii wana utaratibu gani kuhakikisha kwamba tunapata fedha? Suala kwamba hakuna jengo la kuweza kumweka halituhusu, ilitakiwa Serikali ihakikishe kwamba inatafuta sehemu ambapo huyo mjusi akija atawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tupoteze fedha nyingi hivyo za kutoka nje, watu wanaenda pale maelfu kwa maelfu kumwangukia yule mjusi lakini Watanzania hatupati chochote. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii wa-*make sure* kwamba wanatuletea utaratibu kidiplomasia ni jinsi gani huyo mjusi ama analetwa au Tanzania tunapata kiasi gani na hicho kiasi hakianzii leo, kinaanzia miaka hiyo waliyompeleka? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilizungumzwa sana hapa Bungeni na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi mpaka maskini na Ubunge hajakata. Kwa hiyo, ili kumuenzi mwenzetu hebu tuhakikishe hili jambo linafikia mwisho wake. Bahati nzuri ni Mbunge wa CCM kwa hiyo naamini suala hili litashughulikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee suala la itifaki. Siku za nyuma Bunge jipya linapozinduliwa tunakuwa na semina ya masuala ya itifaki ili Waheshimiwa Wabunge waelewe ni mambo gani yanatakiwa na yanakatazwa na tulikuwa tunaletwa *Chief of Protocol* anatupa semina. Sasa hivi utaona mtu amevaa suti bado ina *label* anaingia Bungeni anaenda popote, utaona mtu ana begi lake bado lina *nylon* yuko nalo tu. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo kwa kweli kama Wabunge tunapaswa kuyajua siyo tu hapa na Wabunge wengi wanasafiri nje, wanaenda hivyo hivyo. Kwa hiyo, nadhani ni wakati muafaka watuhakikishe kwamba hilo jambo linafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala la mtangamano wa Afrika Mashariki. Nilikuwa naangalia hivi ni lini tutafikia huo mtangamano wa Shirikisho la Afrika Mashariki kama kila leo tunaongeza nchi. Mimi najua kuna wengine wakiulizwa ni nchi ngapi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki watasema ni tatu, nne, tano na wengine watasema sita. Naomba kujua Sudan tayari imeshakuwa *member* au haijawa, maana yake mimi hata sijui. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaangalia vigezo gani, maana nilikuwa nafikiri, pamoja na *geographical location* lakini vilevile masuala mazima ya tabia yaangaliwe. Kwa hiyo, nadhani imefika wakati sasa tuangalie mambo haya. Pia napenda kujua ni nani wanaotoa kibali cha nchi kuwa ndani ya shirikisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lyimo. Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck na Mheshimiwa Khadija ajiandae.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nianze kwanza na hoja zilizochangiwa na upande wa Upinzani, kila Wizara inayokuja hapa Wazanzibari wanataja Maalim Seif, Maalim Seif, Maalim Seif. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Waheshimiwa Wabunge, sisi ni watu wazima, tumechaguliwa na wananchi ili tuje tuwatetee siyo kumlilia mtu na familia yake. Ninachosikitika zaidi kuna wababa wenye jinsia kama mimi wanamlilia baba mwenzao siwaelewi. (Kicheko)

MBUNGE FULANI: Taarifa Mwenyekiti.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Goodluck naomba utumie lugha nzuri tafadhali.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Ahsante.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MBUNGE FULANI: Rais wetu sisi ni Maalim Seif.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala la pili, sasa hivi kumekuwa na ugumu...

MBUNGE FULANI: Mwenyekiti mwache aseme saizi yetu siye huyo.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Kumekuwa na ugumu Watanzania kupata viza za kwenda China. Ukitaka viza ya China inachukua hadi wiki tatu kuipata, ukiuliza sababu wanasema Watanzania wanafanya uhalifu China. Naomba niulize Watanzania wanaoishi China na Wachina wanaoishi Tanzania wapi wanaofanya uhalifu? Sasa hivi kuna maji feki, matunda feki, mayai feki na maziwa feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Wachina walioko Tanzania hawafiki hata robo ya Watanzania walioko China kwa nini Wizara wa Mambo ya Nje inakubali na inasimamia unyanyasaji wa namna hii kwa Watanzania? Kila leo tunasikia wanafungwa, sisi tukiwakamata Wachina siku ya pili tunawarudisha kwao, mbona hao wanaokamatwa China hawarudishwi huku? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hilo hilo, kupata viza ya kwenda Uingereza ni zaidi ya kwenda peponi.

MBUNGE FULANI: Kabisa, kabisa.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Ukitaka viza ya Uingereza kuna manyanyaso sijui mpaka upate mwaliko, mbona wazungu wakija huku mnawagongea visa *airport* pale hamuwahoji wanakuja kufanya nini? Hiyo ni kero kubwa, naomba Waziri wa Mambo ya Nje alitolee ufafanuzi, kwa nini Watanzania tunapotaka kwenda nje tunanyanyaswa kwani sisi hatuwezi kwenda kutembea Uingereza, kwani hakuna watu wenye uwezo wa kwenda kutembea huko, mbona mnatuwekea matuta mengi tunapotaka kwenda Uingereza? Waziri naomba alisimamie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanatoka nchi za nje ili mradi wawe wazungu hata nauli za kujia Tanzania wamekopa, lakini nashangaa Wizara ya Mambo ya Nje inakuja baadaye inawabadilisha wale watu wanakuwa wawekezaji. Tena wawakezaji hao wanadhaminiwa na nchi yetu wanakwenda kukopa kwenye benki zao kwa kutumia ardhi yetu huku Wizara ya Mambo ya Nje ikiwa inaangalia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba aliangalie na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la lingine ni la uraia pacha, limezungumzwa tangu nikiwa mdogo, uraia pacha, uraia pacha. Hivi kuna ugumu gani katika suala hili la uraia pacha? Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni madhara gani tutapata kutokana na Watanzania kuwa na uraia pacha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumziwa suala la mjiusi, naona Wabunge wengi wanapiga kona. Mimi nitajitolea kama kuna ugumu wa kumsafirisha huyo mjiusi kumleta Tanzania, nitakubali posho zangu zikatwe mjiusi arudishwe. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi, hayo tu yananitoshia. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Hafidh Ali atamalizia.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane tafadhali.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami napenda kuipongeza Wizara hii ya Mambo Nchi za Nje kwa juhudi kubwa inayofanya pamoja na Mabalozi wetu walioko nchi za nje wanaoiwakilisha Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Balozi zetu zilizoko nchi za nje zinafanya kazi kubwa wakati fedha zinazopelekwa ni chache ukiachilia mbali kucheleweshwa kwa baadhi ya mahitaji yao. Pia Balozi zinafanya kazi kubwa kuwapokea Watanzania wanaopata matatizo wakiwa nje ya nchi mfano kama Oman, India, Marekani, Uingereza ambapo wengi wao huenda kwa sababu zao binafsi kama kutafuta ajira baadaye kutelekezwa na waajiri wao, wengine wanakwenda kwa matibabu wanaishiwa fedha na wanakimbilia kwenye Balozi zetu za Tanzania na Balozi zinafanya kila jitihada kuhakikisha wananchi hao wanarejea Tanzania. Napenda kuzipongeza sana Balozi zetu zilizoko nchi za nje kwa uvumilivu wao huu na upendo kwa Watanzania wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri tumearifiwa kwamba Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki imehamia rasmi Zanzibar. Mimi napenda tu kusisitiza kwamba Kamisheni hii ipewe kipaumbele cha vitendea kazi ili iweze kufanya kazi zake vizuri. Kwa sababu kwa kutumia lugha yetu ya Kiswahili tutaongeza ajira kwa vijana wetu, pato la Taifa na tutaitangaza nchi yetu Tanzania duniani kote. Kwa hivyo, kuamua Kiswahili makao makuu yake kuwa ndani ya nchi yetu ya Tanzania ni fahari kwetu sote Watanzania katika umoja huu wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuliongelea sasa hivi ni elimu juu ya fursa za kiuchumi na biashara katika masoko ya Afrika Mashariki. Wananchi wetu wa Tanzania wengi hawaelewi ni mbinu gani na njia gani za kufanya biashara katika masoko hayo ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulizungumza hapa kwa mashirikiano ya pamoja kwa Wizara hii ya Mambo ya Nje na Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha wanadhibiti wasafiri Watanzania na abiria wengine wanaopitia Tanzania kupitia viwanja vyetu vya ndege kwa usafirishaji wa madawa ya kulevya. Tatizo hili linalipa aibu sana Taifa letu wanapokwenda nchi za nje tukaambiwa watu hawa wametokea Tanzania au ni raia wa Tanzania. Udhibiti ufanyike pale kwenye viwanja vyetu vya ndege, madawa haya ya kulevya yasitokee nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba kwa Mabalizi wetu walioko nchi za nje watumie fursa hiyo kuitangaza Tanzania na kutafuta mialiko mbalimbali kama matamasha ya kiutamaduni na biashara yanayokuweco katika nchi hizo wawalete Tanzania ili wananchi wetu waweze kufika huko. Hili nina ushahidi nalo kwa sababu mimi mwenyewe nilishawahi kuwa Naibu Mkurugenzi wa Utamaduni na Mambo ya Sanaa nilikuwa natafuta mwenyewe mialiko kwa viongozi na wasanii kutoka Zanzibar kwenda kuitangaza Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapofika katika baadhi ya Balozi na vikundi vyangu vya utamaduni hata wao wanakuwa hawaelewi kwamba kuna fursa za namna hiyo katika nchi zao. Kwa hiyo, ninachoomba wafanye utafiti na wawe wanatafuta mialiko kama hiyo ya maonesho mbalimbali ili Watanzania waweze kushiriki na kuitangaza nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khadija.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hafidh Ali tutamalizia na Mheshimiwa Keissy.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ndogo ya kutoa mchango mdogo nilionao katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka Wizara ifahamu kwamba Wizara hii kwa nchi za nje ndiyo jicho la Tanzania. Tunapotaka Balozi zetu zifanye vizuri basi Tanzania ndipo itakapoweza kujitosheleza katika kuonesha kwamba na wao wamo katika sura ya ulimwengu. Hata hivyo, kama Wizara hii haikufanya bidii katika kuhamasisha na kuziweka Balozi zetu vizuri kazi tunayoifanya itakuwa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na hilo kwa sababu kuna matatizo mengi ambayo yanazikabili Balozi zetu hivi sasa ukiachilia mambo ya utendaji, lakini kuna tatizo sugu la wafanyakazi wanaostaafu kutorudishwa nyumbani, hawapewi marupurupu yao lakini wafanyakazi wengine wanatoa sababu ambazo hazina msingi kwa kusingizia wana watoto wanasomesha walipofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ichukue hatua, kama wanaweza kuwastaafisha wafanyakazi wawastaafishe, wawalipe haki zao na warudishwe nyumbani. Kama hawawezi wasiwastaafishe na kutoa tamko rasmi kwamba wafanyakazi hao bado ni wafanyakazi katika Balozi zetu. Hili ni tatizo kubwa katika Balozi zetu na lazima Wizara ichukue hatua kuhusiana na wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili limezungumzwa sana hapa nalo ni suala la majengo. Majengo ya Balozi za Tanzania ni aibu. Usije ukajaribu kwenda Maputo au Zambia utaona aibu sana. Kwa nini tunachuka hatua za kutokuwapa pesa Mabalozi wetu katika Balozi mbalimbali lakini wakati huo huo Wizara hii utasikia wanataka kuongeza Balozi nyingine katika nchi za nje. Tuhishe hizi zilizokuwepo halafu tutafute nyingine, tusijitangaze tunataka kufungua Balozi nyingine wakati tulizokuwa nazo hatuwezi kuzihudumia. Hili ni tatizo kubwa ambalo linawapeleka wafanyakazi katika Balozi zetu kuonekana kwamba labda wao ni ombaomba na kama hawawezi kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine namwomba sana Mheshimiwa Waziri wakati umefika hivi sasa Balozi zetu kupewa nafasi ili ziweze kujitetea katika bajeti zao. Bajeti zinazopelekwa kule ni finyu kutokana na kazi ambazo wanafanya kwa sababu hakuna mtu ambaye anashirikishwa katika kutetea bajeti za Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tarehe 22 Aprili, katika Bunge lako hili nilikuwa nimezungumzia suala linalotia aibu Tanzania na linalotia aibu Balozi zetu nje ya nchi. Wakati nilipokuwa nauliza swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwa kufyatua tu jambo ambalo mimi halikuniridhisha na mpango wa kufyatuliana majawabu katika Bunge hili unakuwa haupendezi. Tunapouliza mambo ya msingi tujibiwe kimsingi na ukweli ulivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia deni la Tanzania katika hospitali moja kule London inayoitwa *London Bridge* ambapo kuna *pound* 79,000 zinazodaiwa Tanzania na narudia tena inadaiwa Tanzania. Kilichojitokeza hapa kuna Mtanzania mmoja anatokea Zanzibar alifanyiwa matibabu London kaenda bila kujulikana na mtu yeyote lakini Ubalozi ulichukua hatua ya kumpa matibabu Mtanzania yule. Hospitali imepeleka barua ya gharama katika Ubalozi wetu London na Ubalozi umepeleka barua katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Hafidh muda wako umemalizika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Naomba tumalizie na Mheshimiwa Keissy na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini akae tayari.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi kwa dakika tano nizungumze kuhusu Wizara muhimu sana, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ambayo inahusiana na ushirikiano wa nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyozungumza wenzangu kuhusu Ubalozi wetu mdogo pale Lubumbashi, madereva na wafanyabiashara wetu wanapata tabu sana pale. Ubalozi mdogo Lubumbashi ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchumi wa nchi yetu Congo ni muhimu sana kuliko Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuikamata Congo kwa sababu ni nchi kubwa, ina watu wengi na ina kila kitu itasaidia sana uchumi wa nchi yetu na tukiimarisha reli ya kati. Niliomba siku nyingi na nilipokuwa Kamati ya PAC tuliomba Ubalozi mdogo Lubumbashi na kama haiwezekani tumtafute Mtanzania yeyote ambaye yupo pale apewe hadhi ya kibalozi kusaidia wananchi wetu wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Muungano. Yupo Mbunge anazungumzia mambo ya ajabu kabisa kwamba tumewapunja, sheria ya masuala haya ya mambo ya nje lazima Waziri mmoja atoke Zanzibar sijui Waziri wa Mambo ya Ndani atoke Zanzibar. Ndugu zangu tuna Mawaziri watatu muhimu, Waziri wa Ulinzi katoka Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, tuna Wizara kubwa ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano chini ya Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Naibu Waziri yupo hapa Mheshimiwa Masauni bado mnataka nini zaidi? Ndugu zangu tukitaka hivyo hata sisi tutasema, kwa mujibu wa *population* ni *four percent*. Hata mimi Rukwa nitasema tunataka Waziri maana hatuna Waziri na tuna idadi ya watu kama Zanzibar mbona hatuna Waziri hata Naibu Waziri na hatulalamiki hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuja kulalamika hata Rais akitaka kwenda nje awachukue Wazanzibari. Rais Magufuli anasema safari za nje hakuna unakuja Bungeni unataka safari za nje, hakuna tegemea pesa zako uende nje. Tusianze kuleta mambo ambayo hayatakiwi kwenye Muungano, tumeshaungana ndiyo hivyo hivyo, sasa ninyi mnataka nusu kwa nusu ndugu zangu? Itawezekana wapi? Haiwezekani ndugu yangu! Nusu kwa nusu haiwezekani! Ninyi mpo *four percent* mtapata *four percent* ya kila kitu. *(Makofi)*

MHE. KHATIB SAID HAJI: Hivyo hivyo!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Khatib tulia, usipige kelele hapa kwamba mnataka Mabalozi wengi, hapana! Nchi yote tuna Mabalozi 21 mkipata hata Naibu Mabalozi shukuru Mungu. Mheshimiwa Khatib tukikuambia ulipie Balozi mmoja tu nchi yako italipa gharama ya Balozi kule nje? *(Kicheko/Makofi)*

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Tulieni! Hatuwezi kwenda hivyo unasimama hapa unasema sisi tumepunjwa, hamkupunjwa kitu bado tumewasaidia. Bungeni hapa mmekuja 54, mngejaa kule Zanzibar mngeenea kwenye Jimbo ninyi Ma-CUF, mngeweza kuenea kule kweli? Tukiwaambia tu sasa hivi nendeni kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine amezungumzia ndugu yangu, mimi nilikuwa kwenye Kamati ya PAC kuhusu mgonjwa kutoka Zanzibar, mgonjwa yule alipelekwa na Serikali ya Zanzibar hakuna kukanusha hapa. Nilikuwa mjumbe wa *Public Accounts Committee*, mgonjwa yule alipelekwa na Serikali ya Zanzibar na atahudumiwa na Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Tanganyika ilisema ahudumiwe kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafahamu kwa sababu nilikuwa mjumbe wa *Public Accounts Committee* hesabu hizi zilikuja kwetu. Huyu bwana alipelekwa na Serikali ya Zanzibar akatibiwe kule, Wizara ya Afya siyo ya Muungano. Kwa hiyo, hili deni ni la Serikali ya Zanzibar likadaiwe huko huko, hatuwezi kulipa sisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndugu zangu tusiende papara kwa habari za kutaka zaidi vyeo au namna gani na sisi tutadai vyeo. Rais anapanga Mawaziri kutokana na jinsi anavyotaka yeye huwezi kumlazimisha awape Zanzibar Mawaziri 10 au 15, ninyi kwanza kule kwenu mna Mawaziri zaidi ya 20, mna Wabunge kule kwenu hawatoshi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine na nimezungumza mara nyingi hapa, Wizara ambazo siyo za Muungano muwe mnatungoja nje tunabaki peke yetu hapa tukimaliza za Muungano ndiyo tunawaita mnaingia ndani. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani uje kuchangia Wizara ya Kilimo inakuhusu? Wizara ya Maji inakuhusu. Kwa hiyo, muwe mnachagua Wizara za kuchangia kuanzia sasa, changia Wizara inayokuhusu basi Wizara nyingine tuachiaeni wenyewe. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante muda wako umekwisha.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Tunaendelea.

MBUNGE FULANI: Message imefika.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nipongeze jitihada zinazofanyika katika kuanzisha Vituo vya Pamoja vya Utoaji Huduma Mipakani (OSBP). Kituo cha Horohoro/Lungalunga ni miongoni mwa vituo vilivyokamilika. Hata hivyo, kituo hiki kinakabiliwa na tatizo kubwa la maji. Kituo hiki kimejengwa upande wa Tanzania eneo ambalo kuna tatizo kubwa la maji kiasi kwamba wananchi wanalazimika kufuata huduma ya maji umbali mrefu upande wa Kenya. Halmashauri ya Mkinga imejitahidi kuibua miradi itakayokuwa suluhisho la tatizo la maji katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari ripoti ya *detailed design* imepatikana ikionesha kuwa mradi huu unahitaji kiasi cha takribani shilingi bilioni sita na nusu. Halmashauri ya Mkinga haina uwezo wa kifedha wa kujenga mradi huu. Nashauri Wizara ya Mambo ya Nje ichukue mradi huu kwa kutafuta fedha toka vyanzo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki au ufadhili mwingine wowote utakaowezesha kutekelezwa kwa mradi huu. Itakuwa jambo la aibu endapo kituo hiki kitafunguliwa bila ya kuwepo jawabu la utatuzi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni *European Union* kushinikiza nchi za kiafrika kutia saini mkataba ujulikanao kama *Economic Partnership Agreement*. Mkataba huu ni mbovu na una madhara makubwa kiuchumi kwa nchi za kiafrika Tanzania ikiwemo. Taifa linapaswa kuwa na tahadhari kubwa na mkataba huu hususan sasa ambapo kama Taifa tumedhamiria nchi yetu kuwa nchi ya uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke wazi ndani ya Bunge hili msimamo wetu kama nchi kuhusiana na jambo hili. Waziri atakapokuwa anafanya

majumuisho alieleze Bunge lako ni kwa vipi nchi yetu itaachana na mkataba huu wa kinyonyaji. Wizara ilishirikishe mapema Bunge katika kufahamu kwa undani suala hili la EPA ili Wabunge wawe na uelewa mpana utakaowawezesha kufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Buyungu, Wilaya ya Kakonko bado kuna migogoro midogo midogo ya wananchi wanaoingia Burundi na Warundi wanaoingia Tanzania, wanapata usumbufu wa hapa na pale hasa ule wa polisi. Wilaya imepakana na Burundi kwa eneo lote la Magharibi yaani Vijiji vya Mugunzu/Kiduduye, Katanga, Ihabiro, Gwanumpu, Bukirilo, Malenga/Kikulezo, Kiga, Kasuga, Nyakeyenzi, Muhange, Gwarama/Kabare, Nyakibuye, Rumeshi, Kinyinya na Nyanzige (Kata ya Nyamtukiza).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi hawa wanapata usumbufu kwenda kuuza au kununua mazao/biashara Burundi. Wananchi hawa wanakamatwa na polisi na kunyanga'anywa bidhaa na fedha bila sababu. Aidha, Warundi nao wananyanyaswa na polisi na kuibiwa/kunyang'anywa pesa/bidhaa wanazouza au kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri yafuatayo:-

- (i) Umoja wetu wa Afrika Mashariki uwanufaishe wadau wa nchi wanachama;
- (ii) Polisi wazuiliwe kuwaonea na kuwanyang'anya Warundi bidhaa toka Burundi mfano kama bia za *Primus*, *Amstel*, sabuni na kadhalika; na
- (iii) Masoko ya mipakani (Burundi/Tanzania) yasiwekewe vikwazo vya nani/nini uuze/ununue kutoka nchi zetu za Burundi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaifa nina ushauri ufuatao:-

- (i) Viza za nchi zote zenye Mabalozi hapa nchini zitolewe humu nchini bila urasimu kama za Uingereza zinatolewa South Africa;
- (ii) Mabalozi/ofisi za Tanzania nje ya nchi watangaze vivutio vya utalii vilivyopo hapa nchini kama vile hoteli za kitalii, mbuga za wanyama, Mlima Kilimanjaro na kadhalika. Mfano miaka ya 2005-2008 Uingereza hapakuwa na matangazo ya kutosha kwa watalii kuja Tanzania na hata hoteli zilizoonekana ni za Kenya na Zanzibar tu. Mlima Kilimanjaro uliendelea kujulikana kama upo nchi ya Kenya; na

(iii) Afrika Mashariki haijatulia hasa viongozi wa nchi pale wanapogombania rasilimali zinazopatikana nchi moja au nyingine. Kwa mfano mafuta ya Uganda kuletwa Tanzania, Kenya haifurahi, reli kwenda Rwanda toka Tanzania baadhi ya nchi wanachama hawafurahii. Nashauri wakae na kuelewana ili chokochocho ziishe.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ilikuwa na mzozo wa mpaka na nchi ya Malawi ndani ya Ziwa Nyasa. Naomba Waziri aliambie Bunge hili mzozo huo umefikia hatua gani maana kwenye hotuba yake hajaugusia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni kati ya nchi zenye vivutio vya utalii vinavyopendwa duniani. Sijui ni kwa kiasi gani Ofisi zetu za Ubalozi zinasaidia kutangaza vivutio hivyo. Nchi ya China hivi sasa inakuja juu sana kuleta watalii, nimshauri Mheshimiwa Waziri na Maafisa wake wajipange kutangaza nchi yetu ili tupate fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo jema kuwa na utangamano wa Afrika ya Mashariki lakini isiwe ni kigezo cha kuwanyima watu wetu fursa za kiuchumi. Ni jambo lililopendeza kabisa kuona hata kazi zile ambazo vijana wetu wanaweza kufanya zinafanywa na wageni toka nchi za nje. Mfano ukienda kwenye hoteli za kitalii na mashamba ya wawekezaji kazi za kuhudumia wageni hotelini au kusimamia vibarua mashambani zinafanywa na watu kutoka nje. Mbaya zaidi wageni hao wanawanyanyasa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpaka wa Kenya pale Namanga kuna urasimu mkubwa upande wa Tanzania. Wakati wenzetu wa Kenya upande wao wa mpaka mambo yanaenda haraka, ukija upande wa Tanzania hata kule kugonga muhuri inachukua muda sana.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa na kuaminiwa na wananchi wa Tanzania kuwa Rais wa Awamu ya Tano. Nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa kuunda Baraza la Mawaziri lenye ueledi wa hali ya juu wakiwemo Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kuishauri Serikali kupitia Wizara hii likiwemo suala zima la mabalozi wa utalii. Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa kuwa na vivutio vya aina mbalimbali na vingi. Naishauri Serikali iwahimise mabalozi wetu walio kwenye nchi mbalimbali watangaze utalii na vivutio vyetu ili nchi yetu ipate watalii wengi, iwe ni miongoni mwa kazi na wajibu wa Balozi kutangaza vivutio na utalii wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee ama nishauri kuhusu ulinzi wa Watanzania wanaoishi ughaibuni. Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha wananchi ama Watanzania hawa wanaoishi ughaibuni maisha yao yanakuwa salama kwa maana ya uhai. Matukio mengi ya kikatili yameendelea kuripotiwa wanayofanyiwa Watanzania hawa ikiwemo mauaji na vitendo vya udhalilishaji. Serikali ijitahidi kupunguza ama kuondoa kabisa kupitia Balozi zetu vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa Watanzania hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenye dhamana amezungumzia ukarabati wa majengo ya Balozi zetu. Nami naomba nitumie fursa hii kuishauri ama kuomba Serikali ihakikishe inaipatia Wizara hii fedha ya ukarabati wa majengo ya Balozi zetu kama ilivyooombwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kuitangaza Tanzania. Nina ushauri ufuatao:-

(i) Abiria wanaosafiri nje ya nchi wakaguliwe kwa uhakika ili kudhibiti Watanzania kukamatwa na madawa ya kulevyo;

(ii) Wizara itenge fedha kwa ajili ya dharura kwa Balozi zetu kwa madhumuni ya kuwasaidia Watanzania wanaofika Ubalozi kuomba wasaidiwe baada ya kupata matatizo makubwa huko ugenini; na

(iii) Ofisi ya Makao Makuu ya Kiswahili ipewe vitendea kazi na fedha ili ifanye kazi zake kwa umahiri mkubwa ikiwa ni pamoja na kukitangaza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia Waziri kazi njema katika kutekeleza majukumu yote.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kuchangia hotuba hii kwa kumshukuru Mungu kwa kunijalia kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge hili. Pili nachukua fursa hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuonesha imani na uwezo mkubwa wa kuongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nawapongeza wapiga kura wangu kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao. Natambua imani yao kubwa waliyonayo kwangu na nawaahidi sitowaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa na muda wa wafanyakazi wa Ubalozini. Napenda kuipongeza Wizara na Serikali kwa jumla kwa utaratibu mzuri wa kuwapangia na kuwateua wafanyakazi wa Balozi zetu. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni sifa gani wanazotumia katika kuwateua wafanyakazi wetu pamoja na Mabalozizi katika nchi za nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia. Nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kukiendeleza chuo hiki muhimu katika kuzalisha na kutayarisha wataalam wetu. Chuo hiki kama vilivyo vyuo vingine kinahitaji mahitaji kama vile mikopo na kadhalika. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kuna mpango gani wa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika chuo hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Jumuiya hii ni ya muda mrefu na ina uzoefu mkubwa. Napenda kueleza wasiwasi wangu juu ya ongezeko la nchi wanachama wa jumuiya hii. Nchi hizi zilizo nje ya Afrika Mashariki zina matatizo makubwa katika nchi zao na ndiyo wanaotuongezea watu katika mipaka yetu. Aidha, zimetuongezea uhalifu na ujangili na matatizo mengine. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili na wasite kuongeza wanachama walioko nje ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichangie Wizara hii ya Mambo ya Nje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua Serikali inawatumiaje Mabalozizi waliopo nje ya nchi katika kutangaza nchi yetu kwa maana ya ushiriki katika majukwaa ya kiuchumi. Mfano sekta ya utalii inachangia pato la Taifa kutokana na fedha za kigeni takribani asilimia 25. Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha naomba aniambie wana mpango gani wa kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza Tanzania ili kuendana na kasi ya kukua kwa uchumi wa kati na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ya Mabalozizi hawajui vizuri nchi na vivutio vilivyopo. Ofisi za Mabalozizi hazina wataalam wa utalii ambao wanaweza kuitangaza nchi yetu kupitia Balozi zetu. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu wana mpango gani kuwa na Maafisa wa Utalii katika Balozi zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu ni namna gani wanafunzi wanaosoma nje ya nchi wanapata misaada kupitia Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu deni la matibabu ya ndugu yetu, Marehemu Nassor Moyo ambalo hadi leo Serikali ya Uingereza inadai Tanzania. Deni hili ni aibu kubwa kwa nchi yetu, ni vyema Mheshimiwa Waziri alipatie ufumbuzi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozi wetu walioko nje ya nchi wanadharauliwa kwa sababu nyumba wanazoishi haziridhishi na hazina ubora, hii ni dharau. Mabalozi wanaoishi katika nchi yetu ya Tanzania wanaishi nyumba za hadhi na ubora wa hali ya juu. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri suala hili alisimamie kwa nguvu zake zote ili lirekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Watanzania walioko nchi za nje wanapopatwa na matatizo au dharura, ni njia gani za mawasiliano watumie kupata msaada wa Kibalozi? Naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie suala hili.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo uhusiano wa Mataifa ni sehemu ya kukuza uchumi na pia ni kipimo cha *Nation Brand*. Tanzania ina sifa kubwa na heshima kwa nchi nyingi duniani kutokana na utamaduni, amani, demokrasia na hata historia ya kuwa mstari wa mbele katika ukombozi wa Afrika. *Economic diplomacy* inaenda pamoja na *branding* ya nchi yetu kwa kuhakikisha tunaimarisha *Nation Brand* ya Tanzania. Hii ni pamoja na kuhakikisha Balozi zetu zinaendelea kuitangaza Tanzania na kuangalia ni jinsi gani nchi yetu inakuwa na *competitive advantage* na nchi jirani na Bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara iendeele kuangalia namna ya kuimarisha *diaspora* katika kuchangia uchumi wa Tanzania. Nchi zinazoendelea zilizo nyingi zinategemea sana fedha ya kigeni kutokana na *diaspora*. Tunapoangalia ushiriki wa *diaspora* katika uchumi wetu, napendekeza Wizara iweke utaratibu wa vijana wetu kupanua ajira ya nchi za nje. Kutokana na changamoto za ajira ni bora pia kuangalia soko la ajira la nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na maneno ya mpaka wa Ziwa Nyasa kati ya Tanzania na Malawi. Napendekeza Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge huu mgogoro wa mpaka kama upo umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa nchi jirani imetumia fursa tulizonazo hapa nchini kuzitangaza kuwa zipo kwao. Napendekeza Wizara ichukue hatua mahsusi kukomesha tabia hii. Pia ni wakati muafaka kwa Wizara kuangalia fursa za kibiashara hasa kwa nchi mpya kama Sudan ya Kusini.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba yao hapa Bungeni ili tuweze kuijadili. Yapo mambo ambayo naomba kupatiwa ufafanuzi na mengine napenda kuishauri Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubadilishana wafungwa wa Tanzania na nchi nyingine. Naomba ufafanuzi wa kama upo uwezekano wa Watanzania ambao wamekwenda nchi nyingine wakapata makosa ya kuhukumiwa kifungo, je kuna uwezekano wa wafungwa hao kurudishwa kuja kufungwa hapa nchini au kama kuna uwezekano wa kubadilishana na wafungwa walio hapa nchini kwenda kufungwa katika nchi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda kujua kama Watanzania waliopo nje ya nchi wakikutwa na makosa, Serikali inawapa msaada wa kisheria, kwa vile najua wengine wanafungwa kwa sababu hawana uwezo wa kuweka Mawakili wa kuwatetea, kama nchi ni msaada gani unatolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya Watanzania waishio nje ya nchi; hivi karibuni yamejitokeza matukio ya mauaji ya kutisha baadhi ya vijana wa Kitanzania wanaoishi nchi za nje kama USA kuuawa kwa kupigwa risasi; je, ni jitihada gani ambayo Serikali yetu inachukua kubaini hayo? Ningependa kujua jitihada za Serikali kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali kuwaunganisha wajasiriamali wa Tanzania kuingia ubia na makampuni ya China. Serikali ya Awamu ya Tano, sera yake kubwa kufufua na kujenga viwanda kwa ajili ya kujenga uchumi wa nchi na kuongeza ajira. Kwa kuwa nchi ya China katika hilo ipo mbali sana ina viwanda vidogo vidogo na vikubwa, napenda kujua Tanzania imejipanga vipi kuhakikisha inaingia ubia na makampuni ya China yatakayoweza kusaidia ukuaji wa viwanda vyetu nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata bahati ya kutembelea Ubalozi wa Tanzania nchini China na UK, kwa kweli jengo la Ubalozi wa Tanzania China lilikuwa na hali mbaya sana. Je, ni utaratibu gani huwa unatumika katika kupeleka pesa za ukarabati wa majengo hayo kwa sababu ni aibu sana Mabalozi wetu kuishi katika mazingira mabaya na magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pia nimpongeze Mheshimiwa Balozi Mahiga, Naibu Waziri wake pamoja na Watendaji wake kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala kadhaa pamoja na kuunga mkono hoja, nitaomba yajibiwe au kama bado yafanyiwe kazi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, diplomasia imejikita katika misingi ya *reciprocity*. Tupewe ufafanuzi kama kweli Balozi wa nchi za nje hawataruhusiwa tena kwenda mikoani bila kibali cha Wizara ya Mambo ya Nje. Naamini jambo hili haliwezi kuwa kweli, hii maana yake watu hawatakuwa na uhuru kamili kufanya kazi zao halali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiamua ku-*retaliate* na kuweka sharti hili kwa Mabalozi wetu walio nchi zao inaweza kutuumiza. Nitaelewa kama kwa sababu ya usalama Mabalozi na Maofisa wao watatakiwa kutoa taarifa ya safari zao nje ya Dar es Salaam ili Serikali ikibidi iwawekee ulinzi, hiyo inaeleweka, lakini hivi sasa ni kama suala hili limepotoshwa na Wapinzani kudai wanahitaji ruhusa. Mheshimiwa Waziri atufafanulie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi zetu ziruhusiwe kubaki na maduhuli wanayoyakusanya ili kupata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kutoeleweka vizuri kwa wananchi, ingekuwa vizuri kupata kitabu cha maswali na majibu (Q and A) kuhusu maana ya ushirikiano – sekta kwa sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya nchi hii yote bado haijakamilika. Mpaka kati ya Uganda na Tanzania huko Kagera, uliowahi kusababisha vita hadi leo haujakamilika. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi atueleze ni lini wanakamilisha zoezi hilo. Nilijaribu kulikamilisha nilipokuwa Waziri wa Ardhi, lakini jukumu la mwisho ni Waziri wa Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alikuwa Mwenyekiti wa *Governing Council* ya *UN-Habitat* kati ya 2006 – 2008. Katika wadhifa huo alikuwa *Co-Chair* wa *World Urban Forum* ya *Vancouver Canada* 2006. Kwa kuwa, mkutano wa *Habitat III*, utafanyika Oktoba Ecuador ni mkutano unaotokea kila baada ya miaka 20. Mheshimiwa Waziri unashauriwa ku-check kuona kama Rais anaweza kuhudhuria mkutano huo. Kwa hivi sasa Mheshimiwa Rais wetu tayari anasifika duniani, akihudhuria *Habitat III* jambo hilo Kidiplomasia litaendelea kumsimika kama “*Purposeful Traveller*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maoni yangu kama yakionekana yanafaa yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa matayarisho ya hotuba nzuri yenye kutoa mwelekeo wa kutafakari kwa mabadiliko ya kweli kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri yafuatayo:-

(i) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kukarabati ofisi zetu za Ubalizi. Baadhi ya ofisi zetu hazijakarabatiwa kwa muda mrefu.

(ii) Pia kuwe na uratibu mzuri wa wanafunzi wanaofanya mafunzo mbalimbali katika nchi mbalimbali ili Balozi zetu ziweze kutoa maelezo ya kina pindi wanafunzi hao wanapopatwa na madhila/matatizo wakiwa huko.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi zetu katika nchi mbalimbali hali siyo nzuri sana, Serikali iboreshe ukarabati wa majengo katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mabalozi waliostaafu bado wako nchi za nje, nashauri walipwe haki zao na kurudishwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozi waitangaze nchi yetu kibiashara katika nchi mbalimbali kwa mfano watangaze Mlima Kilimanjaro kuwa upo Tanzania na siyo Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozi wawe na wataalam ambao wanaweza kufanya *research* katika nchi wanazowakilisha ili kupata mahusiano mazuri ya kibiashara na pia kupata ajira kwa vijana wetu katika nchi mbalimbali. Pia Serikali iwape fedha Mabalozi wetu kwa muda muafaka siyo kuchelewesha malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MWANNE I. NCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Balozi, Dkt. Augustine Philip Mahiga, Naibu Waziri Dkt. Susan Kolimba na Katibu Mkuu wa Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara yetu iangalie sana mipaka yetu ambayo ina vichocheo vingi na ambavyo wahamiaji haramu hupenya hasa kwenye mipaka ya Kenya na Tanzania kwa kupitia njia za Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko ya ujirani mwema; elimu itolewe. Hapa nchini kuna wafanyabiashara wadogo ambao wanasafirisha bidhaa zao

kama mahindi, mpunga, kahawa, chai ili wafanye biashara kwa weledi, kwani mikoani hakuna elimu ya kutosha. Waheshimiwa wetu ambao ni Wabunge wa Afrika Mashariki wapewe uwezo wa kuzunguka nchi nzima kutoa elimu hata mashuleni na vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utumishi; Wizara hii iwasiliane na Wizara ya Mambo ya Ndani kuongeza Watumishi wa Uhamiaji ili ajira iongezeke na kusaidia kulinda mipaka yetu kwani mpaka sasa bado watumishi hao ni wachache. Pia suala la utalii Waheshimiwa Mabalozi watangaze vivutio vyetu vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Niiombe Serikali yangu iijipange katika suala zima la wafanyabiashara kwani hawa wanaongeza pato kubwa katika Taifa letu, lakini kunakuwa na ukiritimba wa *passport* pamoja na *Visa*. Sambamba na hayo VAT inakuwa ni shida kwa wafanyabiashara hawa, yaani mzigo unachajiwa mara mbili ya bei aliyonunulia mfanyabiashara huyu. Suala la utoaji wa *passport* unachukua muda mrefu kuipata kwa hiyo niishauri Serikali yangu iliangelie hili *pass* hizo zitoke kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la Mabalozi wetu hawa imefikia wakati sasa watafute wawekezaji pamoja na wafadhili kwa ajili ya kujenga nchi yetu sasa kiuchumi zaidi.

Katika Jimbo la Lushoto kuna ma-sister wana miaka zaidi ya 60 na wamesaidia sana jamii inayowazunguka na mpaka sasa wanaendelea kusaidia. Wamejenga shule, wamejenga zahanati na wamejenga hosteli na pia wanajitolea kuwafundisha watoto wa maeneo hayo. Kwa kuwa ma-sister hawa ni wa muda mrefu sana na wanaendelea kulipia kodi kama kawaida, lakini kwa sasa hawa wamezeeka na shirika limefika hatua wanashindwa kuwalipia ma-sister wale. Niiombe Serikali yangu iweze kuwapa uraia kwani wakiondoka na kurudi kwao itakuwa ni hasara kubwa sana kwa wananchi wa eneo lile la Kifungilo sekondari pamoja na Kata ya Gare kwa ujumla itakosa huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba Mheshimiwa Waziri atembelee Jimbo la Lushoto au atume Mjumbe ili akaone hali halisi kwa haya niliyoongea hasa kwa suala zima la misaada tunayopatiwa na ma-sister hawa, kwa maelezo zaidi Mheshimiwa Waziri naomba nimwone ili nimwelezee kwa undani zaidi.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mahiga, Naibu wake na timu nzima ya Wasaidizi wao katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia hoja kwa kuelezea masikitiko yangu ya utoaji wa Visa katika Balozi zetu zilizopo katika nchi mbalimbali. Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia tunataraji Serikali sasa imefika wakati tuanzishe utaratibu wa kutoa *Visa online*, utaratibu huu sasa wa watu kutakiwa waende wenyewe moja kwa moja ni wenye usumbufu na umepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Wizara ione umuhimu pia wa kufungua ofisi za ubalozi wa Tanzania Korea ya Kusini, kule kuna *potential* kubwa ya kunufaika na fursa za teknolojia na watalii kutembelea nchi yetu. Pia Balozi zetu kutumika vizuri kwa kutangaza Tanzania kiutalii na fursa nyingine za kibiashara ili nchi yetu inufaike na uwepo wa Balozi hizo badala ya utaratibu wa sasa wa kutoa Visa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia ione umuhimu wa kuongeza kasi ya kujenga au kununua majengo kwa ajili ya Balozi zetu wenyewe, baada ya miaka 55 ya uhuru badala ya kuendelea kupanga wakati nchi nyingine ndogo kama Eritrea zimejenga nyumba zao wenyewe. Umefika wakati sasa Serikali iongeze kasi ya ujenzi au ununuzi wa majengo yetu wenyewe kwenye Balozi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wetu kwenye EAC utakuwa na tija kwa Taifa hili na watu wake ikiwa tutatambua na kuzitumia fursa zilizopo ndani ya umoja huo. Pamoja na Ibara ya 10 ya Itifaki ya Soko la Pamoja kuwahakikishia raia wanachama uhuru wa kupata ajira nchi zote za umoja wa EAC. Serikali itupatie takwimu ya Watanzania wangapi wameajiriwa kwenye ajira rasmi za Serikali katika nchi za Umoja wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa ni masoko kwa bidhaa zinazotoka kwenye nchi za Kenya na Uganda. Hata kwa bidhaa ambazo tunatengeneza kwa wingi hapa nchini kama vyombo vya *plastic*, viatu vya *plastic* na kadhalika bado vinavyotoka nje ni vingi kiasi cha bidhaa za viwanda vyetu kukosa soko ndani ya chini. Serikali ieleze ni kwa namna gani tukalinde viwanda vyetu ndani ya nchi, kuna udhibiti wowote wa uingizaji bidhaa hizi ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nchi yetu kuwa na vivutio vingi ya utalii bado hatujaweza kuvitangaza kikamilifu ili tuweze kunufaika vizuri. Ni kwa namna gani tunatumia Balozi zetu zilizoko katika maeneo mengi kutangaza utalii na vivutio vyetu huko waliko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwezesha Balozi zetu ni muhimu sana ili ziweze kutekeleza vizuri majukumu yao. Ni aibu kwa Maafisa wa Ubalozi kushindwa kulipia nyumba za kuishi na kubaki wakilalamika mara kwa mara kila tunapokwenda nje. Maofisa hawa wanalalamikia shida, tabu na kutelekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuelekea kwenye kutumia sarafu moja kwa nchi zote za EAC. Tumejiandaa kiasi gani? Kwa sasa hiyo shilingi ya Tanzania ndio yenye thamani ndogo sana tofauti na fedha za wenzetu. Tusikubali mambo ambayo yatakuja kutuumiza kama hatujajipanga vizuri ndani ya nchi. Tusije tukawa wasindikizaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nchi yetu kuwa na vyuo vinavyotoa mafunzo ya fani za utalii na *customer care*; bado mahoteli mengi makubwa na madogo watumishi wengi ni kutoka Kenya na wanatoa huduma nzuri sana na wanaipenda kazi yao. Naomba Serikali itueleze nini kinakosekana ndani ya vyuo vyetu hapa nchini au kwa vijana wetu wanaosoma fani hiyo kiasi cha kutokubalika kwenye hoteli zetu. Je, Serikali imefuatilia mitaala ya vyuo vya utalii vya Kenya na kuona upungufu wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lipange utaratibu wa Wabunge wa EAC wawe wanatoa semina na mafunzo kwa Wabunge kuhusu yale wanayofanya ndani ya Bunge la EAC ili tupate uelewa mpana na *up to date* yanayoendelea kuliko kusubiri hotuba wakati wa bajeti ya Serikali.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba yao hapa Bungeni ili tuweze kuijadili. Yapo mambo ambayo naomba kupatiwa ufafanuzi wa baadhi ya mambo na mengine kuishauri Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubadilishana wafungwa wa Tanzania na nchi nyingine. Naomba ufafanuzi kama upo uwezekano wa Watanzania ambao wamekwenda nchi nyingine wakapata makosa ya kuhukumiwa kifungo. Je, kuna uwezekano wa wafungwa hao kurudishwa kuja kufungwa hapa nchini au kama kuna uwezekano wa kubadilishana na wafungwa walio hapa nchini kwenda kufungwa katika nchi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda kujua kama Watanzania walio nje wakakutwa na makosa, Serikali inawasaidia msaada wa

kisheria sababu najua wengine wanafungwa kwa sababu hawana uwezo wa kuweka mawakili wa kuwatetea, kama nchi msaada gani unatolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya Watanzania waishio nje ya nchi: Hivi karibuni yamejitokeza matukio ya mauaji ya kutisha baadhi ya vijana wa Kitanzania wanaishi nchi za nje kama USA kuuawa kwa kupigwa risasi je, ni jitihada gani ambayo Serikali yetu inachukua kubaini hayo? Ningependa kujua jitihada za Serikali kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali kuwaunganisha wajasiriamali wa Tanzania kuingia ubia na makampuni ya China. Serikali ya Awamu ya Tano, sera yake kubwa kufufua na kujenga viwanda kwa ajili ya kujenga uchumi wa nchi na kuongeza ajira na kwa kuwa nchi ya China katika hilo ipo mbali sana ina viwanda vidogo vidogo na vikubwa. Napenda kujua Tanzania imejipanga vipi kuhakikisha inaingia ubia na makampuni ya China yatakayoweza kusaidia ukuaji wa viwanda vyetu nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata bahati ya kutembelea Ubalozi wa China na UK. Kwa kweli jengo la Ubalozi wa China lilikuwa lina hali mbaya sana. Je, ni utaratibu gani huwa unatumika katika kupeleka pesa za ukarabati wa majengo hayo kwa sababu ni aibu sana Mabalozzi wetu kuishi katika mazingira mabaya na magumu. Naunga mkono hoja.

MHE. SILAFU JUMBE MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza jitihada ya kazi nzito ifanyikayo katika kuendeleza, kuilinda na kujenga hasa mahusiano nchi za nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki. Waziri na jopo lake kwa kazi yenye matumaini kwa nchi yetu ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Serikali kuona upya namna ya kujipanga na kuweka bajeti yenye tija hasa katika kuwezesha ujenzi wa mahusiano wa nchi za nje, kwa kupata wataalam wa kuwajengea uwezo vijana wetu na kusimama wenyewe na hata upatikanaji wa Wawekezaji mahiri ambao wakitumia malighafi zilizopo na wanapoondoka viwanda vyetu kuendelea kuzalisha, yaani tuweze kubakiwa na viwanda mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuona umuhimu wa kuweka msukumo wa kusimamia ongezeko la bajeti kuwezesha nchi yetu kupiga hatua sasa ya kuwajenga vijana wetu, kwa kuwezesha Chuo cha Kidiplomasia kwa kuongeza idadi ya udahili, tukifahamu kuwa chuo hiki Tanzania ni kimoja tu hivyo kipanuliwe au kuwa na *branch* kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi za Mabalozzi wetu huko nje, kuendelea kupanga na makazi ya Mabalozzi, ni suala la kuangaliwa upya, madamu tunazo Taasisi na Mifuko ya Jamii inaonesha uwezo wa ujenzi wa majengo makubwa,

kwani hawawezi kupewa ukandarasi wa ujenzi wa majengo hayo. Ni lini sasa Serikali itayafanyia kazi na kuondokana na utaratibu wa upangaji huko nje, kwani wao kwetu wanajenga?

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa wananchi katika kusafiri kwenda nchi za nje, kuna urasimu sana, kuliko wanaoingia nchini na sasa idadi yao inatisha na wote wanakuwa ni wafanyabiashara na wawekezaji na baadhi yao kuwa wahalifu nchini. Serikali inalazimika kuongeza nguvu zaidi ya kiusalama katika maeneo yote na kudhibiti hii hali ya mwingiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kutoa ushauri wangu kuhusu mabaki ya mjusi wetu yaliyoko Humburg. Ni aibu kwa Serikali yetu na nchi yetu ya Tanzania kushindwa kuyarudisha mabaki ya mjusi wetu. Hayo mabaki tunaendelea kuwanufaisha Wajerumani na sio Watanzania. Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuyarudisha mabaki hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuishauri Serikali ifanye jitihada na kila iwezalo kuweza kurudisha mabaki hayo ili yanufaishe Watanzania kwani Watalii watakuwa wanakuja kuangalia mabaki hayo kwa tozo ya kiingilio. Ili Serikali iweze kurudisha heshima yake kwa wananchi wake wa Tanzania ilete mabaki ya mjusi wetu yaweze kunufaisha Watanzania wenyewe na si vinginevyo, ni aibu kwa Serikali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi za Balozi zetu zipo hoi, yaani zina hali mbaya sana. Nilitegemea safari hii Serikali ingeona umuhimu mkubwa sana na kuweza kutenga fedha za kutosha ili kukarabati hizo ofisi ili ziwe kwenye hali nzuri. Ni aibu unapokwenda nchi za nje, ukienda ofisi za Ubalozi wa Tanzania ni aibu kubwa, pia inatia uchungu kwa nchi yetu. Balozi zetu kuwa mfano wa ofisi mbaya kuliko kawaida, yaani kuliko nchi yoyote hapa duniani halafu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anasema, watafungua Balozi zingine. Je, ni kwa gharama zipi? Kwa nini Serikali isione umuhimu wa kukarabati kwanza Balozi zilizopo halafu ndiyo ione umuhimu wa kufungua hizo ofisi za Balozi zingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuishauri Serikali ifanye jitihada ya kuwa na Ubalozi wa Uingereza hapa nchini kwetu. Kwani mtu ukitaka kuomba viza ya kwenda Uingereza ilikuwa lazima uende Nairobi, Kenya. Sasa hivi ukitaka viza ya Uingereza sio tena Kenya bali inabidi uende South Africa. Kwa nini Serikali isione umuhimu juu ya jambo hili kwani inaleta usumbufu mkubwa sana na kero

kwa Watanzania. Natumaini Mheshimiwa Waziri, kati ya majukumu yake yote, aweke kipaumbele kwa Ubalozi wa Uingereza uwepo hapa Tanzania.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na fursa ya kuchangia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri na pia kwa kuteua viongozi wenye uzoefu katika Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na bajeti ndogo katika Wizara hii, tunashauri Serikali ipeleke fedha kwa wakati ili majukumu yatekelezwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ifanye juhudi na kukaa na Wizara zingine (*Coordinate*) katika kuboresha huduma za Wizara na pia kuongeza fursa ya kiuchumi na kimahusiano ya nchi yetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri masuala machache ya kuboresha huduma na fursa kwa Watanzania. Kwanza, naomba Watumishi wetu, Waheshimiwa Mabalizi wetu wapatiwe mafunzo ya kiuchumi na *marketing* namna ya kuitangaza nchi yetu (*economic diplomacy*), Mabalizi wa nchi nyingi hufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze wachache niliopata fursa ya kukutana nao mfano, Balozi wetu wa China na Netherland, pia wapate uwezo wa kutafuta masoko ya bidhaa zetu na pia tunapohitaji bidhaa huko watupatie maelezo au vielelezo. Ni muhimu Wizara iwe na dirisha la kuhudumia Watanzania wanaotaka kuagiza bidhaa nje na fursa ya kuwekeza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Tanzania iangalie namna ya kutumia Watanzania wanaoishi nje na waliokuwa Watanzania na sasa ni raia wa nchi zingine kutokana na mazingira *diaspora*. Nashauri tuwe na *pass* au utambulisho maalum ambao utawapa fursa waliokuwa Watanzania na sasa raia wa nchi zingine ili warudi kutembelea nyumbani wapate haki zote sawa na Watanzania isipokuwa kufanya kazi za umma (Serikalini), kuchagua na kuchaguliwa mfano, ni nchi ya India. Tuangalie pia hao raia ambao watoto wao pia wawe na hiyo haki, ambapo leo hawana (*Persons with Tanzania Origin*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wizara iboreshe Chuo cha Diplomasia na pia ishirikiane na Wizara ya Elimu kuboresha mitaala na mafunzo ya *International Relations*. Leo hii wanafunzi wetu wa *International Relations* hawana viwango kabisa, lugha ni shida, wacha lugha nyingine hata kiingereza

ni shida. Vijana wetu wangukuwa wanajua lugha nyingi hata ajira ya ukalimani wangepata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia kiongezewe bajeti kuboresha huduma mbalimbali ili wanaotoka au kuhitimu hapa, waweze kupata ajira kokote katika mashirika ya Kimataifa na pia taasisi za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, tunashauri pia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iwatumie Mabalozi wetu kufanya jitihada ya kuunganisha Taasisi za huko waliko ili kuboresha Taasisi zetu. mfano, vyuo kama SUA, Chuo cha Nelson Mandela, vituo vya utafiti mbalimbali, tuwe na *Program* za kushirikiana (*Exchange*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutufanyia semina Wabunge wote juu ya masuala ya Itifaki, namna ya sisi kuweza kufanya mawasiliano na viongozi mbalimbali. Suala zima la kuweka heshima yetu na namna ya kutuwezesha kufanya mawasiliano (*Etiquette and Diplomacy*) (*Manners and Presentation*).

MHE. JANETH Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kuchangia katika Hotuba ya Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nachukua fursa hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, Naibu Waziri Dkt. Suzan Kolimba, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri na taarifa nyingi za muhimu kwetu sisi juu ya utendaji wa Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua umuhimu wa vituo vya utoaji huduma mipakani hasa katika kurahisisha taratibu za uhamiaji, forodha, ukaguzi wa ubora wa bidhaa, usalama na ulinzi. Dhana hii na angalau vituo hivi kule vilikowekwa kwenye mipaka yetu kama Holili, Taveta, Horohoro, Tunduma na Sirari, Kyaka, Rusumo na kadhalika vimeleta matokeo mazuri sana katika maeneo yote tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ileje ina kituo muhimu sana kwenye Mto Songwe ambako tunapakana na Malawi kwenye Jimbo la Chitipa. Hata hivyo, inasikitisha kuwa ni miaka 42 tangu Wilaya ya Ileje ianzishwe lakini hakuna jengo, kituo wala miundombinu yoyote inayofaa kwa matumizi ya Serikali kuhakikisha kuwa biashara kubwa inayofanywa kati ya Watanzania na Wamalawi inasimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile soko lililoko Isongole, mita 100 tu kutoka mpakani, ni dogo kwa mahitaji ya biashara inayoendelea kati ya nchi hizi mbili.

Kwa bahati mbaya soko hilo limegeuzwa kuwa ghala la kuhifadhi mahindi na NFRA, hivyo hali hii imefanya lisitoshe kukidhi haja ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara chini ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kujenga kituo cha pamoja mpakani na Malawi, pale Isongole ili huduma ziboreshe maana tayari upande wa Malawi (Chitipa) wana miundo mizuri sana na wanatusubiri sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa miundombinu ya kituo hiki umesababisha wahamiaji haramu kutumia mpaka huu kuingia nchini na kutoka nchini kwenda nchi jirani. Silaha zimekuwa zikipitishwa katika mpaka huu huu na hivi sasa pombe haramu ya viroba ambayo imepigwa marufuku Malawi huingia kwa wingi nchini Tanzania kupitia mpaka huu, na vile vile kujikosesha fursa mbalimbali kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa kituo hiki cha pamoja na huduma zote muhimu vile vile kunahatarisha usalama na ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Wizara itoe tamko ni lini Kituo hiki cha Pamoja cha Forodha kitajengwa pamoja na kuweka taasisi zote muhimu ili ileje na Taifa zima liweze kufaidika. Kituo hiki kitafanya biashara iongezeke ndani ya Wilaya na hata fursa za uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Diplomasia ya Uchumi. Mheshimiwa Waziri pamoja na kusoma hotuba ya Wizara kuna mipango mingi mizuri hasa ya namna gani tunaweza kukuza uchumi wetu kupitia balozi zetu za nje ya nchi. Najielekeza katika balozi zetu hasa uendeshaji wa balozi zetu, Majengo (Pango), wafanyakazi katika Balozi, biashara zinazoweza kuingiza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa Balozi; kumekuwa na gharama kubwa za uendeshaji katika balozi zetu kutokana na Balozi nyingi kupanga majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pango la ofisi; kutokana na kukosa majengo ya ofisi, Balozi zimekuwa zikipanga, kitu ambacho ni gharama kubwa ukizingatia Balozi nyingi hawapati bajeti ya kutosha ya uendeshaji na hivyo pesa nyingi zinaishia kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Ni muda sasa wa Serikali kujikita katika kuhakikisha Balozi zinapewa bajeti ya kutosha ili wamiliki majengo kama ofisi na hivyo kuondoa aibu wanayoipata sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kulipa kodi Zimbabwe. Licha ya Balozi kwa sasa kumiliki nyumba kama ofisi lakini pia inamiliki baadhi ya biashara kama Tanzania Club. Watanzania hupangishwa au mtu mwenye vigezo kuweza kuendesha lakini sasa Serikali ihakikishe inasimamia miradi hiyo kwa sababu kumekuwa na ubadhirifu mkubwa wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa za ajira nje ya nchi; pamoja na Tanzania kuwa na fursa za kiuchumi tumeona tatizo la wageni kupewa fursa kirahisi rahisi tu, kitu ambacho ukienda nje ya Tanzania si rahisi kupata fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Work Permit*; Serikali sasa ihakikishe inaweka sheria ambazo zitawabana wageni kutimiza vigezo vya uwekezaji na si kupata fursa za ajira kirahisi rahisi kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wamekuwa wakipoteza fursa za ajira huku wageni wakipewa kazi hizo. Zimbabwe si rahisi kupata *work permit*. Imefikia hatua Watanzania wamekaa kule zaidi ya miaka 10 lakini kupata *work permit* si kazi rahisi na hivyo Zimbabwe ni moja ya nchi ambayo inajipatia pesa kupitia wageni, hivyo Serikali ya Tanzania iwe mfano mzuri ili tukuze uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya mahusiano ya Kimataifa sasa yawe na msaada kwa ajira mbalimbali za maana, si zao wageni wakija Tanzania wanapewa fursa nzuri na kazi za ngazi ya juu huku Watanzania wakiajiriwa nje ya nchi wanapata kazi zisizo na msingi kama viwandani, kusafisha viwanja vya mipira, kulea wazee na kuwasafisha wazee. Ifike sehemu sasa Watanzania waheshimiwe kwa sababu wageni wakija Tanzania wanaheshimika na kupewa fursa zenye maslahi mazuri kwao na si kunyanyasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, balozi zitafute fursa mbalimbali za kiuchumi kwa kufungua miradi mbalimbali kama vile maduka ya vitu vya asili ya Tanzania vitakavyouzwa katika balozi zetu na zisibweteke na kukosa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Tanzania imekuwa kimya sana, Watanzania wanateswa na wananyanyaswa na kuuliwa lakini Serikali imekuwa ya upole bila kutoa matamko makali kama nchi. Mbona wageni wakija Tanzania wanaishi kwa usalama na Serikali inalinda diplomasia ya nje ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadhi ya balozi zetu ni mbaya katika maeneo yafuatayo:-

Mishahara ya wafanyakazi katika balozi zetu, ukarabati wa ofisi zetu, majengo mengi hayana hadhi ya Balozi za Tanzania na ukizingatia majengo ya balozi baadhi unakuta yako nje ya miji mbali na mjini.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyowasilishwa kwenye Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni vizuri ikatekelezwa ipasavyo ili kuweza kuleta matokeo mazuri yaliyotabiriwa. Tatizo kubwa la bajeti za Wizara mbalimbali ni kutopatikana kwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili utekelezaji wa mipango iliyotengewa fedha kwenye bajeti uweze kufanyika kwa wakati uliopangwa. Ni muhimu Hazina izingatie hili na kutoa fedha kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Serikali kwa ujumla haikutoa tamko lolote kwenye Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje, kuhusu vitendo vya ubaguzi na udhalilishaji unaofanywa na baadhi ya wananchi wa India dhidi ya Waafrika waliopo India. Matukio ya udhalilishaji wa Mtanzania mwanafunzi, aliyevuliwa nguo zake na kuburuzwa mtaani, raia mwingine wa Congo ambaye aliua kikatili na matukio mengi dhidi ya Waafrika huko India, haya ni mambo makubwa ya kidiplomasia ambayo hayapaswi kuachwa yapite bila kukemewa na kuyatolea tamko na Waziri mwenye dhamana ya mahusiano na nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 23 Juni, 2016, Uingereza itapiga kura ili wananchi wake waamue ama kuendelea kuwemo ndani ya Jumuiya ya Ulaya (EU) ama kutoka kwenye Jumuiya hiyo, mpango ulio mashuhuri kwa kujulikana kama BREXIT. Ni vizuri Wizara hii ingefanya tathmini na kushauri je, nchi yetu itaathirika vipi na kunufaika vipi na hatua hiyo ya Uingereza hasa kwa kuwa Uingereza imekuwa na ushawishi mkubwa kwa baadhi ya sekta za maendeleo ndani ya Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini hizi ni muhimu ili kuiandaa nchi yetu ipasavyo. Je, kama Uingereza itajitoa kwenye Jumuiya ya Ulaya bila Uingereza kwa nchi yetu itapungua au itaongezeka? Haya ndiyo maswali ambayo wananchi wa Tanzania wangependa kupata majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inabidi kuratibu kwa weledi zaidi mahusiano ya nchi za nje ili nchi wahisani wasiathiri mipango ya maendeleo ya wananchi wetu Watanzania kwa kuvunja makubaliano tunayoyafanya kwa sababu za kisiasa. Uamuzi wa Marekani kusimamisha mpango wa MCC II kwa Tanzania ni mfano mzuri. Hali ya kutegemea misaada kutoka kwa wafadhili na marafiki zetu ina gharama zake. Tusipoweza kuratibu kwa weledi wa hali ya juu tutavuruga mipango mizuri ya maendeleo ya wananchi wetu. Tanzania ni nchi huru ina heshima yake hatutaki mahusiano ya kudharauliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri na inaeleweka vizuri. Napongeza utendaji wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti kwa kuishauri vizuri Serikali. Naomba ushauri wa Kamati uzingatiwe kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushauri; Ofisi zetu za ubalozi na maafisa wetu wasaidie katika kuutangaza utalii wa Tanzania. Wasaidie katika kuleta wawekezaji nchini mwetu na mkazo uwe kwenye ujenzi wa viwanda. Serikali iboreshe ofisi zetu za ubalozi kwa kuweka vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika utendaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Elimu iendelee kutolewa kwa Watanzania. Serikali iweke mpango mkakati wa kuwatambua wanafunzi wetu wanaosoma nje ili kupunguza matatizo ya udhalilishwaji wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wengi wanakwenda kusoma nchi za nje bila utaratibu. Wanafunzi wanaosoma nje bila kuthibitishwa na TCU kwa nini wao hatuwaingizi kwenye ajira za moja kwa moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuangalie kwa kuwa watoto wale ni Watanzania wanakwenda kuchukua ujuzi wa Mataifa mengine si kwa wote lakini wengine tuwape nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni miongoni mwa Wizara zenye umuhimu wa kipekee kwa nchi yetu. Mafanikio ya utendaji kazi wa nchi hii unategemea uwezeshwaji katika rasilimali zote (rasilimali watu na rasilimali fedha). Tabia iliyozoeleka ya Hazina kutoa pesa iliyoidhinishwa na Bunge kwa Wizara zetu ikiwemo hii ya Mambo ya Nje imekuwa kikwazo kikubwa kwa watendaji wa Wizara yetu. Ifike wakati sasa Bunge liheshimiwe kwa kutekeleza maamuzi/maelekezo yake na Wizara zetu zitendewe haki kwa kupewa bajeti walizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa rasilimali watu yenye sifa stahiki ni muhimu sana kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii muhimu, Serikali inabidi iweke mkazo wa kipekee kuandaa Mabalozi wetu wanaotuwakilisha nje ya nchi na watendaji wa Wizara. Lazima *foreign service officers* wapewe

mafunzo maalum ya muda mrefu (angalau mwaka mmoja) ili kupata vyote, *Regional and functional specializations* kwa watendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Regional specialization* ni lazima ijumuishe mafunzo ya lugha kuu ya eneo (*region*) husika. Kwa mfano, Watendaji wetu kwa Kurugenzi ya Mashariki ya Kati (*Middle East and North Africa*) ni lazima wawe na umahiri wa lugha ya Kiarabu. Kurugenzi ya Ulaya wajue Kifaransa na Ki-Spanish na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Wizara hii pia itoe umuhimu wa kipekee kwa Chuo cha Diplomasia ili kiwe na hadhi stahiki. Kwa sasa Chuo kiko katika hali mbaya, miundombinu yake kwa kweli hairidhishi, lakini hata Walimu wa Chuo cha Diplomasia hawapatiwi mafunzo stahiki ya kuwajengea uwezo kwa kuandaa watendaji wa Wizara hii. Kozi fupi nje ya nchi kwa Walimu wa Chuo hiki ni muhimu sana ili kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika harakati/jitihada za kubadili hali ya Chuo cha Diplomasia iliwahi kuundwa Tume ya Profesa Ishumi iliyojumuisha Wataalam mahiri wakiwemo Profesa Daudi Mukangara. Ni muhimu taarifa ya Tume hii ifanyiwe kazi. Kuwa na Wakuu wa Chuo wenye sifa bila ya kufanyia kazi masuala mengine muhimu haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo muhimu sasa Wizara ibadili utendaji kazi wake na utoaji taarifa zake za kila mwaka ikiwemo Hotuba zake za Bajeti za kila Mwaka. Wizara isitoe *descriptive report* tu, ni lazima kutoa taarifa zinazoonisha kuwa Wizara ilikuwa na malengo yanayopimika (*measurable goals/objective*). Hili liwe pia kwa Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Balozi zetu zipewe malengo maalum ya kuyafikia na malengo hayo yazingatie maeneo waliko kulingana na maeneo/nchi wanazotarajia kupata wawekezaji, watalii na kadhalika. Kwa mfano, malengo ya Wizara kwa mwaka ujao wa fedha hasa Kifungu cha 193 (i, ii, iii na iv) yangeweza kuboreshwa na kutaja vigezo mahususi.

MHE. MAKAME MASHAKA FOU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuchangia Wizara hii. Pia namshukuru Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa ya kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona ajabu kwa Wapinzani kwamba kazi yao kubwa ni kuelezea kasoro kwa Serikali. Je, hakuna mema yaliyofanywa na Mabalozi wetu? Yako mengi sana, kama kuanzisha Balozi katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozi wetu waongeze jitihada kubwa ya kuitangaza Tanzania katika suala la utalii. Nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii kama mbuga za wanyama sehemu za kihistoria, fukwe nzuri Zanzibar na Tanganyika. Pia bahari yetu ina vivutio vingi, kwa mfano aina ya papa huko Mafia ambao hawapatikani sehemu nyingine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba Mabalozi kufanya kazi ya kutafuta wawekezaji wakubwa hasa kwa upande wa utalii. Tunayo fursa nzuri ya kuwapata watalii wa daraja la kwanza iwapo tutapata wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mjusi wa Kihistoria (mabaki) Aliye Ujerumani; namshauri Waziri kuharakisha utaratibu mzuri wa kupata mafao au manufaa yatokanayo na mjusi huyo kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina nafasi gani katika ushirikiano wa kibiashara kwenye ukanda wa Kusini mwa Afrika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu wa kifugaji wanaokwenda Zambia na Afrika ya Kusini, wamekwenda kwa ajili ya kusuka nywele za akinamama kwa “style ya kimasai.” Ni sisi pekee nchi hii na Afrika ambao tunaweza kusuka nywele hizi na hazisukwi na mtu mwingine yeyote. Matatizo na adha wanayokumbana nayo wenzetu wa Kimasai katika nchi hizi mbili ni haya yafuatayo:-

(1) Wanakatwa, wanapigwa na kuhukumiwa bila kupewa usaidizi wa kisheria;

(2) Zambia kama nchi, imekuwa ikiwahukumu “Wamasai” bila kuwapa msaada wowote wa kisheria “*fair hearing*” trial hazifanyiki.

(3) Tunaomba nchi ya Zambia ituambie wafugaji hawa wafanye nini ili wakidhi vigezo vya kufanya kazi nchini huko?

(4) Balozi wa Tanzania (Lusaka) amekuwa “*reluctant*” katika kuwasaidia vijana wetu wanaopata matatizo nchini Zambia. Naomba Balozi wa SADC atazame hili ili watusaidie kuwaondolea vijana wetu shida wanayokumbana nayo.

(5) Tunaomba vijana wetu waliofungwa kwenye Magereza ya Zambia wasaidiwe. Wapo wengi Magerezani na sijui kama Wizara ina takwimu zozote. Please hili lifuatiliwe pia.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mahiga, Naibu Waziri Kolimba na timu yote ya Watendaji kwa kuandaa vizuri hotuba ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri katika maeneo mawili. Kwanza, nashauri Wizara iwekeze katika viwanja vilivyoko nje ili kupata fedha za kuendesha balozi zetu. Kwa mfano, kiwanja tulichopewa na Serikali ya Msumbiji tukakiacha, mwisho wake tunaweza kunyang'anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Maafisa wa Korea Kusini waliwahi kuja kuongea na Kamati yetu ya Mambo ya Nje na kuialika iende nchini humo ili kuona uwezekano wa kuanzisha Ofisi ya Ubalozi Korea Kusini. Ni ushauri wangu kwamba Wizara ilifanyie kazi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hotuba hii kama nilivyoainisha hapo juu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea tatizo la wafanyakazi kutopata ajira za kudumu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nilishafanya kazi na Jumuiya kabla sijawa Mbunge kuanzia mwaka 2006 mpaka 2009 kama *IT Assistant*. Wakati najiunga pale nilikuta wafanyakazi wa *temporary* ambao wanafanya kazi kama vibarua, naweza kusema hadi leo hii ni muda wa miaka 10 na zaidi sasa, baadhi yao hawajaajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua toka kwa Mheshimiwa Waziri ni lini ajira za hawa wafanyakazi zitatangazwa ili waweze kuajiriwa? Kwa sababu wangukuwa hawatakiwi, wasingekuwepo kazini hadi leo hii. Naweza kukupa majina yao kama utahitaji pia na wengi ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine, ni Serikali yetu kutopeleka fedha za kuendesha Jumuiya kwa wakati. Mfano, tokea makubaliano ya bajeti iliyopita kati ya *Partner States* hadi leo hii nchi yetu ya Tanzania haijapeleka au kukamilisha mchango wake wa kuendesha Jumuiya hiyo. Hii ni aibu sana kwa nchi yetu na ukizingatia Jumuiya hii Makao Makuu yake yapo Tanzania. Ilitakiwa tuoneshe mfano kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni wafanyakazi wa ngazi ya *profession* kutokupatiwa *Diplomatic Passports*. Kama yalivyokuwa makubaliano ya nchi wanachama, yaani *Headquarters Agreement*, wafanyakazi wa *level* hii wanaotoka nchi nyingine wana *diplomatic passports* isipokuwa nchi yetu. Hili nilishalisemea tena Bungeni mara mbili na Mheshimiwa Waziri akaahidi

watapewa kwani ni haki yao, lakini hadi leo imekuwa ni hadithi tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba kujua ni lini watapewa haki yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wafanyakazi wa Jumuiya wamekuwa na shida ya kupata *Work Permit*. Ni aibu kubwa sana kwa hili jambo. Mtumishi ana mkataba wa miaka mitano, lakini bado Serikali haimpi *Work Permit* ya miaka mitano na kusababisha kero kubwa kwa nchi wanachama wanaokuja kufanya kazi nchini ambako ndiyo sehemu *Headquarter* ilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu maswali yafuatayo:-

(1) Ni lini Wizara hii itanza kukaa na Wabunge wa EAC ili kujadili mambo mbalimbali, kama mtakavyojipangia ratiba, kama Wizara ya EAC ya Awamu ya Nne ilivyokuwa inafanya?

(2) Ni lini mtawapatia ofisi Wabunge wa Tanzania ambao wanaunda Bunge la Afrika Mashariki na waache kufanyia kazi hotelini au nyumbani mwao?

(3) Ni lini Serikali ya Tanzania itanza kuwapa mikopo ya magari Wabunge wa EAC kama zinavyofanya nchi wanachama, mfano Kenya na Uganda, ili waache kutumia mishahara yao na posho kununua magari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ilivyowasilishwa hapo mbele. Miaka ya hivi karibuni Tanzania imewahi kuingia kwenye mgogoro na nchi jirani ya Malawi kuhusu mpaka ndani ya Ziwa Nyasa. Mgogoro huo ulitaka kufifisha mahusiano mema ya kidiplomasia baina ya Malawi na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa mahusiano ya nchi, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge, mgogoro huu umepatiwa ufumbuzi au bado? Kama bado, Waziri aje hapa atueleze, nini kinaendelea? Je, huo mpaka ndani ya Ziwa Nyasa, nchi yetu ina eneo la ukubwa gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Umoja wa Mataifa (UN) umetutaka mataifa yote yapige vita Mataifa yanayotuhumiwa kuzalisha makombora ya nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna taarifa zinaeleza kwamba baadhi ya Balozi za nchi yetu huko ng'ambo zipo taabani kifedha. Namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili hali halisi ya kifedha kwa ofisi za Balozi za Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, niseme machache. Kwanza, nianze na suala la usalama. Katika nchi za maziwa makubwa hali ya usalama ni tete sana, hali siyo shwari katika nchi nyingi za majirani. Kenya hali siyo nzuri; Uchaguzi Mkuu wa mwaka kesho nchini humo inatia shaka kama usalama utakuwepo. Ukabila nchini Kenya sasa ni kidonda ndugu. Hatari iliyopo ni kutengeneza wakimbizi na wengi watakimbia Tanzania. Tanzania ichukue jukumu la usuluhishi na upatanishi ili tuwe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepeleka vijana (Askari) kurejesha amani Kongo; ni jambo jema sana. Tuilinde Kongo kimkakati kama mbia wetu wa biashara na *Foreign Service*. Anzisheni Ofisi ndogo ya biashara pale Lubumbashi ili tulinde maslahi yetu ya kiuchumi na kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu Mgogoro wa Burundi na Usuluhishi. Juhudi zinazoendelea pale Arusha ni njema sana. Ni vizuri katika usuluhishi ule pia, washirikishwe Viongozi wa Dini hasa Wakristo na Waislamu. Haya ni makundi mahususi ambayo yanaweza kusaidia kuwezesha mawasiliano na maelewano. Zaidi usuluhishi huo pia, ushirikishe Baraza la Wazee (*Council of Elders*) ambalo linaweza kuundwa na *Elders* waliopo katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya za Biharamulo na Ngara. Tamaduni za maeneo hayo zinafanana sana na hali/mazingira yaliyopo Burundi, hata lugha yetu ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Kutangaza Lugha yetu ya Kiswahili kilichopo Addis Ababa, Ethiopia, kimeendelezwa kiasi gani? Kimeleta ajira ngapi kwa vijana wetu? Tunataka Kiswahili kiwe bidhaa tena bidhaa ambayo itatungezea mapato kama Taifa. Kwa nini hadi sasa Kiswahili hakitumiki kama lugha rasmi ya EAC? Tatizo ni nini? *We have to promote Kiswahili now.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni watumishi wangapi wa vyeo vya juu wameajiriwa pale *Head Quarters* iliyopo Arusha? Ni watumishi wangapi wa vyeo vya kati walioajiriwa na *EAC Head Quarters* pale Arusha? Watumishi wa vyeo vya chini/*operating staff*, wahudumu/*drivers* ni wangapi? Nataka kujua pia tunavyonufaika na EAC kuwapo katika ardhi ya Tanzania kiajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *protocol* yoyote katika nchi wanachama za kuhakikisha demokrasia inakua na kustawi katika Jumuiya hii? Kitendo cha kung'ang'ania madaraka kwa Viongozi katika Jumuiya hii ni hatari sana, kitaua ustawi wa jamii na uhuru wa watu wetu. Tanzania *must take lead*; tuzungumze, tushauri na tuongoze juhudi hizi za kujenga demokrasia hii ambayo ni changa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kwa maandishi bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuboresha majengo ya ofisi zetu za Balozi za Tanzania nje ya nchi, zinatia aibu kwa majengo kuwa machakavu hata rangi hayabadilishwi. Naishauri Serikali, pale ambapo baadhi ya nchi zinatupatia viwanja kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kudumu ya Ubalozi mfano Oman, tuyajenge haraka iwezekanavyo ili kuepuka kunyang'anywa viwanja hivyo na kupewa nchi nyingine kama ilivyotokea Oman; kiwanja chetu kupewa nchi ya India ambayo tayari wameshajenga jengo la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafungu ya fedha yapelekwe mapema katika Balozi zetu za nje ili kuboresha utendaji bila kusahau kuboresha mishahara na elimu zao na kuwashughulikia Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi ambao wanapata matatizo katika ajira zao au shughuli mbalimbali za kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwepo na tatizo la vyeti vya baadhi ya vyuo vyetu (*certificates*) kutotambulika katika nchi za nje, hali ambayo inasababisha usumbufu katika ajira kwa Watanzania waliopo nje. Mfano, *Dar es Salaam Maritime Institute Certificates*, hazitambuliwi Kimataifa kwa mujibu wa taarifa nilizopata toka kwa Watanzania, mabaharia wanaofanya kazi katika nchi za ng'ambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ihakikishe inavitangaza vyuo vyetu Kimataifa kwa kufuata taratibu za Kimataifa ili vitambulike katika medani za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yetu kufanya taratibu ya kuondoa visa na kutumia *entry* katika nchi za *Nordic United Arab Emirates, United Kingdom, German and Northern America*. Hii itasaidia Watanzania wengi kupata fursa za kibiashara na kielimu, hali itakayoweza Watanzania wengi pia kupata ajira na wale wenye vipaji vya michezo mbalimbali. Pia wataweza kuionesha dunia kuwa Watanzania wanaweza na wao pia watapata ajira. Mfano, wachezaji wa *basketball, football, golf, tennis, athletics* na kadhalika.

MWENYEKITI: Tumemaliza uchangiaji wa jumla sasa tunahamia upande wa Mawaziri na namkaribisha Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Kalemani.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichangie...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

MWENYEKITI: Naomba utulivu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuchangia bajeti ya Wizara hii muhimu. Pamoja na raha sana zilizotolewa na Mheshimiwa aliyemaliza kuzungumza na mimi basi nizungumze machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuchangia kidogo tu kuhusiana na mikakati ya Serikali kuhusiana na masuala ambayo yamezungumzwa na wenzetu wa Kambi ya Upinzani. Nikubaliane na taarifa ya Kambi ya Upinzani ukurasa wa nane na tisa kwamba yapo mambo ya msingi katika mgodi wetu wa Nyamongo kwamba wananchi hawahitaji kunyanyaswa, kudhumiwa na Serikali kufumbia macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufafanua kidogo, nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge kwamba zipo sababu za makusudi za Serikali yetu kuchukua hatua dhidi ya unyonyaji unaoweza kujitokeza kwa wananchi wetu. Nikubaliane kwa kusema tu kwamba, Serikali imechukua hatua madhubuti na niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wa Tarime, Mheshimiwa Heche pamoja na Mheshimiwa Matiko wameshirikiana sana na Serikali hii kuhakikisha kwamba migogoro ya *North Mara* inamalizika mara moja. Hivi karibuni Serikali yetu imechukua hatua ambazo pia ni shirikishi kwa kuwashirikisha viongozi wa vitongoji wa *North Mara* kadhalika kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wanaotoka karibu na mgodi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu inawezekana taarifa ya Kambi ya Upinzani ingekuwa nzuri sana kama ingeweza kutambua juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuondoa matatizo ya Nyamongo kuliko kuacha kama ilivyo. Nitambue tu kwamba Mheshimiwa Heche pamoja na Waheshimiwa Wabunge wameshirikishwa sana kwenye utatuzi wa migogoro hiyo. Wananchi wa Mara wana masuala ya msingi sana, ni kweli kuna masuala ya mazingira, kuna masuala ya mashimo, kuna masuala ya ajira na kadhalika lakini Serikali haijayafumbia macho. Nataka Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wajue kwamba Serikali inachukua hatua madhubuti za kuondokana na migogoro ya *North Mara*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hiyo haitoshi niseme tu kwamba ile timu iliyoungwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ambayo kwa sasa bado inakamilisha taarifa zake hatua zitakazochukuliwa pia zitakuwa ni shirikishi. Zitashirikisha Waheshimiwa Wabunge, Madiwani pamoja na Wenyeviti wa

Vitongoji husika wa *North Mara*. Kwa hiyo, nilitaka kuliweka vizuri hilo siyo kweli kwamba Serikali imeyafumbia macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mgogoro wa Bismarck na mgodi wa Acacia. Ni vizuri tukatambua Sera ya Uwekezaji pamoja na Sera zote za Nishati, Madini na za Mazingira zinahamasisha sana uwekezaji wa ndani na nje. Kwa kutambua hilo, nikubaliane kwamba kampuni ya Bismarck ni ya wazalendo na miaka ya 96 ilipewa leseni ya kutafuta madini kule Mgusu, lakini mwaka 2012 yenyewe ikaamua kuachia leseni zile. Hii ni kwa sababu za kiteknolojia za uchimbaji na mambo mengine. Baadaye sasa maeneo yale yakaombwa kumilikishwa na kampuni ya *Pangea Minerals* ambayo ni *subsidiary company* ya Barrick ambapo sasa wanaita Acacia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme sasa na ni jambo la msingi sana Waheshimiwa Wabunge tukitambua kuwa Bismarck ambayo pia ni kampuni ya Watanzania waliamua tu kufanya makubaliano ya kwao kabisa kimkataba na kampuni ya Acacia. Baada ya kutofautiana wakaamua kupelekana kwenye mahakama za usuluhishi za nje. Nitake tu kukubaliana na Waheshimiwa na niwaombe kwamba inapotokea mazingira ya namna hiyo watuletee taarifa Serikalini ili Serikali iyafanyie kazi kwa ufasaha. Sasa hivi suala linalozungumzwa la Bismarck na kampuni ya Acacia wala halipo hapa, wamepelekana wao kwenye usuluhishi wa kimataifa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa sana Waheshimiwa Wabunge tulateeni taarifa lakini kwa sasa hivi kulizungumza suala hilo lipo kwenye mahakama ya usuluhishi tutakuwa tunaingilia mhimili mwingine. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwaombe sana tuvute subira kwenye masuala haya mawili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nichangie kidogo kuhusu ajira. Mheshimiwa aliyemaliza kuzungumza wa upande wa pili amesema kwamba wananchi wanaachiwa mashimo, hakuna ajira na wanaajiriwa kwenye kazi ndogo ndogo. Nitoe mfano kwa kampuni ya *North Mara*, ajira kwa Watanzania ni 968 ambapo wageni ni 57. Kwenye mgodi wa Bulyanhulu Watanzania walioajiriwa ni 1,755 na wageni wapo 71. Mgodi wa GGM Watanzania walioajiriwa ni 1,568 na wageni 68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uwiano ule bado Watanzania tunapata ajira lakini nikubaliane tuna haja ya kuongeza zaidi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niseme tu kwamba michango ya wawekezaji wa nje nayo ni mikubwa na inachangia kwenye pato la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kalemani. Sasa tunamkaribisha Mheshimiwa January Makamba na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe ajiandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Napenda nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu - Balozi Mlima, watendaji wakuu, watumishi na maafisa wote wa Wizara ya Mambo ya Nje kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kazi yangu ya kwanza baada ya shule nilikuwa Afisa wa Mambo ya Nje, daraja la II, chumba changu kilikuwa 132. Katika Wizara hapa nchini kwetu au taasisi zenye kiwango cha juu cha uweledi wa utendaji ni pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje. Tunayo fahari kubwa ya kusema kwamba utamaduni huo wa uweledi na *professionalism* umeendelea na umezidi kuimarika chini ya Waziri mpya na Serikali mpya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu wanavyohitaji wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje kutoka katika Bunge hili ni *support*, ni kuungwa mkono kwa sababu wanatuwakilisha nje ya nchi wanabeba bendera yetu. *Foreign policy* (Sera ya Mambo ya Nje) ni *extension* ya *domestic policy*, ni *extension* ya mambo tunayotaka kuyafanya, ni kiwezeshi cha malengo ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali hii iingie madarakani sasa hazijafika siku 180. Kwa hiyo, hukumu iliyotolewa leo dhidi ya Serikali hii hasa kwenye hotuba ya Upinzani kwamba hatukufanya vizuri kwenye Sera ya Mambo ya Nje ni hukumu ambayo siyo ya haki kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mambo mengi yakiwemo masuala ya uteuzi wa Mabalozi. Kwanza nadhani Waziri pia atalieleza, *procedure* ya uteuzi wa Mabalozi inabidi uielewe kabla hujatoa hukumu ya aina ya Mabalozi wanaoteuliwa. Vilevile Rais Magufuli ameteua Mabalozi watatu tu tangu aingie madarakani. Amemteua Dkt. Asha Rose Migiro, Dkt. Dau na Chikawe na taratibu za uteuzi zinaeleweka na huwezi kuniambia katika hawa walioteuliwa hakuna mwenye sifa ya kushika nafasi ya Ubalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo tunaruhusiwa kuyafanyia siasa lakini suala la hadhi na heshima ya watu Rais anaowatuma kutuwakilisha nje ya nchi siyo ya kufanyia siasa. Hawa watu tunapowatuma kule nje wanabeba bendera yetu sisi, Bunge hili halipaswi kutumika kuwadhalilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi mkuu wa Sera ya Mambo ya Nje ni kulinda, kutetea na kusukuma maslahi ya Taifa katika mawanda ya kimataifa. Unapoihukumu Serikali hii katika mambo ya Sera ya Nje lazima useme ni wapi, ni lini na ni kwenye jambo gani tumeshindwa kutetea maslahi ya nchi yetu. Huwezi kuihukumu Serikali hii kwenye Sera ya Mambo ya Nje ukashindwa kusema ni kwenye jambo gani, ni lini na ni wapi tumeshindwa kulinda na kutetea maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu ni kwamba wenzetu hawakusema hayo mambo kwa sababu hakuna, tumeweza na tumefanikiwa. Kwa sababu ingekuwapo mahali ambao tume-*fail* tungeona kwenye hotuba yao. Tangu Serikali hii iingie madarakani katika mikutano yote na katika *forum* zote ambazo maslahi ya Tanzania yalikusika tuliwakilishwa na tuliwakilishwa kwa mafanikio makubwa iwe ni Paris, New York na kwingine kokote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Mambo ya Nje haiendeshwi kwenye *vacuum* bali inaendeshwa katika *context* ya sifa ya nchi, katika *context* ya sifa ya Rais na katika historia ya nchi. Sifa ya Tanzania duniani ni nzuri na sifa ya Rais wetu duniani ni nzuri na sifa ya Tanzania leo ni nzuri zaidi kutokana na kazi nzuri anayoifanya Rais hapa ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Rais ameamua kuweka mambo sawa hapa ndani, kazi nzuri anayoifanya ndani inazidi kufungua fursa na milango kwa nchi yetu nje na kwa Watanzania waishio nje. Moja ya nyenzo kubwa ya diplomasia ni *reputation* na sifa ya kiongozi. Sifa ya Rais wetu imeiongezea sifa nchi yetu, imewezesha kazi ya nje ya nchi ambayo wenzetu hawakuifanya vizuri. Kwa hiyo, unaposema Rais hasafiri wakati huo huo kazi anayoifanya inawezesha Sera yetu ya Mambo ya Nje iende vizuri kunakuwa hakuna mantiki hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba moja ya matunda ya kazi nzuri ya Wizara ya Mambo ya Nje ni kwamba sasa hivi sisi tuko kwenye viwanda, ndiyo msingi mkuu wa mpango wetu wa maendeleo ya miaka mitano. Nchi ya China imechagua nchi nne Afrika ambapo itahamishia sehemu ya viwanda vyake. Nchi hizo ni Ethiopia, Kenya, South Africa na Tanzania. Hilo halikutokea kwa ajali, halikutokea kwa kurusha karata, limetokea kutokana na jitihada nzuri za wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje na limetokana na kazi nzuri anayoifanya Rais wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya urithi tunaoachiwa na viongozi waliotutangulia ni sifa ya nchi. Moja ya wajibu wetu viongozi wa siasa bila kujali vyama ni kuulinda urithi. Tunao wajibu Wapinzani na sisi kwenye Serikali na Chama Tawala kulinda urithi tulioachiwa na waliotatangulia kwenye nchi hii.

Unapoitukana nchi yako ndani ya Bunge unajitukana wewe nje kwa watu tunaowawakilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchezo mmoja wa *Shakespeare* unaitwa *Macbeth* na nataka nizungumze kwenye *quote* moja kwenye *act five* inasema:-

*"Life is but a walking shadow, a poor player,
That struts and frets his hour upon the stage,
And then is heard no more.
It is a tale told by an idiot, full of sound and fury,
Signifying nothing".* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni *is full of sound and fury amounting to nothing*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kuzungumzia suala alilolizungumzia Mheshimiwa Jaku na Mheshimiwa Keissy Mohamed. Nchi yetu sisi ni ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar. Baadhi ya kauli tunazozitoa humu ndani lazima ziheshimu Muungano wetu. Mheshimiwa Keissy Mohamed ni Mbunge wa CCM lakini lugha aliyoitumia sisi kama Serikali hatuikubali na Mheshimiwa Jaku vilevile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya mambo makubwa matatu katika *concern* walizoleta. Kwanza, Ofisi ya Rais, Utumishi imetoa Waraka wa kuwezesha taasisi za Muungano zitengeneze utaratibu wa mgawanyo wa watumishi wa umma kutokana na *quota* iliyokubalika ya asilimia 79 na 21. Nimewaandikia Mawaziri wenye taasisi za Muungano kuhakikisha kwamba tunatimiza agizo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Tume ya Pamoja ya Fedha ilitengeneza mapendekezo kuhusu mgawanyo wa mapato na vyanzo vya mapato ya kuchangia shughuli za Muungano. Tumetengeneza Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya mgawanyo mpya kupitiwa ili tuweze kupata mgawanyo unaoakisi ukubwa wa uchumi na idadi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, sasa hivi Zanzibar kwa makubaliano inaweza kutafuta misaada yake yenyewe nje ya Tanzania. Hayo ni mafanikio makubwa yaliyotokana na Serikali yetu katika kuimarisha Muungano wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake na naunga mkono hoja hii. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa January. Sasa hivi tunamkaribisha Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Dkt. Kolimba ajiandae.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuchangia. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja na vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na uongozi wa Wizara kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili, matatu niongee kwa haraka haraka. Nianze na mchango wa Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka ambao ni mchango mzuri. Sisi kama Serikali tunaheshimu sana *constructive criticism*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongelea kuhusu Wabunge wa EALA kwamba hawana ofisi. Nataka kusesitiza tu kwamba tofauti na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki sisi ndiyo wenyeji, sisi ndiyo tume-*provide headquarters* ya EAC. Kwa hiyo, kiti chetu sisi kiko Arusha, ndiyo sehemu kuu ya *East African Community* na pale Wabunge wote wana ofisi zao. Tilitaka Wabunge wa EALA wawe na ofisi Dodoma sijui wakifanya nini, wawe na ofisi Dar es Salaam wakifanya nini? La msingi tukubaliane kwamba tuimarisha ofisi zao za Arusha waweze kukaa pale kwa ajili ya kufanya *research* zao na kutuwakilisha vizuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niongelee kuhusu mchango wa Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali kuwa Kenya na wenzetu wana Wizara mahsusi kwa ajili ya Afrika Mashariki. Nafikiri hapa tuongozwe na *Treaty*. Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukiangalia Ibara ya 8(3)(a) inasema kwamba:-

"Each partner state shall designate a Ministry for East African affairs".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ita-designate ina maana ita-appoint (itateua). Haisemi kwamba itakuwa na *a Ministry exclusive for East African affairs*. Hata ukiangalia *Article 13(a)*, inahusu chombo cha juu cha maamuzi cha *community, The Council of Ministers*, kinasema:-

"The Council shall consist of the Minister responsible for East African Community affairs. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni Wizara ambayo imekuwa *designated*, ni Wizara imekuwa *entrusted* kubeba masuala ya *East Africa*. Hata Serikali ya Kenya walivyoanza chini ya Mheshimiwa Rais Kenyatta walikuwa na Wizara ya Biashara, Utalii na Jumuiya ya Afrika Mashariki na mimi wakati huo nilikuwa *East Africa* na juzi tu wamebadilisha sasa ni Wizara ya Kazi na Jumuiya

ya Afrika Mashariki. Unaangalia mwenyewe *strategic interests* za nchi yako ufanyeje! Hata unaweza kuamua kuwa na Wizara ya Ulinzi na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu hili ni suala tu ku-*entrust* Wizara yeyote iweze kui-house hiyo community. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo napenda niliongelee kidogo, ni hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ukurasa wa sita na wa saba. Kama nilivyosema sisi tunaheshimu sana *constructive criticism*, hatuna tatizo kwa uhuru walionao, wameongea haya, lakini lazima tuweke record sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema kwamba amefanya uchunguzi ambao unaonesha kuwa chini ya Serikali ya CCM Ubalozi unatolewa kama zawadi kwa Makada walioisaidia kwenye kampeni, kwa Makada wa CCM wasiojua kitu kuhusu diplomasia ya uchumi ndiyo wanaokabidhiwa dhamana ya kuhakikisha Tanzania ifanikiwe kimataifa, wengi wao wangeweza kuwa Mabalozi wazuri sana wa nyumba kumi kumi lakini siyo kuwa Mabalozi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona kwamba hili tuliweke vizuri tu, naomba nisisitize kwamba tangu uhuru, viongozi wetu wamejitahidi sana kuwa waangalifu kuteua wanaotuwakilisha nje ya nchi. Ushahidi upo kwamba Mabalozi wetu wanapokuwa nje huko, Jumuiya ya Kimataifa inawaona, inawapa majukumu makubwa zaidi na siyo juzi tu, tumeanza toka kipindi cha Mwalimu Nyerere. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wengine wadogo hapa ngoja niwakumbushe. Tulikuwa na Kada wa CCM, Mzee Daudi Mwakawago alikuwa Katibu Mtendaji wa CCM, akapewa Ubalozi. Cha msingi hapa jamani ni kitabu, jamaa alikuwa amepiga kitabu vizuri hadi Kofi Annan akamuona pamoja na Ubalozi wake akamteua kuwa Mwakilishi wa Kofi Annan Sierra Leone na Mkuu wa UN Mission kule. Yote haya yanaonesha kuwa kitabu ndiyo kitu cha kwanza kinachotuongoza sisi kuteua Mabalozi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo Balozi James Kateka kama mmewahi kumsikia, ni judge wa *International Tribunal for the Law of the Sea* huko Hamburg. Yeye ndiyo Mtanzania wa kwanza kuingia *International Law Commission* amekaa kule 10 years. Huwezi ukasema ana-qualification za nyumba kumi kumi. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Hatujasema wote.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Balozi Dkt. Asha Rose Migiro, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Nitolee mfano wa Balozi mmoja ambaye hafai. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Hatujasema wote.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mimi naomba Wapinzani muwe wavumilivu! Ninyi mkisema sisi tunakaa kimya, mbona utamaduni huo hamna? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi Profesa Costa Ricky Mahalu, mimi naenda kufanya Uzanifu Ujerumani nimemkuta anawafundisha Wajerumani pale *international law*. Hawa ndiyo Mabalozi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi Kagasheki alikuwa hapa hapa, nimemkuta mimi Geneva akiwa *Deputy Secretary General* wa *World Intellectual Property Organization*. Tunajua kuteua watu! Balozi Dkt. Augustine Mahiga jamani huyo ana-record iliyotukuka, ameshakuwa Rais wa Baraza la Umoja wa Mataifa. Bila shule huwezi kuwa Rais UN utajiminyaminyanya tu midomo tu hovyoy! Ameshakuwa mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Somalia na amefanya kazi iliyotukuka kule. Hawa ndiyo Mabalozi wetu wanaoteuliwa na Serikali ya CCM. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Salim Ahmed Salim.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi Getrude Mongela, Spika wa Bunge la Afrika; Balozi Juma Mwapachu, Katibu Mkuu EAC; Balozi Ally Mchumo, Mkurugenzi Mtendaji Mfuko wa Pamoja wa Mazao Brussels na wengine wengi wenye sifa nyingi. Wengine wana sifa zilizotukuka, mchukulie Balozi Ally Hassan Mwinyi nimuelezee nini? Balozi Salim Ahmed Salim nimuelezee nini? Balozi Benjamin Mkapa, naona niishie tu hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema taarifa ya Kambi ya Upinzani imejitahidi kwa kurasa nyingi kutuchora kama Serikali isiyo *serious, non serious government!* Wakisikia wanachama wa *East Africa* kwamba tunaitwa Serikali isiyo *serious* watashangaa kweli kweli kwa sababu sisi tumekuwa *critical* na ndiyo sababu Rais aliyepita Mheshimiwa Kikwete amekuwa Mwenyekiti kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uenyekiti tunaenda kwa *rotation basis* lakini haikuwa *accident* alipoingia Rais mpya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli viongozi wa *East Africa* wakasema mzee tunaomba uendelee wewe mwenyewe kuwa Mwenyekiti, *it is unprecedented!* Ni kwa sababu we *have a critical role* katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi sisi tumefanya mambo mengi *East Africa*. Niwakumbushe machache tu, sisi ndiyo tumesimamia mchakato mzima wa *admission* ya South Sudan tukiwa Wenyekiti wa Jumuiya na mimi wakati huo

nikiwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki. Siku hiyo tumekesha mpaka saa tisa kuweza kutengeneza *proposal* kwenda *Summit* kwa ajili ya *admission* ya South Sudan. *East Africa* inatambua mchango wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mungu kampa macho makini Mheshimiwa Rais kwa kugundua nyota ya Tanzania na kumfanya Waziri wa hii Wizara Mheshimiwa Dkt. Mahiga, *he is a jewel*, lazima tujivunie hapa. Sisi Watanzania tumesimamia mchakato wa kuishawishi Serikali ya Marekani kurefusha ule mpango wa AGOA wa kuuza bidhaa kwenye soko la Marekani bila kulipia ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliongoza ile *delegation* ya Mawaziri wa *East Africa* tumekwenda Marekani ku-*negotiate* na Serikali ya Marekani na *interests* za Tanzania zilikuwa mbele sana. Lengo letu kubwa lilikuwa ni kwamba tuki-*extend* AGOA Watanzania tu-*play a much more meaningful role* katika biashara hiyo. Ndiyo maana tukaishia ku-*sign the Cooperation Agreement on Trade Facilitation, Sanitary and Phytosanitary Measures and Technical Barriers to Trade*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba utatusaidia zaidi Tanzania kuliko nchi nyingine, tuliweza kuwa-*convince* wenzetu kwa sababu sisi Tanzania kinachotuangusha sana ni *packaging*, umaliziaji wa bidhaa zetu hivyo hatuwezi ku-*penetrate* kwenye masoko makubwa. Wenzetu Kenya sasa hivi wamechukua mpaka biashara zetu kwa sababu wao hata vitunguu wanajua namna ya kuvikata, kuvihifadhi na kukidhi zile *sanitary measures* na kuweza kupeleka kwenye masoko ya nje. Chini ya mkataba huu, Wamarekani wamekubali ku-*extend* hiyo *technical service* kwetu hapa na sasa hivi tumeongea na Mheshimiwa Waziri wa Biashara amelivalia njuga suala hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema naunga mkono hoja na namtakia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kazi njema katika kujenga nchi yetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Sasa Tunaendelea na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Kolimba.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii ya kipekee kama wenzangu walivyotangulia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake madhubuti na makini unaoendelea kugusa sio tu Watanzania bali mfano wa kuigwa katika nchi na Bara zima la Afrika na dunia kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza kipekee Mheshimiwa Balozi Dkt. Agustino Philip Mahiga, Waziri wangu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa uongozi makini na kuhakikisha tunapata ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara anayoiongoza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake ndani ya Bunge hili. Aidha, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa namna wanavyoliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Andrew John Chenge; Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan na Mheshimiwa Najma Murtaza, wewe Mheshimiwa Giga kwa kuchaguliwa kuwa Wenyevidi na kwa namna mlivyoonesha uwezo mkubwa wa kuliongoza Bunge hili katika kipindi hiki. Pia nawashukuru sana Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa. Nawaombea kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao hapa Bungeni na kwenye majimbo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa namna ya pekee kuwashukuru sana wananchi wenzangu na wanawake wote wa Mkoa wa Njombe na kwa kipekee Jumuiya ya Wanawake Tanzania, Mkoa wa Njombe kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Viti Maalum katika Mkoa huo na kwa imani kubwa walionipa na wanaoendelea kuonesha kwangu. Nitaendelea kuwa nao karibu na kushirikiana nao kuleta maendeleo makubwa zaidi na naahidi kuwa sitawaangusha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru sana familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpendwa Dkt. George Yesse Mrikaria kwa uvumilivu wao kwangu na kwa namna inavyonisaidia na kuniunga mkono katika majukumu yangu. Aidha, shukrani za dhati ziende kwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, viongozi, watendaji, wasaidizi wangu katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ushauri na msaada wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii. Ni dhahiri kwamba

michango yao itatusaidia sana katika kufanikisha shughuli za Wizara na kuimarisha ufanisi wa watendaji. Tunashukuru michango yote iliyoletwa kwa maandishi, ni michango karibu ya watu 50 na wale ambao wamezungumza moja kwa moja tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kujibu hoja za mzungumzaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani na nitazungumzia baadhi ya vitu na vingine Mheshimiwa Waziri wangu atamalizia. Kwenye suala lililozungumzwa kwamba ni chombo gani hasa kinachotumika kama kiunganishi kati ya Balozi zetu na Wizara nyingine ili Mabalozi hawa waweze kujua na kujifunza mambo mengi mazuri yanayofanywa katika Wizara mbalimbali na lile la namna gani wananchi wanaweza kupata ripoti za Balozi mbalimbali kwa njia rahisi ili wahamasike katika kutafuta fursa za kiuchumi katika nchi hizo zenye uwakilishi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni fupi, hili ni jukumu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na wao kazi yao kubwa ni kuratibu shughuli hizo. Hata Waraka unaolalamikiwa na Waziri Kivuli wa Wizara yangu unatokana na wajibu wa Wizara yetu hii lakini unalenga na unasimamia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utaratibu uliotolewa na Wizara kuwataka Mabalozi kutoa taarifa Wizarani na kadhalika na kadhalika ambazo zimezungumzwa katika Kambi ya Upinzani kwenye taarifa yao, naomba nitoe maelezo haya kwa kirefu ili yaeleweke ili baadaye labda kila mtu apate ufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaolalamikiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani unarejea Waraka wa Rais Namba Mbili (2) ambao ulitolewa mwaka 1964 na unatoa muongozo kuhusu utaratibu wa mawasiliano kati ya Taasisi za Serikali na wanadiplomasia wanaoziwakilisha nchi zao na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini. Utaratibu huo si mpya na wala haujaanza kutumika Awamu hii ya Tano ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli bali umekuwa ukitumika tangu mwaka huo 1964 kwa lengo la kuwa na utaratibu mahususi unaotakiwa kufuatwa ili kuweka mtiririko mzuri wa Mawasiliano baina ya Serikali na Taasisi tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya waraka huo, Mabalozi hawatakiwi kuomba ruhusua kama ilivyoelezwa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani bali hutakiwa kutoa taarifa ya maombi yao ya miadi au safari za nje za kituo chao cha kazi, yaani kama ni Dar es salaam, ili kutoa fursa ya Wizara ya Mambo ya Nje ambao ndiyo wasimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na kumbukumbu kuhusu miadi hiyo na kuratibu. Uratibu huo haupo Tanzania peke yake, bali hufanyika katika nchi zote

duniani na kuwawezesha Mabalozzi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa kuwafikia kwa wepesi viongozi na taasisi mbalimbali za kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuviwezesha vyombo vya Ulinzi na usalama kuhakikisha usalama wa Mabalozzi hao katika nchi hiyo husika wawapo mikoani au sehemu nyingine yoyote. Hivyo Waraka huo wa Kibalozi, unatajwa katika maelezo ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara yetu ikiwa ni utaratibu wa kawaida wa Wizara kuwakumbusha Mabalozzi na taasisi za Serikali kuhusu wajibu wao katika Mawasiliano husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu waraka huo ulipotolewa, Mabalozzi wameendelea kufanya kazi zao vizuri kama kawaida na hatujawahi sisi kama Wizara kupata malalamiko yoyote kutoka kwa Mabalozzi hao wala taasisi hizo; na wala hawajawahi kuhamishwa kwa sababu waraka huo ni sehemu tu ya utekelezaji wa sheria ile inayohusiana na mahusiano ya kidiplomasia iliyotungwa mwaka 1963. Hivyo napenda kutoa wito kwa watumishi wote wa Serikali pamoja na taasisi zake, Mabalozzi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa waendeleo kuzingatia waraka huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea, katika taarifa ile ya Kambi ya Upinzani, ilitumia tu sehemu moja na ikasema tu na ikataja *article* ile ya 41, lakini nataka niwasomee hapa, naomba kwa ruhusa yako Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze kutoa *quotation* hiyo. Katika *section* ya pili ya *article* hiyo ya 41 inasema:

"All officials business with receiving state in entrusted to the mission of the same state shall be conducted with or through the minister of foreign affairs of the receiving state or such other ministry as be agreed. Kwa hiyo, waraka ule ni *supplement* tu ya hii sheria ambayo hata wao wanaitambua. Niliona nitoe maelezo haya yaeleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la *remittance* kutoka *diaspora*. Ni kweli hatuna hesabu kamili ya *remittance* zote zinazofanywa lakini katika taasisi ambazo sisi tumezifanyia kazi, taasisi kama ya CRDB, Bank ya Watu wa Zanzibar, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) na Mfuko wa Mitaji (UTT), tunachojua ni kwamba kwa mchango wa *diaspora* so far kuanzia mwaka wa 2013 mpaka 2015 katika Taasisi hizo tunajua kwamba *diaspora* wamechangia karibu milioni 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujibu hilo, niende kwenye suala la visa kutoka nje ya Tanzania. Kuna suala ambalo limeulizwa kwamba Uingereza wanatoa visa zao kule Pretoria-South Africa na Canada wanatolea Nairobi, Australia wanatolea Nairobi na kadhalika na kadhalika. Tunasema hivi, ili kubana matumizi, nchi mbalimbali duniani zikiwemo zilizotajwa hapo juu,

zimeweka mfumo wa kuweza ku-centralize huduma zao za utoaji wa visa na hizi zinaratibiwa kutokana na wao kwa matakwa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama Tanzania hatuwezi kuwalazimisha wao kufuata utaratibu wa kwetu ila tunaweza tu kushauriana nao na kuwashawishi. Kwa hiyo, ule mtindo wa kutoa visa labda kwa Watanzania kupata visa zao kupitia South Africa, sisi tunajua kwamba hawaendi lakini wana process wao wenyewe na wao wameamua kutolea visa South Africa hatuwezi kuwalazimisha. Hata hivyo, tuahidi tu, kwa sababu sisi ni Wizara ambayo inajali mahusiano na taratibu, tutajaribu kuendelea kuwashawishi ili jambo hilo lifanywe kama lilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushiriki wa Ubalozi wetu Washington katika msiba wa Mtanzania aliyeuawa Houston-Marekani Marehemu Andrew Sanga. Ubalozi ulishiriki kwa kuhudhuria ibada na kutoa rambirambi kupitia Jumuiya yetu ya Watanzania wanaoishi Houston. Aidha, Ubalozi uliwakilishwa na Afisa wetu wa Ubalozi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kutokuwepo kwa Balozi kwa Washington katika msiba ule siku ile ni kwamba Balozi huyo alikuwa anamwakilisha Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli katika Kongamano la Watanzania lililofanyika Dallas-Marekani. Hata hivyo, kama nilivyosema kwamba, Balozi alimtuma Afisa wa Ubalozi kumwakilisha katika msiba huo, kwa hiyo nataka kuweka taarifa hii wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vigezo vya kufungua Ubalozi. Niseme tu kwamba, kwa mujibu wa *article* namba 5 ya Mkataba wa Vienna kuhusu mahusiano ya *Ki-consular* ya mwaka 1963, ziko sababu kadhaa zinazoweza kuchochea kufunguliwa kwa Ofisi za Ubalozi. Baadhi ya sababu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongezeka kwa wigo wa mahusiano kati ya Tanzania na nchi husika;
- (ii) Kuongeza wigo wa kuendeleza mahusiano ya Kibiashara, Kiuchumi, Kiutamaduni; na
- (iii) Ni kuwa na fursa ya kuwahudumia Watanzania waliopo katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoona kwamba katika nchi hizo tunao Watanzania kwa hiyo, hiyo inatusukuma sisi kuhakikisha kwamba tunaweka Ubalozi sehemu husika na vile vile kuwa na Wawakilishi katika nchi husika ili kukuza uhusiano wetu na nchi inayohusika. Ili kwenda sambamba na vigezo hivyo, kwa kuwa hatuwezi kufungua Balozi kila sehemu na uwezo kama mlivyojua kwamba bajeti ni ndogo; lakini kwa mwaka huu na katika mpangilio

na Mkakati wa Wizara tumeweka katika balozi ambazo tunategemea labda tutazifungua tukipata pesa baada ya kufungua ile ya Quwait mwaka huu. Katika mkakati huo, tukipata pesa, tumepanga kufungua Ubalozi Qatar, Uturuki, Korea ya Kusini, Israel, Namibia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali inavyowashughulikia Raia wa Tanzania waliopo Magerezani. Wakati kuna swali ambalo limeuliza kuhusu Maafisa Uhamiaji wanafanya kazi gani katika Balozi zetu? Moja ya kazi ambazo wanazifanya ni kuhakikisha kwamba wanaweza kwenda kuwatembelea wafungwa hao wanapokuwa gerezani na kujua matatizo waliyokuwa nayo na kutoa utatuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Balozi za Tanzania zina utaratibu wa kuwatembelea raia wa Tanzania waliopo gerezani. Utaratibu huo unafanywa kwenye balozi zetu za China, India, Japan na sehemu nyingine ambazo tunazo balozi zetu. Pale ambapo tunasikia na tunapogundua kwamba tunao Watanzania kwenye magereza hayo hufanya hivyo kwa sababu ni moja ya wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafungwa kuja kutumikia vifungo nyumbani, utaratibu huo upo. Nchi yetu imeingia kwenye mikataba ya kubadilishana wafungwa, lakini vilevile katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunayo sheria ambayo tumekubaliana kwamba inapotokea kuna mfungwa anayetoka Uganda, Kenya, Burundi na Rwanda na sasa Sudan ya Kusini basi tuna utaratibu wa kubadilishana na *practice* hiyo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kuhusu hoja kutokana na mwelekeo wa dunia ulivyo hivi sasa kuhusu uhusiano na ushirikiano wa Kimataifa, Serikali kupitia Chuo cha Kidiplomasia, iweke mitaala ambayo itazalisha wataalam wengi wa fani ya diplomasia kiuchumi. Aidha, Chuo kitawanye na kujipanua kuandaa mafunzo ya Kidiplomasia. Maelezo yetu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuanzisha Sera ya Mambo ya Nje inayotilia msisitizo wa Kidiplomasia ya Kiuchumi, Chuo kimeandaa mitaala maalum kufundisha Diplomasia ya Uchumi na tayari Chuo chetu kinatoa shahada ya Uzamili katika Diplomasia ya Uchumi; na Maafisa wa mambo ya nje wote walioko Tanzania na wale ambao wako katika balozi zetu nje ya nchi, wote wamepata mafunzo hayo; na moja ya kigezo ambacho kinamfanya aweze kutoka nje ya Tanzania ni pamoja na kupata mafunzo hayo. Aidha, mipango ya baadaye ni kuongeza mafunzo katika ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kutoa fedha kwenye balozi zetu nje ili kueneza sera ya diplomasia ya uchumi ambayo itaongeza uwekezaji na Watalii. Fedha za matumizi Ubalozi hutengwa kulingana na ukomo wa bajeti na hutolewa na Hazina kwa mwaka hadi mwaka. Tutaendelea kuwashawishi Bunge hili pamoja na Hazina kuhakikisha kwamba ukomo huo wa bajeti unakuwa ni mkubwa ili kuhakikisha kwamba tunawawezesha vijana wetu au watumishi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kuelekeza fedha ubalozi kwa ajili ya kuwarejesha maafisa wetu waliomaliza muda wao katika balozi, aidha, Wizara iangalie uwezekano wa kuacha kutoa barua kwa maafisa kurejea nyumbani kwa fedha kwa ajili ya shughuli hiyo kabla ya fedha hiyo haijatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kwamba, ni kweli kwamba kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa mambo ya nje, ni lazima maafisa wa mambo ya nje warudi nchini kila baada ya miaka minne ili kubadilishana na Maafisa wengine. Changamoto kubwa inayotukabili katika Wizara yetu katika kutekeleza kanuni hiyo, ni ufinyu wa bajeti, ambayo nimekwishaizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa taarifa tu, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imerejesha Mabalozi watano, watumishi tisa na wengine kumaliza muda wao wa kufanya kazi Ubalozi. Mabalozi hao wamerejeshwa kutoka katika Balozi zetu za Tanzania Rome, Tokyo na maelezo zaidi mtayapata tutakapokuwa tunawapa majedwali ya majibu ya hoja zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja binafsi. Mheshimiwa Job Lusinde alikuwa amejaribu kutuuliza, tunazingatia umuhimu wa Chuo cha Diplomasia katika kuwajengea uwezo viongozi wake na Wanadiplomasia? Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kuwawezesha Chuo hicho kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Tunasema katika mwaka wa fedha 2016/2017, Chuo kimetengewa kiasi cha bilioni 3.1, kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi milioni 882.2 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi bilioni 2.2 ni kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi, mengine mtayaona katika *sub votes* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masele Steven, ameuliza Wizara imejipangaje ili kuhakikisha uwezekano unaoongezeka kwenye sekta za kilimo, biashara na viwanda kama ilivyo katika Sekta ya Madini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Wizara imekuwa ikitumia mahusiano mazuri tuliyonayo na nchi nyingine kuvutia uwekezaji hapa nchini. Hii inafanyika kupitia itifaki ya soko la pamoja, kutumia balozi zetu mbalimbali huko nje ya nchi, viongozi wetu kwenye nchi mbalimbali, ziara za viongozi mbalimbali wanaotembelea katika nchi hizo na kadhalika; lakini maelezo zaidi mtayapata pale tutakapokuja kuwaletia majibu katika jedwali la hoja mlizoziulizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la Wabunge wa Afrika Mashariki. Naomba nitoe tu taarifa kuwa mara tu baada ya uchaguzi wa Wabunge wale ambao sasa hivi wanafanya kazi katika Bunge lile, Wizara iliitisha kikao baina ya Wabunge wa Afrika Mashariki, Ofisi ya Bunge na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kujadiliana namna bora ya kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge wa EALA kufanya kazi kwa ufanisi na bila kero. Yote aliyoyasema Mheshimiwa Msigwa yalijadiliwa na kutolewa uamuzi na wao wanafahamu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara zote, Wizara wanapokuwa wanaanza session zozote aidha Dar es Salaam au Arusha tunafanya nao vikao wanapoanza au wanapomaliza ili kuwapa mikakati. Niwaeleze tu, sisi tunapokwenda katika vikao vile, viwe ni vikao vya Bunge la Afrika Mashariki ama vikao vya Mabaraza ya Mawaziri tunakwenda na *position* ya Tanzania na inashauriwa na wale ambao nyinyi mnaowaita Mabalozi wa nyumba kumi kumi na matokeo ya kazi zao za taaluma na ujuzi zimeonekana. Ushindi wa bomba la mafuta la kutoka Tanga kwenda Uganda, hilo pia ni fundisho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mtu ambaye anaweza kuwasaidia katika utafiti, tunae yuko Wizarani na wanajua. Vile vile nisisitize tu, Mheshimiwa Waziri wa Sheria aliposema kwamba hawa Wabunge makao yao ni Arusha, lakini unaposema kwamba tuwatafutie ofisi, ofisi Dar es salaam ziliwekwa. Vile vile hawa watu mfahamu kwamba ni Wabunge wanaotoka katika Majimbo tofauti. Kuna wanaotoka Dar es Salaam, Dodoma, Mara na Zanzibar. Sasa, unaposema watafutiwe ofisi *centre* yao iko wapi? Sisi tumeendelea na tutaendelea na wao wanajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshiriki katika ku-coordinate mambo yao yote, wanapotafuta maelezo wanapewa, wanapohitaji kukusanya wadau tunafanya na Wizara hii itaendelea kufanya hivyo kwa sababu tumepokea jukumu hili kama viongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufuatia uchaguzi wa Burundi 2015 na ule wa Uganda Februari, 2016, makundi ya wanasiasa, wanaharakati wa haki za binadamu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA SHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dokta Suzan Kolimba. Sasa Waheshimiwa Wabunge namkaribisha mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa

Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga ili aweze kuhitimisha hoja yake.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nichukue nafasi hii ya kuhitimisha mjadala huu wa hoja yangu kwa kutoa shukrani za pekee kwa Wabunge wote wa Bunge hili Tukufu kwa mchango wenu wa mawazo, kwa maandishi, lakini pia naamini kabisa kwamba Wizara yangu itaendelea kutegemea mawazo ya ujumla ya Bunge hili katika kutekeleza Sera zake na mipango yake ya kuendeleza uhusiano na nchi za nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wangu ambaye amemaliza tu kujibu baadhi ya maswali. Pia natoa shukrani za pekee kwa wafanyakazi katika Wizara yangu, Wakurugenzi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na wengine wote ambao tumeshirikiana katika kuandaa hotuba hii na kujibu maswali ambayo yamejitokeza ndani ya Bunge hili Tukufu

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru mke wangu Elizabeth Mahiga ambaye amekaa pale, ameniunga mkono na ameendelea kunifariji katika utendaji wangu wa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu maswali yote moja baada ya lingine lakini mengi ya maswali haya tutayajibu kwa maandishi. Nataka kusema yale ambayo ni ya msingi kuhusu Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni suala zima la *Diplomacy* ya jumla ya Tanzania, halafu nitakuja kuzungumzia *Diplomacy* ya uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Diplomacy* ya Tanzania ni urithi na tunu ya pekee kabisa katika Afrika; lazima tuienzi, tuidumishe na tuilinde. Ni kati ya vitu ambavyo tumerithi tangu kwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na viongozi wengine katika Awamu mbalimbali. Bara la Afrika na dunia inatambua hivyo. Nawaomba mkipata fursa mtembelee katika majukwaa ya Kimataifa. Kuna mikutano mingine haiwezi kuanza kama Tanzania haipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inapotoa hotuba inasikilizwa na ulimwengu. Kama watu walikuwa wametoka kunywa chai katika mikutano ya Kimataifa, Tanzania inapoanza kuzungumza waliokuwa wanavuta sigara na kunywa chai wanarudi kwenye ukumbi. Hii ni baadhi tu ya heshima ambayo tunaipata Kimataifa na hapa katika Bara la Afrika na kwa kweli ni kitu ambacho lazima tujivunie na ni jukumu letu; na hakuna mahali pa kuenzi diplomasia ya Tanzania kama ndani ya Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa diplomasia yetu imekua na ni sahihi kabisa kwamba sasa lazima tujikite kwenye diplomasia ya kiuchumi. Diplomasia ya kiuchumi maana yake nini? Ni kweli tumekuwa na kama wimbo tunasema, diplomasia ya kiuchumi lakini ukimuuliza mtu maana yake nini na ukitoa kauli kwamba Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje haijatekeleza diplomasia ya kiuchumi si sahihi hata kidogo! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hutakuta viwanda kwenye Wizara yangu, hutakuta madini kwenye Wizara yangu, hutakuta mazao ya biashara kwenye Wizara yangu, lakini Wizara yangu ndiyo inayoweza Wizara zote ziweze kuungana na ulimwengu katika kutekeleza Sera zao tofauti. Msione vinaelea, vimeundwa! Muundaji ni Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo inayofungua milango na madirisha ya mahusiano kati ya Serikali, sekta binafsi na Mashirika Yasiyo ya Serikali. Wizara hii ndiyo inayoratibu shughuli zote hizo. Kwa hivyo katika *Economic Diplomacy* Wizara inatakiwa kuleta mawasiliano kati ya Serikali nyingine, viwanda na Mashirika mengine. Kwa hivyo *Economic Diplomacy* ni kitu ambacho lazima kifuatiliwe kwa karibu na isiwe ni kitu cha mpito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima pia tuelewe na tufafanue na tuelewane, kwamba katika *Economic Diplomacy* unatengeneza *framework* ambayo itakuonesha dira ya wewe kama nchi kuhusiana na nchi nyingine na kama kuweka kitega uchumi ili uinufaishe nchi yako. Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo inayofungua mlango halafu inaendelea kuratibu, hiyo ni kazi moja (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya pili ya *Economic Diplomacy* ni pale ambapo Tanzania inakwenda katika majukwaa ya Kimataifa na mahali kama pale unazungumza sio peke yako na wenzako. Kama ni suala la biashara, viwanda, au uwekezaji, vitu hivyo utavipata katika jukwaa na mtu wako anayekwenda pale kwenye jukwaa awe na uwezo wa kusema, kutetea na awe na uwezo wa kuwaletea nyumbani vitu kama hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuwahakikishia Wabunge kwamba diplomasia yetu hasa ya uchumi imejikita katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Tanzania inahesabika kama nchi ambayo uchumi wake unakua haraka kuliko nchi nyingine za Afrika, kwa asilimia saba. Sasa kama Tanzania inakua hivyo, hicho ndiyo kipimo cha *Economic Diplomacy*. Katika Afrika ya Mashariki, Tanzania ni ya kwanza katika uwekezaji ndani ya Afrika Mashariki lakini pia kutoka nje. Hivyo ndiyo vipimo vya *Economic Diplomacy*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwa kifupi tu kuwaonesha baadhi ya masuala muhimu ya *Economic Diplomacy* ambayo tumeyavuna hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji ni mfano tu! Uwekezaji wa kiwanda cha cement cha Dangote. Uwekezaji ulioifanya Uchina ichague Tanzania kuwa moja ya nchi nne muhimu za uwekezaji. Wachina wenyewe wamesema, Balizi wenu pale Beijing ndiye aliyewashawishi vya kutosha kwamba Tanzania iwe moja ya nchi ambazo zitapewa kipaumbele katika uwekezaji wa viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotoa hotuba yangu jana nimesema; sisi tutajikita kwenye diplomasia ya viwanda. Yaani hiyo diplomasia ya uchumi naipandisha safu. Tutajikita sasa kama Wizara kwenye diplomasia ya kushawishi na kuleta viwanda. Vile vile katika hotuba ile ile nimesema kukuza diplomasia ya viwanda haifiki popote peke yake, lazima iende sambamba na diplomasia ya kilimo kwa sababu hivi viwanda vitategemea kilimo. Lazima iende sambamba na diplomasia ya miundombinu kwasababu hivi viwanda vitahitaji umeme na uchukuaaji na usafirishaji. Kwahivyo naweza kuwaelezeni ile safu ya *Economic Diplomacy* baada ya kuieleza kwamba ni ya pamoja na ya katika majukwaa sasa inapandishwa grade na Wizara yangu na itaitwa *Economic Diplomacy of Industries*. (Makofi) 0714197930

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utekelezaji wake utakuwaje? Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli amesema; katika Wizara yako punguza watu na napunguza watu, nimepunguza wengi. Hata hivyo, anasema; unapopunguza hawa watu lazima upange na kupangua watu wako. Si tu kuwapeleka kwenye *embassies*, kwamba sasa mimi ni zamu yangu – *posting*, hapana! Nani aende wapi na kule aliko awe na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *Economic Diplomacy* si tu ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, lazima tushirikiane na Wizara nyingine huko nje kama Utalii, Viwanda na Wizara nyingine ambazo zinahitaji wawekezaji lakini wanahitaji ushawishi wa pekee. Kwa hivyo, kutakuwa na kupanga na kupangua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia chuo chetu cha kule kurasini kitatoa mafunzo maalum ambayo yanaitwa *The Economics of Economic Diplomacy*. Lakini pia *Economic Diplomacy* tutaieneza na tutaifuata si tu kwa sababu ya mafunzo lakini pia ndani ya idara yetu tutatengeneza kitu kinaitwa *Economic Unit* ambayo itakuwa ni *unit of economic intelligence* na ambacho kitakuwa ni mtambuka, uchumi mtambuka wa sehemu zote za aina hiyo. Hiyo ndiyo aina ya *diplomacy* ambayo tunataka kuieneza, kuitetea na kuishuhudia katika Wizara yetu ya Mambo ya Nchi za Nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nirudie tena lile suala la *diaspora*. Katika *diaspora* huwezi kuzungumzia *diaspora* bila kuitengenezea *profile* yake, nani yuko wapi na nani anafanya nini? Kuna Watanzania ambao ni wanafunzi, kuna Watanzania ambao ni wataalam wanafanya kazi zao huko, kuna Watanzania ambao ni wazamiaji; lazima tukubali hilo na kuna Watanzania kama nilivyosema ambao wako kwenye majela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni jukumu letu na tumeanzisha idara maalum katika Wizara yangu inayoitwa Idara ya *diaspora*. Tunashirikiana na wenzetu walio huko nje na pia na Serikali nyingine ili tuweze kuwatambua Watanzania wetu. Kuna wengine wanasema siji kwenye Ubalozi nitakamatwa, lakini hao hatimaye wanakuja wakipata shida na sisi tuko tayari kuwapokea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaweka mkakati maalum si tu kuwatambua lakini katika *diaspora* kuna wale wenye ujuzi wa pekee na wako tayari kuja huku nyumbani ama kwa miezi sita au mwaka mmoja wafanye kazi katika Wizara mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nilizungumzie tena suala la uraia pacha au utaratibu mwingine wa kuwawezesha Watanzania walio nje washiriki katika mchakato wa uchumi. Hawa Watanzania walio nje ni wabunifu kweli kweli, wamekuwa na makongamano ya aina mbalimbali, mengine ya utalii, mengine uwekezaji, mengine ni ya kusaidiana tu kama jamii na lazima tuwaelewe zaidi ili tuweze kuwasaidia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafurahi kama ninyi wenyewe kwa umoja wenu au mmoja mmoja mnaweza kutupatia taarifa. Juzi hapa kuna Mbunge kutoka Upinzani amenifuata, anasema Balozi, sijui Waziri/Balozi; nina ndugu yangu alikamatwa na madawa, akatiwa ndani Nigeria, sasa amefunguliwa na lazima arudi nyumbani, Je, Wizara yako inaweza kutusaidia? Mara moja nilichukua hatua za kumrudisha yule kijana na juzi nimepata barua kutoka familia yake wanasema Waziri tunakushukuru. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tukumbushane kwamba hili suala la *diaspora* tumelizungumza mara kwa mara, lakini nina hakika tutafika mahali ambapo itabidi tukubaliane kwamba hawa *diaspora* wawe ni sehemu gani ya Watanzania walioko huko nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa kuzungumzia suala la Mheshimiwa Rais, Dkt John Pombe Magufuli, kwamba haendi nje. Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ana sababu za kutokwenda nje, kwa sababu kuna mambo ambayo lazima afanye hapa nyumbani na wakati ule alikuwa anafanya uteuzi na kukamilisha Serikali yake. Hata hivyo, ningependa

kuwaambia kama wengi hamjui, mimi kama Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje siwezi kwenda popote bila kutumwa na Mheshimiwa Rais! Kila ninakokwenda napata ridhaa ya Mheshimiwa Rais na maagizo ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia huyu Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli amekuwa mkarimu sana kukutana na Mabalozi. Siwezi kusoma orodha yote hapa lakini amekutana na kila Balozi aliyepo Tanzania ambaye anataka kukutana naye na mazungumzo yanakuwa mazuri tu na baada ya hapo yanafuata maagizo ambayo mimi kama Waziri mwenye ridhaa nayatekeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili nimwongeze pia Waziri wetu Mkuu. Juzi hapa nimesafiri naye, katika kile kipindi cha siku mbili cha kufanya kazi ameweza kuwashawishi wawekezaji wengi tu! Wengine wakiwa wamekubali kuleta kiwanda kizima cha matrekta hapa Tanzania. Kampuni ya *Shell* ambayo ndiyo mwekezaji mkuu kwenye gas yetu walikuwa wanasuasua, Waziri Mkuu aliwaita, tukakaa, tukazungumza nao. Wakasema; haa! Sasa tunaelewana na Tanzania na gesi tutaanza kuichimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumzie suala la mjusi. Wiki mbili zilizopita nilikuwa Ujerumani kuangalia mjusi, hapana! Nikawauliza Wajerumani kwamba jamani yule mjusi vipi. (Makofi/ Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajerumani nao wakaniambia vipi ninyi Watanzania. Nikawaambia kwa nini anasema kwa muda mrefu sasa, kumekuwa na Watanzania *delegation after delegation* inayokwenda Ujerumani kutazama mjusi. *Delegation* ya kwanza anasema ilikuwa na watu 19 kutoka Tanzania na ikiongozwa na *National Museums*, wakazungumza wakakubaliana kabisa jamani tufanye nini kuhusu huyu mjusi?. Wakawapa *options* anasema mnaweza kumchukua, lakini mkitaka kuchukua lazima kutafuta ndege maalum ambayo ni *refrigerated* na chemba nzima ambayo huyu mjusi atawekwa iwe katika *temperature* fulani na kila baada ya muda fulani huyu mjusi awe anapakwa vitu fulani, vinginevyo atayeyuka kama *temperature* ile haipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wakasema lakini kama mnataka sisi tutawasaidia. Baada ya hapo yule aliyeongoza ule ujumbe nasikia alifariki. Ukaenda ujumbe mwingine safari hii wakiwa Watanzania 24 kule Ujerumani, wakaenda pale kuzungumzia mjusi, wakasema sisi sasa tunarudi nyumbani na hili tutalipeleka kwa mamlaka husika tuanze kulitekeleza. Sasa mimi juzi nimeulizwa, jamani *what is the problem with you*, mnakuja tunazungumza tunakubaliana mnaondoka halafu mnakwenda tunaona tena *delegation* nyingine inarudi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukakubaliana hivi, tukasema ninyi Wajerumani pamoja na kuwa mnatupa misaada, juzi wametupa ndege za doria kwa ajili ya magaidi, ninyi mna pesa na mna uwezo na mnaweza kutusaidia pesa kama ni kumrudisha mjusi arudi au mnaweza kutusaidia fedha za maendeleo za ziada na zile ambazo mnatupatia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamenipa changamoto, wanasema Waziri Mahiga rudi Tanzania, usiorodheshe tu mjusi maana pale alipogunduliwa huyu mjusi, wanasema kuna mijusi mingine ambayo inaweza ikachimbwa pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wakasema pamoja na kuwa sisi tulikuwa pale kama wakoloni nawaombeni mwende mkaorodheshe maeneo yote ya kihistoria na urithi ambayo yanatokana na kuwepo kwa Wajerumani ndani ya nchi yenu. Tunaamini hii itakuwa ni kivutio maalum kwa watalii kutoka Ujerumani. Wakasema siyo mjusi tu, siyo liemba, siyo barabara ya Bismarck tu, bali ni shule, ni mahospitali hata maeneo mbalimbali ambayo yanatuunganisha sisi na Ujerumani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata taarifa kwamba pamoja na kuwa Wajerumani walirudisha fuvu la Mtwana Mkwawa, mwaka 1954 kumbe nasikia kuna mafuvu na mabaki ya Watanzania wengi tu kwenye *museum zoo*. Hii ni mojawapo ya maeneo ambayo tunaweza kwenda kuzungumza nao. Ukweli ni kwamba, wao wako tayari tukiongozana, tukishirikiana nao, kwamba tuweze kuhamasisha misaada ambayo italeti tija kwa Tanzania ambayo inatokana na kuwepo kwa Wajerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la mjusi kwa kweli nadhani ni suala muhimu sana na lazima tulishughulikie. Nilipokutana na *Deputy Minister* wa Ujerumani, huyu ndiye alitoa ahadi kwamba maeneo alikotoka yule mjusi kuna barabara ambazo zinahitaji kujengwa. Ameeleza pia kwamba kuna maeneo ambayo Wajerumani waliishi, kuna barabara inaitwa sijui *Bismarck road*, nyingine inaitwa sijui *Bismarck rock*, sijui nyingine Bismarck nini; vyote hivi vinaashiria uhusiano fulani kati ya Wajerumani na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajerumani wamesema hiyo timu iundwe, tuanze kutazama vile vitu ambavyo Serikali ya Ujerumani inaweza ikagharimia na inaweza ikafanya ni sehemu ya urithi wa historia kati ya Tanzania na Ujerumani, hilo wametoa kabisa kama *blank cheque* na sasa changamoto ni kwetu na nimeahidi kwamba hilo nitalifuatilia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Ujerumani inasema hakuna nchi ambayo kihistoria Afrika tuko karibu kama Tanzania, pamoja na tofauti zetu

ambazo zimejitokeza hapa katikati nadhani suala la mji ni moja tu kati ya yale ambayo tunaweza kunufaika kutokana na uhusiano wetu na Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia juu ya majirani. Tulipokuwa Uingereza juzi na Waziri Mkuu, msaidizi wa John Kerry, *Minister of Foreign Affairs* au *Minister of State* wa Marekani, ambaye ni namba two wake aliomba kukutana na sisi na Waziri Mkuu. Wakasema Marekani inaamini kabisa kwamba katika ukanda wa maziwa makuu au hata katika Afrika, nchi ambayo inaweza ikazungumza na Kongo na ikasikilizwa ni Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, tunaombeni Watanzania mjenge uhusiano wa karibu na Kongo na pia muisaidie Kongo, kuwa na mtangamano wa kisiasa. Suala la kuanzisha Ubalozi mdogo Lubumbashi ni la siku nyingi sana. Sasa hivi, tunaitisha kikao kinachoitwa *Joint Permanent Commission* kati ya Tanzania na Kongo, kwa sababu inaelekea kwamba wanaweza kuanza kutafuta njia nyingine za kupitishia bidhaa zao. Tukiitisha kikao kile, tutazungumzia suala la *consulate* ya pale Lubumbashi lakini pia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba umalizie

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutazungumzia masuala mengine ya uhusiano na hawa majirani zetu. Siwezi kuzungumza juu ya Burundi kwa sababu inajulikana lakini, ni kwamba nchi yetu imekuwa ikipokea wakimbizi. Hata kabla ya uhuru, wakimbizi wa kwanza kuja Tanzania ilikuwa mwaka 1959 walitoka Rwanda, hata uhuru hatujapata. Kwa hivyo, tuna jukumu la pekee na Jumuiya ya Mataifa nimewaambia lazima mtusaidie na lile suala la mazingira bora na mengineyo yashughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani na nitaendelea kuzungumza nanyi, Upinzani nawashukuruni sana, Ndugu yangu Msigwa, tutazungumza mengi, tutasaidiana, tutabadilishana mawazo na tuendelee kuwa karibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapa, nadhani kuna kutoa hoja. Kutoa hoja baada ya Kamati ya Matumizi kupitisha vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja (Kicheko/Makofi)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mahiga hoja imeungwa mkono na wengi. Katibu tuendelea na utaratibu!

NDG. RAMADHANI ABDALLAH - KATIBU:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

KIF. 1001 *Administration and HR*

Management...Sh. 10, 462,298,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe katika kifungu hicho tumepokea majina tayari kutoka kwa *Chief Whip* wa vyama. Kwa hiyo, tutakuwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Munde Tambwe. Kwa hiyo, tunaanza hapa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona Mheshimiwa Waziri ameeleza kwa kina sana suala zima la majukumu ya Wizara yake ambayo mwanzoni nadhani hata wenzetu walikuwa hawajaelewa vizuri kwamba Wizara hii inafanya mambo gani. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kumpongeza, naomba tu anipe ufafanuzi wa kifuatacho:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maono ya Mheshimiwa Rais ni kuwa na nchi ya viwanda, ni kuwa na nchi ya uchumi wa kati na Wizara hii kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ndiyo kioo cha nchi yetu na hasa ndani na nje ya nchi. Pia kwa kuwa uchumi wa viwanda huu unategemea aina mbili wawekezaji walioko ndani ya nchi na walioko nje ya nchi wanataka kuja kuwekeza hapa ndani ya nchi. Sasa, Waziri anaweza kunipa ufafanuzi amejipangaje ili kuona kwamba sasa yeye na Wizara yake wanaakisi maono ya Mheshimiwa Rais na wanakuja na mpango mkakati ambao utasaidia kutimiza haya malengo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, kwa kuwa uwekezaji katika sekta mbalimbali hapa nchini, sekta muhimu ni ya kilimo na Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri kabisa, nimeridhika na majibu yake kabisa, maelezo yake safi kabisa tena nadhani alikuwa ameshachelewa kuwa Waziri wa Mambo ya

Nje siku nyingi, alikuwa ameshachelewa ana uzoefu mzuri na Watanzania tunapaswa kutumia uzoefu alionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, katika Wizara yake hii ambayo amesema kwamba wameamua kupunguza baadhi ya wafanyakazi au watumishi kulingana na mahitaji ya Wizara hii, sasa nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba huu mkakati anategemea kuutimiza kwa namna gani? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naulizwa kuhusu mkakati wa viwanda. Kwanza kabisa Wizara iko katika hatua ya kutazama upya Sera ya Diplomasia ya Tanzania. Pia katika hii sera ya viwanda, ambapo viwanda vitatekelezwa kwa kipindi au kwa awamu ili hapo tutakapofika mwaka 2025 tuweze kufika uchumi wa kati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama utanza na kiwanda ambacho kwanza kinaanza na *value addition*; korosho, tumbaku, kahawa, hata mahindi, hii *value addition* lazima iwe karibu na pale mazao ya kilimo yaliko. La pili, tunazungumzia REA kupeleka umeme kijijini, huu umeme siyo kwenda tu kuweka *bulb* moja isome, ya kusomea kitabu itawasaidia watoto, lakini REA iwe ni *transformative* kuwe na mashine ndogondogo ambazo utakuwa ndiyo msingi wa viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikisema diplomasia ya viwanda lazima iende sambamba na diplomasia ya kilimo na miundombinu ndiyo maana yangu hiyo. Kwa hiyo tutaanza katika maeneo ambayo kwanza tunaanza na viwanda vidogo tunakuja viwanda vya kati, lakini viwanda huwa vinajiambukiza, ukianza kiwanda kimoja kinaleta kiwanda kingine. Sasa huo ndiyo mkakati, masharti na maagizo nitawapa Maofisa wangu, ni kwamba kama wewe unakwenda mahali si tu kumtafuta mwekezaji, lakini pia Serikali ambayo itatusaidia kutengeneza *technicians*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapeleka umeme vijijini itakuwa kama shule zile, tulipeleka watu tukafungua shule Walimu hatuna, sasa kama unapeleka umeme *technicians* unao? Watakaohakikisha kuunganisha umeme na kufanya *repair* na kuunganisha mashine itakayovuta maji ili kijiji kipate maji na lile bomba likiungua nani ata-repair, mnaanza kusema katuletee *technicians*. Kwa hiyo, lazima kuwa na *package* na hii *package* ieleweke na sisi wa Wizara ambao ni wawezeshaji, tunakwenda tunajua hatua hii tutahitaji hiki, hatua hii itafuata. Huo ndiyo mkakati. (Makofi)

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwa kweli ameyajibu katika kiwango cha hali ya juu. Labda tu napenda niombe ufafanuzi wa mwisho, kwamba kwa kuwa wajibu wa Mabalozzi wetu nje ya nchi katika kusimamia uchumi wa viwanda, ni pamoja na kuwa Mabalozzi ambao wana damu changa na ambao wana uwezo wa kushawishi na kufanya kazi, haoni kwamba sasa kwa vile ameanza kazi hii, Mabalozzi ambao wameshachokachoka warudi nyumbani tupeleke Mabalozzi ambao ni vijana watakaochapa kazi waendane na hali ya sasa ya dunia? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Mawasiliano juzi alisema tuwape fursa vijana, haya mambo ya *computer* siyo kila mtu anayaweza, unaweza kufika umri fulani yanakushinda haya. Haya mambo ya *computer* na nini itakuwa ni sehemu ya hii *strategy* yetu, kwa hivyo lazima tukubaliane, mtu unafika pale huwezi ku-*operate* hizi; ni kweli kwamba siyo tu Mabalozzi, lakini pia vijana ambao watakuwepo, inawezekana kabisa wasitoke Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, wakatoka sehemu nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni zoezi kubwa ambalo lazima tulifanye, ndiyo maana mpaka sasa Rais ameteua Mabalozzi watatu tu na juzi tumelizungumza hilo lakini kwa mantiki hii kwamba tunafanya zoezi ambalo unaunganisha uteuzi na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, tumesema tutafungua Balozi nyingine, hizi Balozi zitokane na *savings* ambazo tutazifanya kwa kupunguza wafanyakazi na kuwa na tija zaidi ya wale wafanyakazi ambao tunawapeleka huko. Hii lazima iwe kazi ya pamoja na Wizara nyingine ambazo kwa pamoja tunatengeneza mkakati wa *industrialization*, lakini isiwe tu sisi peke yetu! Sisi ni Wizara mtambuka, sisi ni Wizara ambayo ina-*facilitate*! Inafungua milango na madirisha, lakini pia, lazima kuratibu. Ndiyo maana hata hawa Mabalozzi tunajua huyu anamwona nani, huyu anamwona nani, tunaweza kumwambia bwana kamwone yule; ndiyo utaratibu huo, si kuwabana. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Matumizi, napenda kuwakumbusha tuzingatia Kanuni ya 101(3) ambayo inataka wachangiaji katika Fungu la Mshahara wa Waziri kuzungumzia jambo moja mahususi la kisera.

Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nimshukuru baba yangu Mheshimiwa Balozi Maiga. Sasa naomba

usinigombanishe na Josephine, lakini nataka mambo ya uhakika kuhusu Chuo cha Diplomasia, yamekuwa mambo ya siasiasa tu, Chuo kile baba hakina hadhi, hakina uwezeshaji. Tulitangaziwa hapa tunampeleka mwenye *PhD* ya *Strategic Studies*! Bila pesa *PhD alone* inasaidia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kauli iliyokuwa ina *mention about targets*, kwamba, Chuo cha Diplomasia *once* hii bajeti inapita *number one* tunafanya hii, namba *two* hii, wanahitaji uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba maelezo ya kina, vinginevyo nitashika shilingi halafu Josephine nitaongea naye nje.

MBUNGE FULANI: Josephine mkwe wangu. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kabla sijateuliwa kuwa Waziri niliporudi kutoka nje nilikuwa nafundisha Chuo Kikuu na Chuo cha Diplomasia kwa kweli, unachosema ndicho nilichoshuhudia.

Naibu Waziri nikamwambia nenda ukatazame pale na kwa kweli, kuna *options* mbalimbali, lakini unalosema ni kweli kabisa. Sasa kiutawala naweza nikatengeneza hoja kwamba, jamani chuo hiki kinahitaji hivi na hivi. Kwa kweli, katika bajeti ya maendeleo zile bilioni nane kuna Kifungu fulani ambacho kitakwenda kwenye Chuo cha Diplomasia. Hata hivyo, nguvu yangu ni sehemu tu, nguvu ya pili ni ninyi wote hapa, mnisaidie, pamoja na Upinzani mnisaidie, ili kutengeneza hoja ya kisiasa ili tuweze kupata labda *allocation* kubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyowaambia moja ya tunu za Tanzania ni Diplomasia ambayo ni uwezo wa kuzungumza na kuwashawishi wengine. Siwezi kutoa ahadi hapa, lakini hili linazungumzwa na baadhi ya marafiki zetu kama wanaweza kutusaidia. Kuna nchi ambazo nazo zingependa kuleta wanafunzi pale na wakachangia katika hili. Kwa hivyo, hili ni moja la majukumu ambalo tumelivalia njuga kuhusu Chuo chetu cha Diplomasia. Kwa kweli, kina hadhi ya juu sana, kinaheshimika, kuna Wataalam pale, lakini kwa kweli, wanakwazwa na, hivi kukosa pesa kunaitwaje?

WABUNGE FULANI: Ukata!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukata! Kinakwazwa na ukata, lakini tusaidiane Wabunge, sisi kiutawala na ninyi kisiasa tuweze kutafuta njia za kukiinua kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kutoa wito. Sasa hivi chuo kile si tu kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia kwa ajili ya Wizara yetu, theluthi mbili ya wanaohudhuria chuo kile wanatoka Wizara nyingine. Wametambua umuhimu wa diplomasia ambayo inatoka mle ndani pamoja na haya matatizo. Mpaka juzi nimemwomba Mheshimiwa Masoud, nikasema bwana siku moja uje ukafundishe pale mambo ya kutengeneza bajeti, wajue bajeti, leo Mheshimiwa Masoud hayupo hapa; akasema yuko tayari kuja kunisaidia pale katika kuwafundisha vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala hili la Chuo chetu cha *Diplomacy* nadhani linahitaji kipaumbele cha pekee kabisa. Ni chuo ambacho kina mengi, kinaweza kutuletea mengi na Wabunge karibuni mkipata nafasi, mpitiepitie pale, kama siyo kusoma angalau kuangalia tu shida zetu. (Makofi)

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sasa sijui Balozi ameliwekaje hili, lakini inanzia kwenye sera zetu, hiki chuo kinapata matatizo kwa sababu, *it's Government owned*. Walipokuwa wanakwenda kwa Wafadhili wanaambiwa ninyi Serikali yenu haiwaweki kama *priority*, sasa watang'oka vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siyo suala tu na kama Bunge linapitisha bajeti Hazina haitoi, Wizara haisimami kukidaia chuo, sasa *what is the policy?* Tunakiwekaje hiki chuo ambacho tunatarajia *ki-train* watu wetu? Walimu wenyewe wako *so local*, hata *on job training* hawapati. Walimu wengine wamesoma hapo UDSM wamekaa pale hawajafika hata hapo Kenya *on a training* fupi! Sasa kweli jamani hii Sera ikoje hii? Wale wanaopika Wataalam wenyewe hawana utaalam! Hawana *motivating environment*, kweli Mheshimiwa Balozi, tutafika hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Sera iwe wazi kweli tuna *priority* gani kwa Sera yetu ya Mambo ya Nje na kwa hiyo hii *centre* ambayo ina-*train* watendaji wetu tunaiweka kwenye nafasi gani? Ziko humo lakini Bunge limepitisha bajeti mara kadhaa, tumeambiwa hata hii sasa hivi imesema zilizopitishwa hazikutolewa! Naangalia hii *development* hizo *eight billion* inasema *Policy and Planning*; chuo kina-*fit* wapi, sijui na kitatokaje hii pesa, sijui! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sijaridhika. Kama hakuna maelezo ya kina kukikwamua hiki chuo kutoka pale, natoa shilingi, naomba mniunge mkono nina hoja ya kushika shilingi. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri! Tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Mtulia! Tunaanza na Mheshimiwa Chumi!

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ni *beneficiary* wa hicho chuo na mazingira hayo anayosema Mheshimiwa pale kweli ni magumu kwa kiwango hicho anachosema na kunahitajika kwa kweli, jicho la pili, ili tuweze kunufaika ipasavyo. Sasa katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri amegusia kwamba, katika hiyo bilioni nane ya *development* sehemu itakwenda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika maelezo yake amesema kwamba, hata yeye alipofundisha pale amekutana na magumu hayo na anaona kabisa iko haja ya kulifanya jambo hili mtambuka kushirikisha pia Wizara nyingine ambazo kwa namna fulani zina-*benefit* kupeleka wanafunzi pale, lakini kuna nchi marafiki ambazo zingependa kuleta wanafunzi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika ujumla wake, ningemwomba Mheshimiwa Mwalimu pale alikuwa Diplomasia arejeshe shilingi, ili kusudi tum-*commit* Waziri kutoka kwenye ile bilioni nane aanze sasa kupeleka pale kwenye kile chuo. (Makofi)

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikiri tu kwamba, Mheshimiwa Maiga, Balozi wetu, Waziri wetu amekuwa mkweli. Amekuwa mkweli kwa kweli; amekuwa mkweli kwamba, chuo chetu kina hali mbaya, amekuwa mkweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima tukubaliane kwamba, mwaka wa jana pesa za maendeleo katika Wizara hii hazikutoka! Vilevile hizi pesa zilizotengwa mwaka huu, bilioni nane ni ndogo na hatuna uhakika kama zitatoka. Tunaomba *commitment* ya Serikali, tusibabaishe maneno, Waziri amekuwa mkweli kabisa hapa tunaomba *commitment* ya Serikali, tunafanyaje kuhusu chuo hiki? Hiki ni chuo chetu, tunafundisha watu wetu kwa ajili ya kujenga Wanadiplomasia makini, sasa tusipopeleka pesa tunakusudia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe *commitment* hapa, tunapeleka pesa chuoni kwetu! (Makofi)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nami naunga hoja ya Mheshimiwa Riziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye Hotuba yetu na nimshukuru Waziri kwa kweli amekuwa mkweli na ametuomba wote hapa kama Wabunge tuunge mkono hoja. Niwaombe Wabunge wa CCM kile chuo kinakuwa kama kasekondari fulani, hawa ni watu ambao ndiyo wanakwenda kwenye Mataifa, ndiyo wanaotuwakilisha, ndiyo wanakwenda kutusemea, wanakwenda ku-*compete* na watu wengine ambao wamepitia kwenye vyuo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wetu tuiombe Kamati ya Bajeti ifanye *reallocation* hizi *funds* nyingine ziende huku ili chuo kiweze kufanya kazi kwa sababu, kama tuna *priorities*, kama tunataka nini kwenye dunia lazima tuwaandae watu wetu ambao watakwenda ku-*negotiate* huko! Hatuwezi kwenda kuwapeleka watu ambao hawana ujuzi! Kwa hiyo, ni chuo cha muhimu. Niwaombe Wabunge wa CCM tushirikiane kwa pamoja ili tumsaidie Waziri kama alivyosema na ndiyo kazi yetu. Sisi kazi yetu kuonesha makosa, ku-*point* na kushauri ili Serikali iende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri ameongea kidiplomasia kuliko watu wengine walikuwa wanaongea siasa hapa. Waziri wa kwanza kuongea kidiplomasia hapa. Naomba watu wa CCM tumuunge mkono ili hii bajeti iweze kupita vizuri, chuo kiweze kufanya kazi vizuri. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe kwa mamlaka niliyopewa kwa Kanuni ya 104(1), naongeza muda wa dakika 30 ili Kamati ya Matumizi iweze kukamilisha kazi yake. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Riziki na Mheshimiwa Msigwa amekiri kwamba, Mheshimiwa Waziri ameongea ukweli na ile tu kuongea ukweli *by itself* ni *commitment* ya Waziri kwenye jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* ya pili ni kwamba, tayari ametambua uzito wa tatizo, amemtuma Naibu Waziri ameona na yeye mwenyewe yuko kwenye mkakati wa namna ya kulifanyia kazi jambo hili. Kwa kuwa, hii ndiyo bajeti yake ya kwanza, kutoka zero kwenda kwenye *eight billion*, *it is a good start*. Waziri kama alivyosema ukweli na wewe ukakiri ni ukweli, amejaribu kuwa *realistic*. Tusije tukaenda kwenye kujiridhisha kwa *figures*, hapa tukasema tufumue. Kuna mwaka tuliwahi kufumua bajeti hizi, lakini kwenye *realistic* hazikufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuwe *realistic*. Mheshimiwa Waziri ameonesha *commitment* na ametambua hali ya chuo ilivyo, amekiri wazi na ameelekeza ni wapi anataka kukipeleka chuo hicho. Kwa hiyo, kwa namna hiyo Mheshimiwa Riziki umepaza sauti na sote tunakubaliana nawe, lakini tu tuirejeshe shilingi kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri amesha-*take commitment* ya kutumia hata njia mbadala kwa ajili ya kwenda hatua nyingine inayofuata. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Riziki. Najua anachokiongea, kama vile Waziri wangu alivyoongea kwamba, kwa kweli, hali ya chuko kile ni mbaya sana na ndiyo maana hata Waziri aliponituma kwenda

kukiangalia kwa kweli, ikabidi tuanze kutafuta njia mbadala ya kuweza kukishughulikia chuo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa Waziri hakupenda sana kusema ule mkakati kwa sababu, ni mkakati ambao unahusisha taasisi nyingine hatutaki sana tuzisemee sana hapa. Hata hivyo, maelekezo ya kwanza yalikuwa ni kwamba, tumewapelekea Waraka Balozi zetu zote nje ya nchi nao watafanya mkakati wa kipekee kwa ajili ya chuo hicho wa kutafuta na kutatua tatizo lao kwanza, la miundombinu, nafikiri Mheshimiwa Riziki nikisema miundombinu anaelewa. Maana nilipofika pale kwa kweli, katika kila kikao cha kila kitengo nilichokaa nacho nilihakikisha kwamba, nawapa wajibu wa kutafuta fursa za kutatua changamoto ya chuo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *staff* wangu wanafahamu na wamejua, kila mtu anawazia hilo na Mheshimiwa Waziri alitupa kazi maalum tumepeleka hiyo na vitengo vyetu vinafanya kazi ya ziada kutafuta mkakati wa kutatua tatizo la chuo chetu. Naahidi mbele ya Bunge hili, kwa sababu, ni ajenda ambayo si ajenda tu ya Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini ni ajenda ya Tanzania, kwa sababu wanaosoma pale ni Watanzania pamoja na watu wengine kutoka nje, lakini ndio hawa ambao wanakuja kuwa viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tungependa kwamba, chuo kile kibadilike kiwe chuo cha mfano, ndiyo maana tukasema lazima tuweke mkakati wa ziada wa kwetu. Mkakati ule tunaomba kwamba Bunge hili lije kutuhukumu sisi kama Wizara, lakini naomba sana Mheshimiwa Riziki urudishe tu Shilingi kwa ajili ya Waziri wangu. Kwanza ndiyo kwanza anaanza wajibu bajeti yake ya kwanza na amesema ukweli na mimi nakubaliana naye, lakini naomba kwa heshima kubwa atusaidie kuturudishia hii Shilingi, halafu atutume aone matokeo yake yatakayokuja wakati ujao. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Riziki, naomba uhitimisha hoja yako.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nawashukuru pia, Mawaziri kwa maelezo yao. Kwa historia ya Balozi na Msaidizi wake narudisha shilingi na naamini diplomasia itakuwa nyingine. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Ndassa!

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge waliompongeza Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama utaridhia, nikiombe kiti chako katika muda ambao tuko hapa tumuwmbe Balozi Mahiga tupate semina angalau ya siku moja kuhusu diplomasia ya kiuchumi. Akipata kama masaa matatu hivi nafikiri tutapata uelewa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano uliofanyika Machi, 2016 kule Arusha uliridhia Sudani ya Kusini kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini tarehe 15 Aprili, 2016 Sudani Kusini rasmi ilisaini makubaliano hayo. Katika kutumia fursa ambayo iko Sudani Kusini, kwa sababu ina idadi ya watu wapatao milioni 160, tungependa kujua kupitia fursa hii ya idadi ya watu wengi zaidi, Tanzania itafaidika nini na Sudani ya Kusini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tungependa kujua...

MWENYEKITI: Mheshimiwa unatakiwa uwe na hoja moja mahususi.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba lijibiwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtoa Hoja!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali zuri sana. Mwelekeo wa dunia sasa hivi si kujenga viuchumi vya kitaifa ni kujenga uchumi wa ushirikiano na huko ndiko tunakokwenda. Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ya pili katika ulimwengu baada ya *European Union*, kuwa na mtangamano ambao una tija na unatoa ahadi nzuri na tusijidanganye *economic intergration* ndiyo fursa ya nchi zote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikia sijui Brazil na *South Africa* na Korea na Uchina na Urusi wanatengeneza *bricks*, sijui Mexico sijui na nani wanatengeneza hivi! Huku ndiko dunia inakokwenda. Hatuwezi kujenga uchumi wa nchi moja moja. Sasa hivi kuna mchakato wa kuunganisha *SADC, East Africa Community* na *COMESA*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulifanyika Mkutano Sharm El-Sheikh kule *Egypt* na kuna Kamati ambayo inafanyia kazi hilo. Kwa hivyo, kuileta Sudan ni kutekeleza hiyo azma ya kuwa na jukwaa kubwa la uhusiano wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Sudani siku ile pale Arusha walisema, mnaweza kututumia ujumbe kutoka Tanzania ili tuanze kufikiria jinsi tunavyoweza kushirikiana kiuchumi. Leo hii pengine nisiseme mengi, Sudani, inafikiria kujenga bomba la mafuta. Hawajaamua wajenge lipite wapi, ni lengo la mbali. Ninachotaka kusema ni kwamba, kwa Waingereza wanasema *the more the merrier*. Katika uchumi lazima tujikomboe kutoka uchumi wa Kitaifa,

Taifa huu uwe uchumi wa ushirikiano na muungano. Ndani ya ushirikiano kutakuwa na ushindani lakini ushindani ndiyo utaleta ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, Sudani Kusini, imepita vigezo kama Waziri Mkuu alivyotuaambia hapa, walitumia vigezo vya hali ya juu sana na hata kama tuli-*fast track*, lakini kuingia kwa Sudani Kusini katika *East African Community* ni kufikia ile *vision* kwamba uchumi wa Afrika utaanza kupanuka zaidi. Nchi nyingine nyingi sasa zinataka kujiunga na East Africa, nadhani tuelekee huko. Hatuwezi kujenga uchumi wa Karne ya 21 kwa kutazama ndani ya uchumi wa nchi moja lazima tupanuke na Afrika huku ndiko tutakakofika. (Makofi)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ndassa. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tulipokuwa watoto tuliimba wimbo mmoja ulikuwa unaitwa *pussy cat, pussy cat where have you been!* Anasema *I have been to London to visit a Queen! What did you see there!* Anasema nimekaona kapanya chini ya kiti cha Malkia. Pamoja na utajiri wa Queen kule London, pussy anaona tu kapanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona akina Mheshimiwa Januari hapa na Dkt. Mwekyembe katika mawazo yote ya hotuba ya Upinzani wameona kapanya tu, lakini nimshukuru Balozi yeye ameona dhahabu zilizokuwemo humu na ndiyo maana majibu yake yamekuwa ya kidiplomasia. Kwa hiyo, sina budi ya kumshukuru na niwashauri saa zingine ni vizuri kabla hatujafungua midomo tuwe tunafungua *brain* kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye hoja yangu, uchumi wa kidiplomasia, *National Interest* ndiyo *Paramount*. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri alivyozungumza kwamba tunahitaji kuhusiana na Mataifa mengine na kwamba tuna urithi wa kidiplomasia nakubaliana, lakini ule urithi tulipata sifa tu wakati ule tunasaidia watu wengine. Hata hivyo, uchumi wa kidiplomasia ni wa maslahi, wa kitanzania na nimetoa kwenye hotuba yangu, ni ajira ngapi zinaongezeka? Fursa ngapi zinatengezwa na hawa wataalam, lakini sasa kwenye hotuba yake, kwenye *policy* na kwenye randama ameeleza kabisa. Hata tulivyomwacha kwenye Kamati ameeleza kwamba katika kipindi toka hii *Policy* ya 2001 imeanza, wamekuwa *trained* watu 32 wanaohusiana na masuala ya kidiplomasia.

Mheshimiwa Waziri, hii ni idadi ndogo sana ukilinganisha na *competition* tuliyonayo kwa sababu kila nchi duniani inajaribu ku-*grub* ipate uchumi kutoka nchi nyingine. Tunaposhirikiana na Kenya *what is our National interest?* Tunaposhirikiana na Zambia *what is our National interest?* Hiyo ndiyo *paramount*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu naomba nipate maelezo ya kina, ni mkakati gani ambao tunatayarisha hawa watu *Lobbyists, negotiators*, hawa watu wanakwenda kutafiti, kwenda huko nje kwa ajili ya uchumi wa Tanzania tuongeze ajira, hivyo viwanda anavyovisema viweze kupatikana kwa sababu tuko kwenye *competition*. Mpaka hapa tunapozungumza sijaona *commitment* yoyote, naomba *commitment*, kama sitopata majibu mazuri kaka yangu itabidi nitoe shilingi. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Peter Msigwa, nafikiri anarudia jambo lile lile, bado nilivyosoma maelezo yake yanaonekana kama vile wale ambao sisi tumewaweka katika mkakati wa kuhakikisha kwamba utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi yeye anaona kama hawatoshlezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimwambie, anasema tuna mkakati gani, mkakati tulionao ni pamoja na kuweka bajeti inayohakikisha kwamba wale maafisa na watumishi wote tunaowatumia katika kiwango cha Wizara na hata wale ambao tunawapeleka kwenye kufanya mazungumzo ya kutafuta fursa, tunaweka watu ambao wana ujuzi wenye tija. Tunafanya hivyo na tunahakikisha hilo kwa kuwapa mafunzo stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata ukiangalia kwenye zile *subvote* utaona kuna bajeti ambayo imewekwa pale, bajeti ambazo zinaonesha kuna sehemu ambayo kuna (*training*) mafunzo ya ndani na mafunzo ya nje. Mafunzo ya ndani yanaweza yakawa ni mafunzo ambayo ni ya muda mfupi na muda mrefu kutegemea na aina gani ya ujuzi tunaoutaka kutokana na mtumishi tunayetaka kumtumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Msigwa kwamba, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake, kuwarudisha au kuwabadilisha na kuwapeleka kwenye *posting* wale watumishi, hatuwapeleki tu kwa sababu wanastahiki kwenda, ila tunaangalia tunampeleka wapi na ana ujuzi wa namna gani. Ndiyo maana kwenye zile bajeti pamoja na kwamba ukomo wa bajeti tuliopewa ni mdogo, bado tumehakikisha kwamba tumeweka kifungu cha mafunzo ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naweza kusema kwamba, sisi mkakati huo tunao na tunaweza tukakwambia kabisa kwamba idadi ya wale ambao watakuwa wanakwenda wako 60. Nao watakwenda kutokana na ujuzi na uwezo waliokuwa nao na tutaendelea kufanya hivyo na tutahakikisha kwamba tunawapa mafunzo stahiki na tunawapeleka mahali stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijapata majibu ya kuridhisha, kwa hiyo nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kabisa kwamba katika kipindi cha miaka karibu 15 Wizara ime-*train* watu 32 kwenye *Economic Diplomacy*, kwa maelezo na takwimu zenu wenyewe. Changamoto tuliyonayo kulingana na uchumi inavyokwenda duniani hata kwa maelezo ya Mheshimiwa Balozi hapa kuna *competition* kubwa. Ukiwachukua kwa mfano wenzetu wa Botswana hata walivyokuwa wanaingia kwenye mikataba kabla hawajawenda kufanya mikataba na makampuni yoyote, wanakuwa wanajua wanakwenda kutaka nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ikija Kampuni yoyote, ikiweka biashara pale kama hawafiti kwenye kile wanachokitaka huwa wanaitupa nje, kwa sababu wana watu ambao wako *trained*, watu ambao wako *knowledgeable*, ambao wana *exposure*. Kwenye randama ya Wizara wanazungumza kwamba wametoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watu 32. Kweli tuko *realist* kwamba hawa watu wanaweza waka-*compete* na uchumi wa kidunia? Halafu Mheshimiwa Waziri kwamba eti hawa mnaona wanatosha. Kama hawa wanatosha tungekuwa tumeona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yangu nimeuliza, nikawa nauliza ni fursa ngapi zinatengenezwa hawa walioko nje ni Watanzania wangapi wanakwenda kuajiriwa nje. Hii *Economic Diplomacy* imetoa fursa hizo ngapi na inaleta kwa kiasi gani hamna takwimu yoyote mnayotuambia hapa mnatupa maneno ya juu, juu, hamjatoa takwimu zozote, fursa zipi zimetengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Bunge lijadili, tujadiliane kwa pamoja kwa mustabali wa taifa letu na naomba Wabunge mniunge mkono, natoa Shilingi ili tujadili kwa kina kwa ajili ya *commitment* ya Serikali.

MWENYEKITI: Haya, mmoja mmoja; Mheshimiwa Possi, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Adadi na Mheshimiwa Januari. Haya tunahamia huku sasa Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa dada pale nani, Mheshimiwa Magereli na mwingine wa mwisho, Mheshimiwa Ali Khamis na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tayari.

Haya tunaendelea. Jamani tunaendelea sasa, tunaanza na Mheshimiwa Possi.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE WALEMAVU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba tunapozungumzia *Economic Diplomacy* tunazungumzia suala pana la kisera na ni lazima tutofautishe pia na shughuli za kila siku ambazo ziko ni more *executive*. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile wale watu ambao *specifically* watakuwa *trained* katika *Economic Diplomacy* tusitegemee kwamba watafika laki moja, wakati tumeambiwa kwamba, tunavyozungumzia *Economic Diplomacy* na suala zima la sera hii ni sera mtambuka ambayo lazima pia itaendana na watu katika fani nyingine mbalimbali ambazo zinatoka nje ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *so much as* ni lazima tulinganishe suala zima la *Economic Diplomacy vis-a-vis* Balozi zetu na nchi ambazo tuna mahusiano nazo ya karibu. Wakati huo huo ni vizuri tuelewe kwamba suala hili ni mtambuka na kwa wakati huo huo huwezi ukategemea kwamba Wizara ya Mambo ya Nje i-*train* wataalam wa kilimo, viwanda, uwekezaji na kadhalika, haya mengine yatafanyika na Wizara nyingine.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Possi, tunaendelea na Mheshimiwa Adadi.

MHE. BALOZI. ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyozungumza awali, sasa hivi tuna-move from *political diplomacy to economic diplomacy*. Waziri ameeleza hapa kabisa kwamba anakwenda far mpaka kuweka *Industrial diplomacy* na huwezi Mheshimiwa Msigwa uka-stick kwa figure ya 32. *Economic Diplomacy it comprises combination* ya vitu vingi, *combination* ya wataalam wa kitalii, *combination* ya watu wa biashara na ndiyo maana tunasema kwamba tunataka kupanua balozi zetu kuweka *trade attache*, kuweka *tourism attache* ili waweze ku-convince wafanyabiashara, ku-convince watalii kuja nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiweka ukajumlisha yote kwa pamoja ndipo unaweza kupata hilo jungu kuu la *Economic Diplomacy*. Kwa hiyo, huwezi uka-isolate ukasema kwamba basi hawa ndiyo *trained* 32.....

(Hapa kengele ililia kuashishiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Adadi. Tunaendelea na Mheshimiwa Magereli.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia nilieleza suala hili la kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri haikuwa imetoa maelezo yanayokidhi katika mambo ambayo tulitamani kuyaona katika Wizara ya Mambo ya Nje. Moja kati ya mambo ni haya ambayo tunayajadili sasa hivi ya habari ya *Economic Diplomacy*. Takwimu pia hazikuonesha kabisa, badala yake wakati anajibu hoja; nimeona ameanza *training* ya vitu vingine na kadhalika. Tunashukuru, lakini naamini hili lingekuwa jepesi kama lingekuwa limeingia kwenye hotuba yake tangu awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini iko haja ya kulitazama na naunga mkono haja ya Mheshimiwa Msigwa kwa sababu naamini hata mikataba ambayo tunaingia ikiwa na upungufu mkubwa ni kwa sababu kwa sehemu ni kukosekana kwa hawa watu wa *Economic Diplomacy*. Mnasema katika

(Hapa kengele ililia kuashishiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Magereli. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Ali Khamis.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naunga hoja ya Waziri Kivuli kwa yale ambayo amezungumza. Waheshimiwa hapa anachokizungumza Waziri Kivuli ni kwamba hakuna ile *comprehensive strategy* na mifano hapa ipo. Leo hapa wenzetu Kenya ambao ni majirani zetu hapa wameweza kuzitangaza bidhaa zetu kama ni za kwao na wanaziua, zikijulikana kwamba hizi bidhaa ni za Kenya kwa sababu tu hatuna watu ambao ni *aggressive*, kufanya hizi kazi za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vipi leo mtatuambia kwamba mmejiandaa kufanya *competition* ya *Economic Diplomacy*? Lazima Serikali itupe mwelekeo uliokuwa sahihi ili tuone. Hapa Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu amesema kwamba hata jinsi ya ku-pack zile bidhaa zetu tukazitangaza nje, tumekuwa tuko chini, hatuwezi ku-compete na watu wengine. Sasa naomba Mheshimiwa tupate commitment kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ili tuweze kujua mwelekeo wa nchi ni upi.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ali Khamis. Tunaendela na Mheshimiwa Mwigulu.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa mantiki suala analoliongelea Mchungaji Msigwa lina *logic* kufuatana na *transformation*, lakini pamoja na aina ya uchumi ambavyo unatakiwa kujengwa. Hata hivyo, niseme tu neno moja kwamba huwezi ukaanza na 100 ama ukaanza 1,000 ama ukaanza na 2,000, lazima pawe na

starting point. Kwa maana hiyo *historical background* ya nchi yetu mtakumbuka kwamba kwa kiwango kikubwa ilikuwa ime-concentrate zaidi kwenye mambo ya kisiasa. Ukiangalia kwenye SADC utaikuta Tanzania ilikuwa mstari wa mbele sana kwenye mambo ya kisiasa, ukija Afrika Mashariki ilikuwa vivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa *move* ambayo tumekuja kugeuka kwa sasa, niseme kwamba Mheshimiwa Waziri *proclamation* yake ya sasa, tamko lake alilolitoa la sasa la mwelekeo wa Wizara anakotaka kuelekea ni jambo ambalo ndilo tunalotakiwa tulizingatie. Tutakavyotoka hapo kwenye idadi ile ile tutakuwa na watu ambao ni *competent* na baada ya hapo tutaendelea kuongeza idadi kulingana na *sectors* lakini pia na idadi ya balozi zetu na maeneo ambapo tunataka kuwapeleka watu hao.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwigulu. Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *nakushukuru, its true Economic Diplomacy is the wider thing lakini within it kuna specific areas ambazo tulipotaka measurable targets tungeambiwa hapa Wizara imepanga ku-train watu kwenye Public Diplomacy wangapi, kwa mwaka gani. Wale trainers wenyewe wanao-train hawa Mabalozi wetu wangapi watakwenda wapi, watapata ujuzi gani. International negotiation and all of those other specific areas ambazo pamoja zinatengeneza Economic Diplomacy. Again tunaomba tu vitu vyenye kuelezeka, vinavyoonekana, vinavyogusika, ambavyo ni measurable given a time period.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu 32 kwa miaka 15 tunazungumzia *Economic Diplomacy as of 2001*. Sasa wale maana yake ni watu wawili kila mwaka na hiyo ku-coordinate maana yake ni pamoja na ku-coordinate database. Hizo Wizara nyingine zimekuwa *coordinated* vipi watu hawa ulio-train hapo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Riziki. Tunaendelea na Mheshimiwa Januari.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Peter Msigwa angekuwa na *exposure* inayolingana na nafasi aliyonayo angeweza kuelewa suala hili la *diplomacy*, ambayo ni suala pana na suala mtambuka. Kwamba, *Economic Diplomacy* ndani ya Serikali, katika nyanja zote ambazo Serikali inafanya mazungumzo na aidha Washirika na Sekta binafsi, huwa kuna *GNTs* katika sehemu zote za Serikali. Kuna *GNT* ya *Oil and Gas*, kuna *GNT* ya masuala ya *East African Community*, kuna *GNT* ya masuala ya *tax*, ambao hawa watu

wanapata *training specifically* kwenye Wizara zao na wote wana-form the bigger part ya capacity ya watu wa Serikali ku-negotiate.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Januari tunamkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha sasa dakika moja tu Mheshimiwa.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tu, nataka nitoe shule kwanza ya *Economic Diplomacy*. Mheshimiwa Peter Msigwa ni kwamba mkakati wa *Economic Diplomacy* unategemea sana kwanza *business environment* ya nchi, hiyo ndiyo Diplomasia ya kwanza. Pili, namna ambavyo unazielezea *opportunity* tulizonazo katika nchi yako, lakini vile vile kuzifahamu vyema *interest* za huko unakokwenda kutafuta ule uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa inajielekeza kwenye mambo hayo kama sehemu muhimu sana ya mkakati wa kufanya *Economic Diplomacy*. Hawa watu 32 unaowasema hawatoshi, *it depends on their effectiveness*, lakini wako pia watu mbadala Mheshimiwa Msigwa. Unatumia mabalozi walioko ndani ya nchi yako, unatumia *Diaspora* yako, unatumia hata Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Msigwa, ukienda uko unatumia hata *former friends* wa nchi yako. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tumemaliza, tunaomba Mheshimiwa Peter Msigwa uhitimisha hoja yako.

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali hapa inajikanyaga, hawana hoja. Ukiangalia kwa mfano nchi ya Australia, asubuhi nilim-quote mmojawapo wa Mawaziri hapa, wao wana hata ajenda. Kwa mfano, ajenda ya kwanza wanasema ni ku-promote trade, hatujaona Serikali inatuambia ajenda ya kwanza ni nini. Ajenda ya pili wanasema ku-encourage growth, attracting investment na ya ku-promote kuhakikisha business people wa ndani wana flourish, lakini hapa mnaongea hadithi ambazo hazigusiki. Tunachozungumza hapa hiyo *Economic Diplomacy* iko wapi ambayo unaigusa kwamba tunaipata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri, unayoyasema, haya mambo ni wajibu wa Serikali yenu myaweke hapa tuyaone ili watu wanapotaka ku-flourish waone kwamba tunagusa hapa, tunagusa hapa, lakini you are coming here with stories. Tunachozungumza tunataka kitengo hiki kiwe kinaweza kuweka mazingira ambayo tutakuza uchumi. Kuwa na utengamano na kuwa na mahusiano na nchi zingine kwa ile diplomasia ya kizamani ya amani haitusaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesifiwa sana, kusaidia Afrika Kusini, kusaidia Mozambique, lakini bado watoto wanakufa na utapiamlo itatusaidia nini, bado watoto wanafukuzwa hapa UDOM inatusaidia nini? Tunahitaji uchumi...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Msigwa, muda wako umemalizika, naomba ukae, naomba ukae muda umemalizika.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado, natoa fedha, si nimetoa shilingi...

MWENYEKITI: Eee! Ndio nasema kwa mujibu wa kanuni ya 104 muda umeshapita kwa hivyo inabidi nisimamishe....

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa hata dakika tatu sijamaliza....

MWENYEKITI: Muda umekwisha tafadhali tunaingia kwenye vifungu kwa ujulma kwa kutumia kanuni ya 104 (2)...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo meseji muifanyie kazi.

MWENYEKITI: tuendeleo Katibu.

Kif. 1002 - Finance and Accounts... ..Sh. 1,156,185,000/=

Kif. 1003 - Foreign Affairs office Zanzibar... ..Sh. 524, 100, 000/=

Kif. 1004 - Policy and Planning... ..Sh. 1, 316, 910,000/=

Kif. 1005 - International Cooperation... ..Sh. 780, 581,000/=

Kif. 1006 - Europe and America... ..Sh. 629,879,000/=

Kif. 1007 - Asia and Australia... ..Sh. 559,228,000/=

Kif. 1008 - Africa... ..Sh. 1, 419, 327,000/=

Kif. 1009 - Regional Cooperation... ..Sh. 597,972,000/=

Kif. 1010 - ProtocolSh. 10, 482,479,000/=

Kif. 1011 - Legal ServiceSh. 1,306,353,000/=

Kif. 1012 - Government comm. Unit... ..Sh.405,245,000/=

Kif. 1013 - Middle East Division... ..Sh. 569, 295,000/=

Kif. 1014 - Internal Audit Unit... ..Sh. 350, 039,000/=

Kif. 1015 - Procurement UnitSh. 365,704,000/=

Kif. 1016 - Information and communication
TechnologySh. 412,583,000/=

Kif. 1017 - Diaspora Engagement and
OpportunitySh. 296,110,000/=

Kif. 1018 - Economic Infra and Social Supp
Servs Div.Sh.651,469,000/=

Kif. 1019 - Political, Defense and Security

	Affairs	Sh. 570,080,000/=
Kif. 1020 - Trade, Investment, and Productiv	Service Div.	Sh. 33,551,869,000/=
Kif. 2001 - Embassy of Tanzania-	Addis Ababa	Sh. 3,157,493,000/=
Kif. 2002 - Embassy of Tanzania Berlin		Sh. 4,295,742,000/=
Kif. 2003 - Embassy of Tanzania Cairo		Sh. 2,019,344,000/=
Kif. 2004 - Embassy of Tanzania	Kinshasa	Sh. 2,686,570,000/=
Kif. 2005 - High Commission of Tanzania	Abuja	Sh.2,411,724,000/=
Kif. 2006 - High Commision of Tanzania	London... ..	Sh.5, 409,333,000/=
Kif. 2007 - High Commision of Tanzania	Lusaka	Sh. 1,434,198,000/=
Kif. 2008 - High Commision of Tanzania	Maputo	Sh. 2,676,349,000/=
Kif. 2009 - Embassy of Tanzania	Moscow	Sh. 3,257,213,000/=
Kif. 2010 High Commission of Tanzania	New Delhi... ..	Sh. 2,557,925,000/=
Kif. 2011 - Permanent Mission to the UN	New York	Sh. 5,440, 716,000/=
Kif. 2012 - High Commission of Tanzania	Ottawa	Sh. 2,654,360,000/=
Kif. 2013 - Embassy of Tanzania - Paris		Sh. 3,218, 433,000/=
Kif. 2014 - Embassy of Tanzania - Beijing.. ...		Sh. 3,811,251,000/=
Kif. 2015 - Embassy of Tanzania - Rome... ..		Sh. 4,220,204,000/=
Kif. 2016 - Embassy of Tanzania -	Stockholm.. ...	Sh. 3,967,343,000/=
Kif. 2017 - Embassy of Tanzania - Tokyo... ..		Sh. 3,217,842,000/=
Kif. 2018 - Embassy of Tanzania	Washington... ..	Sh. 4, 787,718,000/=
Kif. 2017 - Embassy of Tanzania -Brussels... ..		Sh. 3,347858,000/=
Kif. 2020 - Permanent Mission to the UN	Geneva	Sh. 6,276,995,000/=
Kif. 2021 - High Commission of Tanzania	Kampala... ..	Sh. 2, 197,879,000/=
Kif. 2022 - High Commission of Tanzania	Harare	Sh. 1,818,252,000/=
Kif. 2023 - High Commission of Tanzania	Nairobi... ..	Sh. 5,099,228,000/=
Kif. 2024 - Embassy of Tanzania – Riyadh ...		Sh. 2,746,055,000/=
Kif. 2055 - High Commission of Tanzania-		

PretoriaSh. 2,858,121,000/=

Kif. 2026 - Embassy of Tanzania – Kigali.. ...Sh. 1,947,978,000/=

Kif. 2027 - Embassy of Tanzania -
Abu DhabiSh. 3,688, 719,000/=

Kif. 2028 - Embassy of Tanzania -
BujumburaSh. 1,772,946,000/=

Kif. 2029 - Embassy of Tanzania -
MuscatSh. 2,719,527,000/=

Kif. 2030 - High Commission of Tanzania -
Lilongwe..Sh. 2,719,527,000/=

Kif. 2031 - Embassy of Tanzania -
BrasiliaSh. 3,517,832,000/=

Kif. 2032 - High Commission of Tanzania -
Kuala Lumpur... ..Sh. 2,740,230,000/=

Kif. 2033 - Embassy of Tanzania -
The Hague... ..Sh. 2,832,961,000/=

Kif. 2034 - Embassy of Tanzania - Moroni ... Sh. 1,924,551,000/=

Kif. 2035 - Embassy of Tanzania - Kuwait ...Sh. 1,594,601,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 34 - MINISTRY OF FOREIGN AFFAIRS, EAST AFRICA, REGIONAL AND INTERNATIONAL CO-OPERATION

Kif. 2004 Policy and Planning... ..Sh. 8,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda
kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae, mtoa hoja taarifa!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako, lilikaa kama Kamati ya Matumizi
limekamilisha kazi zake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na
Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja (Makofi)

WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.
(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa 2016/2017 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Naibu wake, pamoja na watendaji wote wa Wizara niwape pongezi za dhati na niwaombee kila la kheri katika utekelezaji wa Bajeti hii.

MWONGOZO WA SPIKA

Mwongozo wa Spika kuhusu Hoja ya Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa juu ya Kiapo cha Uaminifu kutofautiana na kiapo kinachotumika Bungeni na kinachotumika Serikalini.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kuna mwongozo wa Spika mmoja naomba niwasomee. Mwongozo wa Spika, kwa hoja ya Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge kuhusu kiapo cha Uaminifu kutofautiana na kiapo kinachotumika Bungeni na kinachotumika Serikalini.

Waheshimiwa Wabunge katika orodha ya shughuli za tarehe 31 Mei, 2016, katika kikao cha 33 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge, shughuli ya kwanza asubuhi ilikuwa ni kiapo cha uaminifu ambapo Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub Mbunge aliapishwa.

Baada ya kipindi cha maswali na majibu Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge, aliomba mwongozo wa Spika, kuhusiana na kiapo. Msingi wa mwongozo wake ni kwamba Wabunge wanapoapa mwishoni wanatamka kuwa, nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

Mheshimiwa Mwambalaswa aliendelea kueleza kuwa Serikalini wanaapa kwa kumalizia na maneno kwa mujibu wa sheria, hivyo Mheshimiwa Mwambalaswa anaona kama wanakosea katika kiapo hiki kati ya Wabunge na Watumishi wengine Serikalini, alisema nanukuu:

"Mheshimiwa Mwenyekiti, nahisi kwamba kundi mojawapo limekosea hiki kiapo na kama limekosea inabidi liape upya kwa sababu ni mkataba wa msingi mno, naomba mwongozo wako." Mwisho wa kunukuu.

Mwongozo wa Kiti ni kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa sheria ya viapo vya Viongozi, *The Official Oath Act, Cap 266* ya 2002 katika jedwali la kwanza (*first schedule*) kiapo cha uaminifu (*Oath of allegiance*) ambayo ndiyo inaainisha viapo kwa viongozi imetumia maneno ya mwishoni kama ifuatavyo: *"Na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa, Ewe Mwenyezi Mungu nisaide."*

Hiki ndicho kiapo rasmi ambacho Wabunge na Watumishi wengine Serikalini waliotajwa katika Sheria hii wanatakiwa kuapa. Aidha, hata katika kiapo kilichotolewa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub na walivyoapa Wabunge wote ni kwa kutumia maneno haya yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 24(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inayohusu kiapo cha uaminifu kwa Wabunge imeazima maneno hayo hayo ya sheria ya viapo kwa Viongozi kama nilivyonukuu hapo juu. Hivyo mwongozo wangu ni kwamba kiapo cha Wabunge ni sahihi kwa mujibu wa sheria na kanuni na viongozi wengine Serikalini wanatakiwa kuapa kwa mujibu wa viapo vilivyowekwa kisheria. Huo ndio mwongozo wangu, umetolewa leo tarehe 31 Mei, 2016.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja hapa, Mheshimiwa Kanali Masoud anatangaza kwamba Wabunge wote wa CCM wanaotoka Zanzibar wakutane kwenye Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirishwa Bunge hili usiku huu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli yetu imekamilika, sasa naliahirisha Bunge hadi kesho Jumatano tarehe moja Juni, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.27 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 1 Juni, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*